

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha kumi na Sita – Tarehe 29 Juni, 2009

(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:-

Hotuba ya bajeti ya Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI WA KATIBA SHERIA NA UTAWALA):-

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2009/2010.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS:-

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya ya Makamu wa Rais, kwa mwaka 2009/2010.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:-

Randama za Makadirio ya Mafungu na Kasma za Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 119

Miji Midogo ya Kongwa na Kibaigwa kuwa Mamlaka ya Miji Midogo.

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishaamua na kuagiza kuwa Miji Midogo ya Kongwa na Kibaigwa sasa iwe na hadhi ya Mamlaka ya Miji Midogo.

Je, kwa nini hadi sasa Mji wa Kongwa ambao ni Makao Makuu ya Wilaya haujawa Mamlaka ya Mji Mdogo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Miji Midogo ya Kongwa na Kibaigwa zilitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 353 la tarehe 17/9/2004. Baada tangazo hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ambamo Mamlaka za Miji midogo hiyo imo iliteua Wajumbe waliokwenda Wilaya ya Kondoa kujifunza namna ya kuunda na kuendesha Mamlaka za Miji midogo.

Aidha hoja ya kuanzisha Mamlaka za Miji midogo ya Kongwa na Kibaigwa ilijadiliwa katika kikao cha Kamati ya Uchumi, ujenzi na mazingira na kisha kuwasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani mwezi Machi, 2006. Kikao hicho kiliweka azimio la kuanzisha Mamlaka hizo kwa awamu, kwa kuanza na Mamlaka ya Mji mdogo wa Kibaigwa na baadae Kongwa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo ulifanyika kwa kuzingatia kwamba kuanzisha Mamlaka mbili za Miji midogo kwa wakati mmoja ulikuwa mzigo mkubwa kwa Halmashauri ya Wilaya ambayo mapato yake wakati huo yalikuwa chini ya shilingi milioni 80/- kwa mwaka na upungufu mkubwa wa watumishi na miundombinu mingine kama vile majengo ambayo yanahitajika kwa ajili ya Ofisi za Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji mdogo wa Kibaigwa ni vema sasa , Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ikaagiza kuanza mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Mji mdogo wa Kongwa. Aidha inashauriwa kutumia uzoefu

ulipatikana katika uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji wa Kibaigwa katika kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kongwa amba ni Makao Makuu ya Wilaya.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nina maswali mawili madogo ya nyongeza, la kwanza inaelekeea Serikali imeiachia Halmashauri ya Kongwa peke yake jukumu na mzigo wa kuanzisha mamlaka ya mji mdogo, lakini swali langu haswa ni kwamba kwa kuwa tuna Uchaguzi wa Serikali za mitaa mwezi wa kumi mwaka huu na Uchaguzi wa miji midogo unahusisha katika muundo wake mitaa, na siyo vitongoji kama ilivyo sasa kwa vijiji kwa maana ya mji wa Kongwa kama unakuwa mji mdogo. Je kati ya sasa na mwezi wa kumi maandalizi haya yanatosha kwa maana ya kukubalika mitaa yake ili uchaguzi wa mwezi wa kumi wa Kongwa mjini kwa maana ya mamalka ya mji mdogo uwe katika mitaa na siyo vitongoji?

La pili, katika miji midogo ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya kama hapa Dodoma Kongwa, Mpwapwa, Kondoa isingekuwa vema kama katika miji midogo hiyo pakawekwa lami angalau ya kilometra tatu nne pale mjini katikati ikizingatiwa kwamba kwa mji wa Kongwa lami ya kwanza iliwekwa katika mji wa Kongwa mwaka 1947, leo hakuna chochote, Kongwa hakuna chochote, Mpwapwa hakuna chochote na Kondoa pia. Je, haiwezi kuwa ni mpango mzuri kwa kilometra tatu, nne, tano zikawekwa lami katikati ya miji hii ili kuifanya miji hiyo midogo iitwe miji kweli?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika liko moja hili la kwanza analogumzia kwamba Kongwa nayo iweze kuwa mji kamili na kwamba utaratibu huo umekamilika kati ya sasa na mwezi wa kumi, na kwamba sasa uchaguzi wa Serikali za mitaa pale uweze kufanyika. Sijui jinsi ambavyo hii inaweza ikafanyika kwa sababu hili lilikuwa linakiwa liwe limeshafika, limeshakamilikika. Kipindi kilichobaki hapa sasa hivi ni *almost* tumemaliza mpangilio wenyewe ninachowenza kabisa labda Kibaigwa, lakini Kongwa kwamba utaiweka katika utaratibu sasa hivi hapa labda niseme vizuri msimamo wa Serikali katika jambo, hili tulisha kubaliana hapa na lilishawekwa wazi wakati wa Mheshimiwa Ngwilizi, mimi nakumbuka nilikuwa nimekaa pale nasikilza vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwamba popote pale ambapo pana makao makuu ya Wilaya tulishaanza kupatambua kama mji mdogo. Lakini ukitaka kufika hatua hiyo lazima mkutane wenyewe wenye mji mdogo ule, lazima mkutane wenyewe wenye Halmashauri wenyewe mkae mzungumze mkubaliane, kama tulivyozungumza hapa tuliona kwamba utakuwa ni mzigo Kongwa nayo kuingizwa katika mpango huu kwasababu Kongwa nayo ikiwa mji mdogo Bajeti yake itatokana na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa.

Sasa kama Mheshimiwa Job Ndungai anafikiri kama anaweza aka- *fast truck* habari zote harakaharaka ikaja bado jambo hili linabakia katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, ndiyo inatakiwa iamue lakini mimi natakiwa nimwambie kwamba hatuna

objection yoyote wala hatuna tatizo lolote kuanzisha mji wa Kongwa. Kwa sababu kimsingi maamuzi yale yalishafanyika kwa hiyo ni suala tu la kukaa.

Mheshimiwa Spika, la pili,kuhusu kwamba tuwe na kilomita mbili au tatu katika miji hii midogo. Hii ni uamuza wako, mheshimiwa Spika pale kwako Urambo mkiamua ninyi kwamba mnataka kuweka kilomita mbili tatu za lami pale mtapima. Mtaangalia kama mtaona ni kipaumbele mtafanya hivyo lakini mimi nikiangalia bajeti inavyokwenda hapa; na juzi nilimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akizungumza habari hizi za kilomita mbili tatu kule ndani wakati kuna maeneo mengine yamekuwa hayajaungashwa na nini, nilimsikia akijibu yale. Sasa lakini mimi nasema kama Kongwa wanafika mahali wakaona ni kipaumbele wakaamua kuwa waweke kilomita mbili, tatu hakuna mtu atakaye wapinga kwa sababu wao wamepewa mamlaka ya kufanya hivyo.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna Wilaya mpya kama Longodo , Siha na Wilaya zingine ambazo bado hazina hadhi ya kuwa miji ya Wilaya. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa sasa tuwe na mitaa badala ya kuwa vitongoji na uchaguzi ukija tayari umekwisha kamilika kuwa miji midogo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, sijui kama nitakuwa nimempata vizuri sana Mheshimiwa Lekule Laizer, kwa sababu hapa vijiji na vitongoji hivi unavipata tu katika Halmashauri ya Wilaya . Unapoanza kuzungumza habari ya mtaa unaanza kuzungumza habari ya mahali ambapo pamepimwa , mahali ambapo ni pa mji mji tumepakubali kama mamlaka ya mji mdogo, na ndio maana mkishakubalika mnakuwa nyinyi ni mji mdogo na vijiji vinafutika pale na wanaokwenda sasa pale ni madiwani wawili halafu wanakwenda Wenyeviti wa vitongoji ndio wanakwenda pale kwa kweli suala lile linakuwa limekwisha pale.

Mheshimiwa Spika, sasa huwezi ukaitisha mkutano wa mtaa na waende wakafanye mkutano wa mtaa na waende wakafanye uchaguzi wa mtaa pale wakati mamlaka ile hajatambullika kama mamlaka ya mji mdogo. Kwahiyoo tulikuwa tunashauri hapa na nina mshukuru sana kwamba anaizungumzia hata na Wilaya yangu ya Siha kwamba turuhusiwe kufanya hivyo lakini lazima tufuate utaratibu huo kwanza tuka – *declear* pale kwamba ni mji mdogo ndipo sasa paweze kujulikana kama Halmashauri ya mji mdogo na uweze kupata mitaa mle ndani yake lakini hili suala la mchakato wenyewe utakavyokwenda pale Wilayani.

Na. 120

Kuchimba Visima vyat Mji kwa Matumizi ya Shulen

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa shule ya sekondari ya Kipili ambapo ipo katika Kata ya Kipili Tarafa ya Kilanda Wilaya ya Nkasi haina bomba la maji wala kisima kwa matumizi ya shule , na kwa kuwa hali hiyo husabaisha mlipuko wa magonjwa hatari na kuliwa na mamba.

Je ,Serikali ina mpango gani wa kuona wa kuchimba visima katika shule zilizoko Rukwa ili kuepuka magonjwa ya mlipuko?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka fedha wa 2008/2009 kuititia mpango wa *quick wins* Serikali ilianza kutekeleza mpango wa kuchimba kisima kirefu kimoja katika shule ya Sekondari Kipili hali ya uekelezaji hadi sasa imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

.Uchunguzi wa sehemu ya kuchimba kisima (*geophysical survey*) umekamilika.

. Ununuzi wa pampu ya mkono (*India mark II*) umekamilika.

.Mkandarasi wa kuchimba amepatikana ambaye ni RWE- Rukwa, maandalizi ya kupeleka mitambo (*mobilization*)yako kwenye hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati iliyopo ya kuipatia shule ya sekondari Kipili maji kwa kuchimba kisima kirefu kuititia mpango wa *quick wins* serikali inafanya mpango kuhakikisha kuwa shule zote za sekondari Mkoani zinapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kueleza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika shule za sekondari Wilayani Nkasi .

Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina jumla ya shule sekondari 18 ambapo kati ya hizo sekondari 10 za Nkasi ni Mkole, Mtenga, Kabwe, Chala, Milundikwa, Kipande, Wampembe na Kala zinahuduma ya maji.Huduma ya maji inapatikana kuititia kutumia njia ya Kupitia mifumo ifuatayo:-

- (i) Visima virefu.
- (ii) Visima vifupi.
- (iii) Chemchem kingwa.
- (iv) Maji ya bomba (*Gravity*).

Mheshimiwa Spika, sekondari nne (4) za ntuchi, sentali, kipili na kirando ambazo zilitengewa Bajeti kwa ajili ya kuchimba visima virefu utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Katika sekondari ya Sintali uchimbaji wa kisima umekamilika, maandalizi ya ujenzi na ufungaji wa pampu za mkono yanaendelea. Vilevile katika Sekondari ya Kirando uchimbaji umekamilika na maandalizi ya ujenzi na ufungaji wa pamp za mkono unaendelea. Katika sekondari ya Kipili mkandarasi amekwisha chimba mashimo wawili na bado hajapata maji hivyo anafanya utafiti sehemu nyingine ili achimbe kisima hicho, Aidha katika sekondari ya Ntuchi mkandarasi amekwisha patikana na uchimbaji unatakiwa kufanyika hivi karibuni. Shule zingine nne (4) za Mkwamaba, Ninde, Mkanagale na Nkomolo 1 zitajengewa mfumo wa uvunaji maji ya mvua kwa kutumia paa la nyumba kupitia programu ya Mji na Usafi wa Mazingira katika mwaka wa fedha 2009/2010.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Nkasi na hii shule ya Kipili ipo kandokando kabisa ya Ziwa Tanganyika na kwa kuwa tumeona mfano mzuri ambao ni wa Ziwa victoria mapakaa sasa hivi watu wa Shinyanga wanafaidika na maji ya kutoka ziwa Victoria.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani na mipango gani kwa ajili ziwa Tanganyika lina kina kirefu, likipangiwa mipango mizuri kama ilivyopangiwa mipango ya ziwa Victoria wananchi wa Wilaya ya Nkasi pamoja na shule zote ambazo zina matatizo ya maji zitafaidika?(*Makofii*)

(b) Kwa kuwa ,amesema Naibu Waziri hapa kuna hizi shule Nkwamba, Ninde, wanasema ndio kwanza wanaweka mikakati ya kuvuna maji ya mvua ndio yatumike katika hizi shule. Je, Serikali hauoni kwa wale watoto sasa hivi wanapata tabu sana kuhusu maji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, labda nikuhabarishhe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote mlioko hapa . Wakati Mheshimiwa Anna Lupembe alipozungumzia masuala ya barabara , niliahidi mimi ntatoka hapa nitakwenda mpaka Rukwa, na niliahidi pia nitafanya hivyo kwasababu Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoka maeneo yale nilitaka niende nikajionee mimi mwenyewe katika eneo lile pakaje.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie kwamba nilikwenda mpaka Rukwa. Na nilikwenda pale nilifanya Ziara ya wiki ya mbili , matatizo ya maji yanayozungumzwa hapa ni ya kweli. Na nilyaona hayo na matatizo yako pale na nilitaka nithibitishie nyumba hii kwamba mimi nilikwenda pale na nimeona.

Mheshimiwa Spika, na Wilaya ya Nkasi ambayo inazungumzwa hapa mimi nilikwenda mpaka kule Nkasi na nikaona matatizo makubwa yaliyokuwepo pale, wakati ule ushauri niliota ni kwamba tulifikiri kwa harakaharaka kwa matatizo ya maji niliyoyaona katika Mkoaa mzima wa rukwa:-

(a)kuelimisha wananchi kuhusu kuvuna maji, na hili limepokelewa ndio maana umesikia katika jimbo langu hapa nimelizungumza. Lakini sasa tunaambiwa na Mheshimiwa Mbunge kuwa tuangalie uwezekano wa kupata maji kutoka ziwa Tanganyika kama ilivyofanyika katika ziwa Victoria .

Mimi nakumbuka tulikuwa tumekaa hapa wote nilimsikia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji akizungumzia kuhusu mipango ambayo inafanyika na ninataka nitaje hapa ,alikuwa anaonyesha Wilaya, Halmashauri 54 ambazo ziko katika benki ya dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya ku-sign mkataba .Katika hizo wilaya Mkao wa Rukwa ametaja mji wa Mpanda, Wilaya ya Sumbawanga, na Wilaya ya Nkasi.

Mimi nafikiria tuchukulie mpango huu kuwa ni mpango kabambe ambao utasaidia sana. Namwona Mheshimiwa Naibu Waziri ana niangalia pale kwamba wako katika mpango huu na wanasubiri ku-sign, mimi nina hakika kwamba kwa mpango huu wa Serikali ambao umezungumzwa hapa tutaondokana na hili tatizo.

(b)Kuhusu hizi shule ambazo amezizungumza hapa , ambazo zimeonekana kuwa zina tatizo hilo mimi napenda niamini kwamba kwa mipango hii ambayo tumeonyeshwa hapa na programu hii iko hapa. Iko katika ukurasa wa kumi na tatu, mimi nina hakika kwamba matatizo haya yatakuwa yameondoka na ninataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote wanaotoka katika Mkao wa Rukwa, kwamba ofisi yetu itashirikiana nao kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la maji katika Mkao wa Rukwa.(*Makofi*)

SPIKA: maelezo ya ziada Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba niseme tunao utaratibu na mpango wa kuzishughulikia shule za sekondari hata shule za msingi kwa kuweka mifumo ya kuvuna maji kwa ajili ya shule hizo. Tunataka utaratibu huo utumike siyo tu kwa ajili ya taasisi hizo lakini utatumika pia kama ni mafunzo kwa kutumia Teknlojia hii ya kuvuna maji kwa ajili ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, la pili ni hili alilosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba sasa hivi mchakato wetu unakwenda vizuri tofauti na ilivyokuwa huko nyuma kwa hiyo mji wa Nkasi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya ya Nkasi na hata mji wenye wa Nkasi programu yetu ya kutekeleza miradi ile chini ya ufadhili huu wa *World bank* inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya sasa hivi ni pale ambapo wamechelewa ikiwa ni pamoja na Nkasi tunapeleka wataalamu wa Wizara kuharakisha mchakato huo.Nataka niwahakikishie kwamba itatekezwa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inahimiza shule za bweni hasa kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya wafugaji, na kwa kuwa shida iliyopo kwenye shule ya Kipili Wilayani Nkasi inafanana sana na shule nyingi za Wilaya ya Kiteto hasa Kata ya Dongo na kwingineko.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipeleke juhudu kama hizohizo katika maeneo hayo ya wafugaji ili wanafunzi hao wasiendelee kutoroka katika shule za bweni?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, mimi naiona mantiki kubwa sana katika jambo ambalo anazungumza Mheshimiwa Mbunge hapa. Na kama mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa hotuba yake hapa, na Waziri wa Nchi walipozungumza hapa walizungumzia suala la kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira mazuri katika maeneo yale ambayo yanaonekana yamekaa pembedni kidogo na huduma zinaonekana kwamba ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, napenda hapa nikubaliane na maeneo ambayo yanazungumzwa ya wafugaji. Maeneo kama ya Ngorongoro yale Maeneo kama ya Longido, maeneo ya Kusini mwa Rufiji ni maeneo ambayo yameainishwa kwamba yatapewa kipaumbele. (*Makofii*)

Tutaangalia utaratibu wa kuweka *solar systems* ni pamoja na huduma ambazo zinazungumzwa hapa kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Umbulla kwamba kuna haja ya kuangalia kwa karibu na hususani katika shule hizi za bweni ambazo watoto wetu wengi wanapata matatizo. Kwa hiyo, tuweze kuwa shule waweze kusaidiwa.

Na. 121

**Kamati ya Kulinda Utamaduni wa Mtanzania
Kushindwa Kufanya Kazi**

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuza:-

Kwa kuwa mara kadhaa Serikali imekuwa ikijitapa kuwa imeunda kamati ya kulinda Utamaduni wa Mtanzania na mavazi ya heshima;jambo ambalo Serikali inaonekana kushindwa katika nyanja zote:-

(a) Je, Serikali haioni uchafu wa mavazi kwa vijana wetu hasa wa kike; na Serikali imechukulia hatua gani?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuliacha suala hili si maendeleo au kwenda na wakati bali kupotosha umma na vizazi vijavyo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO aijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa habari Utamaduni na Michezo napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kusema sio kweli kuwa Serikali imeunda Kamati ya kulinda Utamaduni wa Mtanzania ambayo Mheshimiwa Mbunge anadai kuwa inaonekana kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Hata hivyo napenda kukiri kwamba ,wapo baadhi ya vijana wetu wa kike na wa kiume pia wanaendelea kucaa mavazi yasiyo na heshima licha ya jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu kuitia vyombo vya habari, warsha, makongamano na kadhalika juu ya umuhimu wa kulinda heshima na maadili ya nchi yetu katika nyanja mbalimbali hususan utamaduni wetu. Kuendelea kucaa mavazi yasiyo na heshima kunatoa picha mbaya.

Serikali na hata jamii kwa ujumla haifurahishwi na mambo hayo. Serikali imekwisha toa maonyo mengi, Serikali yenyewe kuitia Mheshimiwa Waziri wetu pia chombo chake yaani (BASATA), kuitia vyombo vya habari juu ya matumizi mabaya ya mavazi yanayofanywa na vijana wetu na baadhi ya vikundi vinavyojishughulisha na sanaa kama vile ngoma,muziki wa dansi na pia katika kuendesha shughuli za mashindano ya ulimbwende , matamasha na kadhalika.

Aidha Serikali inaendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa vijana wetu kulinda na kuuenzi utamaduni wetu.

(b) Mheshimiwa spika, Serikali inatambua kwamba, kuliacha suala hili likiendelea hakutaleta maendeleo au kukubali dhana iliyopo ya “kwenda na wakati” bali kuendelea kupotosha jamii na vizazi vijavyo. Ndio maana Serikali inaendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kulinda mila na desturi zetu na kuendeleza utamaduni wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo suala la kukemea tabia chafu inayoharibu vijana wetu ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya mavazi na vitendo mbalimbali vinavyofanywa kinyume na mila na desturi ya Watanzania ,haliwezi kuachiwa Serikali peke yake, bali ningependa kutoa wito pia jamii yenyewe isaidie kwa ujumla ili suala hili lisiwepo ikiwa ni pamoja na wazazi na viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu lake kwenye suala mama. Lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika elimu kwa vyombo nya habari, warsha, kongamano, onyo kwenye vyombo nya habari, hivi Mheshimiwa Waziri haoni kuwa imeshatosha na hivi sasa Serikali inatakiwa kuwa na meno kwa kuweka Sheria ama amri kutokana na mambo hayo yanayofanyika hivi sasa Tanzania ili kukinga vizazi vijavyo hapo baadaye?

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu jamii isaidie.

Jamii itaweza kusaidia kipindi ipo kutakuwa na amri kutoka Serikalini au Sheria iliyotungwa kuhusu mambo hayo kuhusu jamii itasaidia, lakini Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge hili kule Lagos na sehemu nyingine kuna mavazi maalumu.

Hivi ni nini vazi rasmi la Tanzania kwa Mwanamke na Mwanaume na kama hakuna, hivi haoni kama pia hii inapotosha kuwa na msimamo kuwa na mavazi rasmi ya Tanzania?

Nashukuru Mheshimiwa Spika.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba tumetoa maonyo mbalimbali kwenye vyombo nya habari, nataka nikubaliane naye lakini namkumbusha tu kwamba chombo hiki kwa maana ya Bunge tayari wameshaunda kitu kinachoitwa BASATA.

Hiki ni chombo ambacho kimeundwa kisheria, sheria hii imeundwa mwaka 1984 inaendelea kufanya kazi na ndiyo chombo tunachokitegemea na kwa kumpa tu ushahidi ni kwamba chombo hicho hutumia mamlaka iliyopewa na Bunge kimeshatoa maonyo saba ambayo siwezi nikapoteza muda kwa sababu yapo mengi, kwa vyombo mbalimbali ambavyo vimekiuka, sheria ipo isipokuwa nataka nikubaliane naye kwamba ni lazima tuiwekee mikakati ili sheria hii ifanye kazi zaidi.

Ni kwamba tuwaonye na tuwakumbushe kwamba wafuate taratibu, na ndiyo maana sheria hii inakwenda mpaka kwenye Wilaya, Halmashauri za Wilaya zinatakiwa wawe wakali kuhakikisha kwamba mavazi, kelele kwenye mitaa sheria hii yote ipo na iko chini ya BASATA.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda baada ya kuliona hili alitiisha kikao maalum na yeze mwenyewe akawa

Mwenyekiti ili tuweze kulipatia mkakati kama Serikali na tumeunda Kamati ya kuweza kutathmini na kuona uvurugaji na matatizo ya mila na desturi Tanzania, kwa hiyo sheria hii ipo na inaendelea.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nikubaliane naye kwamba suala la vazi la Taifa, Kamati imeshaundwa imeshafanya kazi yake, Wizara imeshamaliza shughuli tayari suala la vazi la Taifa Muswada umeandalila na uko kwenye Baraza la Mawaziri utakapopitiwa tayari sheria italetwa Bungeni tutaambiwa ni vazi gani Tanzania itumie kama ambavyo Nigeria na nchi nyingine wanavyofanya.(*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Waheshimiwa, tumeambiwa Kilimo Kwanza kwa hiyo tunaenda Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

Na. 122

Ushuru wa Mazao

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa, Bodi za mazao zilikuwa zikijiendesa zenyewe kutokana na ushuru wa mazao husika na kwa kuwa, Serikali iliondoa ushuru huo na kuahidi kuzihudumia Bodi hizo kwa asilimia mia moja (100%).

- (a) Je, kwa nini Serikali inashindwa kutekeleza ahadi zake kwa bodi hizo?
- (b) Je, Bodi hizo zinaposhindwa kazi kwa ukosefu wa fedha, Serikali haioni kuwa inatengeneza mianya ya ubadhilifu kwa watendaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali katika kusitisha utozaji wa ushuru wa mazao ilikuwa kuhakikisha kuwa mkulima habebeshwi mzigo mkubwa kutokana na ushuru na kodi zilizokuwa zinatozwa. Kutokana na hali hiyo mwaka 2005 Serikali iliamua kwamba Bodi za mazao zigharamiwe na Serikali kwa asilimia mia moja kwa shughuli za usimamizi (*regulatory services*). Katika kutekeleza azma hiyo kuanzia Julai 2006, Serikali ilianza kuzigharamia Bodi za mazao kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga jumla ya shilingi 14,852,159,900; mwaka 2007/2008 ilitenga shilingi 11,308,783,000 na mwaka 2008/2009 zilitengwa shilingi 21,085,611,000. katika Bajeti ya 2009/2010, Serikali imetenga jumla ya shilingi 22,379,816,600. Hata hivyo kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali fedha

zilizotengwa hazitoshelezi mahitaji halisi ya kuziwezesha Bodi kutekeleza majukumu yake.

(b) Mheshimiwa Spika, sio kweli Serikali inatengeneza mianya ya ubadhirifu kwa watendaji, kwa kuzingatia azma ya kutombebesha mkulima mzigo mkubwa wa makato ya kodi na ushuru, Serikali imerazinisha majukumu miundo na namna ya ugharimiaji wa Bodi za mazao. Aidha Serikali imependekeza marekebisho ya sheria za mazao ili kubainisha shughuli zisizo za usimamizi *non regulatory services* na kuweka msingi wa kufanya maamuzi ya namna ya wadau wa zao husika kugharamia shughuli hizo ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa mifuko ya hiari ya mazao kwa madhumuni hayo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Bodi za mazao ni kuendeleza kwa njia mbalimbali ili hatimaye tija ionekane kwa Mkulima, kama hili linafanyika, na tija inapatikana, kuna ubaya gani kwa bodi kuchukua ushuru kidogo kama jasho lao lakini kama hili halifanyiki. Je, umuhimu wa bodi upo wapi?

(ii) Mheshimiwa Spika, kama Waziri alivyoleza hapa kwamba Serikali inatumia hela nyinyi sana katika kuzigharamia uendeshaji wa Bodi hizo kwa mfano 2006/2007 bilioni 14, 2007/08 bilioni 11, na 2009/2010 bilioni 2. Kwa sababu kuna tatizo la uwajibikaji siyo katika bodi za mazao tu lakini katika sekta mbalimbali pia katika nchi hii, Je Wizara au Serikali imefanya tathmini kama Bodi kweli zinatimiza majibu yao barabara, kabla ya kubeba mzigo huu wa kuziendeleza na kuzigharamia bodi kwa asilimia mia moja. Je, mmefanya tathmini ya kuangalia kama utekelezaji wa Bodi ni sawa sawa au mnatoa tu hela?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la kuondoa ushuru kwa wakulima ni kwa ajili ya kuwaongezea kipato, na niseme tu kwamba ni kweli kutoptana na uwezo wa Serikali fedha ambazo zinapewa Bodi hazitoshi lakini tunachokifanya sasa hivi ni kwamba yale majukumu ambayo hayatokani na usimamizi kwa maana ya kusimamia sheria, kutoa leseni au ukaguzi wa mazao, hayo ndiyo majukumu halisi ya bodi ambayo wanatakiwa wayafanye. Kwa hiyo, tunaondoa yale ambayo hayahusiani na usimamizi kama vile huduma za ugani pamoja na promosheni ya mazao kusudi hayo yachukuliwe na mifuko ya hiari itakayoundwa kutoptana na baada ya kwamba tumeefanya marekebisho ya mazao. Hiyo itakuwa imeshapunguzia mzigo bodi zile. Kwa hiyo, itaweza kufanya kazi ya usimamizi ambayo ni *regulatory services*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufanya tathmini, tunafanya tathmini kila siku na ndiyo maana utakuta hali ya uzalishaji wa mazao inaongezeka mwaka hata mwaka, kwa hiyo bodi zetu zinafanya kazi vizuri na kila mwaka tunazifanya tathmini na tunarekebisha. Ndiyo maana unaona kwamba mwaka huu tunawaongezea tena fedha kutoptana na kwamba tumeona majukumu yao kwa jinsi tulivyofanya tathimini wanahitaji kiasi gani cha fedha.

Ahadi ya Maji-Kata ya Itangano

MCH. LUCKSON N. MWANJALE K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA
aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitoa ahadi ya kuwapatia maji wakazi wa Kata ya Itangano ifikapo mwaka 2007 lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo?
- (b) Je, isingekuwa vema kutumia chanzo cha malagala kuwapatia maji wakazi hao?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Benson Mpresa, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la maji katika Kata ya Itangano Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka jijini Mbeya iliomba kuingiza Kata ya Itangano katika awamu ya pili ya Mradi wa maji safi na maji taka unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia shirika la *KfW* na Jumuiya ya nchi za Ulaya *EU*.

Mheshimiwa Spika, kata ya Itangano haikufaikiwa kuingizwa kwenye mradi huo kutokana na masharti ya wafadhili yaliyozuia kugharamia miradi yenyehadhi ya vijiji na iliyombali na mtandao wa maji wa Jiji la Mbeya ikiwemo Itangano.

Ili kutimiza ahadi ya kuwapatia wananchi wa Itangano maji safi na salama Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya iliamua kuingiza Kata ya Itangano katika vijiji 10 vilivyopo kwenye programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya tayari imeshafanya mazungumzo *Negotiation* na Mhandisi Mshauri M/S *DON Consult* kwa ajili ya kusaini mkataba wa kusanifu miradi ya vijiji 10 pamoja na Itangano. Viji vingien vitakavyonufaika na mradi huo ni Nsoho, Iziwa, Mwansekwa, Tembela, Mwasanga na Ilomba (Ituha).

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuangalia uwezekano wa kutumia mto Malagala kuwa chanzo cha maji kwa ajili ya wananchi wa Itangano nimeupokea hasa ukizingatia kwamba upo uwezekano wa kupata maji ya mtiririko (*gravity*) kutoka kwenye chanzo hicho. Suala hili litachunguzwa wakati Mhandisi mshauri atakapofanya usanifu wa kina na uamuzi wa chanzo kipi kitumike.

MHE. MCHUNGAJI LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri aliahidi kwa Kata zote mbili Itagano na Ihango watapatiwa maji kupitia chanzo cha Malagala na Kata ya Ihango na Itagana ni jirani.

Je, Serikali haioni kwamba kukamilisha mradi huu wa maji utatua matatizo ya majimbo yote mawili, yaani Mbeya Vijijini na Mbeya Mjini.(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mchungaji Mwanjale, kwa kunikumbusha hiyo Kata nyingine inayofuatia. Nataka nimhakikishie kwamba katika upembuzi ambao umekwishafanyika, ni kweli kabisa inaonekana kwamba Kata zote mbili zinaweza zikanufaika na mpango huo na ndiyo maana tumeamua kwamba kwa sababu mradi ule wa Jiji la Mbeya haukuweza kujumuisha mradi huu tunaozungumzia au Kata ya Itagano, basi hizi Kata hizi mbili zote wakati tukitekeleza au tukifanya usanifu zitaangaliwa.

Kazi kubwa atakayoifanya mtaalamu huyo ni kutazama ni chanzo kipi na wka gharama ipi naweza kunufaisha Kata zote hizi mbili, na hata suala la Malagala ambalo ni chemi chemi hili tunalichukua kwa sababu lina *element* ya *gravity floor* na mhandisi mshauri tutashirikiana naye kumwonesha ni wapi panaweza kunufaisha Kata zote mbili. Naomba asiwe na wasiwasi.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa Serikali ilisema kwamba kuanzia mwaka 2007 itapeleka maji katika kijiji cha Sawala, Mtwango na Kibao, toka mwaka 2007 mpaka sasa haijatekeleza ahadi yake hiyo.

Je, ni lini hasa Serikali itatekeleza hiyo ahadi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kwa kifupi tu nimhakikishie Mheshimiwa Malangalila kwamba Vijiji vya Sawala, Mtwango na Kibao ambavyo yeye mwenyewe mara kadhaa amenitembelea ofisini akinikumbusha ahadi hii. Nataka nimhakikishie kwamba katika mwaka huu 2009/2010 kwa hakika kabisa tutaangalia hivi vijiji vitatu na tutavipa kipaumbele kuhakikisha kwamba vinapata maji.(*Makofi*)

Na. 124

Malipo kwa Walimu wa Mkataba

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa wapo Walimu wanaofundisha kwa mkataba katika Shule za Sekondari za Kata Wilayani Singida, ambapo hadi sasa wamefundisha kwa miezi kumi na tano bila kupata mishahara yao na kusababisha waishi kwa taabu:-

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kuwalipa mishahara yao pamoja na malimbikizo yote?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na kwa ridhaa yako ninakuomba kwa heshima kubwa nitumie sekunde chache kutoa salamu zangu za pole kwa Mufti Shekhe Mkuu wa Tanzania na waumini wote kwa kifo cha Naibu Mufti na Shekh Mkuu wa Mkoa wa Lindi Suleiman Gorogosi kilichotokea juzi na maziko yake kufanyika jana, Mwenyezi Mungu aipokee roho yake na aiweke mahala pema alipomwandalia *Innalillahi Wainailaihi Rajiuun.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo kwa heshima na unyenyekevu mkubwa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum katika ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wapo Walimu wastaafu 11 wanaofundisha kwa mkataba katika shule za Sekondari za Mkoa wa Singida ambao walichelewa kupata mishahara yao kutokana na kuchelewa kuwasilishwa taarifa zao Wizarani kwa sababu ajira hizo zilifanyika Wilayani ikiwa ni jitihada za Wilaya kukabili tatizo la uhaba wa Walimu. Hata hivyo Walimu wastaafu hao tayari wameshaingizwa katika orodha ya mishahara ya mishahara ya watumishi wa Serikali (*payroll*) na wanaendelea kulipwa mishahara yao.

Madai ya malimbikizo ya mishahara yao kwa miezi ya nyuma kabla hawajaingia kwenye orodha ya mishahara ya watumishi wa Serikali tayari yameshapokelewa Wizarani baada ya Walimu hao kuikamilisha kujaza fomu za madai ya malimbikizo ya mishahara (*salary arrears claim form*). Walimu hao watalipwa malimbikizo yao baada ya zoezi zima la uhakiki wa madeni ya Walimu lililofanyika nchi nzima kukamilika mwezi huu Juni, 2009.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa kuwa hodari sana wa kujibu maswali na vile vile amekuwa hodari wa kufuutilia kero mbalimbali anazozipata hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nimwuulize maswali amwili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa madeni haya ya malimbikizo ya mishahara ni ya muda mrefu sana miezi 15 ni wazi kwamba walimu hawa waliishi kwa madeni kwa kipindi kirefu sana, kwa kuwa Naibu Waziri ni mtu wa kasi na Viwango kama wewe Spika, Je, anaweza

akatoa *timeframe* ili walimu hawa waweze kuwa na lugha nzuri kuwajibu maeneo waliko kopa kopa ili waendelee kuaminika atoe muda tu kwamba mwezi kadhaa watapata.

(ii)Kwa kuwa, hata mshahara waliosaini katika mkataba wao umekuwa tofauti na mshara walioanza kuipata toka Februari mwaka huu, Je, Naibu Waziri atakuwa tayari pia kuihakiki mishahara ile ili waweze kupata mishahara waliosaini kwenye mikataba yao.(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba ni kweli walimu hao na wengine wote waliopatwa na mikasa kama hii wameishi kwa taabu na madhila makubwa nami nachukua nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Elimu kuwapa pole, niahidi tu kwamba baada ya ya kukokotoa na kutambua madai yao ambayo nakala yao ninayo na nitampatia Mheshimiwa Mbunge kwa uthibitisho aone kwamba tumeshafanya kazi na kuadihi mara madai haya yatakapofikishwa Hazina tutalipa. Ipo dhamira nzuri ya Serikali chini ya usimamizi wa Rais kwamba madai haya yalipwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu tofauti ya mishahara ambayo wameipata baada ya kusaini mkataba namwomba tushirikiane tupate kumbukumbu za walimu hao ili niweze kutambua tatizo liko wapi, ahsante.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, chini ya utaratibu mpya shule za Sekondari sasa zitakuwa chini ya Halmashauri za Wilaya na kwa kuwa hao Walimu wa mikataba walikuwa wamesaini mikataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sasa chini ya utaratibu huu wa shule kurudi kwenye Halmashauri mikataba yao itakuwaje?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba walimu wale waliposaini mikataba wengi wao walisaini mikataba chini ya Halmashauri walizokuwa wameomba kufanya kazi, na Halmashauri zote ziko chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, hata wale ambao walisaini mikataba kuititia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba ifahamike kwamba sote tupo chini ya Tume ya Utumishi wa Umma ambayo inatuongoza sote. Haki zao na maslahi yao yatalindwa na hakuna atakayepoteza haki yake. (*Makofi*)

Na. 125

Ukamilishaji wa Shule kwa Mipango wa MMEM

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa katika mpango wa MMEM shule zilizojengwa, kukarabatiwa na hata kuongezwa madarasa:-

Je, Serikali iko tayari kuikamilisha shule zote zilizojengwa kwa mpango huo na ambazo hazijakamilika kutokana na utekelezaji wa mpango wa MMES?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, MMEM ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na MMES ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari. Hii ni mipango miwili tofauti ya Serikali na utekelezaji wake umetofautishwa. Hata hivyo mipango hii miwili inashabihiana (*Complimentary to each other*).

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Wa Elimu ya Msingi(MMEM).

Hata hivyo kumekuwa na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji huo. Aidha Serikali ninahimiza majengo ambayo bado hayajakamilika yakamilihwe kwa kutumia Bajeti za Elimu za maendeleo zinazotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mfano mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Mji wa Mpanda ilipewa shilingi 66,199,000/- katika Bajeti ya Maendeleo ya Elimu na mwaka 2008/2009 pia walipewa shilingi 70,323,000/-. Halmashauri pia zinaweza kutumia fedha za ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa *LGCDG* kuikamilisha majengo hayo kulingana na vipaumbele vya Halmashauri husika. Katika mwaka wa fedha ujao Halmashauri ya Mji wa Mpanda imetengewa ruzuku ya Maendeleo kiasi cha shilingi milioni 180.8.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imetoea mwongozo mpya wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeagizwa kumaliza majengo ambayo hayajakamilika kujengwa kwanza kabla ya kuanza ujenzi wa majengo mapya. Wananchi nao wahamishishwe kuendelea kushiriki katika ujenzi na kukamilisha miundombinu ya shule. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza, napenda kumhakikishia Naibu Waziri kwamba nafahamu vema kwamba mipango hii miwili ni tofauti na utekelezaji wake ni tofauti, lakini inashabihiana, kadhalika ilikwenda sambamba.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo ya kwenda sambamba iliwapunguzia sana uwezo wananchi kuweza kuchangia katika ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari na shule za msingi kwa wakati mmoja, na kipaumbele kikaelekezwa katika shule za Sekondari ambazo tumefanya vizuri mpaka sasa hivi. (*Makofi*)

(i)Je Waziri ataisaidiaje Halmashauri ya Mji wa Mpanda ambayo ina wanafunzi ellfu kumi nanne na sabini na tisa mahitaji ya vyumba vya madarasa kwa ajili ya shule za msingi ni 313 vilivyopo ni 140. Tunaupungufu wa vyumba 173 vya madarasa katika shule za msingi. Serikali itasaidia vipi kumaliza tatizo hili kwa sababu ni dhahiri nguvu za wananchi haziwezi kabisa kukamilisha hili?

(ii)Kutokana na tatizo hilo la uhaba wa vyumba vya madarasa shule nyingi wanafunzi wanasoma kwa awamu, kipindi cha asubuhi na kipindi cha jioni. Kama Waziri na mwalimu anadhani watoto hawa wanapata elimu inayotosheleza? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUND (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)I: Mheshimiwa Spika, naomba niungane naye na nimpongeze sana kwa kuguswa zaidi na Maendeleo ya elimu katika Jimbo lake, naomba tu niseme wazi kwamba tulilazimisha mipango hii miwili kuenda pamoja hasa baada ya kuona mafanikio ya mpango wa awali yaani MMEM.

Mheshimiwa Spika, isingelikuwa Busara kuacha Idadi kubwa ya wanafunzi wanaofaulu wakaendelea kubaki nyumbani hali ya kuwa tuna kitu tunachowezu kukifanya. Naomba nikuahidi kwamba madarasa hayo pungufu 173 nizielekeze Halmashauri husika na wewe mwenyewe ukiwa Mjumbe katika Halmashauri hiyo mketi kwa pamoja muweze kuchambua na kuona kiasi cha fedha kilichotengwa mwaka huu mtakitumiae, jukumu la kuweka kipaumbele bado kingali kwa Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni sawa na kusema *tulikata pua tukaunga wajih*. Uhaba wa vyumba vya madarasa na kwamba wanafunzi wanasoma kwa awamu kwa kweli hili linapunguza uwezo mkubwa kwanza wa walimu wenyewe lakini pili hata wanafunzi wenyewe naamini wale wanaoingia mchana usikivu utakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niziombe Halmashauri husika zione namna ya kumaliza tatizo hili kwa kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo *TASAF*.

Mwisho nimwahidi Mheshimiwa Mbunge nitapenda kujionea mwenyewe ninatarajia kufanya ziara mara Mwenyezi Mungu atakapotuhitimisha salama nije niione hii hali kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko. (*Makofi*)

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI)
aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kahama ndiyo mzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara katika Mkoa wa Shinyanga hasa mazao ya Mahindi, Mpunga, Karanga, Mihogo, Pamba na mazao ya misitu kama Mbao, Mkaa, Nta na Asali.

Kwa kuwa miaka mingine miundombinu ya barabara kuelekea maeneo ya Chambo, Ulava, Bulungwa katika Jimbo la Kahama na Bulige katika Jimbo la Msalaba ambayo ni mzalishaji mkubwa wa mazao hayo, imekuwa ni mibovu kupindukia kiasi cha wananchi kuuza mazao yao kwa bei ya kutupa na hivyo kuathiri kiwango cha uzalishaji wa uchumi wa Taifa kwa ujumla:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kupandisha hadhi barabara nchini zikiwemo zilizotajwa hapo juu ili zihudumiwe na *TANROADS* badala ya Halmashauri ya Kahama ambayo uwezo wake ni mdogo sana.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa, barabara hizo zimekuwa mbovu kupindukia, kwani kutokana na umuhimu wa barabara hii kiuchumi, kuanzia mwaka wa fedha 2006/07 Serikali imekuwa inatenga fedha kila mwaka ili kuisaidia Halmashauri ya Kahama kuikarabati barabara hii. Hadi mwaka 2008/2009, jumla ya shilingi Milioni 170 zimetumika kuifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, mchakato wa kupandisha hadhi barabara nchini umekamilika.

Kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za Januari 2009, barabara ya Kahama- Chambo, ni mionganoni mwa barabara zilizokidhi vigezo na kupandishwa hadhi kutoka barabara ya Wilaya na kuwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Bulungwa na Bulige, hazikukidhi vigezo kwa sasa. Kwa hiyo, hazikupandishwa daraja na zitabakia kuwa barabara za Wilaya.

Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge, aendelee kushirikiana na Halmashauri yake ya Kahama ili barabara hizo ziendelee kutengewa fedha za matengenezo kutoka kwenye Mfuko wa Barabara amba hutengwa kwa kila Wilaya kila mwaka.

Wizara yangu itaendelea kusaidia Halmashauri ya Kahama, kila inapowezekana ili kuziwezesha barabara hizo kuitika wakati wote.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Waziri, nishukuru kwa kupandisha barabara moja katika barabara zilizombwa.

Kwa kuwa, Jimbo la Kahama na Wilaya ya Kahama kwa ujumla kuna migodi mingi sana na magari makubwa yanapita katika maneo hayo hususani pale Mjini na yanaharibu sana Barabara wakati wale watu wenye migodi hawakarabati barabara hizo.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Kahama?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba katika Wilaya ya Kahama iko hiyo migodi na watu wa migodi wanatumia barabara hizo kufika kwenye machimbo hayo.

Sasa suala hili la kwamba uharibifu wa barabara umeendelea kutokea wakati wanapitisha vifaa vizito vizito, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Kahama kwamba hili ni suala tu la ushirikiano na wenzetu amba wanahuksika na machimbo hayo.

Kwa hiyo, nishauri tu kwamba kuwe na ushirikiano wa karibu na kwa sababu barabara hizi zinatumiwa na watu wenye migodi. Bila sina shaka tukiwa karibu nao wanaweza wakasaidia vile vile katika suala la kuzitengeneza.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa ukomo wa maswali umetimia tutaendelea tumalize haya maswali mawili. Lakini kwanza swali la nyongeza.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kahama ni Wilaya mojawapo nchini Tanzania yenyе wawekezaji wengi hasa waliowekeza kwa upande wa migodi na kwa kuwa wawekezaji hawa wanachangia sehemu kubwa sana kuharibu barabara. Je, haoni kwamba umefika wakati kwamba wawekezaji hawa wachangie kutengeneza barabara hizo kwa kutumia rasilimali zetu hizo hizo zinatoka nchini mwetu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nilipokuwa najibu swali la nyongeza lililokwisha hivi karibuni, nimeeleza tu kwamba kwa sababu hawa wenye migodi wanazitumia hizi barabara na kwa kweli wangependa barabara hizi ziweze kuwa imara na kuitika mara kwa mara, suala la ushirikiano na kuwa nao karibu ili waweze kutengeneza barabara hii litahitaji kuwa la karibu.

Kwa hiyo, nilishauri kwamba wananchi pamoja na viongozi wa maeneo hayo washirikiane na hawa wenyewe migodi ili kuhakikisha kwamba wanazitengeneza hizo barabara ili ziweze kuitika wakati wote. (*Makofi*)

Na. 127

Barabara ya Iringa – Msembe

MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Iringa (km.6) hadi njia panda ya Kalenga – Ipamba, na kwa kuwa barabara ya Iringa – Msembe ni muhimu kwa sababu kutokea njia panda ya Kalenga inakwenda Hospitali ya Wilaya ya Ipamba km. 5 bila shida. Pili Mkoa umeazimia kukuza utalii kuititia *Ruaha National Park* na pori la uwindaji la Lunda, Utalii ambao utanufaisha Mkoa na taifa kwa ujumla kuititia barabara hiyo ya Iringa – Msembe ikiwa ya taifa na kuwekewa lami:-

Je, Serikali itakubaliana na mimi juu ya kuimarisha barabara hii kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iringa – Msembe ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu na ina urefu wa kilometra 105 ambapo kati ya hizo kilometra 9.5 ni za lami na zinazosalia ni za changarawe. Kwa upande wa barabara inayotoka njia panda ya Kalenga kwenda Hospitali ya Ipamba, barabara hii inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba barabara ya Iringa – Msembe inayoelekea kwenye Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama ya Ruaha ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa na taifa kwa ujumla. Serikali pia inaona umuhimu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili iweze kuwa imara zaidi na kuitika kwa urahisi. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina fedha za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sasa. Serikali inaendelea kutekeleza mipango ya ujenzi wa barabara kuu nchini hususani zile za kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yetu nchini ili kuwezesha Mikoa yote kufikia kwa urahisi. Hata hivyo Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuifanya matengenezo ya kawaida kwa kiwango cha changarawe barabara ya Iringa Msembe ili iendelee kuitika wakati wote.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu barabara ya kwenda hospitali ili barabara hiyo iweze kufikiriwa kuwekewa lami.

(a) Je, barabara hiyo isingefaa kuipandisha hadhi kuwa ya taifa?

(b) Kuhusu Iringa Busemba ninaamini kwamba hapa panakosekana utashi wa kisiasa. Mwaka jana tumejengewa mita siyo kilomita, mita 250, mwaka huu tumejengewa mita 250 kwa kasi hii itatuchukua miaka 400 au karne nne kufika kule. Je, siyo utani huu? Je, Waziri atakubaliana nami kuwa angalau ungefanyika upembuzi ili michakato ijayo ya Bajeti tujue, ni fedha gani inahitajiwa kuliko kujumlisha tu kwamba fedha hakuna. Ahsante sana. (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya hospitali kupandishwa hadhi nimetoka kujibu hapa swali lililotangulia ya kwamba mchakato wa kuzipandisha hadhi barabara umekamilika na kwa kuzingatia vigezo vilivyokuwa vimewekwa baadhi ya barabara zimepandishwa na zingine bado. Lakini kuhusu barabara hii kupandishwa hadhi kwa sasa haikudhi vigezo vilivyopo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa sababu zoezi la kupandisha hadhi barabara ni zoezi la kudumu litakuwa ni endelevu tutaangalia kadri itakavyokuwa inawezekana ili hapo baadaye barabara hii iweze kuingizwa kwenye vigezo vinavyostahili na kupandishwa hadhi.

Swali la pili kuhusu kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kuijenga barabara hii ya Iringa Busemba niseme tu katika majibu ya msingi hapa nilieleza kwamba nia ya Serikali kusema kweli ingependa sana barabara hii yote ikajengwa kwa lami kwa kipindi kifupi iwezekanavyo. Lakini kwa kusema kweli ni uwezo wetu mdogo wa Serikali ndiyo maana hata hicho kidogo kidogo kinachotengwa kuweza kuimarisha katika baadhi ya maeneo.

Lakini niseme tu kwamba mpango mkubwa wa Serikali kama nilivyokuwa nimesema katika jibu la msingi hapa ni kuangalia sasa hivi maeneo haya makuu ya kuunganisha Mikoa yetu hapa nchini. Lakini utafika wakati barabara hii tukubaliane tu na Mheshimiwa Mbunge kwamba nayo itafikiwa kuweza kufanyiwa upembuzi yakinifu na hatimaye kuijengea kwa lami kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

Na. 128

Uchunguzi wa Mafuvu 40 ya Binadamu Wilayani Kishapu

MHE. JAMES P. MUSALIKA aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka jana yaligundulika mafuvu 40 ya binadamu katika Wilaya ya Kishapu na kwa kuwa Serikali iliyapeleka mafuvu hayo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali yafanyiwe uchunguzi:-

- (a) Je, Uchunguzi huo umeonyesha ni nini chanzo cha vifo hivyo?
- (b) Je, Serikali inasemaje juu ya tafsiri ya vifo hivyo kwa baadhi ya watu kwa kuwa sehemu yalipogundulika hayo ni kambi ya misukule maarufu kwa Usukumanii

Gamboshi ambapo kambi hiyo ilitekelezwa na wamiliki wake hivyo kusababisha vifo vya watu hao.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa James P Musalika Mbunge wa Nyang'wale lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwishoni mwa mwaka jana jumla ya mafuvu 40 ya binadamu yaligunduliwa katika pango lililokuwemo katika mti mkubwa wa Mbuyu katika Wilaya ya Kishapu. Mafuvu hayo yamechuliwa na kukabidhiwa kwa Mkemia Mkuu ili aweze kubainisha ni lini watu hao waliuawa na jinsia na viumbe wenye mafuvu hayo na Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wake.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha vifo hivyo bado hakijajulikana na uchunguzi unaendelea. Kwa sasa Serikali haiwezi kutoa taarifa kuhusiana na chanzo cha vifo hivyo wala tafsiri kuhusu uhusiano na kuwepo kwa mafuvu hayo katika sehemu aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ambapo inasemakana ilikuwa ni kambi ya misukule maarufu kama *Gamboshi* ambayo ilitekezwaa na wamiliki wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa kipolisi na kimaabara wananchi watafahamishwa matokeo ya uchunguzi huo.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini sambamba na suala hili pia juzi Serikali ilipigwa kura za maoni kuhusiana na waganga wa jadi wanaojihusisha na mauaji ya albino na kwamba matokeo yake bado na wengi sasa wale waganga wa jadi safi wanashindwa nao kufanyakazi. Ni lini Serikali itatoa matokeo ya kura za maoni iliyopiga mwaka huu kuhusiana na waganga ambao wanajihusisha na masuala haya ikiwemo na mauaji ya albino? Ni lini matokea yatatolewa?

SPIKA: Swali hili limepandikishwa tu juu ya swali hili, kwanza imekuwa ni misukule sasa tena hawa wanaouaua ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi. Kwa kuwa muda umekwisha basi tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha haya mambo ya uchawi tuyaaache kwanza.

Matangazo. Nitaanza na wageni. Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambayo ni mama Helena Mwambegele Mwenyekiti wa *African Women Mining Network* Tawi la Tanzania. Naomba asimame pale alipo. Yule pale ahsante sana mama. Tunawatachia kazi njema katika masuala ya migodi.

Kazi hizi siku za nyuma zilikuwa hazionekani kama ni za wanawake. Nawapongeza wanawake wa Tanzania kwa kuanza kuingia katika fani zote ambazo zamani zilikuwa zinaonekana za wanaume tu.

Bibi Margaret Fundi Mjumbe kutoka Mkoa wa Dodoma wa Chama hicho hicho, Bi Jacqueline Nitwa ambaye naona hapa ndio Miss Dodoma mwaka 2009 ahsante sana. Ameambatana na mama yake mzazi mama Nitwa mama mzazi. Yule pale ahsante sana. Tunakutakia mema Miss Dodoma kwenye hatua zinazofuata. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano yupo mwanae ambaye hakumtaja jina yule pale ahsante. Nadhifu kama baba alivyo mambo mazuri sana. (*Makofi*)

Wapo viongozi wa CCM na Jumuiya zake 11 kutoka Jimbo la Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Uzini na Kiongozi wa Msafara ni Bwana Ramadhan Ali Mohamed. Naomba wageni wetu kutoka Uzini Zanzibar wasimame tafadhali. Ahsante sana. Hapa tena tunaona idadi kubwa ya viongozi ni wanawake kutoka Jimbo hilo. Jambo zuri sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Balozi Hamis S. Kagasheki ni kwaya kuu kutoka Usharika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, Bukoba Mjini. Ahsante sana. Hakika mmependeza kweli na kama mpo, inaelekea bado mpo tutapenda kusikia nyimbo zenu. Sisi wengine ni wapenzi wa muziki huo. Viongozi wa Msafara naomba wasimame ni Mchungaji Jackson Ruguma wa Bukoba na Mchungaji Eda Mbambo Mkuu wa Jimbo Dodoma Mjini. Ahsanteni sana. Muendelee na kazi njema ya kuhubiri neno la Mungu kupitia nyimbo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Samuel Chitalilo kutoka Wilaya ya Sengerema ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Sengerema yule pale wote na Mwenyekiti wa Wazazi Diwani Mheshimiwa Kasundwa pamoja na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ambao wameambatana na ndugu Deus Ngelanizwa yule pale. Ahsante sana. Karibuni sana kutoka Sengerema. Naamini ninyi pia ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ambaye anatoka huko huko. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kutoka Jimbo lake la Muyuni ni Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka. Naomba asimame. Wako wengi kumbe. Mheshimiwa Asha. Jumla wageni wako 19. Leo tuna baraka kubwa sana hapa sisi Wabunge kupata wageni kutoka Zanzibar. Tunafurahi kila mara ndugu Zanzibar kuwepo hapa. Sasa kiongozi wa Msafara ni Katibu wa UWT Jimbo la Muyuni Bi. Maliki Salamara. Naomba asimame. Kwa kweli anayesema Tanzania wanawake hawapigi hatua haoni tu. Kiongozi wa Msafara ni Mama, jambo zuri sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Luhahula ni Ndugu Isaac Saliboko ambaye ni mjomba wake na Mheshimiwa Lung'wesula Bebea mpiga kura. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Nyawazwa ambaye ametokea Mwanza Bi. Elizabeth Alex, yule pale. Ahsante karibuni sana. Ahsante sana Wageni wetu.

Sasa ni matangazo ya kazi kwa Wabunge. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane saa 7.00 mchana ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane saa nane mchana leo katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Alhaji Mohammed Missanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anahitaji wajumbe wake wa Kamati hiyo ya Miundombinu mkutane saa 7.00 katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Radhamani Maneno Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mkutane saa saba mchana leo katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii mkutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Waheshimiwa Wabunge Ofisi inatangaza kwamba Maonyesho ya asasi za Kiraia AZAKI yanaendelea pale katika Ukumbi wetu wa Maonyesha na leo kutakuwa na tafrija saa saba mchana ambako mgeni Rasmi atakuwa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Utaratibu na Bunge. Mheshimiwa Philip Marmo. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuzipa nguzu AZAKI Asasa za Kiraia ambazo ni 83 zina maonyesho pale saa saba mchana. Lakini saa saba mchana mambo mengi sana yanagongana pamoja na hili nitakalolisema ambalo nalo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu anatoa mwaliko kwa Wabunge wa Kamati ya Miundombinu lakini pia Waheshimiwa Wabunge wanaopenda kuhudhuria hususani wale wa Mikoa ya Kagera, Rukwa, Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro kule viwanja vya VETA saa saba na nusu. Tutakuwa na sherehe ya kushuhudia utiwaji sahihi wakandarasi zifuatazo za barabara Kagoma, Rusahunga, Sumbawanga Kanazi, Kinazi – Kizi Kibaoni, Lwanjilo Chunya, Magole Turiani, Dumila Ludewa.

Hii haiwezi kuwa ya Iringa nadhani nayo ni ya Morogoro. *Ubungo Bus Teminal* kwenda Kigogo mpaka Kawawa Road Dar es Salaam Mjini, Kawawa Road Round About, Msimbaji Valley, Twiga Jangwani Junction na Korogwe Handeni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hii ni hatua kubwa katika nchi yetu kwamba barabara zote hizi sasa Serikali inaingia mikataba na wakandarasi. Ni vizuri kushuhudia ili muweze kuona. (Makofî)

Waheshimiwa Wabunge, kuna sahihi hapa kuhusu wageni kutoka Muyuni ni wa Dr. Haji Mwita Haji. Huu mwandiko naona wa haraka haraka basi ngoja niliache kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kuwafahamisha kwamba katika michezo iliyochezwa Jumamosi dhidi ya timu ya madaktari wa Mirembe kwanza ni wahakikishie tu kwamba wachezaji wetu wote wako salama. (*Makofi*)

Sasa matokeo ni kama ifuatavyo: Nikianza na *netball* Bunge ilifunga vikapu 28 kwa 8. tunawapongeza sana timu yetu ya *Netball* kwa ushindi huo mnono. Kwenye mpira miguu *football* Bunge goli 1 na Madaktari 0. Nawapongeza sana timu yetu. Kwa kweli imekuwa ni kawaida timu zetu kufanya vizuri kwa sababu Wabunge wa Bunge hili la 9 ni Wabunge makini katika lolote wanadolifanya. Ahsante sana. Huo ndiyo mwisho wa matangazo ya kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, nilitaka kuelezea jambo moja ambalo kwa msemo wa kihabari nimenukuliwa vibaya. Waheshimiwa Wabunge, wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Dr. Willibrod Slaa anawasilisha hoja yake nilichomzuia ni kile kinachohusu Meremeta ambayo ndiyo kampuni iliyohusiana na Jeshi. Tafsiri imejitokeza kwamba nimekataa mambo yote ya Sekta ya Madini wanataja sijui *deep green*, sijui *tangold* na mengine. Hoja hizo bado ziko wazi. Iliyozuiliwa inahu Meremeta ambayo ndiyo tulikaa na Serikali kwenye kikao mahususi kuelezwaa kwa undani kama Kamati ya Uongozi kuhusu hilo. Kwa hiyo isieleweke wazi kwamba Spika alizua kila kitu kinachohusu sekta ya madini. Yale masuala mengine ambayo bado yana utata yanafuatiliwa kwa njia mbalimbali. Nilipenda mfahamu hivyo na baada ya tangazo hilo basi Katibu atuongoze kwa shughuli inayofuata. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mtumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 – Ofisi ya Makamu wa Rais

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira na ile ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa shughuli katika Ofisi ya Makamu wa Rais, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupidisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote viliwyomo duniani, kwa kuniwezesha kusimama hapa kuwasilisha hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliojiunga na Bunge hili kwa kuchaguliwa, nao ni Mheshimiwa Charles Mwera (Tarime), Mheshimiwa Mchungaji Lackson Ndaga Mwanjale (Mbeya Vijijini) na Mheshimiwa Lorencia Bukwimba (Busanda). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliozuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi kilichopita, na ambao wamezuwezesha kuandaa mipango ya mwaka wa fedha 2009/2010 na kuboresha hoja yangu ambayo naiwasilisha katika Hotuba hii. Napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za Kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai Mbunge, na ile ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa pamoja na ushauri na maelekezo ya msingi, ambapo kwa kiasi kikubwa kimesaidia sana kuimarisha utendaji na ufanisi katika kazi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Ali Khamisi Seif, Mbunge na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge ambao ni Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), kwa ushirikiano na michango yao katika kuboresha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee ziende kwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib Mbunge, Katibu Mkuu Bibi Ruth H. Mollel, Naibu Katibu Mkuu Bwana Mbarak Mohammed Abdulwakil na watendaji katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia, kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wote walotangulia kuwasilisha hoja zao, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge na Waziri wa Fedha Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo Mbunge, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya mipango, uchumi, mapato na matumizi, utumishi na utendaji wa Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa na Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwlomba. Aidha, natoa pole kwa familia ya aliyekuwa Kaimu Mufti, Marehemu Alhaj Sheikh Suleiman Gorogosi na aliyekuwa Mwalimu wangu, Marehemu Profesa Haroub Othman, wote hawa nawaombea pepo ya Mwenyezi Mungu na ajalie familia zao mioyo ya subira. Pia pole nyingi kwa wananchi walioathirika na kupoteza maisha kwa ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2008, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea na utekelezaji wa majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 na Ahadi za Serikali Bungeni za mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, masuala ya Muungano. Kama ilivyo ada, hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, imezingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake katika maeneo makuu mawili yaani masuala ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira endelevu.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake, Ibara 143 ukurasa 167 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza kwamba, nanukuu:

“Ushirikiano wa kiuchumi na kijamii umeanza kuimarika na mfano mzuri wa ushirikiano huo umedhifurika katika utekelezaji wa miradi ya TASAF katika Jamhuri nzima, Bara na Zanzibar. Katika kipindi cha Ilani hii CCM itazielekeza Serikali zote mbili kuanzisha miradi ya kiuchumi, Maingiliano ya kiuchumi ni njia muhimu ya kuimarisha Muungano”.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha miradi ya pamoja inaandaliwa na kutekelezwa pande zote za Muungano ili kuwa na uwiano mzuri wa maendeleo. Miradi na programu za pamoja zinazotekeliza pande mbili za Muungano ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – *TASAF II*. Fedha za kutekeleza mradi huu ni jumla ya dola za Marekani milioni 178.5. Kati ya hizo, dola za Marekani milioni 15 ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dola za Marekani milioni 13.5 ni mchango wa Jamii na dola za Marekani milioni 150 ni mchango kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia Oktoba, 2008 jumla ya Shilingi bilioni 111.6 zilitolewa kwa miradi 4,842 inayotekelawa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Shilingi bilioni 5.3 zilitolewa kwa miradi 318.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Tanzania – *MACEMP*, mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa jumla ya dola za Marekani milioni 51 kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo (*International Development Agency - IDA*) ambalo limetua mkopo wenye masharti nafuu kwa mgawanyo wa asilimia 60 Tanzania Bara na asilimia 40 Zanzibar, pamoja na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environmental Facility -GEF*) ambao umetoa msaada wa dola za Marekani milioni 10 kwa mgawanyo wa asilimia 50 Tanzania Bara na asilimia 50 Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009 mradi wa *MACEMP* ulianza kutekelezwa katika Halmashauri 14 za Ukanda wa Pwani ya Tanzania Bara (Jiji la Tanga, Manispaa za Mtwara-Mikindani, Temeke, Kinondoni na Ilala, Wilaya za Mkuranga, Mkinga, Muheza, Lindi Mjini, Kilwa, Mtwara Vijijini, Pangani, Lindi Vijijini na Bagamoyo). Kwa upande wa Zanzibar mradi huu unatekelezwa katika Wilaya zote kumi ambazo ni Wilaya za Mjini, Magharibi, Kati, Kusini, Kaskazini A, Kaskazini B, Wete, Micheweni, Chake Chake na Mkoani.

Mheshimiwa Spika, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji – *PADEP*. Mradi huu uko katika sekta ya kilimo, unatekelezwa pande zote za Muungano na unafadhiliwa na Benki ya Dunia iliyotoa dola za Marekani milioni 54 kwa mradi wote. Tanzania Zanzibar ilipata dola za Marekani milioni 4.5 na mradi unatekelezwa katika Wilaya 5, tatu za Unguja na mbili za Pemba. Kwa upande wa Tanzania Bara mradi huu unatekelezwa katika Wilaya 32 (rejea kiambatisho Na. 1). Mradi huu ulipaswa kwisha Disemba, 2008 lakini umeongezewa muda hadi Juni, 2010 ili kukamilisha utekelezaji wa mradi na kwa upande wa Tanzania Zanzibar utekelezaji umeongezwa katika Wilaya nne zaidi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni pamoja na Ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvvi katika Bahari Kuu Fumba, Zanziba; Uimarishaji na ukarabati wa njia ya umeme kutoka Dar-es-Salaam hadi Fumba; na Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Pemba za Mzambarauni Takao hadi Finya kilometra 8.3, Mzambarauni Karimu hadi Mapofu kilometra 8.3, Bahanasa Daya mpaka Mtambwe kilometra 13.1, Chwale mpaka Kojani kilometra 2 na Barabara ya Kipangani hadi Kangagani Chwale mpaka Kojani kilometra 2 na Barabara ya Kipangani hadi Kangagani kilometra 3 chini ya ufadhili wa mfuko wa maalum wa Serikali ya Marekani (*Millennium Challenge Account -MCA*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kufuutilia utekelezaji wa siku hadi siku wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano katika kudumisha ushirikiano wa Serikali zote mbili. Aidha, mwaka huu tumeshuhudia Muungano wetu ukitimiza miaka 45 yenye maendeleo katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanayonufaisha wananchi kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni jambo linalojidhihirisha kuwa Muungano wetu umeendelea kudumu na kimsingi umekuwa nyenzo na utambulisho muhimu wa umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi iliratibu vikao viwili vya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kujadili vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Vikao hivi vilifanyika tarehe 8 Julai, 2008 na tarehe 19 Januari, 2009. Vikao viwili vya Mawaziri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilifanyika tarehe 6 Oktoba, 2008 na tarehe 18 Mei, 2009.

Mheshimiwa Spika, vikao hivi vilikuwa ni maandalizi ya vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vikao hivi vilifanyika tarehe 11 Oktoba, 2008 na tarehe 19 Mei, 2009 na vilijadili utekelezaji wa maamuzi na maagizo yaliyotolewa katika vikao vilivyopita. Vikao hivi vilifanyika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua kero za Muungano hoja tatu zimejadiliwa na kupatiwa ufumbuzi kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sheria Na. 7 ya mwaka 2001 iliyorekebishwa mwezi Oktoba, 2006 zimeshakamilika. Aidha, Taarifa ya utekelezaji ya kazi za Tume ya mwaka 2006/2007 imewasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu Zanzibar;

(ii) Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu iliyofanyiwa marekebisho na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari, 2007 zimekamilika na kuthibitishwa na Serikali zote mbili tayari kwa utekelezaji. Kwa sasa Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ni moja; na

(iii) Uanachama katika *International Maritime Organisation* (IMO) ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo baada ya mashauriano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na IMO, Zanzibar sasa inayo mamlaka yake ya usafiri majini (*Zanzibar Maritime Administration*) ambayo inatekeleza baadhi ya majukumu kulingana na mikataba ya kimataifa chini ya usimamizi wa Serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi ni kama ifuatavyo:-

(i) Utaratibu wa kuchangia gharama na kugawana mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Mshauri Mwelekezi anakamilisha taarifa yake ili aweze kuiwasilisha Serikalini;

(ii) Miradi minane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imeingizwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuombewa ufadhili inaendelea kufanyiwa kazi. Miradi minne ya kikanda kati ya minane imepewa kipaumbele kwa ajili ya kuandaliwa andiko la miradi, usanifu na tathmini ya gharama tayari kwa kuombewa fedha za utekelezaji. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar; Mradi wa Uendelezaji wa Bandari ya Maruhubi na Uendelezaji wa Miundombinu katika Ukanda wa Bahari Kuu- Ujenzi wa Bandari Kavu; Mradi wa Ukuzaji wa Zao la Taifa na Karantini ya Wanyama na Programu ya kuifanya Zanzibar kuwa eneo huru la milipuko ya maradhi ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, miradi minne ya kitaifa ambayo iko katika hatua mbalimbali za matayarisho ni; Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Njia ya Upopo, Programu ya Kilimo na Chakula, Uratibu wa Magonjwa ya Mifugo Ukanda wa Zanzibar, Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Pemba na Mradi wa usafiri wa boti ziendazo kasi ambao utaunganisha Zanzibar na Pwani ya Afrika Mashariki (*roll on roll off services*; na

(iii) Suala la ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano linaendelea kufanyiwa kazi. Mapendekezo ya kuimarisha ajira katika Taasisi za Muungano yaliandaliwa na Makatibu Wakuu wa pande mbili za Muungano na kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 19 Mei, 2009 na kuridhiwa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo yapo katika hatua za awali za kushughulikiwa na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni pamoja na:- Malalamiko ya wafanyakishara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki; uwezo wa SMZ kukopa nje ya nchi; faida ya Benki Kuu na misaada kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalotokana na mchango wa Wahisani kwa misaada isiyokuwa na masharti kwa Tanzania. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitengewa Shilingi bilioni 23. Hadi kufikia Mei, 2009, Shilingi bilioni 23.5 zilikwishatolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwa na ongezeko la shilingi milioni 517. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichangia Shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya Mradi wa Umeme kutoka Pangani Tanga kwenda Pemba.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusu Muungano. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Ofisi iliendelea kuchukua hatua za makusudi katika kukuza weledi wa umma katika masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa kushiriki katika maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika mwezi Agosti 2008 Mkoani Dodoma na kuandaa maonyesho maalumu katika viwanja vya Bunge kuanzia tarehe 19 hadi 20 Agosti, 2008.

Aidha, Ofisi ilishiriki katika maonyesho ya 21 ya Wiki ya Maji yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Kagera kuanzia tarehe 16 hadi 22 Machi 2009, Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni 2009 na maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Tabora kuanzia tarehe 1 hadi 5 Juni 2009.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanapata habari za masuala ya Muungano, vipeperushi 25,000 viliandaliwa, kuchapishwa na kugawiwa wakati wa maonyesho na siku za Kitaifa na kwa wadau wengine. Nakala 500 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilichapishwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, vipindi 40 vya redio na 16 vya luninga viliandaliwa na kurushwa hewani kuanzia mwezi Februari, 2009, vipindi hivyo hurushwa hewani kila siku ya Jumatano. Aidha, vipindi vya luninga vilianza kurushwa kila siku ya Jumanne kuanzia tarehe 21 Aprili, 2009 kupitia *TBC1*.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha sherehe za Muungano, Ofisi ilifanya mahojiano na wananchi wa pande mbili za Muungano kuhusu miaka 45 ya Muungano kwa ajili ya uandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma. Jumla ya watu 90 walihojiwa; vipindi 8 maalumu vya redio vilirushwa hewani kupitia TBC Taifa, Redio Uhuru na Redio Zenji FM na vipindi 6 maalumu vya luninga vilirushwa hewani kupitia, TBC1, TVZ, Channel Ten na Star TV. Makala za Muungano zilitolewa katika magazeti ya Habari Leo, Zanzibar Leo, Uhuru na Majira. Aidha, Ofisi ilifanikiwa kuwaleta Mashuhuda wa Muungano katika Maadhimisho ya miaka 45 ya Muungano na walipata nafasi ya kufanya mahojiano na vyombo vya habari. Lengo la kuwaleta mashuhuda hao lilikuwa ni kuwafanya Watanzania waelewe historia ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano. Mbali na kushughulikia masuala ya Muungano, Ofisi inaratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuongeza ushirikiano kwa pande zote mbili katika masuala ya kisera, kubadilishana utaalamu na watalamu, ushiriki katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi itaratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano. Vikao hivi vitatanguliwa na vikao vya Makatibu Wakuu wa pande mbili za Muungano na vikao vya Mawaziri wa pande mbili za Muungano. Aidha, Ofisi itaratibu utekelezaji wa maamuzi ya vikao hivyo na kuandaa taarifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uelewa wa wananchi juu ya mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano Ofisi itaandaa Jarida la Muungano wetu, vipindi vya

redio na luninga, makala za magazeti, vipeperushi na kushiriki katika maonyesho ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria na mambo yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano. Aidha, Ofisi itaendelea kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba Sekta, Wizara na Asasi zisizo za Muungano zinakutana angalau mara nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na uharibifu wa mazingira na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii mtambuka, hususan athari zinazotokana na Mabadiliko ya Tabianchi, Serikali imeendelea kutekeleza Sera, Mikakati, Sheria na Kanuni zinazolenga kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali na maliasili katika shughuli zetu za kila siku, ili kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii na mazingira endelevu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mtikisiko katika Mfumo wa Fedha Duniani uliosababisha kudorora kwa uchumi mwaka huu, dunia pia inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na janga na athari mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza na zinazotarajiwa kujitokeza, Umoja wa Kutokana na janga na athari mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza na zinazotarajiwa kujitokeza, Umoja wa Mataifa umetangaza mwaka huu kuwa Mwaka wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Lengo ni kukuza ufahamu kuhusu janga na athari za mabadiliko ya tabianchi, kukuza ubunifu wa kuhimili athari hizi; kuweka mikakati ya kitaifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kushirikisha wadau wote nchini; na kukuza ushirikiano wa kimataifa kuhusu janga hili.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2005 na Utekelezaji Wake. Ibara ya 112 ukurasa wa 138-139 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaelekeza kwamba, nanukuu;

(a) “*Kuendeleza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa wao kuhusu hifadhi ya mazingira*”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeandaa Programu ya Kitaifa ya Elimu kwa Umma. Programu hii imeanza kutekelezwa kwa kutumia vyombo vya habari, kuendesha mafunzo, kutoa makala, machapisho na kushiriki katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu hifadhi ya mazingira kama Siku ya Ardhi-oevu, Siku ya Wakulima-Nanenane, Siku ya Mazingira Afrika na Siku ya Mazingira Duniani. Pia elimu ya mazingira imeendelea kutolewa kuititia waratibu na maafisa mazingira ili waweze kutoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira, kanuni tisa (9) zimeandaliwa, miongozo mitatu (3) inaendelea kukamilishwa. Aidha, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji unatekelezwa na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa utaanza

kutekelezwa. Vile vile, Ofisi imeratibu na kutekeleza miradi na programu kama vile Programu Endelevu ya Ziwa Tanganyika; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Kihansi; Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani na Bahari na Mradi wa Kuteketeza Madawa Chakavu na Viuatilifu.

(b) “*Kuhamasisha na kuwezesha utumiaji wa matanuri ya kisasa ya kuchomea mkaa yenye sifa ya kupunguza upotevu wa miti*”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na TaTEDO na wadau wengine ilitoa mafunzo ya matumizi ya tanuru la kisasa aina ya *Half Orange* kwa wachoma mkaa 120 katika wilaya za Rufiji, Muheza na Kilindi. Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya tanuru la kisasa aina *Rocket Burn* la kukaushia tumbaku katika Mikoa ya Tabora na Ruvuma ulifanyika kwa kushirikiana na Kampuni ya Sigara Tanzania. Aidha, utafiti umeonyesha kwamba tekinolojia hii imeweza kupunguza matumizi ya kuni kutoka tani 9 hadi tani 4.5 kwa kukausha tumbaku inayovunwa kutoka ekari moja. Wakulima na makampuni yamehamasishwa kuanzisha mashamba ya miti kwa lengo la kupunguza matumizi ya misitu asilia.

(c) “*Kutazama uwezekano wa kutumia mkaa ya mawe kwa kupikia*”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za Kijamii, imeendelea kuhamasisha utumiaji wa mkaa ya mawe kwa matumizi mbalimbali kama kupikia. Kutokana na uhamasishaji huu jamii na taasisi kama vile Magereza, hospitali na shule zimeanza kutumia nishati hii. Mgodi wa Kiwira, Mbeya na sekte binafsi wamehamasika na kuanza kutengeneza nishati aina ya Briketi kutokana na mkaa ya mawe (Kwa mfano kampuni ya *Space Engineering* kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia). Aidha, tafiti zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha matumizi yake yanakuwa salama kwa mazingira na afya ya binadamu.

(d) “*Kuhamasisha matumizi ya majiko yenye kutumia mkaa/kuni kidogo*”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na makampuni binafsi na vikundi vya kijamii inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia majiko banifu kwa matumizi ya nyumbani. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na wadau ilishiriki katika maadhisho mbalimbali ya Kitaifa ambapo maonyesho ya matumizi ya majiko banifu yalifanyika. Mikakati inafanyika kuingiza misaada ya majiko banifu kwa vikundi vya jamii kuititia miradi ya kupunguza gesijoto kwa kuzuia uharibifu wa misitu (*Reduced Emissions from Deforestation and Degradation in Developing Countries-REDD*).

(e) “*Kujenga mwamko katika jamii wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi*”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na jinsi ya kukabiliana nayo. Elimu hii imetolewa kuititia warsha, vyombo vya habari, makala, maonyesho na maadhisho ya siku za

kitaifa zinazohusu mazingira. Katika maadhisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu, ujumbe ulioongoza maadhisho ni “*Wananchi Tuungane Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi*”. Aidha, Ofisi inahamasisha wananchi kuandaa na kutekeleza miradi ya ushirikiano na mashirika ya kimataifa kwa lengo la kupunguza gesijoto (*Clean Development Mechanism-CDM*) na kuleta maendeleo endelevu chini ya Mkataba wa Kyoto pamoja na majoribio ya kukausha samaki kwa kutumia gesi asilia Mkoani Dar es Salaam katika soko la samaki Feri ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Vile vile, Ofisi inaratibu Mradi wa Kupunguza gesijoto kwa kuzuia uharibifu wa misitu *REDD* kwa kuhamasisha wananchi kupanda na kutunza miti.

(f) “Kuendeleza kampeni ya upandaji miti ambayo imekuwa ikifanywa kila mwaka na kuhakikisha kwamba miti inayopandwa inatunzwa ipasavyo na kuhimiza tabia ya kutokukata miti ovyo”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya upandaji miti. Kwa mujibu wa taarifa ya kipindi cha mwaka 2007/2008 jumla ya miti 245,970,955 ilipandwa na miti 213,872,564 iliota sawa na asilimia 87 ya miti iliyopandwa. Jumla ya Wilaya 43 zimevuka lengo la kupanda miti milioni moja na nusu (1,500,000), lengo lililoainishwa kwenye Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji (rejea kiambatisho Na 2).

(g) “Kutoa elimu kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa wananchi”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza imeendelea kutoa elimu kwa umma kuitia warsha, vyombo vya habari, makala mbalimbali na kwenye maonyesho ya maadhisho mbalimbali. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Baraza imetua mafunzo yahusuyo usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa maafisa mazingira walioteuliwa katika Jiji, Manispaa na Halmashauri za Wilaya katika kanda za Ziwa, Kusini na Magharibi; na mahakimu wakazi wa Kanda ya Ziwa. Lengo kuu la mafunzo haya lilikuwa ni kuainisha majukumu ya watendaji wakuu wa Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

(h) “Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka ngumu ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuitia vyombo vya habari, makala katika magazeti na majorida na kwenye maadhisho ya sikukuu za kitaifa na kimataifa zinazohusu mazingira. Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na SUMATRA, Ofisi iliendesha kampeni ya usafi na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kukusanya na kutenganisha taka kwenye vyombo vya usafiri. Aidha, elimu hii ilitolewa kwa maafisa wa Polisi katika jiji la Dar es Salaam. Ili kuwa na mpango endelevu wa usimamizi wa taka nchini, Ofisi inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka kwa kushirikiana na wadau. Pia, Ofisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imesaini makubaliano ya mashirikiano na Jeshi la Polisi katika usimamizi wa hifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira nchini.

(i) “Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vitakavyotumia taka ngumu kama malighafi”.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali imeendelea kuhamasisha utekelezaji wa mikakati ifuatayo: Kuchakata bidhaa chakavu ili kutengeneza malighafi ya viwanda vingine; kutumia taka ngumu kuzalisha vitofali (*briquettes*) kwa ajili ya nishati viwandani na katika sehemu za biashara; kuzalisha nishati ya umeme kutokana na mabaki ya taka; na kutumia taka ngumu kuzalisha bidhaa

nyingine. Naomba nichukue nafasi hii kuhimiza makampuni yanayozalisha taka kujenga dhana ya kupunguza, kutumia tena na kurejeleza taka kama njia salama ya kulinda na kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kufikiwa kwa malengo ya Milenia na yale ya MKUKUTA, umetoa msukumo kwa Serikali kuendelea kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu. Tafiti zimeonyesha kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya kiwango cha umaskini na uharibifu wa mazingira. Katika kukabili ana changamoto za hifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi imeendelea kutekeleza Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Act-Implementation Support Programme-EMA-ISP*) iliyoanza mwaka 2007. Katika kipindi hiki kanuni zifuatazo zinaendelea kuandaliwa:- Kanuni za Usimamizi wa Taka za Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu (*Persistent Organic Pollutants -POPs*); Kanuni za Viwango vya Kudhibiti Kelele na Uchafuzi unaotokana na Mitikisiko (*Standards for control of noise and vibration pollution*); Kanuni za Nyenzo za Kiuchumi (*Economic Instruments Regulations*); Kanuni za Udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira (*Integrated Prevention and Control of Pollution Regulations*); Kanuni za usimamizi wa majitaka ya Viwandani (*Treatment of Hazardous and non Hazardous liquid waste from industries Regulations*); na Kanuni za Wakaguzi wa Mazingira (*Environmental Inspectors Regulations*).

Mheshimiwa Spika, aidha, rasimu ya Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Mazingira ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa (*Guidelines for Environmental Action Plan for MDAs and Local Government Authorities*) na rasimu ya Mwongozo wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano zinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuelimisha umma juu ya Sheria ya Usimamizi Mazingira, Ofisi ilianda na kusambaza kwa wadau vipeperushi 10,000 vinavyohusu Viwango vya Ubora wa Mazingira katika Maji, Hewa na Udongo; Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji; Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa; na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Taka. Vile vile ilichapisha na kusambaza kalenda 1500 zenye ujumbe wa uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga uwezo wa kiutendaji wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuititia programu ya *EMA-ISP*, jumla ya maafisa kumi na mbili (12) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika kituo cha ESAMI, Arusha. Mafunzo haya yalihusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira; Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira; Uchambuzi wa Sera za Mazingira; na Mbinu za Majadiliano katika Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Kwa kushirikiana na TAMISEMI, chini ya Programu ya Maendeleo Mijini na Usimamizi wa Mazingira (*Urban Development and Environmental Framework –UDEM*) Ofisi imetoea mafunzo kwa waratibu wa Mazingira wa UDEM

kutoka Manispaa na Miji 33 kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sera ya Taifa ya Mazingira. Aidha, Ofisi iliandaa na kusambaza vipeperushi 5000 vyenye kuainisha nafasi ya serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Vile vile rasimu ya mwongozo wa kuandaa taarifa ya hali ya Mazingira kwa Serikali za Mitaa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, inamtaka Waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa mazingira, kuwasilisha Bungeni ripoti ya hali ya mazingira kila baada ya miaka miwili. Katika kutekeleza matakwa haya, Ofisi kwa kushirikiana na wadau wengine katika kipindi cha mwaka 2008/2009 imekamilisha Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini. Madhumuni ya ripoti hii ni pamoja na kusaidia katika kutoa maamuzi sahihi kuhusu kukabiliana na changamoto za mazingira katika juhudzi za kuleta maendeleo endelevu. Aidha, ripoti hii imeonyesha hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto za mazingira ikiwa ni pamoja na mikakati na mipango iliyopo. Pia imechambua jinsi mabadiliko ya mazingira na ikolojia hususan kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri sekta muhimu za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ardhi, mifugo, misitu, wanyamapori, urithi wa utamaduni, madini, nishati na maji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itaendelea na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, miongozo na kanuni itakamilishwa na kusambazwa kwa wadau. Vile vile, Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini itatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau ili waweze kutumia kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika maeneo yao. Nachukua fursa hii kuwaomba waheshimiwa Wabunge kushirikiana na wadau kutumia taarifa hii kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Spika, mazingira na umaskini, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Kujumuisha Masuala ya Mazingira katika utekelezaji wa MKUKUTA iliyanza Septemba, 2007. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi kupitia programu hii imetekeliza shughuli zifuatazo: kuandaa Mwongozo wa Mafunzo ya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (*Training Modules for Strategic Environmental Assessment*); kuwezesha mafunzo kwa watumishi 42 wa Wizara na Serikali za Mitaa kutoka mikoa 17 kuhusu uzingatiaji wa uhusiano wa mazingira na umaskini katika mipango yao na utekelezaji wa MKUKUTA; kutoa elimu ya mazingira kupitia vipindi vya redio na luninga, vipeperushi na majarida; kutoa mafunzo kwa Asasi 40 za Kijamii zinazojishughulisha na Umaskini na Mazingira katika maeneo ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati; kukusanya na kuchambua takwimu za umaskini na mazingira ili kusaidia utekelezaji wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekeliza ni kufanya tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika kilimo, ufugaji na hifadhi ya vyanzo vya maji katika Wilaya za Monduli- Arusha, Meatu-Shinyanga, Iramba-Singida na Chamwino-Dodoma; kuendesha warsha za mafunzo kwa wajasiriamali wa bidhaa zitokanazo na mazao ya asili kutoka Mikoa kame ya Manyara,

Dodoma, Singida na Shinyanga juu ya kuboresha mazao yao, kuyaongeza thamani na kutafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, chini ya Programu hiFi kazi zifuatazo zitafanyika:- Kuwezesha wakufunzi wa serikali za mitaa kuendesha mafunzo ya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira katika Halmashauri zao. Ushirikishwaji wa wadau wa mazingira katika maandalizi ya awamu ya Pili ya MKUKUTA ili kuhakikisha kuwa vipaumbele vyao vinajumuishwa; kutafiti jinsi sera zinazohusiana na ufugaji zinavyowiana na utunzaji mazingira; kuendelea kuelimisha jamii kwa kutumia majorida, vipeperushi, vipindi vya redio na luninga juu ya uhusiano wa umaskini na mazingira; na ukusanyaji wa takwimu zinazohusiana na umaskini na mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo katika Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira kuhusu Kupunguza Umaskini, unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (*UNEP*). Katika kipindi hiki, Asasi 12 zinazojishughulisha na hifadhi ya mazingira na shughuli za kuondoa umaskini katika Mikoa ya Kagera, Dodoma, Singida, Mara, Mwanza, Pwani na Mtwara ziliendelea kutekeleza miradi midogo midogo ya kijamii katika ngazi za vijiji chini ya ufadhili wa *UNEP*.

Mheshimiwa Spika, Kazi zilizotekelawa chini ya miradi hii ni pamoja na uanzishaji wa bustani za miche ya miti ya aina mbalimbali, uchimbaji wa visima, kilimo-mseto, kukinga na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika maeneo ya kilimo na uhamasishaji wa jamii kuhusu hifadhi ya mazingira na kuondoa umaskini. Mradi huu umekamilika mwezi Disemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Ofisi itafuatilia utekelezaji wa miradi midogo midogo iliyofadhiliwa na mradi huu ili kuhakikisha miradi inakuwa endelevu hata baada ya muda wa ufadhili kwisha.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Taifa ya Upandaji Miti. Nachukua fursa hii kuzipongeza wilaya zilizovuka lengo kama ilivyoolezwa katika aya 34 ya hotuba hii (rejea kiambatisho Na.2). Aidha, natoa wito kwa halmashauri ambazo hazikuweza kufikia lengo hili ziongeze juhudii katika upandaji na utunzaji miti. Katika mwaka 2009/2010 ufuutiliaji wa taarifa za utekelezaji wa Kampeni hii utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti umekamilika. Aidha, Mwongozo huu umetafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza, umechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itaanza kuratibu mashindano hayo kwa kuhamasisha wananchi na Taasisi ili kushiriki. Aidha, katika kipindi hicho mchakato wa kuwapata washindi utafanyika na hatimaye Tuzo ya Rais itaanza kutolewa kila baada ya miaka miwili katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Sambamba na hili, elimu ya Mazingira itaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi ilishirikiana na Manispaa ya Ilala kuandaa Rasimu ya Mkakati wa Kudhibiti Uchafuzi na Kuboresha mandhari ya Manispaa ya Ilala. Rasimu hii itawasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni yao. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi kwa kushirikiana na Manispaa ya Ilala itafutilia ukamilishaji wa mkakati na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Kama nilivyolarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana maandalizi ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa yamekamilika. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Mkakati huu umetafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza. Aidha, warsha mbili (2) za kikanda za wadau za uhamasishaji wa jamii kuhusu nafasi ya Sekta, Halmashauri na Wananchi katika utekelezaji wa Mkakati zimefanyika kanda ya ziwa ikihusisha mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga na kanda ya Magharibi ikihusisha ya mikoa ya Kigoma, Rukwa na Tabora. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Ofisi itaendelea kuratibu, kufutilia na kuhamasisha wadau kushiriki kwenye utekelezaji wa mkakati.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendelea na uratibu wa utekelezaji wa Programu Endelevu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika inayohusisha nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Mamlaka ya Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika ilizinduliwa rasmi mnamo tarehe 19 Disemba 2008, Jijini Bujumbura. Tanzania, tayari imechangia dola za Marekani 303,900 kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika. Aidha, mradi wa Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (*Catchment*) ambao ni msaada wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) umeanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Novemba 2008. Katika utekelezaji wa mradi, Ofisi imeunda Kamati ya uendeshaji wa mradi ambayo inajumuisha wajumbe kutoka mikoa ya Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, warsha ya wadau ya uzinduzi wa Programu Endelevu ya Hifadhi ya Ziwa Tanganyika ilifanyika Kigoma mwezi Januari 2009 kwa lengo la kupitia rasimu ya mpango wa kazi na bajeti kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Aidha, ukarabati wa Ofisi tano (5) za mradi zilizopo katika jengo la Mkuu wa Mkoa Kigoma ulifanyika, pamoja na ununuzi wa samani za Ofisi na magari mawili (2) ya mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga uwezo wa usimamizi wa majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji utakaogharimu Euro milioni 6 toka *NORDIC Fund* na Mradi wa uendelezaji wa uvuvi na hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika utakaogharimu dola za Marekani milioni 7.4 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) umeanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Juni, 2009; tayari Dola za Marekani 270,000 zimetolewa na AfDB kwa ajili ya utekelezaji. Miradi hii inatekelezwa kwa pamoja katika Mikoa ya Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Endelevu ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika. Mradi wa Hifadhi ya Bonde unaofadhiliwa na UNDP/GEF utatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma (KUWASA) na Manispaa ya Kigoma-Ujiji katika masuala ya usimamizi wa maji taka na watendaji wa Halmashauri na Manispaa za Mikoa ya Kigoma na Rukwa kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira ya bonde la Ziwa Tanganyika;

(ii) Kuwezesha Serikali za vijiji kuanzisha Kamati za Mazingira za vijiji na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, misitu na kuendeleza njia za asili za kuhifadhi mazingira; na

(iii) Kuendesha kampeni za hifadhi ya mazingira katika mikoa ya Kigoma na Rukwa.

Aidha, Ofisi itaendelea na uratibu wa utekelezaji wa miradi miwili (2) inayolenga kujenga uwezo wa usimamizi wa majitaka katika manispaa ya Kigoma ujiji na uvuvi endelevu katika Ziwa Tanganyika kwa mikoa ya Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Nile. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya hifadhi ya mazingira ya bonde la Mto Nile. Programu hii inatekelezwa kwa pamoja na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya, Ethiopia, Misri na Sudan. Lengo la Programu hii ni kujenga uwezo na mfumo wa ushirikiano katika kusimamia, kuhifadhi na kulinda mazingira ya bonde la Mto Nile kwa kutoa elimu ya mazingira kwa umma; hifadhi ya ardhi oevu na bioanuai na ufuutilaji wa hali ya ubora wa maji katika bonde la Mto Nile. Programu hii inatekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*GEF*) kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Maendeleo la Canada (*CIDA*) na itagharimu jumla ya dola za Marekani milioni 3.6 hadi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi ya ardhi oevu na bioanuai katika mikoa ya Mwanza na Mara kwa kuhusisha miradi midogo midogo ya hifadhi ya mazingira. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi na matumizi endelevu ya fukwe za Ziwa Victoria katika wilaya ya Bunda na mradi wa kuhifadhi ardhi, msitu na udongo katika Shule ya Sekondari Shibula, Wilaya ya Ilemela. Miradi hii itatekelezwa kwa jumla ya dola za Marekani 78,876. Mradi pia umewezesha mafunzo ya mwezi mmoja nchini Kenya kuhusu hifadhi ya maeneo ya ardhi oevu kwa watumishi wawili (2), mmoja kutoka TANAPA na mwagine kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Aidha, Mpango endelevu wa mradi unaojumuisha elimu ya mazingira umeandalifi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 shughuli zitakazotekelizwa ni pamoja na kuhusisha shughuli za mradi katika majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kuendesha warsha za wadau ili kuainisha majukumu yao katika utekelezaji endelevu wa mradi baada ya muda wake kumalizika ifikapo Septemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa, katika mwaka 2008/2009, kufuatia majadiliano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Benki Dunia kuhusu hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa, Ofisi iliandaa wazo la mradi (*Project Concept*) na kulijadili pamoja na wadau kutoka Wizara za Maliasili na Utalii, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Maji na Umwagiliaji, Kilimo, Chakula na Ushirika na Fedha na Uchumi ambazo kwa pamoja ziliunda kikundi kazi kitakachofuatalia utekelezaji wa programu ya hifadhi ya Bonde la Ziwa Nyasa. Aidha, Ofisi iliendesha kikao cha pamoja mjini Dodoma mwezi Aprili, 2009 ikihusisha Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili, Mazingira na Wizara za Kiseka na mshauri kutoka Benki ya Dunia aliyekuwa amefanya mazungumzo na Nchi za Malawi na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara husika itakamilisha andiko la mradi wa hifadhi ya bonde la Ziwa Nyasa. Aidha, itaratibu na kuandaa vikao vya wadau pamoja na kikundi kazi ili kubaini maeneo ya kipaumbele katika programu hii hapa nchini pamoja na kukuza uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kuhusu mchakato wa kuandaa makubaliano mapya ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (*Bali Road-Map*) utakaokamilishwa huko Denmark, Disemba, 2009. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Tanzania imeandaa msimamo wa nchi, hususan katika kuhakikisha kuwa masuala muhimu kwa nchi yetu yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, masuala muhimu kwa nchi yetu ni yafuatayo; upatikanaji wa fedha za kutosha na za ziada, mbali ya misaada ya kawaida ya maendeleo (*ODA*) kwa njia inayotabirika, inayopimika na endelevu kuhusu mabadiliko ya tabianchi; upatikanaji wa misaada ya kifedha na tekinolojia kuhusu kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuweka mfumo kamili fuwa utekelezaji wake; mfumo wa kutoa motisha kwa ajili ya kuhifadhi misitu, kudhibiti uharibifu wake na usimamizi endelevu wa misitu; kuanzisha mfuko wa kimataifa wa kutoa tuzo na motisha kwa ajili ya kuhifadhi misitu, usimamizi endelevu wa misitu na kudhibiti uharibifu wake; upatikanaji wa misaada ya kupata tekinolojia mpya na kukuza tekinolojia nchini na kujenga uwezo wa kitaalam na nyenzo za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi nakudhibiti uzalishaji wa gesijoto; na kuboresha matumizi ya mfumo wa miradi ya CDM kwa kurahisisha taratibu zake ili kutoa mchango wake katika kuleta maendeleo endelevu nchini. Vile vile kuendelea kuhimiza nchi zilizoendelea kupunguza uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 40 ifikapo mwaka 2020 na kwa asilimia 80 hadi 95 ifikapo mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha uwezo wa nchi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Ofisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa inatekeleza Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Denmark kwa jumla ya shilingi bilioni 1.0. Katika kipindi hiki, shughuli zifuatazo zimetekelizwa: kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 30,000 za vitini kuhusu dhana na sayansi ya mabadiliko ya tabianchi, upunguzaji wa gesijoto na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kuandaa na kusambaza nakala 2,000 za kalenda ya mwaka 2009 yenye ujumbe kuhusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kuyakabili; na nakala 1,000 za kijitabu cha katuni zinazohusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana nayo; kuendesha mjadala kuhusu mabadiliko ya tabianchi ulioshirikisha watendaji na wananchi kutoka Tanzania, Kenya na Uganda, Wanafunzi wa vyuo vikuu vya Mzumbe na Dar es Salaam na Waandishi wa habari; na kufanya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika Mikoa ya Tanga, Mwanza, Dar es Salaam, Pwani, Shinyanga, Manyara, Mbeya pamoja na mikoa yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kuhusu kusainiwa kwa Mkataba wa Ushirikiano kati ya Serikali ya Norway na Tanzania ambapo Norway iliahidi kutoa jumla ya dola za Marekani milioni 100 ili kushughulikia suala la

mabadiliko ya Tabianchi katika sekta ya misitu kwa kipindi cha miaka mitano (5). Msaada huu unalenga kuisaidia nchi yetu kubaini njia bora ya kutoa motisha kwa wananchi na taasisi mbalimbali zinazotunza na kuhifadhi misitu; kuanzisha mfuko wa fedha kwa ajili ya suala la upunguzaji wa gesijoto itokanayo na ufyekaji na uharibifu wa misitu *REDD*, kwa ajili ya kusaidia shughuli za *REDD* nchini ikiwa ni pamoja na kununua hewamkaa inayonyonywa na miti inayotunzwa katika misitu mbalimbali nchini. Fedha hizi pia zitasaidia kuweka mfumo bora na madhubuti wa soko na biashara ya hewamkaa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na juhudni za uhifadhi wa misitu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya kubaini miradi mbalimbali kufuatia makubaliano ya ushirikiano wa Tanzania na Norway imeanza. Kikundi kazi cha kitaifa kinachoshirikisha wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira-Zanzibar; na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeundwa ili kuratibu shughuli za utayarishaji wa Mkakati wa Taifa kuhusu *REDD* na shughuli nyingine zinazohusiana na *REDD* nchini. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizobainishwa kwenye mkataba zitatolewa kwa Serikali za Mitaa, Asasi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali zitakazowasilisha miradi inayokidhi vigezo vilivywerekwa na watalaamu.

Mheshimiwa Spika, ili kuratibu na kusimamia vyema suala la Mabadiliko ya Tabianchi nchini, Ofisi imeanzisha kamati mbili za kitaifa za mabadiliko ya tabianchi. Kamati hizi ni Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*National Climate Change Technical Committee-NCCCTC*) na Kamati Elekezi ya Kitaifa kuhusu mabadilko ya Tabianchi (*National Climate Change Steering Committee-NCCSC*). Wajumbe wa kamati hizi ni sekta, taasisi za serikali pamoja na wawakilishi wa sekta binafsi, vyombo vya habari na mashirika yasiyo ya kiserikali. Kamati hizi zimeanza kazi Machi, 2009. Aidha, Mradi wa kutekeleza baadhi ya shughuli za Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Adaptation Programme of Action–NAPA*) wenye thamani ya Shilingi bilioni 3 umewasilishwa katika Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kwa ufadhili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendesha semina kwa waandishi wa habari, maafisa mazingira wilayani, tawala za mkoa na taasisi zisizo za kiserikali pamoja na Wataalamu wa sheria na vyuo vya elimu ya juu ili kukuza weledi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhusiano wake na juhudni za kupunguza umasikini nchini. Katika semina hizi vitini kuhusu Mkataba vilisambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha fedha 2009/2010 Ofisi itafanya mapitio ya Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ili pamoja na mambo mengine kupata makadirio ya gharama za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kwenye Programu hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Kyoto, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, miradi miwili (2) imekamilishwa na kuwasilishwa katika Bodi ya kimataifa ya *Clean Development Mechanism - CDM* kwa ajili ya kuidhinishwa. Miradi hii ni Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara unaotekelizwa na Kampuni ya Artumas na Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia mabaki ya Mkonge, Hale Tanga.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza weledi wa wadau wa mazingira kuhusu *CDM*, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi iliendesha Semina mkoani Iringa kuhusu upandaji miti kama sehemu ya juhudzi za kupunguza gesijoto chini ya mfumo wa Miradi ya *CDM*. Aidha, nakala za Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi ya *CDM* nchini zimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, juhudzi zaidi zitaelekezwa katika kuimarisha weledi wa Taasisi na watumishi wa Serikali na Makampuni binafsi ili kujenga uwezo wa kuandaa na kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Mpango maalumu wa Afrika wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*TerrAfrica*) ambao uliipatia Tanzania dola za Marekani milioni 3 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi unaohusu maendeleo endelevu ya ardhi katika mkoa wa Kilimanjaro umeanza kutekelezwa. Serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wadau, taasisi za kijamii pamoja na wataalamu toka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na wale wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Kilimo-Mseto (*ICRAF*) wamekutana na kuainisha maeneo yatakayohusika katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa mradi huu. Aidha, wananchi na wadau wengine watashirikishwa kwa ukaribu zaidi ili waweze kunufaika na matokeo mazuri ya mradi wa matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha wa 2008/2009 Ofisi ilipanga kuitia upya maeneo ya kipaumbele chini ya Programu ya Taifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*National Action Plan to Combat Desertification – NAP*) ili yaendane na Mpango Mkakati wa miaka kumi (2008/2018). Mpango huu ulipitishwa na Mkutano wa Nane wa Nchi zilizoridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*United Nations Convention to Combat Desertification-UNCCD*) Septemba, 2007 huko nchini Hispania. Sekretarieti ya Mkataba huu sasa inakamilisha miongozo itakayotumiwa na nchi wanachama wakati wa kuitia maeneo ya kipaumbele ya NAP. Miongozo hiyo inatarajiwa kukamilika na kuitishwa na mkutano wa nchi zilizoridhia mkataba utakaofanyika Septemba, 2009 huko Buenos-Aires, Argentina. Uamuzi huu wa kuwa na miongozo ulifikiwa ili kuepusha uwezekano wa nchi kutofautiana wakati wa kufanya mapitio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi kwa kushirikiana na taasisi ya *Global Mechanism* inayohusika na utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkataba Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya

Jangwa na Ukame (*UNCCD*) itaendesha semina kwa kuwashirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Ofisi iliendelea na uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi wa Mazingira. Kutokana na juhudzi za wananchi mafanikio yafuatayo yamepatikana: Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (*Wildlife Management Areas- WMAs*) 16 zimeanzishwa na kati ya hizo Jumuiya 10 zimeshaptishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Wanajumuiya wamekuwa mstari wa mbele katika kulinda maliasili katika maeneo yao kwa kukamata wahalifu na vifaa vyao na kuwafikisha katika vyombo vyia sheria. Aidha, wanajumuiya wameanza kunufaika kutokana na mapato yanayotokana na utalii wa picha na uwindaji wa kitalii, mfano mwaka 2007/08 Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge-Babati ilipata shilingi milioni 76 na Jumuiya ya Ipole-Sikonge shilingi milioni 21.15.

Mheshimiwa Spika, Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira. Katika Uchimbaji Madini katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi imeendelea kuratibu mchakato wa utoaji wa Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika Uchimbaji wa Madini. Mchakato wa kumpata mshindi wa tuzo hii umekamilika. Aidha, miongozo na vigezo vyia ushindani vimefanyiwa marekebisho ili kuhakikisha makampuni ya uchimbaji madini na watu binafsi wanaojishughulisha na uchimbaji madini wanashiriki. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi itaendelea kuratibu mchakato wa kuwapata washindi wa tuzo hii ambayo ni muhimu katika utunzaji wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Cartagena unaohusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari zitokanazo na bioteknolojia ya kisasa. Aidha, Ofisi inaendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa. Katika utekelezaji wa mradi huu nyenzo muhimu za usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa zimeandaliwa. Nyenzo hizo ni:-

(i) *Manual for Risk assessment and Risk management* kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira zinazoweza kusababishwa na mimea, bidhaa na viumbwe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki;

(ii) *Manual for Contained and Confined trials* kwa ajili ya kuendesha majaribio yanayohusu mimea, bidhaa na viumbwe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki (GMOs);

(iii) Mwongozo kuhusu utaratibu wa maombi ya uingizaji wa mimea, bidhaa, viumbwe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki; na

(iv) Utaratibu wa utambuzi wa mimea, bidhaa na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, warsha mbili (2) za kikanda zimefanyika ili kutoa elimu na kukuza weledi kwa wadau mbalimbali kuhusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari zitokanazo na biotekinolojia ya kisasa. Aidha, Kanuni za matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Cartagena na shughuli zifuatazo zitafanyika:-

(i) Kutoa mafunzo kwa sekta husika juu ya utambuzi, udhibiti, tathmini na masuala ya kisheria kuhusu bidhaa na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki (GMOs);

(ii) Kuboresha maabara mbili zilizoainishwa kwa ajili ya utafiti na utambuzi wa bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki;

(iii) Kuendesha warsha za kanda ili kutoa elimu na kukuza weledi kwa wadau kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa; na

(iv) Kutafsiri kanuni na miongozo kuhusu usimamizi wa mazingira dhidi ya biotekinolojia ya kisasa katika lugha ya Kiswahili na kusambaza kwa wadau kwa lengo la kujenga uwezo na upashanaji habari za matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Usafi wa Mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira Tanzania. Kituo kiliendelea kuratibu shughuli za Sekretariati ya *Roundtable on Sustainable Consumption and Production*. Aidha, kiliratibu na kukamilisha utafiti wa biashara ya bidhaa zenyе kemikali za sumu aina ya *cadmium*, risasi na zebaki katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kituo kilifanya tathmini na ukaguzi wa mazingira katika kiwanda cha *Tanpack Tissues Ltd* na kutayarisha mpango wa usimamizi wa mazingira (*Environmental Management Plan*) ya kiwanda. Vile vile, Kituo kiliendesha Semina ya Waandishi wa Habari na Semina ya Wenyeviti wa Kamati za Bunge kuhusu dhana ya Matumizi na Uzalishaji Endelevu ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Kituo kitaendelea kutoa mafunzo, kukuza tathmini ya uzalishaji bora viwandani chini ya awamu ya pili ya Programu ya Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria; kufanya tathmini ya uzalishaji bora kwenye viwanda mbalimbali nchini na kutayarisha Mipango ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya viwanda vinavyohitaji huduma hiyo; na kuendesha semina kwa wadau wa mazingira kuhusu matumizi endelevu na uzalishaji bora. Ofisi itaendelea

kushirikiana na sekta ya afya na maji na Halmashauri za miji katika kuhamasisha usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Montreal kuhusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni angani. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendesha semina ya wadau kuhusu mkataba na utekelezaji wake katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Ozoni yaliyofanyika tarehe 16 Septemba, 2008 jijini Mwanza. Jumla ya wadau 70 wakiwakilisha Idara na Taasisi za Serikali, Asasi zisizo za kiserikali, makampuni ya biashara ya kemikali hizo au vifaa vyake, karakana za ufundi wa majokofu na viyoyozi, makampuni ya madini na vyombo vya habari walishiriki. Kauli mbiu ya maadhimisho haya yalikuwa "*Ushirikiano wa Kimataifa kwa Manufaa ya Dunia*". Kauli mbiu hii inalenga katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa baina ya nchi na nchi katika kuhifadhi tabaka la Ozoni kwa manufaa ya dunia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi kwa kushirikiana na VETA na Chuo cha Kodi ilitoa mafunzo kwa maafisa forodha 70 mafundi mchundo 150 wa majokofu na viyoyozi yalifanyika jijini Dar es Salaam na Mwanza kuhusu majukumu yao katika utekelezaji Mkataba wa Montreal na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni) za mwaka 2007 na juu ya njia bora za kuhudumia majokofu na viyoyozi na tekinolojia mbadala.

Mheshimiwa Spika, shughuli nydingine zilizotekelawa ni: kusambaza kwa wadau vipeperushi kuhusu Kanuni za Udhibiti wa Kemikali hizo na kusambaza mwongozo kwa maafisa forodha kuhusu kemikali haribifu na mbadala ili kuwasaidia kuzitambua kwa urahisi katika bidhaa ziingizwazo nchini; Kufanya maandalizi ya kuanzisha vituo vitano vya kanda vya kusafisha na kurejeleza gesi iliyotumika kwa kubainisha mahitaji ya vifaa na kuwasilisha UNDP kwa ajili ya ununuvi. Vile vile Mtaala wa Mafunzo ya maafisa forodha wa Chuo cha Kodi umefanyiwa mapitio ili kujumuisha masuala ya Mkataba wa Montreal na Kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Ofisi kwa kushirikiana na VETA na Chuo cha Kodi itaendelea kutoa mafunzo kwa maafisa forodha na mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi kuhusu majukumu yao katika utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni) za mwaka 2007 na njia bora za kuhudumia vifaa hivyo na tekinolojia mbadala; kukusanya takwimu kuhusu matumizi ya kemikali mbadala aina ya *Hydrochlorofluorocarbons* (HCFCs) nchini ambazo matumizi yake yataanza kudhibitiwa kuanzia mwaka 2011; kuandaa mpango wa kitaifa wa usitishaji wa matumizi ya kemikali hizo na kukamilisha uanzishwaji wa vituo vitano vya kanda vitakavyojishughulisha na kusafisha na kurejeleza gesi iliyotumika kutoka kwa makampuni yenye mitambo ya kunasa gesi iliyotumika. Vile vile Ofisi kwa kushirikiana na waratibu wa mazingira itaendelea kuelimisha umma kuhusiana na matumizi ya kemikali mbadala ili kuhifadhi ukanda wa Ozoni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliratibu utekelezaji wa Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu na nyinginezo baina ya nchi na nchi na Mkataba wa Bamako unaozuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Basel umeweka taratibu za kimataifa za kudhibiti usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi zinazozalisha taka za aina hii na zile zinazopokea kwa madhumuni ya kurejeleza au kuziharibu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zilitekelezwa: kusambaza vipeperushi kuhusu Mkataba wa Basel kwa wadau mbalimbali ili kukuza weledi kuhusu umuhimu wa Mkataba huu; kuendesha warsha moja ya kanda iliyofanyika Morogoro Septemba, 2008 kwa ajili ya kujadili rasimu ya awali ya Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka na kuiboresha.

Aidha, Ofisi ilifanya utafiti wa taka za vifaa vya umeme na elektroniki katika taasisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania, vyuo vinavyotoa mafunzo ya kompyuta na elektroniki na karakana zinazojishughulisha na matengenezo ya vifaa hivi katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza na Dodoma. Matokeo yatatumika kuweka mkakati ya kuimarisha usimamizi wa taka hizo. Vile vile, Ofisi ilifanya utafiti wa matumizi ya zebaki na uchafuzi wake kwenye mazingira katika shughuli za migodi, hospitali, usafirishaji na viwanda; na kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:- kukamilisha majadiliano na wadau kuhusu Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taka pamoja na kuuchapisha na kuusambaza kwa wadau; kukamilisha Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Zebaki na kuusambaza kwa wadau; kukuza weledi juu ya madhara yatokanayo na zebaki na kuongeza hamasa ya matumizi ya bidhaa na teknolojia zisizo na zebaki ambazo ni salama kwa mazingira hususan kwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu na masonara kwa kushirikiana na Sekta za Madini na Afya; kufanya tathmini ya matumizi na usimamizi wa taka za vifaa vya umeme na elektroniki katika mikoa kumi (10); kuandaa mwongozo wa usimamizi wa taka za elektroniki; na kutoa mafunzo kwa wadau juu ya usimamizi wa taka za sumu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi iliandaa mwongozo wa usimamizi wa kemikali hizi na mwongozo wa ukarabati wa maeneo yaliyochafuliwa na kemikali. Aidha, vipeperushi kuhusu Mkataba na Mpango wake wa utekelezaji wa mwaka 2005 viliandaliwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, vile vile, andiko la mradi wa kujenga uwezo wa taasisi katika sekta za Kilimo, Misitu, Afya, Viwanda, Mazingira na Elimu katika utekelezaji wa Mkataba limekamilishwa. Mradi huu ni wa miaka miwili na utafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (UNEP). Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo wa taasisi husika utaanza.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa Mifuko ya Plastiki. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa kanuni za kuzuia utengenezaji, uuzaaji na matumizi ya mifuko laini ya plastiki, viroba vya maji na juisi. Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi, Ofisi imeendelea kuhamasisha viwanda vinavyozalisha bidhaa za plastiki kama chupa, ndoo n.k kuendeleza urejelezaji wa taka zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itafanya mapitio ya kanuni za kupiga marufuku mifuko laini na viroba vya maji na juisi kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi wa faida na hasara za kupiga marufuku matumizi ya aina zote za mifuko ya plastiki nchini. Lengo ni kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo kutokana na athari zake kwa mazingira na afya za binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Juni kila mwaka Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Kauli-mbiu ya Siku ya Mazingira Duniani Kimataifa ilikuwa “*Dunia inakuhitaji: Tuungane Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi*” (*Your Planet Needs You-Unite to Combat Climate Change*). Kauli-mbiu hii inahimiza kuwajibika kwa kila mtu katika kupambana na kujiweka tayari kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuhifadhi mazingira. Kitaifa kauli-mbiu ilioongoza maadhimisho haya ni “*Wananchi Tuungane Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi*”.

Mheshimiwa Spika, Kimataifa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu yamefanyika katika Jiji la Mexico na kitaifa yalifanyika mkoani Tabora. Mwaka huu maadhimisho yalifanyika kwa kuhusisha shughuli mbalimbali, ambazo ni pamoja na:- upandaji na palizi ya miti, mafunzo mbalimbali kuhusu mazingira kuititia maonyesho na mashindano ya nyimbo na ngonjera ili kukuza weledi juu ya umuhimu wa hifadhi na usafi wa mazingira. Shughuli hizo zilifanyika kwa kipindi cha wiki moja hadi siku ya kilele.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wote walioshiriki katika maadhimisho haya. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa uongozi wa mkoa wa Tabora kwa kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo kitaifa na kwa wananchi wa mkoa wa Tabora na Watanzania wote kwa ushiriki wao. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na uratibu na uhamasishaji wa ushiriki wa wadau mbalimbali kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) hapa nchini. Mfuko huu umekuwa ukifadhilli miradi midogomidogo, miradi ya kati na mikubwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi ilipitisha miradi mikubwa minne yenye thamani ya dola za Marekani

milioni 14.3. Miradi hii ni pamoja na mradi wa Uboreshaji wa Usimamizi wa Mfumo wa Hifadhi za Taifa za Usangu, Rungwe, Kitulo, milima ya Livingstone na mbuga za Saadani na Serengeti; mradi wa usimamizi endelevu wa misitu ya miombo iliyoko Magharibi mwa Tanzania; mradi wa utekelezaji wa Mkataba wa Cartagena kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa; na mradi wa uzalishaji umeme vijiji kwa kutumia nishati ya maji (*Micro Hydro Power*).

Mheshimiwa Spika, Ofisi iliendelea kupokea, kuchambua na kupidisha maombi ya miradi midogomidogo, kwa ajili ya kupata ufadhili kutoka Mfuko wa *GEF* kwa uratibu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) hapa nchini. Jumla ya miradi ya mazingira 15 yenye thamani ya dola za Marekani 409,158 ilipata ufadhili kutoka katika Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Ofisi ilikagua na kutathmini miradi iliyopata ufadhili kutoka mfuko huu na kuona shughuli za miradi hii katika vikundi na taasisi mbalimbali katika mikoa ya Kagera, Mara na Mtwara. Jumla ya miradi kumi na tatu (13) ilikaguliwa na kutathminiwa ili kuona jinsi wananchi wanavyofaidika na miradi hii katika kuhifadhi mazingira na kuondoa umaskini (Rejea kiambatisho Na 3). Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za *GEF* nchini kwa kuhamasisha na kushauri vikundi, kuandaa miradi kwa ajili ya ufadhili wa *GEF* na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi iliyopata ufadhili wa *GEF* katika mikoa ya Tanga, Rukwa na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Sasa ni mwaka wa nne (4), tangu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira sura 191 ianze kutekelezwa. Kati ya wadau muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria hii ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Mpango Mkakati wake (*NEMC Strategic Plan 2004-2009*), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, nyaraka na mikakati mbalimbali ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, elimu ya mazingira ni muhimu sana ili jamii iweze kufanya maamuzi sahihi yanayohusu matumizi endelevu ya maliasili na mazingira kwa ujumla. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Baraza liliandaa Programu ya Kitaifa ya Elimu kwa Umma na kuanza kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya washiriki 27 kutoka Wilaya za mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma walipata mafunzo ya siku tatu (3) kuhusu masuala ya kuhifadhi mazingira ikiwemo kilimo endelevu kwenye maeneo ya miinuko, matumizi ya majiko banifu, upandaji wa miti na uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, makala mbalimbali kuhusu utunzaji na usimamizi wa mazingira zimeendelea kutolewa kupidisha jarida la Umasikini na Mazingira pamoja na Jarida la Mazingira la Baraza ili kukuza weledi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Baraza liliandaa na kurusha hewani kupidisha vipindi vyta luninga na redio; makala katika magazeti, majarida, vipeperushi na kalenda zilichapishwa

na kusambazwa. Vipindi vya luninga vilihu mada za hifadhi ya mazingira kuhusu upigwaji marufuku wa mifuko ya plastiki, utunzaji wa vyanzo vya maji na matumizi ya majiko banifu.

Aidha, Tovuti ya Baraza iliboresha kwa kuingiza taarifa mbalimbali za mazingira na matangazo ya Baraza zikiwemo taarifa kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) pamoja na viwanda vilivyoziiliwa kuendelea na uzalishaji kwa kukiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendelea na kazi ya kuelimisha wananchi kuacha kutumia mifuko laini ya plastiki na viroba vya kufungia maji na juisi iliyopigwa marufuku na Serikali. Baraza lilitoa elimu kwa wananchi kwa kupitia vyombo vya habari kuhusu athari kwa afya na mazingira zitokanazo na matumizi ya mifuko ya plastiki. Aidha, elimu kuhusu matumizi ya mifuko mbadala hususan matumizi ya vikapu, mifuko ya karatasi na vitambaa ilitolewa. Baraza lilishiriki katika maadhisho mbalimbali ya kitaifa. Aidha, Baraza lilifanya kampeni katika vyombo vya usafiri ili kutoa elimu kwa wasafiri na wamiliki wa vyombo hivyo juu ya utunzaji wa taka wakati wakiwa safarini.

Mheshimiwa Spika, Baraza liliandaa mashindano kuhusu mazingira kwa shule za msingi za Manispaa ya Tabora ambako maadhisho ya Siku ya Mazingira Duniani yalifanyika kitaifa. Shule za Msingi Mtendeni na Ipuli zilipewa vyeti na vifaa vya usafi. Pia Baraza lilitoa zawadi kwa Asasi zilizofanya vizuri katika suala la kuhifadhi mazingira; mfano Kiwanda cha Saruji cha Tanga kilipata zawadi ya ngao kutokana na kuongoa machimbo ya Pozolana, yaliyopo Holili.

Vile vile, wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibaha waliokuwa washindi katika utafiti wa mazingira, walizawadiwa cheti, ngao na fedha taslimu. Zawadi hizo zilitolewa siku ya kilele cha Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa utunzaji taarifa za mazingira kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 174 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Baraza limeboresha Mfumo wa Mawasiliano ambao unaweka kumbukumbu na taarifa za mazingira zinazokusanywa nchini. Baraza pia, kwa kushirikiana na wadau wa mazingira limeweka mfumo wa upatikanaji wa taarifa hizo kwa kubadilishana ili kuhakikisha kuwa taarifa husika zinawafikia walengwa kwa muda muafaka ili zitumike katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Baraza lilichapisha na kusambaza programu ya elimu kwa umma katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Tabora, Singida na Kigoma. Programu hii inalenga kuhamasisha watoa elimu kwa jamii juu ya mbinu mbalimbali za kuelimisha umma kuhusu matumizi endelevu ya mazingira. Mbinu hizi ni pamoja na kufanya mikutano, vikundi vya kijamii kutembeleana, kutumia vyombo vya habari kama luninga, redio, magazeti pamoja na sinema.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza litaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa kutumia njia mbalimbali kama vipeperushi, vijarida, mabango, maonyesho, luninga, redio na magazeti. Aidha, Baraza litaboresha maktaba yake kwa kununua vitabu na majarida ya mazingira. Vile vile, Baraza litatoa mafunzo ya kuandaa *database*, mifumo mingine ya taarifa za mazingira pamoja na programu za elimu kwa umma kwa watanza taarifa Wilayani.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya athari kwa mazingira (*TAM*). Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Baraza lilipokea taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira za miradi 88 kwa ajili ya kufanyiwa mapitio ili miradi hiyo ipate Hati za Mazingira (*EIA Certificates*).

Mheshimiwa Spika, Kati ya hiyo, miradi 72 ilipata Hati za Mazingira zilitolewa ili kuhakikisha uwekezaji endelevu. Miradi iliyopewa Hati ni ya uchimbaji madini 4, mawasiliano 18, ujenzi na uendelezaji wa hoteli kwenye vivutio vya utalii 13, nishati 8, viwanda 18, miundombinu 4, misitu 3, kilimo 2 na uvuvi 2. Miradi mingine 16 iko katika hatua mbalimbali za mapitio ili kutolewa uamuvi. (Rejea kiambatisho Na. 4)

Mheshimiwa Spika, Baraza liliendelea kufuatilia na kuandaa taarifa ya ukaguzi kwa miradi 5. Miradi hiyo ni *Nile Perch Musoma, Fish processing Mwanza, Tulawaka Mines Biharamulo, North Mara Gold Mine* na *Nyakato Steel Mills Mwanza*. Pia, Baraza lilifuatilia suala la minara ya mawasiliano inayoongezeka kwa kasi sana nchini. Taarifa za minara 68 ya makampuni mbalimbali ziliwasilishwa katika Baraza ili kufanyiwa mapitio. Kati ya hiyo minara 51 ilipatiwa Hati za Mazingira. Aidha, Baraza limefanya mikutano na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) na Tume ya Nguvu za Atomiki ili kuweka mfumo shirikishi kuhusu utoaji wa leseni na vibali mbalimbali na kuweka mikakati ya kukagua wenye vibali hivyo iwapo wanazingatia masharti ya uwekezaji na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Baraza lilitoa mafunzo ya TAM kwa maofisa wa mazingira na watendaji 60 wa Mikoa ya Mtwara na Lindi. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, mafunzo haya yalitolewa kwa Wahandisi 64 na Mafundi mchundo 67 kutoka mikoa ya Morogoro, Shinyanga na Pwani. Pia, mafunzo yalitolewa kwa maofisa mazingira 21 wa Wilaya na Halmashauri za Mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza linatarajia kufanya mapitio ya taarifa zaidi ya 90 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kutoa ushauri kuhusu utoaji Hati. Baraza litafuatilia miradi zaidi ya 30 iliyokwishapata Hati ili kubaini kama inatekeleza masharti ya mazingira yaliyoainishwa kwenye Hati hizo. Pia, litapitia taarifa za ukaguzi wa mazingira na kutoa maelekezo ya kuboresha mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapitio ya fomu za usajili wa miradi, taarifa za awali na mipango ya usimamizi wa mazingira na masuala ya jamii yataendelea kufanyika ili kudhibiti athari kwa mazingira zinazoweza kusababishwa na shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Baraza lilipokea jumla ya maombi 105 kwa ajili ya usajili wa wataalamu wa TAM. Maombi haya yalifanyiwa tathmini ili kukamilisha usajili rasmi wa wataalamu hawa. Wataalamu 50 wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na 19 wa ukaguzi wa mazingira (*Environmental Audit*) wamesajiliwa kwenye Gazeti la Serikali. Usajili huu unatarajiwa kuongeza ubora wa taarifa za tathmini na ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayofanywa. Pia taarifa hizo zitatumika katika maamuzi ya mipango ya maendeleo endelevu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 Baraza kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine litajenga uwezo kwa wataalamu na wadau wengine kuhusu TAM ili kuhakikisha elimu ya mazingira inafika katika ngazi zote husika.

Mheshimiwa Spika, utafiti na Mipango ya Mazingira. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Baraza liliandaa na kuendesha Kongamano la tatu la Kitaifa la Kisayansi kuhusu Mazingira na Uchimbaji wa Madini lililofanyika Mkoani Mwanza mwezi Mei, 2009. Kongamano hilo lilijumuisha washiriki 100 kutoka jumuiya ya watafiti, sekta mbalimbali na wadau wa uchimbaji wa madini ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa kampuni za madini zilizopo nchini. Lengo la kongamano lilikuwa ni kubadilishana uzoefu na kujadili changamoto zinazohusiana na athari za mazingira zitokanazo na uchimbaji wa madini na kutoa mapendekezo ya kisera, kiutendaji na utafiti ili kuboresha sekta ya madini kimazingira.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza liliendesha warsha kwa Maafisa 120 kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Utafiti wa Masuala ya Mazingira (*National Environmental Research Agenda - NERA*) kwa ajili ya watendaji na Maafisa Mazingira wa Mikoa, Wilaya na Manispaa katika mikoa ya Mara, Kagera, Mwanza, Tabora, Kigoma na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Baraza litaendesha warsha kwa Maafisa Mazingira wa Mikoa, Wilaya na Manispaa katika kanda nyingine mbili na kuendesha vikao vitatu vya Kamati ya Ushauri wa Masuala ya Utafiti wa Mazingira kama njia ya kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa kuhusu utafiti wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Baraza liliendesha warsha ya siku tatu katika Jiji la Mwanza kwa Maafisa Mazingira kutoka mikoa ya Shinyanga, Kagera, Mara na Mwanza na kupokea taarifa za hali ya milima katika Mikoa hiyo. Taarifa hiyo itatumwa katika kufanya tathmini na kutoa taarifa ya hali ya mazingira ya milima nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Baraza linatarajia kufanya tathmini ya hali na mifumo

ikolojia ya milima katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendesa warsha kwa watendaji 60 iliojumuisha Madiwani, Watendaji Kata, Wakuu wa Idara na Taasisi Zisizo za Serikali iliyofanyika Wilayani Nzega. Lengo la warsha hii lilikuwa kujenga uwezo kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza litaendelea kujenga uwezo kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Uhifadhi Mazingira ya Maeneo ya Pwani, kwa kushirikiana na Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Mkuranga kupitia mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani (*Tanzania Coastal Management Partnership – Sustainable Coastal Communities and Ecosystems TCMP - SUCCESS*).

Mheshimiwa Spika, shughuli za uboreshaji wa maisha ya wakazi wa pwani na mazingira yao ziliendelea hasa katika uendelezaji wa ufugaji samaki aina ya *mwatiko* katika wilaya za Bagamoyo, Mkuranga na Pangani, ufugaji endelevu wa nyuki na uanzishaji wa SACCOS pamoja na kilimo cha zao la paprika katika maeneo ya pwani. Kwa ujumla shughuli hizi ambazo zinafanyika kwa kujali mazingira zimeonesha kuwa zinaweza kuinua hali ya maisha ya mwananchi wa pwani kimapato.

Mheshimiwa Spika, aidha, uainishaji wa maeneo muhimu ya kimazingira na kiuchumi katika wilaya ya Mkuranga uliendelea kwa ushirikiano na wadau wote. Fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo tekechu ya pwani ziliainishwa na utaratibu wa kutoa vibali kwa ajili ya matumizi ya maeneo hayo kwa sasa umeanza kutayarishwa. Utaratibu huu utakapoanza kutumika, wilaya ya Mkuranga itakuwa ni mfano kwa wilaya nyingine za pwani. Aidha, mradi huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bonde la Wami - Ruvu ulizisaidia jamii kuboresha mazingira ya maji na afya katika wilaya za Kilosa, Mvomero na Bagamoyo kwa kujenga vyoo na kutoa elimu ya usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia katika kutekeleza Mipango ya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (*Intergrated Coastal Environment Management Plan - ICEM*) kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani (MACEMP). Pia, Baraza lilitoa mafunzo kuhusu mchakato wa uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa ICEM kwa watendaji 345 wa halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani, Ilala, Temeke na Kinondoni; watendaji 364 wa halmashauri za wilaya za Mkinga, Pangani, Muheza, Mkuranga, Bagamoyo, Lindi na Mtwara na watendaji 32 kutoka Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Spika, Wilaya hizo zimeingia katika awamu ya pili ya ufadhili wa mradi wa MACEMP na ziko katika hatua mbalimbali za maandalizi ya mipango ya utekelezaji wa ICEM. Aidha, Baraza lilifanya mapitio na kukamilisha Taarifa ya Mazingira ya Pwani (*State of the Coast Environment Report*) toleo la mwaka 2009.

Shughuli hizi za utekelezaji wa masuala ya ICEM kupitia mradi wa MACEMP zitaendelea katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Baraza limeendelea kuratibu na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa awamu ya pili ya Mkakati na Mpango endelevu wa kuhifadhi rasilimali na viumbe adimu katika korongo na Bonde la Mto Kihansi kwa kushirikiana na Halmashauri za Kilolo, Mufindi na Kilombero. Aidha, maandalizi ya kurejesha vyura katika mazingira ya asili yanaendelea kwa kufanya tafiti na uperembaji wa mifumo ikolojia ya Bonde la Mto Kihansi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor (TAWIRI). Vile vile ujenzi wa sehemu salama kibaiolojia (*Biosecure Facility*) kwa ajili ya vyura umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Baraza linatarajia kuanza kurudisha baadhi ya vyura wanaohifadhiwa nchini Marekani. Aidha, katika kipindi hicho, Baraza kupitia mradi wa Kihansi litaendelea kusaidia miradi ya kuinua vipato kwa wananchi kupitia vikundi vidogo vidogo na kuongeza uwezo wa wilaya za Mufindi, Kilolo na Kilombero katika shughuli za uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Baraza lilifanya ukaguzi wa viwanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Kilimanjaro na kuandaa Taarifa ya hali ya Mazingira (*Environmental Profiles*) za viwanda hivyo. Viwanda vilivyokaguliwa ni *Tanpack Tissues Ltd, M.M.I Steel Mills Ltd, Motisun Industries Ltd, Karibu Textile Mills Ltd, Iron & Steel Mills Ltd*, Kiwanda cha viberiti cha *Mbagala na Yuasa Battery Ltd* vya Dar es Salaam; *21st Century Textile Mills* cha Morogoro na viwanda vya ngozi vya Moshi na Kibaha. Baraza lilibaini upungufu unaosababisha uchafuzi wa mazingira na lilitoa maelekezo ya marekebisho ya matatizo hayo ambayo yalitekelezwa na viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka fedha 2009/2010 Baraza litaimarisha shughuli zauzingatiaji na usimamizi wa Sheria ili liweze kufanya shughuli zake kikamilifu kama ilivyoainishwa katika Sheria. Aidha, Baraza litafanya ukaguzi wa mara kwa mara kufuatilia viwanda na miradi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa viwango vya mazingira na masharti mengine ya kuboresha uzalishaji viwandani yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Baraza liliendelea kutoa mafunzo yanayohusu usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa Madiwani na watendaji 30 wa Manispaa ya Morogoro; maafisa mazingira, wakurugenzi watendaji na Waheshimiwa Wabunge kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara 25 na maafisa mazingira kutoka Tabora, Kigoma na Singida 45. Mafunzo haya yaliwawezesha kutekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika Sheria.

Aidha, ili kuwezesha ufanisi wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Baraza lilifanya warsha ya siku mbili kwa viongozi wakuu wa Serikali za Mitaa katika Mikoa hiyo. Lengo kuu la warsha hii lilikuwa kuainisha majukumu ya

watendaji wakuu wa Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni iliyopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni 30 na vifungashio vya maji na juisi bila kujali unene wake, Baraza kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Shirika la Viwango na Wizara ya Mambo ya Ndani walifanya ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na mji wa Musoma. Kwa mwaka 2008/09 watuhumiwa watatu 3 walifishwa katika vyombo vya sheria. Misako inaendelea kwa kushirikiana na wadau (Polisi, Manispaa, Wanahabari na Wazalishaji wa bidhaa za plastiki).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza litaendelea na usimamizi na ufuutiliaji wa Sheria iliyopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na majukumu mengine kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mkakati wa Kuhifadhi Ardhi na Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Wakaguzi wa Mazingira 21 waliteuliwa kutoka mionganii mwa watumishi wa Baraza na kuanza kazi. Taratibu za kuteua Wakaguzi zaidi kutoka Wizara za Maji na Umwagiliaji, Afya na Ustawi wa Jamii na Mambo ya Ndani ya Nchi zinaendelea. Aidha, tunatarajia kuanza utaratibu wa tozo ya ‘papo kwa papo’ katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Baraza liliendelea kutekeleza mradi wa *African Stockpile Programme* (ASP) unaofadhiliwa na *Global Environmental Facility* (GEF) na wafadhili wengine. Kupitia mradi huu Baraza liliorodhesha viuatilifu chakavu vinavyofikia tani 1,200 katika Kanda nne (4) kwa lengo la kukusanya na kuteketeza. Kanda hizo ni Pwani (Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara); Kati (Morogoro, Dodoma na Singida); Kaskazini (Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga); na Magharibi (Shinyanga, Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma na Tabora). Vile vile Baraza lilifanya tathmini na kuratibu zoezi la kuchukua sampuli katika maeneo yapatayo 20 (rejea kiambatisho Na.5) ambayo viuatilifu chakavu vimefukiwa ardhini kwa lengo la kupima viwango vya kuathirika kwa udongo ili kutafuta ufumbuzi. Zoezi hili lilifanyika kwa ushirikiano wa Baraza na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na cha Auckland - New Zealand.

Mheshimiwa Spika, Aidha, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Baraza liliandaa mkakati wa kitaifa wa mawasiliano wa ASP ambao utasaidia katika kuhakikisha kwamba jamii kwa ujumla inapata ujumbe kuhusu madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya viuatilifu na kuelimisha jamii itoe ushirikiano ili kuhakikisha kuwa mlundikano wa viuatilifu chakavu haujirudii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza litakamilisha kuratibu maeneo yenye viuatilifu chakavu katika kanda ya Nyanda za Kusini inayojumuisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa; pamoja na Zanzibar

ikijumuisha Unguja na Pemba. Aidha, Baraza litaendelea kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wadau nchini ili watoe ushirikiano katika kuainisha maeneo yenye mlundikano wa viuatilifu chakavu. Vile vile Baraza litaainisha na kuboresha vituo vya kati vitakavyotumika kuhifadhia shehena ya viuatilifu chakavu kutoka maghala madogo madogo yaliyotapaka nchini kote vikisubiri kusafirishwa kwa ajili ya kuteketezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza lilifanya mazungumzo na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam na Mamlaka za Maji (DAWASA na DAWASCO) kuhusu namna ya kuanzisha na kusimamia mifumo ya majitaka na kuhakikisha kuwa majitaka yanasaishwa kulingana na viwango vya mazingira kabla ya kuelekezwa kwenye mito na bahari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Baraza litafanya warsha ili kujenga uwezo na kukuza weledi wa watendaji kuhusu udhibiti wa taka ngumu kuziba mifumo ya maji taka. Ili kuhakikisha shughuli hii inafanyika kwa ufanisi, kikundi kazi *Municipal Wastewater Management Working Group* kitaanzishwa ili kutoa ushauri wa mara kwa mara kwa manispaa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Baraza litatoa mafunzo kwa wafanyakazi 50 kuhusu misingi ya ukaguzi wa mazingira kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa Sheria. Mafunzo haya yatasaidia kujenga uwezo wao katika kukagua maeneo mbalimbali. Baraza litawezesha wafanyakazi wake kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ya kujenga uwezo katika utekelezaji wa Sheria na kuendesha warsha za mafunzo kwa Maafisa Mazingira wateuliwa wa Majiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya na mahakimu wakazi katika kanda za Kati na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Utumishi katika Baraza, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza liliendelea kudumisha nidhamu na uwajibikaji wa watumishi katika kutoa huduma. Aidha, kanuni za utumishi, fedha na manunu zilizingatiwa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Ili kuongeza uwezo wa utendaji, Baraza liliajiri watumishi 30 katika fani mbalimbali na kufanya idadi ya watumishi wa Baraza kufikia 150. Aidha, katika kuongeza ufanisi kwa watumishi jumla ya watumishi 77 waliwezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Baraza lilianza kutatua tatizo lake la muda mrefu la kutokuwa na Ofisi zenye hadhi kwa kununua kiwanja na majengo mawili eneo la Mikocheni, Dar es Salaam kwa ajili ya kuanza kujenga Ofisi za Baraza (*Mazingira House*). Katika kipindi hiki Baraza pia liliendelea kuimarisha Ofisi za kanda zilizopo Mwanza, Mbeya na Arusha ili kuboresha huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2009/2010 Baraza litaanza ujenzi wa Ofisi za kudumu na pia litaendelea kuimarisha ofisi katika kanda hizo.

Mheshimiwa Spika, masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi ya Makamu wa Rais imeajiri watumishi tisa (9) ili

kujaza nafasi zilizokuwa wazi, watumishi kumi (10) wameajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni, watumishi kumi (10) wamethibitishwa kazini. Watumishi wanane (8) wa Kada mbalimbali wamepandishwa vyeo kwa kuzingatia Miundo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi imeendeleza Utawala Bora, kulinda, kudumisha na kuendeleza haki za wafanyakazi kwa kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi na masuala mbalimbali yanayohusu wafanyakazi na utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais yalijadiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Ofisi imewawezesha watumishi wapatao themanini na sita (86) kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali kwa kuzingatia kada na majukumu yao kazini. Kati ya hao, kumi (10) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu, hamsini na wanane (58) ya muda mfupi na kumi na wanane (18) walihudhuria mafunzo ya elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa michezo na mazoezi ya viungo kwa Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais umezingatiwa. Wanamichezo walishiriki kikamilifu katika michezo ya SHIMIWI. Hii ni katika kuahakisha kuwa watumishi wanakuwa na afya bora na wanajenga mahusiano mazuri baina yao na watumishi wa umma wa sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Kiwanja Na.10 Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam umekamilika na sasa watumishi wote wako katika jengo moja. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais katika eneo la Tunguu - Zanzibar unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Machi, 2010. Awamu ya pili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam, unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi itaendelea kuratibu, kusimamia na kushughulikia masuala yote ya Watumishi yahusuyo ajira, maslahi, nidhamu, mafunzo, utawala bora na uwajibikaji, mapambano dhidi ya rushwa na kuahakisha kuwa Watumishi wanapata vitendea kazi ili kuongeza ufanisi. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya Muungano na Uhifadhi wa Mazingira. Pia, Ofisi itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari hususan virusi vya UKIMWI na kutoa huduma kwa watakaojitokeza kuwa wameathirika na VVU/UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio tuliyoyapata katika kutekeleza mpango wa mwaka wa fedha 2008/2009 wa Ofisi ya Makamu wa Rais, zipo changamoto zilizojitokeza katika masuala ya Muungano na Mazingira.

Changamoto mbalimbali zimejitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kwani kuanganisha nchi mbili zilizokuwa huru ni kazi kubwa hasa katika masuala ya utawala. Mifumo tofauti ya Sheria kwa mfano katika masuala ya kodi na usajili wa magari, hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika

kutatua vikwazo vya Muungano. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa, vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano vinatafutiwa ufumbuzi kwa kufanya vikao vya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizopo katika sekta ya mazingira ni; kukuza weledi wa wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kujenga uwezo katika halmashauri za miji katika usimamizi wa taka hususan kuweka miundombinu inayokubalika kurejeleza na kutupa taka husika; kuinua uwekezaji katika nishati jadidifu, majiko banifu na teknolojia zinazohifadhi maliasili na mazingira; na migongano baina ya wakulima na wafugaji kutokana na kasi ndogo ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na usimamizi wake. Aidha, kuna mahitaji makubwa ya rasilimali watu na fedha katika utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, shukrani, baada ya kueleza haya napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kabisa kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake yaliyowezesha Ofisi yetu kutekeleza vizuri majukumu yake. Namshukuru pia Mheshimiwa Samwel Sitta Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Anna Makinda, Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wadau wa maendeleo ambao wameendelea kuisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kugharamia miradi katika kuratibu utekelezaji wa masuala ya Muungano, Mikakati ya Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira na kuondoa umaskini. Wadau hao ni pamoja na Umoja wa Ulaya, Serikali ya Norway, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Serikali ya Uhlanzi, Serikali ya Marekani, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo (UNDP), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF), Benki ya Dunia, *International Development Agency* (IDA), *Danish International Development Agency* (DANIDA), SADC-REEP, *Wildlife Conservation Society* (WCS), WWF, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), *Crop Life International* (CLI), *African Development Bank* (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani (GTZ), Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE), Makampuni binafsi, Vyombo vya Habari, wananchi na Wadau wengine kwa kushirikiana vyema na Ofisi katika kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Aidha, zipo nchi ambazo zimeonyesha nia ya kushirikiana nasi katika masuala ya mazingira. Nchi hizo ni pamoja na Finland, Canada, Brazil, Sweden na China. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote hawa kwa ushirikiano wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mwaka wa fedha 2009/2010. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26, Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2009/2010, naomba Bunge lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Sh. 4,492,974,000/= kwa ajili ya kugharimia matumizi ya kawaida ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Kati ya fedha hizo Sh. 493,818,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Sh. 3, 999,156,000/= kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2009/2010, naomba Bunge lako tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya jumla ya Sh.63,397,505,000=/. Kati ya fedha hizo, jumla ya Sh.1,005,428,800/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi Makamu wa Rais na Sh.62,397,076,200/= ni kwa ajili ya matumizi mengine ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Sh.15,870,888,900/= zinaombwa kwa ajili ya shughuli za Maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni Sh.8,649,299,000/= na fedha za nje ni Sh.7,221,659,900/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. PHILIP S. MARMO – WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JOHN P. LWANJI – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipatia Kamati yangu, kazi ya kujadili Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati ilikutana na watendaji wa ofisi hiyo, tarehe 02 Juni, 2009 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, kushughulikia makadirio hayo.

Aidha, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi hiyo kuhusu Utekelezaji wa majukumu yaliyofanywa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano inahusisha Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa mwaka 2008/2009. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Fungu 26 –

Makamu wa Rais liliidhinishiwa Sh.2,455,156,000/= kwa ajili ya matumizi ya Makamu wa Rais. Shughuli ambazo zilitekelezwa kutokana na Fungu hili, ni pamoja na kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais:-

- (i) Kutekeleza majukumu yake kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya Kitaifa na Kimataifa;
- (ii) Kumshauri ipasavyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya Kitaifa na Kimataifa;
- (iii) Kusimamia kwa kikamilifu masuala yote yanayohusu Muungano; na
- (iv) Kusimamia kwa ufanisi masuala yote yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa kazi hizo, Ofisi hii ilikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo zifuatazo:-

- (i) Ufinyu wa Bajeti kwa Fungu hili ambalo liliidhinishiwa Sh.1,999,156,000/= ukilinganisha na maombi yao ya Sh.4,176,890,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo ambayo sio ya Mshahara (O.C);
- (ii) Kupanda kwa gharama za kukodi ndege kwa ajili ya ziara za Mheshimiwa Makamu wa Rais; na
- (iii) Ukosefu wa fanicha ambazo zilihitajika mara baada ya kukamilisha ukarabati wa Ikulu Ndogo za Dodoma na Wete-Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka ujao wa Fedha 2009/2010, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia Fungu hili ni kama ifuatazo:-

- (i) Kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake;
- (ii) Kukamilisha uwekaji wa samani katika Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais yaliyopo Dar es Salaam, Dodoma na Wete – Pemba;
- (iii) Kujenga eneo la mapokezi katika Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais yaliyopo Dodoma; na
- (iv) Kumwezesha Makamu wa Rais kufanya ziara za Mikoani kwa ajili ya kuangalia shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano, katika mwaka wa 2008/2009, Fungu hili liliidhinishiwa Sh. 54,869,078,400/=

ambazo kati yake Sh.35,157,086,000/= ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Sh.19,711,992,400/= ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea na kazi yake kubwa ya kuratibu mambo ya Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuratibu gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar litokanalo na misaada kutoka nje;

(ii) Kuangalia miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa katika pande zote za Muungano. Miradi hiyo ni pamoja na *TASAF, SELF, MACEMP* na *PADEP*; na

(iii) Kusimamia utekelezaji wa ufumbuzi wa kero za Muungano, ambapo iliarifiwa kuwa hoja tatu zilipatiwa ufumbuzi. Hoja hizo, ni tatizo la Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu, Na. 7 ya Mwaka 2001, Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu; na Uanachama katika *International Maritime Organization (IMO)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilielezwa kuwa masuala mengine ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi ni kama ifuatavyo:-

(i) Suala la Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia liko katika hatua za mwisho za utekelezaji. Mshauri Mwelekezi anakamilisha taarifa yake ili aweze kuikabidhi Serikali;

(ii) Ushiriki wa Zanzibar katika masuala ya Kimataifa unazingatiwa na Viongozi wa pande zote mbili za Muungano kuandaa Taarifa ya pamoja;

(iii) Kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, maeneo yenye faida za kiuchumi yameainishwa ikiwemo miradi minane ya Zanzibar ambayo imeingizwa kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa ajili ya kuombewa ufadhilli; na

(iv) Elimu kwa umma inaendelea kutolewa kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kupitia vipindi vya radio, televisheni, vipepeprushi, maonyesho ya Kitaifa na magazeti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kazi za Maendeleo zilizotekeliza Kipindi cha mwaka uliopita wa 2008/2009. Katika Kipindi cha Mwaka 2008/2009, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano pamoja na mambo mengine ilitekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Imekamilisha ujenzi wa jengo la ofisi lililopo Mtaa wa Luthuli, Kiwanja Namba 10. Watumishi wote wa Ofisi hiyo kwa sasa wapo katika jengo hilo; na

(ii) Imeendelea na ujenzi wa ofisi na Makaazi ya Makamu wa Rais huko Tunguu, Zanzibar na Kamati iliarifiwa kuwa kazi inaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha 2009/2010 kupitia Fungu 31, ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kukabiliana na utatuzi wa changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2008/2009. Aidha, changamoto kubwa mbili zitakazopewa umuhimu wa kipekee, ni kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano na kuweka ulinganifu wa Sheria kwa pande zote mbili za Muungano hasa katika masuala ya kodi na usajili wa magari;

(ii) Kuendelea kuratibu shughuli za kutatua vikwazo vyta utekelezaji wa masuala ya Muungano;

(iii) Kuratibu masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria na mambo yanayohusiana na hayo kwa faida ya pande mbili za Muungano; na

(iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo yafuatayo:-

(i) Kuhusu ziara za Makamu wa Rais, Serikali itenye fedha za kutosha zitakazomwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kufanya ziara za kutosha Mikoani ili aweze kutekeleza jukumu lake la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano;

(ii) Kuhusu masuala ya fedha, Serikali ikamilishe kazi ya muda mrefu kuhusu masuala ya kuchangia na kugawana mapato na matumizi ya fedha za Muungano ambayo yanashughulikiwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Ushirikiano katika mambo ambayo sio ya Muungano, Serikali iweke utaratibu ulio wazi na ulioandikwa baada ya makubaliano kuhusu ushirikiano wa Wizara na mambo mengine ambayo si ya Muungano;

(iv) Kuhusu gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ilishughulikie suala la mgao wa fedha hizo kama ilivyoahidi huko nyuma kwa kutafuta kiwango muafaka;

(v) Kurekebisha Sheria za Kibiashara zinazotumika pande zote za Muungano. Kamati imebaini kuwa kumekuwepo Sheria mbili tofauti za Kodi ya makampuni katika kila upande wa Muungano. Wananchi wanalillalamikia sana jambo hili ambalo pamoja na kuwasilishwa Serikalini kwa muda mrefu bado halijapatiwa ufumbuzi. Kamati inashauri Serikali kulitatu jambo hili kwa faida ya wananchi wa pande zote za Muungano; na

(vi) Taasisi za Muungano kuonesha sura na muundo wa Muungano. Kamati inashauri taasisi zote ambazo ni za Muungano, viongozi na Watendaji wake nao waonekane kuwa na sura na muundo wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na baadhi ya changamoto zinazoukabili Muungano wetu, Kamati yangu inaupongeza Muungano wetu huu amba ni wa kipekee kwa Bara la Afrika na Duniani kote.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa kila Mtanzania anayeitakia mema nchi yake, anaunga mkono kuwepo kwa Muungano amba uliasisiwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mzee Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pili, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano, Katibu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakuu wa Taasisi; Idara na Vitengo na Maafisa wake, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walizoutoa kwa Kamati na kuiwezesha kuwasilisha maoni yaliyoboresha Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano.

Mwisho kabisa, nachukua fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua makisio haya ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa mwaka ujao wa fedha 2009/2010. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za sekta za Utumishi wa Umma, kisiasa na huduma za jamii ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti na Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbiri, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro. (*Makofu*)

Aidha, napenda kumshukuru, Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa, bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, ndugu Ramadhan Abdallah na ndugu Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeiomba Kamati yangu ipitishe jumla ya Sh.4,492,974,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Fungu 26 – Makamu wa Rais na Sh.79,868,393,000/= kwa ajili ya Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais; ambapo Sh.63,397,505,000/= ni Matumizi ya Kawaida na Sh.15,870,958,900/= ni Fedha za Maendeleo. Kamati iliyapokea maombi hayo na kuyapitisha Fungu kwa Fungu ili yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. RIZIKI OMAR JUMA – MSEMADI WA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako, napenda kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Masuala ya Muungano) kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge toleo la Mwaka 2007, Ibara ya 99 (3) na (7).

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kutoa mtazamo wa Kambi hii. Naushukuru pia uongozi mzima wa Chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF- The Civic United Front*), viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, kwa imani na ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vikao baina ya Ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi na Hatima ya matatizo ya Muungano. Isingekuwa ni lazima kutimiza jukumu la Kambi ya Upinzani la angalau kusema chochote katika kila kikao cha Bunge la Bajeti, basi leo sisi tungenyamaza kimya kuhusu suala hili la Muungano. Sababu ni kwamba, namna Serikali ya Muungano inavyofanya kazi ya kushughulikia matatizo ya Muungano, ni kama kwamba haitaki kusikia upande mwingine wa mawazo. Inapenda kujifungia chumbani na kujisikiliza yenyewe ndani ya viambaza vinne.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo, kwa kuwa zile hoja za msingi tunazozitoa kuhusu matatizo ya Muungano, hazionekani kabisa kupewa nafasi katika maamuzi ya vipi Muungano huu uendeshwe. Kwa mfano, tumekuwa tukisema mara kadhaa huko nyuma na hapa tutarejea kwamba, tatizo kubwa la Muungano huu, ni kutokuheshimiwa kwa Mkataba wake uliouunda na kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano inahalifu, kwa kiasi kikubwa, makubaliano hayo na kwa hivyo, ni Katiba iliyokwenda kinyume na msingi iliyoienda. Kwamba Muungano huu haukuundwa na wala hautakiwi uongozwe na Katiba bali Mkataba. Kile Katiba zote mbili, ya Muungano na ya Zanzibar, zilichotakiwa kukifanya, ni kuutafsiri Mkataba ule tu na si vyenginevyo. Inapotokezea kuwa Katiba

imesema kinyume na Mkataba wa Muungano, ni Katiba ndiyo ambayo itakuwa imekosea na lazima irekebishwe mara moja kuondoa kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivi tukielewa kuna hivi vikao vya pamoja baina ya Serikali ya Muungano na ya Zanzibar kujadili 'kero' za Muungano. Sisi tunahoji mambo mawili kuhusiana na vikao hivi, kwanza, uhalali wake panapohusika dhati ya Muungano huu na pili, utayarifu wake wa kushughulikia tatizo halisi lililopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhalali wa vikao vya pamoja na dhati ya Muungano. Kwa kuzingatia asili ya Muungano huu, ambayo iko wazi, ni kwamba Muungano wetu ni Muungano uliotokana na sababu kuu tatu, ambazo ni udugu wa kihistoria baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar, vuguvugu la kulileta pamoja Bara la Afrika maarufu kama '*Pan-Africanism Spirit*', na zile hisia kwamba Umoja ni Nguvu (*United We Stand*). Kunatajwa pia sababu za kuipatia ulinzi Zanzibar, ambayo siku mia moja tu kabla ya Aprili 26, 1964 ilikuwa imefanya mabadiliko ya utawala kwa njia ya Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ama iwe sababu hizo zinatosha kueleza asili ya Muungano huu au la, ukweli ni kwamba Muungano ulifanyika na Mkataba wake ukasainiwa na Mwakilishi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Rais Abeid Karume na wa Jamhuri ya Tanganyika, Marehemu Rais Julius Nyerere. Ukweli huu wa kwamba walioitia saini Mkataba wa Muungano, ni wawakilishi wa Tanganyika na Zanzibar, ndio unaojenga hoja ya ukosefu wa uhalali kwa kikao chochote cha kuujadili Muungano ambacho hakihuishi pande husika za Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sisi wa Kambi ya Upinzani, tunaamini kwamba ni kosa kubwa dhidi ya Sheria zinazolinda Mikataba ya Kimataifa na kwa hakika, ni hatua ya hatari kwa hatima njema ya Muungano huu, kwa Ofisi za Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ambayo Zanzibar ni sehemu yake) na Waziri Kiongozi (ambayo ni ya Zanzibar tu kama Mwasisi wa Muungano wenyewe), kujadili mustakbali wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, tunajenga hoja hii kuhusiana na hili, kwanza, wanaostahili kuujadili na kuutolea maamuzi Muungano, ni Serikali ya Zanzibar na mwenzake aliyetiliana saini Mkataba wa Muungano, ambayo ni Serikali ya Tanganyika. Uongozi wa Serikali hizo, ndio waliokuwa washiriki wa mazungumzo ya kuunda Muungano kwa niaba ya nchi zao. Pili, kilichotokea mwaka 1964 ni Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Tanganyika kukubaliana kuanzisha ushirika wao unaoitwa Muungano. Katika kulinda heshima za mataifa yao, viongozi hao waliweka saini Mkataba wa makubaliano yao, ambao una kila sifa ya kuwa Mkataba wa Kimataifa unaostahiki kuheshimiwa na pande husika. Tatu, kutohakana na kwanza na pili hapo juu, kwa hivyo, ni upotoshaji wa makusudi kuuchukuwa mjadala wa nchi mbili zilizoungana na kuukabidhisha mikononi mwa vyombo visivyohusika na kuvipa vyombo hivyo mamlaka ya kufanya maamuzi yote.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha rahisi ni kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, haina sifa ya kuuwakilisha upande wa pili wa Muungano, maana hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo Zanzibar ni sehemu yake. Ifahamike kwamba, hatuhoji uwezo wa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda, kama mtu binafsi. Tunahojoji uwezo wa kisheria wa taasisi anayosimamia kwa mujibu wa Mikataba wa Muungano. Taasisi hii ni taasisi ya Muungano, ambao ndio unaojadiliwa hapa na si taasisi ya Tanganyika, ambayo tunaambiwa haipo!

Mheshimiwa Spika, tunachelea sana kusema kwamba kile kinachofanywa sasa na ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ni kizungumkuti; maana ni kukichukuwa kiumbe na kukiweka na mmoja kati ya waumbaji wake kukijadili kiumbe hicho. Kiumbe hapa ni Serikali ya Muungano na mmoja wa waumbaji ni Serikali ya Zanzibar. Tutaendelea kufanya kizungumkuti hiki hadi lini? Huku, kwa makusudi, tukizikengeuka Sheria za Kimataifa, kama ile ya *Common Law* na *Vienna Convention*, ambazo hutakiwa kuongoza Mikataba ya Kimataifa kama huu wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, Kambi yetu inasema haya ikijuwa wazi kwamba, kumekuwa na kisingizio kutoka upande wa Serikali ya Muungano kwamba hakuna Serikali ya Tanganyika na hivyo, haiwezekani kwa Serikali ya Zanzibar kufanya mazungumzo na Serikali isiyokuwepo. Sisi tunasema kwamba hiki ni kisingizio dhaifu na cha hila tu. Ni dhaifu kwa kuwa hata kwa kuuliza swali jepesi la “kwani Muungano huu ni wa nani na nani?”, jibu litakuwa ni wa Tanganyika na Zanzibar. Ni cha hila kwa sababu mbili, kwanza, hakuna popote kwenye Mikataba wa Muungano ambapo paliagizwa kufutwa kwa Serikali ya Tanganyika baada ya Muungano huu. Kwa mujibu wa Makubaliano hayo, Serikali ya Tanganyika, kama ilivyo ile ya Zanzibar, imelindwa na Kifungu Na.(v) kinachosomeka kwamba:-

“The existing laws of Tanganyika and of Zanzibar, shall remain in force in their existing territories.”

Mheshimiwa Spika, Wataalamu wa Katiba na Sheria, wanafahamu kwamba Katiba ndiyo “Sheria Mama” ya sheria zote na hivyo, Katiba ya Tanganyika imelindwa na inapaswa kuwepo na Serikali yake iwepo pamoja na viongozi wake kuwepo na kusimamia mambo ya Tanganyika yasiyokuwa ya Muungano. Katiba na Sheria za Tanganyika ndizo zilizotakiwa zitumike katika eneo la Tanganyika kwa yale mambo yasiyokuwamo kwenye Muungano. Hiyo ndiyo maana ya ‘respective territories.’

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kilichofanywa na Bunge la Tanganyika, tarehe 25 Aprili 1964, siku moja kabla ya Muungano, kuifuta Serikali ya Tanganyika kwa kutumia Sheria Na.22 iliyoitwa *“The Union of Tanganyika and Zanzibar”*, kilikuwa kinyume na makubaliano ya Muungano. Bahati mbaya, kitendo kile mpaka leo kimebakia kikiongeza shaka kwamba Tanganyika ilijiingiza kwenye Serikali ya Muungano na kujifanya nchi mpya yenye jina jipya la Tanzania na yenye mipaka mipyga ya kijiografia.

Mheshimiwa Spika, tunasema haya tukijua uzito na uchungu wake. Ni vigumu kukiri kwamba tulifanya makosa, ikiwa kosa hilo linaonekana kuwa na maslahi. Lakini ukweli ni kuwa, kosa haliwezi kuwa na maslahi ya kudumu, hata kama linajaribiwa kufifilishwa kila mara. Kufuta Katiba ya Tanganyika kulikofanywa na vifungu vya

Sheria, hii kulikuwa ni kosa. Kuifuta Serikali ya Tanganyika, kulikuwa ni kosa na kosa hilo ndilo leo hii lililozaa kosa lingine la kiumbe kuzungumza na mmoja wa waumbaji kuhusiana na hatima ya kiumbe hicho. Hivi ndivyo tunavyohoji uhalali wa vikao baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano (ambayo inawakilisha kiumbe, Muungano) na Ofisi ya Waziri Kiongozi (ambayo inawakilisha Muumba, Zanzibar).

Mheshimiwa Spika, tunapenda kurejea kauli yetu ya mwaka jana, kwamba pale mwaka 1992, Bunge hili Tukufu lilipofanya maamuzi ya kurejeshwa kwa Serikali ya Tanganyika, lilikuwa limepitisha uamuzi wa busara kama uliopitishwa na Chama cha TANU mwaka 1958 kule Tabora kuingia kwenye mfumo wa kura tatu. Bali zaidi ya hapo, Bunge hili Tukufu lilikuwa limefanya kitendo cha kisheria na cha kimantiki. Uamuzi ule ulikuwa sahihi wakati ule, ni sahihi leo hii na utakuwa sahihi kesho, maana sio tu kwamba uliakisi matakwa halisi ya Mkataba wa Muungano uliokuwa umetiwa saini zaidi ya nusu karne nyuma yake, bali pia ulikuwa ni kielelezo cha kujitathmini kulikofanywa na Waheshimiwa Wawakilishi wa Watanzania kupitia chombo chao hiki. Ni bahati mbaya sana kwamba, maamuzi yale ya Bunge yalikuja kuwekwa kando na kufanya busara iliyotumika kuonekana kama si lolote si chochote!

Mheshimiwa Spika, ni kutekelezwa kwa Azimio lile tu, ndiko ambako kungelivipa maana vikao hivi baina ya Ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Bila ya kuwepo kwa Serikali ya Tanganyika iliyo hai na inayotambulika, vikao hivi vyta mazungumzo vinabakia kuwa vikao vyta mazungumzo tu. Kwani hata Katiba inasema, matatizo ya Muungano yatatatuliwa kwa kupitia Mahakama ya Katiba na sio vikao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchelea kuitumia Mahakama ya Katiba, ndio leo tunashuhudia kushindwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Pamoja wa Fedha wa Muungano, kuwa na chombo kinachoshughulikia michezo, mgawano wa mapato ya Muungano, kuondolewa kwa nafasi ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais au mbadala wake na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utayarifu wa kushughulikia tatizo halisi. Labda kwa manufaa ya mjadala huu, tunaweza kusema tujipumbaze kidogo na tuseme ni kweli vikao vyta pamoja kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ofisi ya Waziri Kiongozi, vina uhalali wa kisheria kuwepo na vinawakilisha dhati yenewe ya Muungano. Natukubaliane kutokukubaliana na hilo ili mjadala uende mbele. Hata ikiwa ndivyo, basi bado vikao hivi vitahojika kwamba havikai kwa mnasaba wa kutatua tatizo halisi la Muungano lililopo, bali kwa kuziba dalili za tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, sisi wa Kambi ya Upinzani, tumekuwa wazi sana katika hili. Hatutafuni maneno kusema kwamba tatizo kubwa na la msingi ni kutokuheshimiwa kwa Mkataba wa Muungano, ambako kunatokana na ukosefu wa dhamira njema. Tulilisema hilo mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu tunalirudia kwamba wa kujadiliwa ni Mkataba wa Muungano tu, *Article of Union* na kuona namna gani Muungano uliozaliwa na Mkataba huo unakidhi vipengele vilivyokubaliwa na wale waliouwekea saini. Ni mjadala wa kina juu ya Mkataba wa Muungano ndio utakaothibitisha kuwa Serikali ya Tanganyika haikutakiwa kufa na kama imekufa iliuliwa kimakosa na kama ni kosa, basi

linaweza kurekebishwa kwa kutangazwa rasmi kuwepo kwa Serikali ya Tanganyika kama yalivyokuwa maamuzi ya Bunge hili Tukufu mwaka 1992. Maana, kwa hakika hasa, hili la kutokuheshimiwa kwa Mkataba wa Muungano, ndilo tatizo sugu la Muungano huu na ambalo vikao hivi nya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, havioneckani kuiona haja ya kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Muungano si mgao wa asilimia 4.5 kutoka kwa Serikali ya Muungano kwenda kwa Zanzibar. Tatizo si Zanzibar kuwa na au kutokuwa nchi ndani ya Muungano. Tatizo si nishati za gesi na mafuta kuwa na au kutokuwa za Muungano. Tatizo si Zanzibar kuijunga na au kutokujiunga na Jumuiya ya Nchi za Kiislam Duniani, *OIC*. Tatizo si Wazanzibari kushikilia nafasi katika Serikali ya Muungano katika mambo ambayo si ya Muungano wakati ambapo Watanganyika hawawezi kufanya hivyo katika Serikali ya Zanzibar. Haya yote ni matokeo ya tatizo moja kubwa, nalo ni kutokuheshimiwa kwa Mkataba wa Muungano kuanzia mwanzo kabisa wa Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, ni hapa ndipo ambapo mjadala wa vikao nya Ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ulikuwa utuame. Kuuzungusha na kuuelekeza mjadala huu kwingine kokote kule, hakusaidii chochote katika kutatua hiki kilichopewa jina la kero za Muungano, bali kuzidi kukitia matata. Hatusemi hivi kwa kuwa tunadharau umuhimu wa kuzungumza, bali kwa kuwa tunatiwa hofu na maendeleo na mwendelezo wa mazungumzo yenye. Tunajiuliza, Hivi hawa wenzetu wanakusudia kutupeleka wapi? Pale penye visheni ya “Tanzania yenyeye Muungano Imara” au penye misheni ya ”Kuwa na Ufanisi katika Kuimarisha Muungano” kama inavyoelezwa kwenye dira na muelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)?

Mheshimiwa Spika, baada ya yote, kwani nini maana ya Muungano Imara na hivyo, kuimarisha Muungano? Je, si kukichukua kila kitu cha upande mmoja wa Muungano na kukiingiza kwenye Muungano au kukifanya kila cha upande mmoja kuvuuka maji na kuwa cha upande wa pili?

Mheshimiwa Spika, baada ya ile Semina Elekezi kwa Watendaji wa Serikali iliyofanyika Ngurdoto, mwanzoni mwa muhula wa uraisi wake, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, akizungumzia mipango yake ya kuimarisha Muungano, alisema kwamba, hakuona kuwa Muungano ulikuwa na tatizo kubwa zaidi ya kukosekana kwa mazungumzo ya mara kwa mara baina ya pande mbili zinazohusika. Kwa hivyo, hima akaitisha utaratibu huu ili hata kama hapana jambo kubwa sana, basi angalau watu wakutane kwa kunywa chai na kahawa pamoja na kubadilishana mawazo.

Mheshimiwa Spika, hakika kabisa, kukutana kunywa chai na kuzungumza mambo yanayohusu hatima ya Taifa, ni jambo zuri sana, lakini mwenendo wa mambo katika kukutana huku unatukumbusha kile kisa cha tarehe 10 Agosti 1957, wakati Chama cha Kupigania Uhuru cha Tanganyika, *Tanganyika African Union, TANU*, kilipokuwa

kinafungua tawi lake katika mtaa wa Mvita, nyumba namba 10, Dar es Salaam. Katika sherehe hiyo muhimu, *TANU* iliwaalika wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria, wengi wao wakiwa Machifu kama vile Chifu Kidaha Makwaia, Humbi Ziota, Msabila Lugusha, Mwami Theresa Ntare na wengineo na ikawakirimu waalikwa wao vitafunwa, vinywaji baridi na chai. Katika kutoa shukrani za *TANU* kwa wananchama wa *TANU*, Mwalimu Nyerere alikamata kikombe cha chai na kukionyesha juu kwa wasikilizaji wake. Akawaambia:-

“Msidhani kwamba kitendo cha kumpa mtu chai ni kitu kidogo, maana kuna watu wameiuza nchi hii kwa kupewa kikombe cha chai na Wakoloni”.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaheshimu sana na tunaamini njia ya mazungumzo kama suluhisho la pekee kufikia utatuzi wa matatizo yanayolikabili Taifa, hatuamini kuwa mazungumzo kwa maana ya mazungumzo tu, yanaweza kutufikisha popote. Mazungumzo yenye uwezo huo wa kutoa suluhisho, ni yale yanayozingatia nini kinazungumzwa, nani wanazungumza vipi na kwa nini yanazungumzwa. Kila moja kati ya maswali haya, lina maana kubwa kwa hitimisho na suluhisho litokanalo na mazungumzo yenye. Tunachelea kusema kwamba, haya yanayofanyika baina ya Ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ni mazungumzo kwa manufaa ya mazungumzo na sio mazungumzo kwa manufaa ya suluhisho na kwayo, fedha za walipa kodi wa nchi hii zinateketea lakini tatizo la Muungano halitatuliwi, zaidi ya kulizidisha.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe mfano mmoja wa karibuni kati ya mingi iliyokwishatokeza, kuthibitisha hofu yetu kwamba mazungumzo haya hayatatui tatizo halisi la Muungano. Mfano huu unahu Ripoti ya Baraza la Mapinduzi la Zanzibar ya 2003.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Mei 2003, Ikulu ya Zanzibar ilichapisha Ripoti ya Baraza la Mapinduzi juu ya Matatizo na Kero za Muungano na Taratibu za Kuziondoa, ambapo katika Sura yake ya Tatu, ripoti hiyo ilitoa orodha ya mambo yanayopaswa kuondolewa katika Muungano. Mambo hayo ni; Mafuta na Gesi Asilia, Elimu ya Juu, Posta, Simu (Mawasiliano), Biashara ya Nje, Kodi ya Mapato, Ushuru wa Bidhaa, Usafiri wa Anga, Takwimu, Utafiti, Ushirikiano wa Kimataifa, Leseni za Viwanda, Polisi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa haya yanatekelezwa, *SMZ* ilitaka kuwepo kwa misingi mitano ya kuzingatiwa, ambayo ni:-

(a) Masuala ya Muungano yalindwe kwa misingi ya Katiba na Sheria badala ya siasa na maelewano;

(b) Muungano uwe na maeneo machache yanayoweza kusimamiwa na kutekelezwa kwa urahisi;

- (c) Muungano uanishe washirika wake wakuu, mipaka na haki zao;
- (d) Muungano utoe fursa sawa za kiuchumi kwa pande zote mbili za Muungano; na
- (e) Lazima pawe na Muungano unaoweza kuhimili mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo *SMZ* ilivyosema tangu mwaka 2003 na kwa hakika angalau katika hili, Serikali hii imesema vile ambavyo Wazanzibari wamekuwa wakisema tangu siku za mwanzo za Muungano huu. Ni wazi kuwa, ripoti hii ya *SMZ* iko mezani kwenye Ofisi zote mbili, ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Lakini kinachotokezea kila baada ya kikao cha Watendaji Wakuu wa Serikali mbili, ni taarifa ya kuhuzunisha panapohusika kile hasa kinachohitajika kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, taarifa ya kikao cha mwisho cha mwezi Mei 2009, iliyotolewa na Ofisi ya Makamu Rais, Idara ya Muungano, ilisema kwamba kero tatu za Muungano zimeshafutwa na sasa si kero tena. Kero hizo ni Tume ya Haki za Binaadamu, Uvuvi wa Ukanda wa Bahari na Shughuli za Biashara ya Meli. Katika mawili ya mwanzo, kufutwa kwake kutoka orodha ya kero, ni kwa mambo hayo kukubalika rasmi kuwa ya Muungano, ambapo sasa upande wa Zanzibar umeridhia. La mwisho kufutwa kwake ni kwamba Zanzibar inaruhusiwa kuendesha shughuli za biashara ya meli kwa kushirikiana na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni nini? Ni kwamba, kumbe hakuna pendekezo lolote la kupunguza idadi ya mambo ya Muungano, kama yalivyo matakwa ya Zanzibar, linaloweza kuwa linajadiliwa na vikao hivi vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi; maana inaonekana wahusika wa vikao hivi wameshaamua kuwa kupunguza orodha ya mambo ya Muungano hakuwezi kuimarisha Muungano, bali kinyume chake ndicho sawa! Yaani, kuimarisha Muungano kuna maana moja tu, nayo ni ama kukichukua kila cha Zanzibar na kukifanya cha Muungano na, au, kukifanya kila kilichoko Tanzania Bara kivuke maji na kiwe cha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge hili Tukufu na Watanzania, waniwie radhi kwa kusema kwamba, wakubwa wetu wameufanya Muungano huu ushabihiane sana na kile kisa cha Mfalme Jeta aliyemo kwenye riwaya ya Kusadikika ya Marehemu Sheikh Shaaban Robert. Mfalme huyu alikutwa na mjumbe wa Kusadikika akiwa amekaa katika eneo ambapo mto uliokuwa unakokozoa kila kitu, mawe, magogo, majengo, na kadhalika, unatiririkia kinywani na kuishia tumboni mwake, lakini kila mara alisikikana akilia: "Njaa! Njaa! Kiu! Kiu!". Hivyo ndivyo Muungano wetu ulivyofanywa, kwamba uwe unakula na kunywa kila kitu na bado kila siku uwe unalalamika kufa njaa na kiu. Ili kuufanya usife, wakubwa wanaamua kuulisha kila cha Zanzibar na kila cha Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ikiwa hali ni hii, je, si sawa kusema kwamba tunatoka kwenye Serikali mbili zilizopo sasa kuelekea Serikali moja? Je, jukumu la vikao hivi vya Ofisi za Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ni kuratibu na kusimamia mchakato wa kubadilisha muundo wa Muungano? Je, hivyo ndivyo Wazanzibari na Watanganyika walivyotaka yawe matokeo ya vikao hivi vya kunywa chai na kahawa? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sisi wa Kambi ya Upinzani, hatuoni kwamba Vikao hivi vya Pamoja vinakuja na suluhisho la tatizo la Muungano huu, bali vyenyewe ni sehemu ya tatizo. Kwa hivyo, ili kutimiza wajibu wetu kama Bunge la Watu lenye jukumu la kusimamia matumizi fedha za walipa kodi, tunaliomba Bunge hili liitake Serikali ya Muungano isitishe mara moja vikao hivi na badala yake Mkataba wa Muungano uletwe Bungeni hapa kama nukta kuu ya mjadala. Hapo ndipo tuanzie na tumalizie kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu siasa za Serikali ya Muungano Kuelekea Muungano. Nimetangulia kusema kwamba, kinachonisimamisha hapa ni utamaduni wa kawaida kwamba kila Wizara ya Serikali lazima isemewe na Wizara Kivuli Bungeni baada ya Wizara hiyo kuwasilisha bajeti yake, lakini sio kwa imani kwamba hiki tunachokisema kinachukuliwa na Serikali kwa umakini kama sehemu ya mawazo ya Watanzania yanayopasa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi yetu inaitupia lawama za moja kwa moja Serikali ya Muungano kwamba imejiundia siasa zake maalum kuelekea suala la Muungano huu. Siasa hizo zinasomeka katika nukta mbili; moja ni kupuuzia maoni yoyote yanayotolewa na watu kuhusiana na Muungano wenyewe na ya pili ni kuudharau uhalisia wa Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kupuuzia maoni yanayohusu Muungano, nilitangulia kusema kwamba, panapohusika suala la Muungano, Watanzania tuna bahati mbaya ya kuwa na Serikali yenyе utamaduni wa kujifungia kwenye kuta nne, ikajisemesha yenyewe, ikitisikiliza yenyewe na kisha ikatoka na mwangwi wa sauti yake yenyewe kwenda kuufanya kazi. Bila ya shaka, haya hayakuanza leo, bali ni muendelezo wa utamaduni huo mkongwe; kwamba kila kinachosemwa na Watanzania wengine wowote ambao hawamo kwenye *Super Structure* ya Muungano, ni kelele za mlango ambazo hazimzuii mwenye nyumba kulala. Kitabu cha bajeti iliyopo mbele yetu sasa ni shahidi wa hayo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia *Hansard* ya tarehe 20 Agosti, 2008, wakati Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Rais (Muungano), akifanya majumuisho ya michango ya bajeti ya Wizara yake, utakuta ahadi ya Mheshimiwa Waziri kuyachukua na kuyafanya kazi maoni ya Kambi ya Upinzani. Labda nikumbushe tu kuwa, maoni ya Kambi hii mwaka jana yalijikita katika mambo tisa muhimu ambayo ni; Muundo wa Muungano, Shughuli za Muungano, Mambo ya Muungano, Nafasi ya Muungano katika Mpasuko na Muafaka wa Wazanzibari, Mapungufu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Matumizi ya Tanzania Bara Ndani ya

Muungano, Akaunti ya Pamoja ya Fedha, Nafasi ya Zanzibar katika Benki Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Katiba, Jaji Mkuu na Mahakama ya Rufaa na Hoja ya Serikali Tatu.

Mheshimiwa Spika, katika kila moja ya mambo hayo, tulionesha tatizo lilipo na tukapendekeza Suluhisho lake. Leo hii, mwaka mmoja baadaye, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), inawasilisha bajeti yake, ikiwa sio tu kwamba haikutekeleza ahadi yake ya kuyafanya kazi maoni yetu, bali hata maelezo ya kushindwa kufanywa hivyo hayapo. Katika hali kama hii, ambapo mtu ameshasema kila kile alichopaswa kukisema na bado pakawa hapana mabadiliko, Waingereza wana msemo: “*Need we say more!?*” Nasi tunaiuliza Ofisi ya Makamo wa Rais (Muungano), kipi chengine tukiseme hata kitoshe kuisaidia kuuimarisha Muungano huu kwa misingi ya uadilifu na usawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi zimekuwa ndizo siasa za Muungano kuelekea Muungano wenyewe. Kwamba yejote ambaye anashauri chochote kuhusu Muungano huu na ikiwa hayumo kwenye “*super structure*” ya Muungano wenyewe, basi mawazo yake yaishie hapo hapo anapoyatoa. Serikali ya Muungano haikumsikiliza Mzee Aboud Jumbe aliyekuwa Rais wa Zanzibar, haikulisikiliza hata Bunge hili lilipopitisha Azimio la Kuundwa kwa Serikali ya Tanganyika, haikusikiliza Tume za Nyalali na Kisanga zilizoshauri muundo wa Serikali Tatu na haitusikilizi sisi wa Kambi ya Upinzani. Ni nani inayemsikiliza? Inajisikiliza yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuudharau uhalisia wa Muungano. Tunapozungumzia Muungano wetu, kuna mambo mawili ambayo ndio uhalisia wake, kwanza, huu ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, nchi mbili zilizokuwa na mamlaka kamili na ambazo zilisalimisha baadhi ya mamlaka yake hayo kwenye chombo kimoja huku kila upande ukibakia na sehemu nyingine ya mamlaka yake. Huu si Muungano baina ya mkubwa na mdogo panapohusika hadhi ya nchi zilizoungana, maana eneo la kijiografia wala idadi ya watu havikuwa vitu vilivyoamua kuwepo na kutokuwepo kwa Muungano, kwa hivyo, haviwezi leo kuamua uendeshwaji wa Muungano wenyewe. Pili, ni ukweli kwamba huu Muungano ni kitu kikubwa na muhimu sana kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, wakati huo, ndio uhalisia kuhusu Muungano, siasa ya Serikali ya Muungano inaonesha vingine. Angalia, kwa mfano, mjengeko wa Serikali hii katika uwiano wa nafasi zinazoshikiliwa na watu kutoka pande hizi mbili kwenye Wizara za Muungano. Uwakilishi wa Zanzibar ni wa kulazimisha kama kwamba Zanzibar ni mwalikwa tu na sio mwenza wa Muungano wenyewe. Inapotokea Mzanzibari amepewa nafasi katika Wizara hiyo, huwa ni kwa kukaribishwa na, au, kukirimwi tu. Hata hii Idara ya Muungano iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, mambo ni hayo hayo. Tunamuomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, alieleze Bunge lako, uwiano uliomo kwenye Idara yake panapohusika mizania ya pande mbili za Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linakwenda sambamba na utatanishi wa makusudi unaofanywa na Serikali ya Muungano na, kwa hakika, hata hili Bunge lako Tukufu. Utatanishi wenyewe ni kwamba, kwa upande wa Serikali ya Muungano, imefanya mara nyingi huko nyuma, kumpa Mzanzibari kuongoza Wizara ambayo si ya Muungano; ikijua fika kwamba huko ni kinyume cha mantiki ya Muungano wenyewe na kwamba kunachochea malalamiko ya haki kutoka kwa Watanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, si jambo la haki hata kidogo, kwa mfano, kwa Mzanzibari kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, au Maliasili na Nishati, maana hayo si mambo ya Muungano. Wako Watanzania Bara wenyewe uwezo mkubwa kuongoza Wizara hizo na hata humu Bungeni, si jambo la haki kwa Wabunge kutoka Zanzibar kujadili na kuamua mambo ya Tanzania Bara ambayo si ya Muungano. Si haki pia kwa Serikali ya Muungano kuunda Wizara ambazo zinachanganya mambo yaliyo na yasiyo ya Muungano katika kapu moja, kama ilivyo, kwa mfano, katika suala la elimu ya juu, sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utatanishi wa kwanza unazalisha malalamiko kwamba Wazanzibari wanafaidika na kudekezwa sana na Muungano huu, kama yaliyo mawazo ya wenzetu wengi wa Tanzania Bara, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu, kama ilivyodhirika mwaka jana katika michangio ya mjadala wa Zanzibar kuwa na kutokuwa nchi. Utatanishi wa pili unazalisha malalamiko kwamba Serikali ya Muungano inafanya hila za makusudi kuinyang'anya Zanzibar kila kile kilichokuwa chake.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba huu ni utatanishi wa kimtego na wa kufunika kombe, ambao azma yake kubwa ni kufilisha ile hoja tunayojenga kila siku ya kwamba lazima Serikali ya Tanganyika ije juu, ionekane na ifanye kazi zake rasmi kuwakilisha na kusimamia matakwa na maslahi ya Watanganyika yasiyokuwa ya Muungano. Bila ya kuwa na Chombo cha Kutunga Sheria cha Tanganyika kama kulivyo na Chombo cha Kutunga Sheria cha Zanzibar na bila ya kuwa na mamlaka tafauti ya utawala ya Tanganyika kama kulivyo na mamlaka ya utawala ya Zanzibar, tutaendelea kuwa mbali kabisa na uhalisia wa Muungano kama yaliyo matakwa ya Mkatuba.

Mheshimiwa Spika, kuudharau kwingine uhalisia wa Muungano, ni kulidogosha suala zima linalohusu Muungano wenyewe. Angalia, kwa mfano, Muungano mzima umewekwa ni Idara tu ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo ina idara nyingine kadhaa. Wakati Rais Jakaya Kikwete aliona umuhimu wa kuunda Wizara maalum kushughulikia Afrika ya Mashariki, hakuona kabisa umuhimu wa kuwa na Wizara kamili kushughulikia Muungano. Hili linaonesha namna Serikali inavyoudharau Muungano kama kwamba ni suala dogo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda hapa linakuja suala la ufundi na la kimantiki kwa wakati mmoja; kwamba katika mjengeko wa utawala Serikalini, majina ya vyeo vya wakuu wa vitengo hunasibiana na vitengo vyao, kwa mfano Mkuu wa Kurugenzi, ni

Mkurugenzi na Mkuu wa Wizara, ni Waziri. Sasa, kwa kuwa hakuna Wizara ya Muungano, isipokuwa kuna Idara ya Muungano kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, Mkuu wa Idara hiyo ni nani? Ni vyema tukaeleweshwa!

Mheshimiwa Spika, hitimisho na mapendekezo, kutokana na kupuuzwa na kudharauliwa kwa makusudi kwa matatizo ya Muungano huu, hakujawahi kupita muongo ambapo Muungano hautikiswi na kutikisika. Kwa bahati mbaya ni kwamba, kila Muungano unapotikisika, machoni mwa wakubwa huonekana kama kwamba unatikisika kwa kuwa hauna mambo ya kutosha na, hivyo, kama vile Mfalme Jeta wa Shaaban Robert alivyokuwa akila na kunywa kila kilichopo, basi nao wakubwa huzidi kuumiminia Muungano kila cha Zanzibar na kila cha Tanzania Bara tumboni mwake. Hilo ni kosa kubwa katika sayansi ya utatuzi wa migogoro. Wahenga husema:-

"Ganga shina, matawi hayagangika!"

Kwa maana ya kuwa, kutibu maradhi ni kukitibu chanzo chake na sio dalili zake. Ni kosa kutokujuiliza kwa nini Muungano huu unatikisika, haushibi na kujiuliza tu vipi unatikisika, unalilia njaa na kiu. La kujiuliza ni ikiwa hivi kweli Muungano huu uliumbwu na roho ya kushiba na kukinai au uliumbwu na uroho wa kufakamia na kusaza kila kitu? Ikiwa hivyo ndivyo, kuna siku kutakuwa na cha Zanzibar tena na, au, cha Tanzania Bara peke yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika jumla ya michango iliyotoka hapa mwaka jana wakati wa mjadala wa Zanzibar kuwa na kutokuwa nchi, wabunge wako kutoka Zanzibar walikumbushwa msemo wa Kiingereza usemao:-

"You can not eat your cake and have it!"

Kwa maana ya kuwa, mtu hawezi kuila keki yake na bado akaendelea kuwa nayo. Ni ama aile imalizike na asiwe nayo au asiile kabisa ikiwa anataka kubakia nayo.

Mheshimiwa Spika, leo hii nataka nilikumbushe Bunge hili Tukufu kwamba kuna pande nyingine za ukweli katika suala hili la keki; nazo ni kuwa, kwanza, kuna mtu kutokuila keki yake na bado asiwe nayo na, pili, kuna mtu kuila keki yake na kuendelea kuwa nayo. Ripoti niliyoitaja hapo juu, iliyotayarishwa na *SMZ* Mei, 2003, inaweza kabisa kuthibitisha pande hizi za ukweli mwengine kuhusu keki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukionesha mara zote kwamba chanzo cha matatizo ya Muungano huu ni kutokuheshimiwa kwa Mkataba wake uliouunda. Tunarejea tena kusema hapa kwamba Muungano huu hauongozwi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, bali unaongozwa na Mkataba wa Muungano wa mwaka 1964. Katiba ya Muungano na ile ya Zanzibar, zinatakiwa zitafsiri tu yale yaliyomo kwenye Mkataba na sio kuongeza wala kupunguza.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, basi kama ni suluhisho, sisi wa Kambi ya Upinzani tunatoa jibu kama lile alilowahi kulitoa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, mwaka 1985, alipoulizwa ni kipi kiapumbele chake katika kujenga Tanzania. Mzee Mwinyi alijibu: "Barabara!" Alipoulizwa kipi kingine, akajibu "Ni barabara!" Alipoulizwa kipi kingine akasema "Ni barabara!". Kwenye Uislam kuna hadithi kwamba Mtume, SAW, aliwahi kuulizwa, ni nani wa kutendewa mema zaidi baina ya wazazi wawili, akajibu: "Mama!" alipoulizwa tena nani, akajibu: "Mama!" Alipoulizwa tena, nani, akajibu: "Mama!"

Mheshimiwa Spika, basi ikiwa Bunge lako hili Tukufu litataka kujuwa ni kipi ambacho sisi wa Kambi ya Upinzani tunaamini kuwa ni suluhisho la matatizo yote ya Muungano huu, tutajibu kuwa ni "Kurudi kwenye Mkataba wa Muungano!" Tukiulizwa ni kipi kingine, tutasema "Ni kurudi kwenye Mkataba wa Muungano!" Hata tukiulizwa mara ya tatu, tutasema "Ni kurudi kwenye Mkataba wa Muungano!" Si vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, wala si Tume zisizokwisha za kuangalia kero za Muungano. Ni kuutekeleza na kuuheshimu Mkataba wa Muungano tu ndiko kunakotakiwa. Tukitaka kubadili, turudi kwa Watanganyika na Wazanzibari, tuwaulize ili watupe majibu.

Mungu Ibariki Tanzania. Mungu Ibariki Afrika. Naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Nilikuwa nataka kukumbusha tu kwamba Mkataba wowote wa Kimataifa ili ufanye kazi ni lazima utafsiriwe katika Katiba na Sheria.

Tunaendelea, sasa ni zamu ya Mwenyekiti, kwenye masuala ya mazingira, Mheshimiwa Ndugai!

MHE. JOB Y. NDUGAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lolesia J.M. Bukwimba, Mbunge, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Busanda. Kamati inakukaribisha sana katika ujenzi wa Taifa na kutetea maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati, tunatoa salamu za rambirambi kwa Watanzania wote kwa vifo vya Sheikh Gorogosi na Mwalimu wetu, Profesa Haroub Othman. Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu hao mahali Pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Watendaji Wakuu wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri hapa Dodoma na kupitia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa mwaka 2008/09 na pia kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Aidha, katika majadiliano, Kamati ilifahamishwa dira na mwelekeo wa ofisi pamoja na majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina idara nne, vitengo vinne pamoja na Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais. Idara hizo ni; Idara ya Mazingira, Idara ya Muungano, Idara ya Utawala na Utumishi, Idara ya Sera na Mipango. Vitengo vya Ofisi ya Makamu wa Rais ni Uhasibu na Fedha, Ukaguzi wa Ndani, Manunuzi pamoja na Habari. Aidha Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ina Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira, *NEMC*.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kujadili viambatisho (ripoti zinazotoa maelezo ya ziada) vifuatavyo; Mihtasari mbalimbali ya miradi inayoratibiwa na Idara ya Mazingira, Muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*GEF*), Muhtasari wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira inayoratibiwa na Idara ya Mazingira, Taarifa ya upandaji miti kipindi cha 2007-2008, Utaratibu wa kushiriki katika biashara ya hewa-mkaa (*carbon trading*), Taarifa ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) 2008/2009 kuhusu Mipango ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha ujao 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili bajeti ya Ofisi hii, Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Batilda Buriani, kwamba maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010, yamezingatia mikakati na maagizo ya Serikali yaliyohusu usimamizi na uhifadhi wa Mazingira, mchakato wa kufikiwa kwa malengo ya milenia na yale ya *MKUKUTA* pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Sera mbalimbali na Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008. Katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali yaliyohusu sekta ya mazingira. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kiasi kikubwa imefanya kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Baadhi ya utekelezaji huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa tamko la Mheshimiwa Makamu wa Rais la kuitaka kila Wilaya kupanda miti milioni 1.5. Jumla ya

Wilaya 43 zimevuka lengo hilo kama lilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji;

(ii) Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini (2008) imekamilika na kupidishwa na Baraza la Mawaziri, ripoti hii itawasilishwa Bungeni pindi itakapomalizika kupigwa chapa;

(iii) Kanuni tisa za Sheria ya Mazingira zimekamilika na nyingine bado zipo kwenye mchakato. Kanuni zilizokamilika ni:-

- Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira;
- Kanuni za Viwango vya Ubora wa Mazingira katika Maji, Udongo na Hewa;
- Kanuni za Usajili wa Wataalamu wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira;
- Kanuni za Kudhibiti Utengenezaji na Uuzaji wa Mifuko ya Plastiki;
- Kanuni za Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira;
- Kanuni za Tozo mbalimbali za Mazingira;
- Kanuni za Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni.

(iv) Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, zimeandaa Programu ya Kitaifa ya Elimu kwa Umma na imeanzwa kutekelezwa kwa kutumia vyombo vya habari, makala, machapisho pamoja na kushiriki katika maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa; na

(v) Baraza limeendelea kufanya tathmini ya athari ya mazingira kwa miradi mbalimbali inayoanzishwa nchini. Aidha, katika maeneo mbalimbali ambayo Kamati imeona juhudzi zaidi zinahitajika, imetoe maelekezo na kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009, ofisi ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 3,603,000/= kama mapato ya Serikali yanayotokana na makato mbalimbali. Hadi kufikia mwezi mei 2009, makusanyo halisi ya mapato yalifikia Shilingi 11,986,600=/. Ongezeko la mapato haya, yametokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya masurufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, iliidhinishiwa na Bunge, kiasi cha Shilingi 35,157,086,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Fungu 31. Hadi kufikia tarehe 25 Mei 2009 jumla ya shilingi 33,918,684,661/= zilipokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya Fungu hili. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya shilingi 19,711,992,400/= ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 31- Mazingira ili kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2009 jumla ya shilingi 9,247,262,463/= tu, zilikuwa zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, mafanikio; kwa kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya Mwaka 2004 na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji; mafanikio yafuatayo yameonekana:-

- (i) Utekelezaji wa Mradi wa Hifadhi ya Bonde la Ziwa Tanganyika chini ya Programu endelevu ya Ziwa Tanganyika ulianza kutekelezwa rasmi Novemba 2008;
- (ii) Kiasi cha dola za Marekani milioni mia moja (100,000,000) zilitolewa na Serikali ya Norway kwa ajili ya utunzaji wa misitu na udhibiti wa uharibifu wa misitu kwa lengo la kupunguza gesijoto chini ya mfumo wa *Reducing Emissions from Deforestation and Forest Degradation, REDD*;
- (iii) Mwamko wa matumizi ya nishati mbadala umeanza kuonekana hasa katika matumizi ya gesi asilia, tungamotaka, makaa ya mawe na mabaki ya mbao (*saw dust*);
- (iv) Kampeni ya kupanda miti na kuitunza imeendelea nchini kwa mafanikio makubwa. Katika mwaka 2007/08 jumla ya miti 245,970,955 ilipandwa na miti 213,872,564 ilioti hii ikiwa sawa na asilimia 87 ya miti iliyopandwa;
- (v) Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini 2008, imekamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri. Ripoti hii ipo mbioni kuwasilishwa Bungeni;
- (vi) Uoto wa asili unaohifadhi unyevunyevu na maji umeongezeka katika bonde la Ihefu baada ya mifugo kuondolewa;
- (vii) Ukaguzi wa mara kwa mara kwa viwanda umefanyika ili kulinda mazingira na kutoa maelekezo ya kuyarekebisha. Aidha Ofisi imesimamia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Kanuni iliyopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, kama ilivyoeleza kabla yangu na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mazingira, Mheshimiwa Dokta Batilda Buriani kwenye Hotuba yake hapa Bungeni mapema leo;
- (viii) Elimu ya mazingira kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali hususan ardhi, maji na nishati imeendelea kutolewa kwa umma kupitia vipindi vya elimu kwa

umma kwa kupitia televisheni, redio, machapisho, vipeperushi, mabango, kalenda na maonesho;

(ix) Ripoti za tathmini ya athari kwa Mazingira zimeendelea kuandaliwa ili kuongeza utekelezaji na uwezeshaji wa miradi ya maendeleo. Ofisi kwa kushirikiana na makampuni ya simu za mkononi imehakikisha minara yote ya mawasiliano ya simu inaandikishwa, kutambuliwa na kukaguliwa ili kuondoa kero zilizotolewa na wananchi kuhusu kelele za mitambo ya simu;

(x) Ofisi imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lilipo Mtaa wa Luthuli Kiwanja Na. 10 na Watumishi wote wa Idara na Vitengo wameshamamia. Aidha ujenzi wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar unaendelea vizuri;

(xi) Baraza la Hifadhi ya Mazingira, *NEMC*, limeendelea kuchapisha Kanuni za Kisheria na kusambaza miongozo kuhusu usimamizi wa mazingira inayolenga kuzuia na kupunguza uharibifu wa mazingira;

(xii) Mazungumzo ya awali kuhusu andiko la Mradi wa Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde na Ziwa Nyasa yameanza, hii inajumuisha nchi ya Tanzania, Malawi na Msumbiji; na

(xiii) Weledi kwa watendaji wakuu wa Halmashauri za Wilaya, Miji, jiji na Mitaa katika kutekeleza Sheria ya Mazingira umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaniko yaliyopatikana, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti hususan katika kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati na Programu za Hifadhi ya Mazingira. Hapa tunapendekeza Serikali iendelee kuingalia Sekta hii ya Mazingira kipekee na kuongezea bajeti kadiri hali itakavyoruhusu;

(ii) Mgongano baina ya wakulima na wafugaji katika utekelezaji wa Mkakati wa Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya Maji katika kusimamia matumizi bora ya ardhi uendelee kuangaliwa kipekee;

(iii) Ukosefu wa Ofisi za kudumu za Baraza la Taifa la usimamizi wa Mazingira litazamwe. Tunafahamu kwamba kuna bajeti imetengwa kwa ajili ya jengo; tungeliomba siku zijazo bajeti hiyo iongezeke;

(iv) Ukosekanaji wa taarifa sahihi na uwezo wa kuhakiki taarifa za upandaji miti kwa lengo la milioni moja na nusu kwa kila Wilaya kila mwaka kama ilivyoainishwa

katika Mkakati wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Taarifa hizi ambazo zinakosekana, ni lazima pawe na ufuutiliaji na uhakiki kwamba kweli miti hii milioni moja na nusu au zaidi imepandwa;

(v) Uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kwa matumizi mbalimbali, umwagiliaji usio endelevu, kilimo kisicho endelevu na uvamizi wa wafugaji kwenye baadhi vyanzo vya maji, ni sehemu tu ya changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana;

(vi) Ukosefu wa vitendea kazi na wataalam wa mazingira hasa katika Idara ya Mazingira katika Baraza na Halmashauri karibu zote katika nchi yetu kuwa na Maofisa wa Mazingira katika kila Halmashauri, Miji, Majiji na Mitaa;

(vii) Ongezeko la idadi ya watu inayopelekea matumizi makubwa ya mazingira katika kupata mahitaji yao kwa vile wengi wao wanayategemea mazingira moja kwa moja katika maisha yao ya kila siku; na

(viii) Ufinyu wa bajeti inazotengwa na Serikali, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilipata maelezo mbalimbali toka kwa wataalam kuhusu kazi zinazotarajiwa kufanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Ni dhahiri kabisa utunzaji wa Mazingira ni muhimu sana katika kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu hasa katika sura nne zifuatazo:-

- Mazingira yanaipatia nchi yetu mahitaji yote muhimu kwa ajili ya uchumi na ustawi wa jamii;
- Mazingira ndio makazi ya viumbe vyote;
- Mazingira ni chombo kinachopokea taka zinazozalishwa na binadamu; na
- Mazingira ni msingi wa jawabu la kupunguza unyonge na umaskini wetu.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya mazingira inahitaji msukumo wa viongozi wa ngazi zote na wananchi kwa ujumla. Kwa kuzingatia haya, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, maamuzi sahihi katika usimamizi wa mazingira unahitaji takwimu sahihi na za uhakika kuhusu hali ya mazingira nchini. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) kifungu cha (1), imeelekeza kuandaliwa kwa Ripoti ya Hali ya Mazingira nchini kila baada ya miaka miwili, hii itasaidia Serikali kutoa maamuzi sahihi kuhusu usimamizi wa mazingira hasa katika maeneo muhimu kama Ihefu ambayo yanawajibu mkubwa katika kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira iliyoandaliwa mwaka 1997 imeainisha changamoto za mazingira katika makundi sita makubwa ambayo ni:-

uharibifu wa ardhi, upungufu wa misitu na miti, utowekaji wa mapori na upunguaji wa maliasili iliyomo, uchafuzi na upungufu wa maji safi, uharibifu wa maliasili ya majini na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla. Changamoto hizi ni kubwa mno ukilinganisha na nguvukazi iliyopo kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Baraza la Hifadhi ya Mazingira. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wenyewe elimu ya usimamizi na utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 40 kwa nchi nzima, inakadiriwa kwamba kila kilomita moja ya mraba ina watu 45. Ongezeko la idadi ya watu nchini limeendelea kuwa tatizo kubwa linalochangia uharibifu wa mazingira na tatizo hili limekuwa halipewi uzito unaostahili. Kamati inatoa wito kwa viongozi wote na wananchi kwa ujumla kujitahidi kuchukua tahadhari juu ya suala hili kwa kuzingatia uzazi wa mpango ili kupunguza athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Baraza zimekuwa zikikabiliwa na gharama kubwa katika kuhakikisha kuwa mazingira ya nchi vikiwemo vyanzo vya maji, ardhi oevu na bionuai zake yanatunzwa ipasavyo. Sekta nyingi kama zinazotoa nishati ya umeme na mamlaka za maji zimekuwa zikifaidika na utunzaji bora wa mazingira unaosimamiwa na Idara ya Mazingira pamoja na Baraza. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha sekta hizi zinaanza kushiriki katika kuchangia gharama za utunzaji na usimamizi wa mazingira nchini kama Sheria ya Mazingira inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi katika kutoa elimu ya mazingira kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali hasa katika maeneo ya wafugaji na wakulima. Elimu hii itolewe kwa kutumia njia nyepesi hasa mikutano ya vijiji, redio, machapisho, vipeperushi na maonyesho ambazo zitaeleweka haraka kwa wafugaji na wakulima na kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kuweza kukamilisha Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini 2008, hii itasaidia kutathmini hali ya mazingira nchini. Aidha, Kamati inaiagiza Ofisi kuharakisha tafsiri ya ripoti hii kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka vizuri kwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuwa wabunifu katika kuandaa mikakati mbalimbali ya kusimamia na kutunza mazingira ambayo itakuwa mfano wa kuigwa na watendaji wa Halmashauri pamoja na wadau mbalimbali katika kutekeleza ushauri mbalimbali unaohusu usimamizi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ihakikishe inakamilisha Kanuni za Sheria ya Mazingira haraka zote ambazo bado zipo kwenye mchakato ili kuhakikisha uratibu, usimamizi na utekelezaji wa shughuli za mazingira unazingatia Sheria ya Mazingira ipasavyo ikiwemo kutoa adhabu zinazostahili kwa wale wote wanakiuka Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na baadhi ya wawekezaji wasio waaminifu ambao wamekuwa wakikiuka maelekezo na taratibu zinazotolewa kwenye ripoti za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ambazo zinahusu miradi yao. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha hatua zinazostahili zinachukuliwa kwa wawekezaji wote nchi wanaokiuka ripoti hizi na katika jambo hili, Kamati inaomba Serikali itoe tamko humu Bungeni, kupitia Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira au Waziri wa Madini na Nishati kuhusu athari kubwa za uharibu wa mazingira na afya za watu na mifugo ambazo zinaendelea huko North Mara kutokana na uwekezaji wa migodi ya madini katika enelo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tamko hilo lieleze Bunge kuhusu athari husika na chanzo chake, *effect accident*, hatua zilizochukuliwa dhidi ya wenyewe migodi, fidia ambazo wananchi wanaoathirika wamepewa au wanakutarajiwa kupewa na hatua ya kuzuia hali kama hiyo isitokee tena.

Mheshimiwa Spika, kama ni kuchagua kati ya maisha ya watu wetu na dhahabu, nina hakika kabisa chaguo ni wazi kwamba tutachagua watu wetu. Lakini pia tunapendekeza kwamba ikikupendeza iundwe Kamati Maalum ya wajumbe angalau watano watano, kati ya Kamati ya Madini na Kamati ya Mazingira, wajumbe kama kumi waende huko katika Mkoa wa Mara kujionea wenyewe jinsi ya uharibifu wa mazingira unavyowaathiri wananchi kwa kiasi ambacho kinatisha kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka 2009/2010. Jumla ya Shilingi 79,868,393,900/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais. Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa aji Fungu 31, Mazingira ni shilingi 63,397,505,000/=, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 15,870,888,900/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hassa R. Khatib, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvu, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dkt. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwaloyosi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Seleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimia Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mheshimiwa Dkt. Guido G. Sigonda na Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Batilda S. Burian (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Katibu Mkuu wake, Ndugu Ruth Mollel, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Ofisi hii na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya ofisi hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatachia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati, kuongoza Kamati hii, michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru kwa dhati, Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii, Ndugu Michael Kadebe, Yona kirumbi na Grace Bidya, kwa kazi nzuri walioifanya Kamati ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na wewe Mheshimiwa Spika kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. ALI KHAMIS SEIF (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya mazingira kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99(3) na (7) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Chama changu cha Wananchi *CUF* na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkoani. Wapiga kura hao ninawaahidi nitaendelea kuwa pamoja nao na sitowaangusha. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika shukrani lakini kwa umuhimu mkubwa, natoa shukrani na pongezi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kazi kubwa ya kuliongoza vyema Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, mazingira endelevu yana uhusiano mkubwa na maisha ya binadamu pamoja na viumbe hai wengine. Binadamu anahitaji maji, chakula, nishati na kadhalika katika kuendeleza maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia nchi, ni mabadiliko yanayotokezea juu ya uso wa dunia kwa kasi na kwa muda mfupi (mfano mafuriko, vimbunga, ukosefu wa mvua mfululizo) ama yanayotokeea taratibu na yanayochukuwa muda mrefu ambayo ni ya kudumu kutokana na ongezeko la gesi joto zinazozalishwa na shughuli za binadamu.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mabadiliko hayo ni kina cha bahari kimepanda kwa sentimeta 17 juu ya usawa wa bahari kwa miaka 100 iliyopita. Joto la dunia limeongezeka kwa nyuzi joto 0.74°C kwa kipindi cha miaka 50 iliyopita na gesi joto aina ya *Carbon Dioxide* limeongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi yetu utafiti uliofanywa nchini kote umeonyesha joto limeongezeka kwa nyuzi joto 0.2°C na kwa Nyanda za Juu Kusini ni nyuzi joti 0.6°C .

Mheshimiwa Spika, athari ya mabadiliko ya tabia kwa dunia ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ongezeko la vimbunga na majanga mengine ya kimazingira kama ukame na mafuriko;
- (ii) Baadhi ya mazao na mifugo haitaweza kuhimili hali ya joto kubwa;
- (iii) Upatikanaji wa maji duniani kote utapungua sana, vilele vyta milima vitayeyuka;
- (iv) Nchi maskini duniani ndizo zitakazoathirika zaidi;
- (v) Wanyamapori watakuwa ama kukosa mazingira ya kuzaliana;
- (vi) Viumbe vyta bahari ikiwa ni pamoja na matumbawe vitaathirika au kupotea kabisa; na
- (vii) Visiwa vidogo vitamezwa.

Mheshimiwa Spika, athari ya mabadiliko ya tabia nchi yanaanza kuonekana katika nchi yetu kama ifuatavyo:-

- (i) Malaria sasa iko katika maeneo ya baridi ambapo haikuwepo kabisa;
- (ii) Ziwa Rukwa limerudi ndani kwa kilometra saba;
- (iii) Uyeyukaji wa theluthi Mlima Kilimanjaro;
- (iv) Maji ya chumvi yanaingia katika visima vyta maji baridi katika ukanda wa pwani Bagamoyo, Pangani na Rufiji;

(v) Kutoweka kwa kisiwa cha Maziwe (Pangani) na Fungu la Nyani (Rufiji); na

(vi) Ukuta wa Pangani sasa maji yanapita juu wakati wa maji kujaa na kuhatarisha maisha ya wakazi wa mji huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu lazima iwe na mikakati madhubuti ya kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia nchi, haitoshi kuridhia mkataba wa mabadiliko ya tabia nchi na Itifaki ya Kyoto peke yake. Je, Serikali imefanya miradi gani kama nchi kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia nchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006 wafugaji walihamishwa eneo la Ihefu kwa nia ya kuilinda ardhi oevu ya hapo ili hali irejee katika uoto wake wa asili na kuwezesha maji yaweze kutiririka mwaka mzima kwenda Mto Ruaha Mkubwa na hatima yake yafike Bwawa la Mtera kwa kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, mto Ruaha Mkubwa humwaga maji yake kiasi ya 56% kwenye Bwawa la Mtera. Mito mingine Ruaha mdogo (18%) na Mto Kisigo 26%. Bonde la Usangu linapata maji kutoka mito ya Kioga, Mbarali, Kimbi, Mkoji na Ndembera. Mito mingine inayotiririsha maji mwaka mzima ni sehemu ya juu ya Ruaha Mkubwa, Kimani na Chimala.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo hili lina mteremko mdogo sana kati ya (1020m – 1050m) juu ya usawa wa bahari inabidi eneo hilo liwe na maji mengi ili yawezeshe kutiririka kutoka ardhi oevu ya Magharibi – Mashariki – Ihefu Ngiriamma Mto Ruaha mkubwa – Mtera – Kidatu kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa eneo hilo lilikuwa likiathiriwa na ufugaji na ndio wafugaji wakahamishwa, hivi sasa katika kupatikana maji ya kutosha ili yaweze kutiririka mwaka mzima kwenda Mto Ruaha mkubwa kunaweza kuathiriwa na kilimo cha mpunga cha wakulima wadogo wadogo kwani maji yanayotumika mengi hayaendi kwenye Mto Ruaha mkubwa. Hili ni tatizo kwani wananchi wengi wa maeneo hayo, wanategemea kilimo cha mpunga katika maisha yao pia.

Mheshimiwa Spika, katika kulitatua tatizo hilo, Serikali iwe makini sana kwa kuona njia gani wakulima hawa hawataathirika na ufumbuzi wa tatizo hilo. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali hao wananchi watakaoathirika na tatizo hilo wagawiwe kwenye mashamba makubwa yaliyobinafsishwa ili wakulima hao wayaache mashamba yao madogo na kuruhusu maji kuweza kutiririka kwa mwaka mzima kuelekea Mto Ruaha Mkubwa Bwawa la Mtera na Kidatu ili tuweze kupata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa sana ya wananchi wa nchi hii wanatumia nishati ya kuni na mkaa kwa kupikia. Ni dhahiri kabisa ukataji wa miti ili kukidhi haja hiyo ni mkubwa kila mwaka. Inabidi iwe hivyo kwa sababu Serikali haijakuwa na mkakati wa kuwa na nishati mbadala ya kupikia itakayotumiwa na wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kusamehewa ushuru Moto Poa sio suluhu kuunusuru uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti kwani wenyewe uwezo wa kutumia nishati hiyo ya kupikia ni wachache mno.

Mheshimiwa Spika, Serikali bila ya kuwa makini kwa suala hilo la nishati mbadala ya kupikia badala ya mkaa au kuni, uhifadhi wa mazingira kwa kutokata miti utakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, nchini Malawi kwa kupitia taasisi inayoitwa *Habitant for Humanity* ilianzisha mradi wa kupunguza ukataji mkubwa wa miti. Taasisi hiyo ilihakikisha upunguzwaji wa bei za saruji ili wanajamii waweze kuhimili hiyo kwa kutumia saruji badala ya miti lakini kama kwamba haitoshi pia walihakikisha bei za umeme zinakuwa chini, pia walianzisha teknolojia ya kutumia majiko ya nguvu ya jua na yanayotumia mkaa kidogo (*Solar box cooker and fuel efficient charcoal stoves*). Je, Serikali ina mkakati gani wa uhakika wa kupatikana nishati mbadala ya kupikia tena yenyewe bei nafuu baadala ya kutegemea kuni na mkaa?

Mheshimiwa Spika, bila maji hakuna maisha na ili maji yapatikane lazima vyanzo hivyo vya maji vilindwe . Bado tafsiri ya chanzo cha maji kina utata kisheria, kwa kuangalia Sheria ya mwaka 2002 na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Sheria zote hizi zina vipengele vya utunzaji au kuhifadhi vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Maji hairuhusu kufanyika shughuli za kudumu za binadamu katika mita 200 kutoka mto au vijito na mita 500 kutoka kwenye maziwa au bahari, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 yenyewe katika kipengele cha 57(1) hairuhusu kazi za kibinaadamu kufanyika kwenye vianzio vya maji mita 60. Sheria hizo zinakinzana pamoja na kwamba kipengele namba 232 kinaipa uwezo Sheria ya Mazingira kuamua umbali huo.

Mheshimiwa Spika, Uhifadhi wa mazingira uendane na uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuyalinda maji yasichafuliwe ili tupate maji safi na salama. Kwa mfano mgodi wa Geita unamwaga taka taka zake zenye sumu katika bwawa la Mtakuja. Mgodi wa North Mara ni hivyo hivyo nao unatoa taka taka za sumu.

Mheshimiwa Spika, leo hii kijiji cha Nyakabale chenye watu zaidi ya 600 Kaskazini ya machimbo ya Geita watu wake wanaishi kwa wasiwasi mkubwa juu ya maisha yao, kwani wengi wao wanakunywa maji hayo ambayo si salama kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zetu za Kambi ya Upinzani mwaka 2007/08 na 2008/09 tulielezea wasiwasi wetu juu ya Mgodi wa North Mara huko Tarime na kemikali

zinazotiririka kwenye mto, naomba ninukuu kutoka katika hotuba ya mwaka 2007/08, inasema:-

“Madhara mengine ambayo yanatarajiwa kutokea ni yale yanayosababishwa na Mgodi wa North Mara kutupia taka zeny sumu katika mto Tigit amba ni tawi la mto Mara unaoingia ziwa Viktoria. Hapa tujaribu kujiliza ni watu wangapi wanatumia maji na samaki kutoka katika ziwa Viktoria”.

Mheshimiwa Spika, tuliiatka Serikali kuchukua hatua zinazostahili, lakini kwa sababu wasemaji na wapinzani tukapuuzwa. Leo Serikali inatamka nini kuhusu yaliyotokeu huko Mara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni majuzi tu imeripotiwa na gazeti la Mtanzania Jumapili la tarehe 21/06/2009 kuwa watu 21 wafa kwa kuoga maji ya sumu na watu walinusurika wanachubuka ngozi, mifugo 270 yapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, tunazidi kuieleza Serikali kuwa uzembe na kutokujali kunakofanywa na wale waliopewa mamlaka kutatupeleka pabaya. Angalizo hili la kuwepo kwa hatari tulikwishalitoa. Hivyo basi Kambi ya Upinzani inawataka walioshindwa kuchukua hatua katika kuhakikisha sumu hizo zinasitishwa kuingia katika mto Tigit wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inaendelea wakati Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (*NEMC*) lipo, na hatujui hatua gani imechukuwa kwa makampuni hayo au inaogopa kuwakera wawekezaji. Serikali itueleze vipi usalama wa afya zao unalindwaje kwa wananchi hao? Pia Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maeleo juu ya fidia wanayotakiwa kupata waathirika wa uharibifu huo wa mazingira toka makampuni ya madini kuwepo maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), Baraza hili ndio chombo kikuu kisheria kinachohusiana na usimamizi wa mazingira. Uwezo huo uko kwenye sheria Na. 20 ya mwaka 2004. Kwa kuwa Baraza hili lina wafanyakazi wachache na karibu wote wako Dar es Salaam ni dhahiri utendaji wake kwa nchi nzima utakuwa hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, utumiaji wa mifuko ya plastiki isiyo ruhusiwa hasa kwa mikoa nje ya Dar es Salaam unaendelea kama kwamba haijapigwa marufuku. Hilo linafanyika kwa sababu Baraza halikuenea nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali itueleze kwa uchache wa wafanyakazi kwenye Baraza hili kweli linasimamia suala zima la mazingira?

Mheshimiwa Spika, niungane hapa na Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa iundwe Tume ili iende Mara kuchunguza maafa yaliyotokeu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ali Seif.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, ni nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge, kuchangia. Nina majina sita na sina hakika kama yote yatafikiwa. Tutaanza na wale ambao hawajachangia kabisa ambao ni wawili, ambao ni Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa na tunao katika orodha, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Lucas Siyame. Nadhani mpaka wanenam na wale, ngoja tuone tutakavyokwenda halafu tutazama jioni kwa sababu Wizara hii, Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, bajeti inajadiliwa kwa muda wa siku moja tu. Kwa hiyo, namuita sasa Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, akifuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa wakati Mheshimiwa Charles Mwera ajiandae.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nichangie kwenye hoja hii ya Wizara ambayo ni muhimu sana ambayo inatakiwa iwe inasimamia Wizara zingine zote kiutaratibu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wote waliohusika kuandaa hotuba hii nzuri na kwa kweli inajitosheleza na nimeisoma na nikilinganisha na ya mwaka jana, hii ni bora sana, inaonyesha kumefanyika juhudini na maendeleo katika utendaji kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, pongozi maalum ziende kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuanzisha Mchakato wa Programu ya Uhifadhi wa Bonde Ziwa Nyasa. Naomba tu Mheshimiwa Waziri aongeze juhudini ili mchakato huo ufkie mwishoni ili tuweze kudhibiti uharibifu wa mazingira ambao unaendelea kutokea kwa kasi sana katika bonde la ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia ndani kwenye hotuba, niruhusu kidogo na mimi nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Makamu au Kaimu Mufti wa Tanzania, Sheikh Gologosi lakini vilevile ndugu yangu Prof. mwenzagu ambaye nilikuwa namfahamu na kumheshimu sana, Prof. Othuman ambaye amefariki jana. Mungu aziweke roho za ndugu zetu hawa wawili mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitangaze mapema kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na naunga mkono yale yote yaliyosemwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, lakini ninapenda niseme mambo machache kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika sekta hii ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, nataka kuamini kwamba matatizo mengi na makubwa tunayoyaona kwenye sekta ya mazingira, yanatokana sana na dhana ambayo inaelekeaa kuonekana kana kwamba Wizara hii ya Makamu wa Rais, Mazingira haipo. Uwepo wa Wizara hii unaweza ukahojiwaa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu matatizo yaliyojitokeza Ihefu, matatizo tuliyoyasikia sasa hivi kwenye mgodi wa North Mara na kadhalika, kama Wizara hii inahusika na mazingira, kwani wako wapi, wanahusika vipi, inakuwajekuwaje mpaka matatizo yafikie hapa na Wizara ipo?

Mheshimiwa Spika, nataka niamini kwamba Wizara haitoi msukumo na maelekezo ya kutosha kwa sekta nyingine kwenye Halmashauri za Wilaya kuhusu utendaji kazi na ndiyo maana kuna matatizo makubwa ya uharibifu wa uoto, udongo, uchafuzi wa mito, maziwa na kadhalika. Miongozo ipo kwenye makaratasi lakini utekelezaji kule chini hatuoni na matatizo yanaendelea. *Deforestation* inaendelea, milima inaendelea kunyolewa kana kwamba hakuna mtu wa kusimamia, mito inaendelea kukauka, tumeambiwa Ziwa Rukwa linaendelea kukauka lakini hatuoni juhudzi zozote zinazofanyika kana kwamba watu wanaoshughulika na mazingira hawapo.

Mheshimiwa Spika, inaelekea ngazi za chini hakuna, utendaji wa Wizara hii umberakia ngazi za kitaifa sijui kuna tatizo kati ya Ofisi ya TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba uhusiano wao kiutendaji labda kuna mushikeri ndiyo maana kule chini utendaji hauonekani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya mazingira wanasema kwamba shughuli zote za mazingira zinashughulikiwa ngazi ya Halmashauri. Lakini wanatakiwa wawe na wataalamu wao wafanye kazi kule, lakini vipaumbele vya Halmashauri hizi sio mazingira, vipaumbele vya Halmashauri hizi ni tofauti kabisa na mambo ya mazingira. Kwa hiyo, hawawezi kushughulikia inahitaji kuwe na *guidance*, kuwe na maelekezo madhubuti ya mifano ya kiutendaji kwenye ngazi zile na washauriwe kwa ukaribu, wataalam wanatakiwa wawepo kule ili wasaidie katika utendaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini ilivyo kila mtu atapiga mpira kwamba zile ni kazi za Halmashauri na wale kule vijijini na Halmashauri wanasema *NEMC* huku haipo, hatuwaoni watu wa mazingira, kwa hiyo, matatizo yanaendelea. Tungeomba kwa kweli Wizara itusaidie ku-*brigde* hilo pengo, kuna pengo kubwa sana kati ya ofisi ya Makamu wa Rais na TAMISEMI kwenye Halimashauri ili kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa ilivyo.

Mheshimiwa Spika, pia naamini vilevile kwamba tatizo la mazingira hapa nchini linatokana na ongezeko kubwa la watu. Serikali iko kimpya kabisa kuhusu ongezeko kubwa linaloendelea la watu hapa nchini na ongezeko la watu ndiyo linaleta mabadiliko ya hali ya nchi, ambapo watu wanahitaji kulima na kufuga zaidi. Unaona watu wanahama kutoka maeneo mengine kwenda kutafuta malisho mahali pengine kwa sababu kule wamemaliza kwa vile watu wako wengi. Watu wanaongezeka, wanahitaji maeneo ya kulima, tunapanua kilimo, tunatumia maji zaidi iwe kwa umwagiliaji au kwa matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Serikali, hatutaki kuzungumza tatizo la ongezeko la watu hapa nchini. Tuchukue mikakati gani ku-deal na tatizo la ongezeko la watu ambalo mimi kwangu naita ni *time bomb*. Matatizo yote hayo ya Ihefu, watu kutoka Kaskazini kwenda Kusini na mifugo, ni tatizo la matumizi ya ardhi, ardhi haitoshi, rasilimali zimepungua hazitoshi wala hazongezeki. Lakini Serikali haizungumzi suala hili, imenyamaza kimya, lakini siku moja itakuja kutokea *indicators*, ndiyo hizi za matatizo ya mifugo, North Mara, Ihefu, na yataongezeka mengine mengi tu ndiyo pengine tutashtuka lakini tutakuwa tumechelewa. Kupitia Wizara hii, hebu tujitahidi kuisukuma Serikali kuweka mipango kabambe ya kuanisha uongezekaji wa watu na rasilimali zilizopo hapa nchini ili twende sambamba na matumizi endelevu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nadhani linachangia sana kwenye uharibufu wa mazingira, ni umaskini. Wananchi wetu wanaishi leo sio kesho. Uhifadhi maana yake kuhifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo, kesho na kesho kutwa. Wananchi wetu ni maskini kiasi kwamba hawafikiri kesho wanafikiri leo. Ndiyo maana katika kilimo chetu, wanaharibu udongo, wanalima kila mwaka humo humo bila mbolea na unaendelea kuharibika, uvuvi haramu na uharibifu wa uoto.

Mheshimiwa Spika, sasa huu MKUKUTA, Wizara hebu mtusaidie kutoa miongozo mizuri zaidi ya kivitendo, ni vipi tatizo la *poverty* (umaskini), tutaliboresha ili wananchi waache kuendelea kuharibu mazingira na rasimali? La sivyo tutakuwa tunaweka mikakati, mipango ambayo haitekelezeki na haina manufaa.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni upandaji miti, imekuwa ndiyo kama Sera ya Mazingira maana yake kupanda miti na wanaangalia tu imeota mingapi, lakini tuulize *cost benefit analysis* imefanywa lini tangu mwaka 2002 mpaka leo? Je, tunaweza tukalinganisha gharama tulizoingia katika upandaji miti kwa mfano na faida zilizotokana na upandaji huo? Je, *trend* ikoje, ili tuone ni mkakati mzuri au tuachane nao maana kuna mikakati mingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa vyanzo vya maji, mikakati iliyopo inakingana sana na tatizo zima la umaskini. Ukitzungumzia kulima kwenye vyanzo na maeneo oevu, milimani watu wanalima kwa sababu hawana maeneo mengine ya kulima, watu ni wengi na hata ukipiga marufuku wasilime maeneo haya, unataka wakalime wapi sasa? Kuna haja ya kufikiri zaidi kwa undani tuone tatizo hili tutalitatuaje, kwa sababu watu ni wengi, wanaingia mpaka kwenye maeneo oevu, maeneo ambayo hawatakiwi kulima sio kwa sababu wanapenda, hawana *options*! Sasa Wizara itusaidie kuleta mbadala na kuweka mipango bora ya kuhifadhi maeneo haya kuliko tunavyofanya sasa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninataka nilizungumzie, linahusu kidogo ndugu zangu wa *NEMC*. Nimeona hapa mnazungumza kwamba wameandikishwa wataalam wa *Environment Impact Assessment (EIA)* 50 na wa *Audit* 19, ndiyo wataalam wanaofanya *EIA* hapa nchini. Nchi kubwa kama Tanzania, watu 50 ni kitu gani hiki? Hakuna mikakati yoyote inayoonekana kwenye bajeti, ya *training in a mass* ili tuzalishie wataalam wengi wa ku-deal na miradi mikubwa ambayo inaanishwa kila siku. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji ni mdogo, upelembaji (*monitoring*), haipo, ndiyo maana yanajengwa mahoteli ovyo ovyo...

SPIKA: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA. Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, nawashukuru Waasisi wote wa Muungano, Marehemu Abeid Aman Karume na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Pili, nawapongeza Marais wetu wote wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar - Mheshimiwa Aman Abeid Aman Karume.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu alisema kwamba, mtu akikanyagwa na akanyamaza kimya, hakuna atakayejua kwamba amekanyagwa na itakuwa kimya kabisa. Lakini, mtu akikanyagwa akapiga kelele, ina maana ameumia na walio majirani wote watapata habari kwamba mtu huyu amekanyagwa na ameumia. Hii inamaanisha nini? Hii inamaanisha kwamba, sisi Wazanzibar tumeshindwa kunyamaza kimya kutokana na baadhi ya mambo ya Muungano. (*Makofi*)

Kuna mambo ambayo yanajitokeza, kwa kweli hayaridhishi katika Muungano wetu. Ukiangalia kitabu hiki cha leo, ukurasa wa 12 Ibara ya 17 inazungumzia kuhusu Wafanyabiashara wa Zanzibar, mimi nasema kwa kweli hata hiyo Zanzibar yenyewe Bandari tunaweza kusema imekufa kutokana na tunakotoka. Wafanyabishara hawa utaona kwamba, hawana maslahi na bajeti ya mwaka 2007/2008 kitabu kama hiki ukursa wa 11, ilizungumza kwamba, mambo haya yamemalizika, yalishaweza kurekebishwa 2008/2009 wakabana pale kidogo kwamba mambo haya yanarekebishwa na kitabu hiki leo, masuala ya Muungano nasema Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni pamoja na malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nahisi haya ni mazungumzo ambayo ni ya siku zote. Mahali popote uhakikishe kwamba uchumi ukishaanguka hata wale Wazanzibari wote umewaangusha, kwa sababu pale palikuwa na Wafanyakazi, leo hata kazi hawana na wenzetu mimi nasema ndio mliotuangusha; licha ya umoja wetu, licha ya kufahamiana kwetu, licha ya kuishi wote vizuri, lakini wenzetu kwa vita hivi ndiyo sababu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, hata ukasema hivyo umewaangusha hawa? Leo mimi nakumbuka hasa watu wa Tanzania Bara, walikuwa wanakuja Zanzibar kwa biashara kwa boti za asubuhi, boti za jioni na mimi mwenyewe

nimo ndani ya chombo, lakini wakifika Bandarini, Tanzania Bara, hivyo vituko vyake havisemeki. Hujui hata biashara ile ukauze wapi, maana unatakiwa wewe usipate faida katika biashara ile. Kwa hiyo, nani ataendelea kufanya baishara ile? Makontena yalikuwa yanashuka kule Zanzibar, Wafanyakazi kweli wako Dar es Salaam, lakini baada ya kufika kule wanachukua biashara zao wanaleta Dar es Salaam, basi utajuta kwa vile mateso na matatizo yanayojitokeza pale bandarini. (*Makofi*)

Lakini mfano mzuri zaidi, juzi tarehe 25 nilikuwa katika boti kuja zangu Dar es Salaam. Kulikuwa na kijana kachukua Televisheni tu, moja tu, kwa bahati mimi sikushuka pale *VIP* nilipoona jamaa wanashusha TV, nikasema leo hebu nihakikishe kuna ukweli gani? Nami nikatelemka, tukapanda wote pale juu, kufika pale wanazuiwa, kuzuiwa pale wanatozwa fedha wala hakuna risiti, sasa katika suala uchumi kwa kweli wenzetu mnatuweka mahali pabaya na hii ni nyimbo ambayo mnaendeleza na Rais kasema kwamba, matatizo haya yaondolewe, mkutane mwondoe matatizo haya. Kasema Rais, ilikuwa mwezi Machi, 2006 huko Arusha. Rais alichotaka ni utatuzi ili vikwazo vyta Muungano viondolewe na hili ni suala ambalo alisema biashara inawapiga wananchi wote wa Zanzibar. Kwa hiyo, hii ni hatari, wenzetu mnatupeleka mahali pabaya na hakuna leo atakayezungumzia hapa mambo ya Muungano na kusikitika kama sio Mzanzibari. Atatokea mtu wa Zanzibar tu, hatokei mtu wa bara kusikitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Muungano tunauthamini sana na ndiyo uliotufikisha hapa na hatuna matatizo nao, lakini wenzetu mnatuwekeva vikwazo juu ya Muungano na siku zote mambo haya mnasema mtarekebisha, hakuna kinachorekebishiwa. Mtarekebisha sijui Sharia, sijui nini, sie kule hatupigani wala hatuna matatizo, leteni vitu vyta uchumi ambavyo vitasaidia Zanzibar, ndivyo tunavyotaka sisi, sisi hatuna tatizo lakini mweleze mambo ambayo yatasaidia Zanzibar.

Kuna suala ambalo na sisi sote tunajua Zanzibar ilikuwa na soko kubwa sana kibishara, lakini leo hakuna kitu, hakuna asiyejua. Sasa tunasema 2010/2011 tutakutana tena hapa, mambo haya tusije tukayasikia tena. Nasema hivyo kwa niaba ya Zanzibar, hatutaki kusikia tena hadithi hizi za paukwa pakawa, hatutaki. Tuambieni kwamba tumefanya hili, tumemaliza hili, hili ndilo jawabu tunalolitaka. Msidanganyike mkasema kwamba mtakwenda kinyume, mwaka 2011 Mungu akipenda tukawa na uzima tunarudi sisi hapa! Tutakuja kukutana tena! (*Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili kuna suala la elimu. Juzi hapa niliuliza swali kuhusu elimu na nikajibiwa. Kule Zanzibar kuna Chuo Kikuu, Tunguu, vijana wanosomea Sheria na nikasema kwamba hawa jamaa kwa kweli haki yao wametaka kupata mkopo hawakupata, nikajibiwa kwamba, hawawezi kupata kwa sababu watakuwa wameshamaliza. Lakini, bado Wazanzibari wale wako katika shughuli za masomo na wengine wametupwa Shinyanga, wengine wametupwa Dodoma, wengine wametupwa Lindi, kweli leo utasema kwamba, wameshamaliza? Ni kitu cha ajabu kabisa! Mimi najua kuwa chuoni pale mkimaliza mnafanyiwa *Graduation* kila mmoja, pale mnakuwa mmemaliza, sio kwamba, mko katika *field* halafu useme mmemaliza.

Leo ndugu zetu mmewafanyisha hata ile shughuli wasifanye! Walioletwa Dodoma hapa wako Zanzibar, waliopelekwa Shinyanga wengine wameshindwa , lakini mtu ukitaka kumtawala, mnyime elimu na haya siku zote hapa nasema katika Bunge hili, mtu ukitaka kumtawala vizuri mnyime elimu, utamtawala vizuri sana kwa sababu anakuwa mjinga. (*Makofii*)

Tunasema kama chombo hiki cha Muungano tunataka kuona Mzanzibari anapata haki kama mwininge, kama tunahisi matatizo, Marehemu Karume Mungu amrehemu, alisema, kila miaka 10 (na ndilo kosa tulilolifanya) tukutane tutazame lipi linafaa, lipi halifai. Mungu amemchukua kiumbe yule kwa miaka Minane tu, katika uongozi wake na haya ndiyo yanayosababisha, kama tungekuwa tunakutana tusingefika hapa leo, wala haya tusingezungumza na ndiyo, ukaona Baraza la Wawikilishi wakasema kwamba, mafuta, wakaja juu, lazima haki yao.

Kisiwa kama kile, nchi kama ile, leo mna mambo 22 tunayaingiza kwenye Muungano sio mchezo, ni hatari kwa sababu ndiyo tatizo linavyojoitokeza. Kama hivi, mambo 22 yako katika Muungano! Inakuwa kama sisi tunagaiwa. Tunakwenda wapi?

Sisi hatujaomba, nataka kusema kwamba, sisi tumeungana, nchi kamilii Zanzibar, tumeungana, hizi ni nchi mbili, ukisema udogo haijawa sababu, hata hapa maumbile yetu, Mheshimiwa Msindai nafikiri umbo lake tunalijua na mimi ukaja umbo langu utalijua, sio sawa sawa, haya ni mambo ya Mungu. Tunasema tujue kwamba, Zanzibar ni nchi kama ilivyokuwa nchi ya huku Tanzania Bara, tumeungana kwa kupata Tanzania, haki ziende sawa bila hivyo, tatizo la Muungano litakuwa bado liko na sisi kama Wazanzibar hatutaridhika. Kidumu Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa hauko kwenye mkutano wa siasa hapa, kwa hiyo, matamko kuhusu kupongeza vyama na nini au salamu za chama haziruhusiwi. Tunaendelea. Msemaji wa mwisho kwa mchana huu ni Mheshimiwa Charles Mwera - Mbunge wa Tarime.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii. Kwanza, nakushukuru kwa namna unavyoongoza hili Bunge Tukufu na nimshukuru pia Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Kabla sijakwenda kwenye hoja yangu, nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Ranya na Tarime, kwa vita ambavyo vimetokea pale ambavyo vimesababishwa na wizi wa mifugo. Nawaomba wananchi wangu wa Tarime na Ranya kwamba, sisi tupambane na wezi ambao wametuletea vita hivi na tuiombe Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba, hayo majambazi ambayo yanatumia silaha kutoka Kenya, yawe yamekamatwa kwa sababu askari wa kwetu kila mara wamekuwa wakizidiwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nikipitia haya majedwali ya kwenye upandaji wa miti. Kwa kweli niwashukuru Watanzania kwa kazi kubwa waliyoifanya katika upandaji wa miti ambalo ndiyo njia moja ya kuhahakisha kwamba, hali yetu ya mazingira

inakwenda vizuri. Lakini, nimeangalia kwenye Mkao wa Iringa pale nimeona Kilolo ina zaidi ya *percentage* 900 na Njombe pale ni *percentage* 826.11, tuwapongeze kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuotesha hiyo miti.

Nilikuwa nikiliangalia hilo nikaona pale Serengeti ina *percerntage* ndogo sana, basi katika majumuisho niweze kujua kwamba, tatizo lilikuwa wapi na wakati tunapokadiria wakati wa kupanda miti ni vizuri tukadirie vizuri, tunapanda kwa kiasi, tusije tukajikadiria kwa hali ya chini kumbe, tulikuwa na uwezo wa kupanda miti mingei.

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwangu katika mgodi wa *North Mara*, ambao wananchi wangu wamepata shida sana, wananchi wengi wamekufa pale, ng'ombe wengi wamekufa, akina mama mimba zimekuwa zikitoka pale, huku tukijiliza kwamba kuna tatizo gani hapa?

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mwenyekiti wa Halmashauri, tuliyaongea hayo tukapeleka watu wakaenda wakapima maji, sasa tunasikitika kwamba, maafa makubwa yametokea, maji yanayotoka katika ule mgodi ambayo yana *Mercury*, yanaingia mto Tigite, yakishaingia maafa makubwa hutokea, yanaingia mto Mara, yanaingia Ziwa Victoria. Kwa hiyo, Waheshimiwa ambao tuko hapa, tumeshakula Samaki, kwa hiyo unaweza ukakuta na sisi tumeshapata madhara makubwa. Unaweza ukafikiri ni mtu wa Tarime, lakini kumbe madhara yameshaenea nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, tuangalie ni akina nani hao walikwenda kupima maji wakaleta matokeo kwamba, maji ni safi. Tumekuwa na Watanzania ambao ni Wazalendo, ambao wamepewa nyadhifa mbalimbali katika kuwakilisha nchi, lakini, walipopewa wanapima maji wanaleta majibu ambayo siyo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, tuombe kwamba, hawa watu wachukuliwe hatua, ni muda mwangi tumeigania hilo neno kwamba, hali ya maji sio nzuri, namshukuru sana Waziri Mkuu. Juzi nilipomwuliza swali la papo kwa papo, kwa kweli akafanya juhudhi na akamtuma Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Balozi Kagasheki na ameleta majibu ambayo atamwasilishia Waziri Mkuu, tufahamu kwamba hiyo ni hatua moja nzuri ya Serikali.

Napenda kuipongeza Serikali, kwenye suala hili la maji ambalo kwa kweli Waziri wakati wa majumuisho atatwambia; Je, ni mara ngapi amefanya ziara ya kutembelea hii migodi ambayo iko Tanzania kuhakikisha kwamba, inafanya kazi vizuri? Katika bajeti ambazo tunazo tunavyoziona, wamekuwa wakipangwa posho kwa ajili ya safari hizo, tumekuwa tukilalamika hatuoni, katika Migodi kuna Mawaziri mengi wanaohusika hapo, Waziri wa Mazingira anahusika, Waziri Mkuu anahusika, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto anahusika, Waziri wa Nishati na Madini anahusika, Waziri wa Mambo ya Ndani anahusika, Waziri wa Afya anahusika, kwa hiyo, Mawaziri wengi wanahusika pale. Mimi nasikitika kwa hilo, basi tuiombe Serikali iweze kulichukulia hilo hatua ambazo zinaweza kusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wale wamekuwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukipagania pale Nyamongo, zile Kata za Gibasuka, Matongo na Kemambo, lakini yale maji yanateremka na yameishaingia Kata nyingine ya Nyandoto, ambayo ni Kijiji cha Nkerege, Ng'ombe wamekuwa wengi pale, lakini tunapokuwa tunaiambia Serikali na hata nilipokuwa katika *Alat Mko*, wakati ukiongea mtu anasimama anakwambia unaongea upinzani, wakati tunaangalia masilahi ya Mtanzania, lakini mjambe anasimama anakwambia usitulee mambo ya upinzani, wakati tunaongelea mambo ambayo yanaendelea ambayo ni ya kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati Diwani wa Kata ile ya Gibasuka akifuatilia yale mambo, alianza kutishiwa na Serikali, akaitwa pale Musoma, Polisi, wakamwuliza kwanini unakwenda kuongea haya maafa? Mimi nikamwambia, uende uongee haya maafa, nimeyaongea kwa muda mrefu na kama Serikali inanihitaji, ije inishike mimi kwa sababu ndiye nilianzisha haya mambo. (*Makofi*)

Sasa unakuta Diwani anashitakiwa wakati ni mambo ya ukweli. Vitu vimeonekana kwenye Televisheni vinasikitisha sana na sisi Wabunge tuko hapa, kwa kweli na mimi niungane na Wabunge kwamba, kuna umuhimu wa kuunda Tume ambayo itashirikisha Kamati hizi mbili, Nishati na Madini pamoja na Ardhi na Mazingira, ili ianze kuhakikisha kwamba, nini kinafanyika. Pamoja na kuunda hiyo Tume, naomba Kamati Teule ya Bunge iundwe ambayo inaweza ikaleta jibu la haraka kuhakikisha kwamba wananchi wale hawapati madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunda hizo Kamati, ninafikiri kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali itoe Tamko la haraka kwamba, huo mgodi ufungwe ili wananchi wasumie zaidi wakati wakihitaji suluhu gani iweze kufanyika. Sasa hivi tunavyoongea, maji bado yanaendelea kuingia kwenye ule mto, tunaweza tukakaa hapa tunaongea, lakini wananchi wanazidi kudhurika zaidi. Kwa hiyo, naomba hiyo iweze kusimamiwa.

Mheshimiwa Spika, hayo nimeyaongea kwa muda ambao unaweza kutosha, sasa niingie kwenye suala la magereji yanayowekwa katika miji yetu. Viwanda vimejengwa katika miji yetu, ndani ya Halmashauri zetu, viwanda vimejengwa ndani ya mji, moshi uko pale, kelele ziko pale, zinafanyika katika miji yetu, kwa hiyo tuhakikishe kwamba, Serikali inalisimamia hilo ili gereji zisikae ndani ya miji. Utakuta ndani ya mji, katikati ya mji kelele zinapigwa, moshi unatoka pale kiasi kwamba, uchafu unakuwa ni mkubwa zaidi. Kwa hiyo, inatakiwa Serikali, Halmashauri zitenge sehemu ambazo zinaweza kujengwa viwanda vidogo, magereji ili wananchi wasumie zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, twende kwenye upande wa mkaa. Najua kwamba, mkaa ni kwa sababu ya umasikini. Kama tunavyoona, kwa hili tuhakikishe kwamba tunakuwa na majiko ya kisasa. Wananchi wengi wamekuwa wakikata miti, wanachoma mkaa, lakini tujue kwamba, kwenye mkaa mle kunakuwa kunatoka hewa ya *carbon monoxide* ambayo inakuwa inasababisha hali ya uchafuzi katika anga yetu. Kwa hiyo, tunatakiwa tuhakikishe kwamba, majiko yanawekwa mazuri yenye bei rahisi ili wananchi waweze kutumia kuni kidogo katika majiko hayo na hali ya uchafuzi isiwepo.

Mheshimiwa Spika, halafu vilevile kwenye bei ya mafuta, mafuta yamekuwa na bei ya juu sana kiasi kwamba mwananchi wa kawaida hawezi akamudu kununua mafuta ya taa. Kwa hiyo, bei ya mafuta ya taa ni muhimu sana iweze kuangaliwa ili iweze kupungua, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi, ambalo nahitaji Serikali ilichukulie hatua, ni suala la hali ya Mgodi wa North Mara. Katika nchi za Magharibi, nilifikiri katika hatua hii ya Nyamongo ambayo imeonekana kwenye vyombo vyahabari, nitaamka nisikie kwamba mawaziri wamejiuzulu, lakini naona katika Serikali yetu hakuna viongozi ambao wana ujasiri wa kujiuzulu kwa kuona hiki kitu ambacho kimefanyika imekuwa aibu kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mawaziri, wajijengee utaratibu kwamba ukishapewa dhamana ni lazima usimamie. Ni lazima utambue namna gani unawenza ukamwangalia Mtanzania. Yule Mtanzania wa Tarime ni mmoja kati wa Watanzania na kama mwananchi wa Tarime haangaliwi hivyo, mnafikiri ni Watanzania wengine ndiyo wana haki, mimi kama mwakilishi wa wananchi wangu wa Tarime, nitawatetea na Serikali kwenye hili nione ni namna gani na kwenye Bunge hili, tupate majibu kamili juu ya namna gani suala hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Charles Mwera wa Tarime. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, muda sasa unakaribia ukomo, bahati njema ninao wachangiaji watatu tu, ambao wote wataweza kuongea kuanzia saa 11.00 nao nawatamka. Tutaanza na Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na tutamalizia na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame.

Baada ya hapo kwa mpangilio, Waheshimiwa Mawaziri watakubaliana, watakuwa na fursa ya dakika 45 kujibu hoja zetu, baada ya hapo tutaingia katika Kamati ya Matumizi. Kwa sasa kwa kuwa, muda wenyewe haututoshi kuendelea nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 leo jioni.

(*Saa 6.52 mchana Shughuli za Bunge Zilisitishwa
hadi Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, habari za mchana. Tunaendelea tena, nilikuwa na wachangiaji watatu wamesalia ambao wote watapata nafasi na nitawataja. Kwanza ni Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na hatimaye tutahitimisha na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kupata nafasi hii na kabla ya yote uniwie radhi kwamba na mimi

nitume rambirambi zangu kwa ndugu na jamaa wa familia ya Marehemu Prof. Haroub Othman, Mwalimu wangu aliyefariki dunia. Mchango wake mkubwa kwangu pamoja na rehema ya Mungu imenifikasiha hapa. Pili, familia ya Marehemu Suleiman Gorogosi, Mwenyezi Mungu kwa pamoja azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa nijikite katika mchango wa hotuba hii ya makadirio na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mambo ya Muungano na Mazingira. Kwanza nampongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Riziki Omar Juma kwa hotuba yake aliyoitoa leo hii asubuhi ambayo imeja nasaha na busara yenye maudhui makubwa sana kwa wale wanaozingatia. Kwa namna ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani alivyochangua mambo manane ambayo yalianzia muundo wa Muungano, shughuli za Muungano mpaka akamalizia na mambo ya Mahakama ya Katiba na akadiriki kusema "*No need to say more*". Kwa kweli ukiisoma ile hotuba hakuna cha kuongezea. "*No need to say more!*" Lakini kitakachosababisha tuseme zaidi ni ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu kidogo cha 3(a) na (b) pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge Kanuni ya 97(1) na (2). Vitu hivyo viwili ndio vinavyotusababisha tuseme vinginevyo hakukuwa na haja tena ya kuichambua hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hakuna mtu ye yeyote mwenye akili timamu Tanzania hii awe wa Zanzibar au Tanganyika atakayesema Muungano hauna maana. Hakuna mtu yoyote mwenye akili timamu atakayesema Muungano haujatusaidia, hakuna! Kama yupo akajitokeza mtu wa namna hiyo ina maana huyo ana kasoro. Kwa maana hiyo, mjadala huu sio wa kuwepo au kutokuwepo Muungano, hapana. Mjadala ni kuhusu muundo na kufuatwa makubaliano ya Muungano; mjadala huu ni kuchelewa kurekebishwa matatizo ya Muungano; mjadala huu ni namna na kutokuondoa kasoro za Muungano; mjadala huu ni kutokuwepo chombo kilichowekwa kisheria cha kutatua matatizo ya Muungano, sio Timu ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, hapana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wanaofanya mazungumzo yao bado sio chombo kilichoundwa kisheria kwa mujibu wa *article of union*, wote wawili wanafuata sera za Chama cha Mapinduzi. Nchi hii tumekubali kuwa ni nchi ya vyama vingi. Hivi vyama vingine 16 vilivyobakia waliokuwa hawana vyama, Taasisi za Kidini wote wanahitajika kwa upana wao kupata mjadala mahsus kwa kuchambua mambo ya Muungano. Wana umuhimu katika Taifa hili wote. Kwa hiyo, timu ya Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu haitoshi na sio sahihi katika kutafuta ufumbuzi wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea na mfumo huu tutapata matatizo makubwa siku hadi siku kwa sababu vizazi vyetu vya baadaye vitakuja kuwa na maswali ambayo hayawajibiki. Tukiacha vizazi vya baadaye kwa bahati mbaya au nzuri mtoto wangu mimi hivi sasa kuna maswali ya Muungano ananiuliza nilishindwa kumjibu. Kwa mfano, mwanangu ananiuliza kila zikikaribia siku za sherehe za Muungano anapoona Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anachanganyisha ule udongo ananiuliza, baba Karume yuko wapi pale? Huu sio Muungano wa Tanganyika na Zanzibar? Si wangekuwa wawili wanachanganyisha? Hapo mmoja amekamata huku na mmoja amekamata huku,

mbona ni mtu mmoja tu anayechanganyisha? Nashindwa kumjibu. Ukitazama, ni kweli ni mtu mmoja anachanganya udongo. Sasa mtoto mdogo wa miaka 12 leo ananihoji suala hilo, nashindwa kupata jibu sahihi. Labda Mheshimiwa Waziri aje anisaidie kama analo jibu sahihi. Kwa hiyo, tukiachia haya yanakuwa siku hadi siku tutazidisha matatizo, tutakuja kusababisha makaburi yetu yafukuliwe wavuruge wapige magongo mafuvu yetu. Tusiache haya kuendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1968 katika rekodi za *Hansard* nilizonazo hapa alikuweko Mbunge mmoja anaitwa Mheshimiwa Choga, sijui yuko hai au ameshafariki! Mheshimiwa huyu Choga mwaka 1968 ilipoletwa katika ile *interring constitution* kwamba kuwe na mabadiliko ya Katiba kuhusu suala hili hili la mafuta, ni Mbunge pekee katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano aliyesimama kidete akasema, hapana, tusibadilishe haya mambo madogo tutafute mambo makubwa kwanza tubadilishe. Katiba yetu kwa wakati huo inasema nchi hii ni ya chama kimoja wakati humu ndani ya Bunge, Bunge la wakati huo ambalo linawakilishwa upande wa Zanzibar Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na watu wengine wa kuteuliwa. Lakini tayari wakati huo kuna Afro-Shiraz na TANU, lakini Katiba ya nchi ya chama kimoja. Mheshimiwa Choga akasimama kidete akasema tubadilishe Katiba kwanza iwe ya mfumo wa vyama vingi na naweza nikamnuu na hizi hapa nakala zipo, akakataliwa.

Mheshimiwa Choga mawazo yake yote aliyoysesema tubadilishe wakati huo alionekana Mpinzani, alionekana huyu sio mpenda maendeleo na mwisho wake akafukuzwa. Lakini bahati nzuri yale ya Mheshimiwa Choga aliyoyataja, mengi sana asilimia 50 hivi sasa yameshatekelezwa. Sasa tazameni mtu mmoja ambaye alikuwa na mawazo hayo mwaka 1968 lakini mawazo yake leo tayari nusu yake yamekuwa *implemented* au zaidi. Kwa hiyo, kwa msemo huo huo tusifanye makosa haya ya kila siku, ni lazima tubadilike tuone hali inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kujiuliza, awamu zote sita zilizokaa Zanzibar hakuna hata awamu moja ambayo haijaleta migogoro ya Muungano. Mwaka 1965 mwaka mmoja tu baada ya Muungano Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Abeid Amani Karume tayari alishahitilafiana kuhusu kuanzishwa kwa *BoT* na ndipo alipotafuta Mshauri Herbert na baada ya mzozo kuwa mkubwa ndio kuanzishwa kwa Benki ya Watu wa Zanzibar mwaka 1965. Hilo kama halijatosha, awamu ya pili Mheshimiwa Aboud Jumbe hakuridhika na masuala ya Muungano akaleta mtaalamu wa sheria kutoka Ghana kushauri na kukosoa na kutafuta njia za Kikatiba kutatua matatizo ya Muungano yaliyompata mnayafahamu.

Mpaka hii awamu ya sita, hivi karibuni sote tunajua nini kiliendelea Baraza la Wawakilishi walipokutana Wabunge wote wa CCM na *CUF* wakaungana kuhusu suala la mafuta. Sasa ikiwa Wawakilishi wote wa CCM na *CUF* mwaka 1965, sasa ikiwa awamu zote kila awamu inaleta matatizo hayo, awamu ya Dr. Salmin hali kadhalika bado hatujajua *magnitude* au ukubwa wa hili tatizo likafanyiwa ufumbuzi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar peke yake 1990 mpaka mwaka 2003 waliunda Kamati 12 kwa upande wa Zanzibar kutafuta kasoro na kuchambua ili kuishauri Jamhuri ya Muungano wakubaliane kuondoa kasoro hizo, hakuna kilichokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ushahidi nizitaje. Mwaka 1990 mpaka 2003 iliundwa Kamati ya Baraza la Mapinduzi ilivyoitwa Kamati ya Amina, Kamati ya Rais ya Kupambana na Kasoro za Muungano, Kamati ya Rais ya Kuchambua Ripoti ya Kissanga, Kamati ya Rais ya Kuandaa Mapendekezo ya SMZ juu ya kero za Muungano, iliitwa Kamati ya Ramia, Kamati ya Serikali ya Mapinduzi juu ya Sera ya Mambo ya Nje, Kamati ya Rais juu ya Kero za Muungano, Kamati ya Baraza la Mapinduzi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati ya Mafuta, Kamati ya Madeni baina ya SMT na SMZ, Kamati ya Masuala la *Explosive Economic Zone*, Kamati ya Masuala ya Fedha na Benki Kuu, Kamati ya Rais ya Masuala ya Simu. Zote 12 ushauri wa SMZ juhud zote za SMZ hazikufua dafu, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano yenye na Serikali ya Mapinduzi wakakaa pamoja wakaunda Tume saba jumla kushauri masuala ya Muungano, naomba nizitaje. Kamati ya Mtei, Kamati ya Nyalali, Kamati ya Shellukindo (yuko humu humu ndani Mwenyekiti wangu), Kamati ya Bomani, Kamati ya Shellukindo Na.2 ya Kuandaa Muafaka juu ya Mambo baina SMT na SMZ, Kamati ya *Harmonisation*, Kamati ya Masuala ya Simu, Kamati ya Kusila hiyo, zote hizo zinatumia fedha za walipa kodi, zote hizo iwe bado hakuna kilichopatikana, tukaweza kuwa na mfumo ule unaokubalika, bado mpaka leo tuzungumze kasoro za Muungano?

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi au tunajifunza nini? Au ndio tunataka kuthibitisha kwamba huu Muungano ulikuwa wa ujanja ujanja, mmoja mkubwa amtawale mtu mwingine? Nina rafiki yangu mmoja tulikuwa tukitaniana katika mambo ya Unguja na Pemba akaniambia nyinyi Wapemba nyote bora tuwaondoeni tuwahamisheni hapa Unguja kile kisiwa tuwakodishe Waitaliano muache hizo sogo zenu. Halafu baadaye akaniambia kutokana na matatizo ya Muungano, bora sasa wote wa Visiwa vya Unguja na Pemba tupelekwe huko Bara tutafutiwe eneo hivi visiwa tuwape wawekeze huku. Sasa nini tunatafuta? Ina maana yale maneno nayayosemwa tukiacha yale yanayoendelea, yale mambo yanayosemwa kwamba upande mmoja wa Muungano una nia ya kummeza mwingine ndiyo yanadhihirika! Tutakuja kupata matatizo baadaye.

Mheshimiwa Spika, niende katika suala la mazingira. Kama utakumbuka siku moja nilisimama hapa katika maswali ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Spika, ni wewe mwenyewe uliyeniambia Makamu wa Rais yupo pale kwa mambo ya Muungano, amewekwa pale baada ya kubadilika Katiba. Leo Ofisi hii ya Makamu wa Rais kuna masuala ya mazingira. Mazingira sio suala la Muungano, lakini liko katika Ofisi ya Makamu ya Rais ambayo inashughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kizungumkuti kwa sababu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, leo amezungumzia masuala ya Bonde la Mto *Nile*, alizungumzia masuala ya Ukanda wa Pwani wa Bahari lakini Visiwa vya Unguja na Pemba vinatoweka.

Bahari inakula vile visiwa siku hadi siku kila mwaka zaidi ya mita moja na nusu bahari inaingia ndani. Mipango yote hii inafanywa ambayo sio ya Muungano iko katika

Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, pale hatujaona mpango wowote wa kuvinusuru Visiwa vya Unguja na Pemba. Kuna njia tele za kujenga mipango tofauti, pale Durban wamefanya namna gani kuzuia mmonyoko wa ardhi?

Mheshimiwa Spika, kengele ya pili hiyo?

SPIKA: Ndiyo.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Siku nyingine unisaidie tena, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa ujumbe wako uliojaa hisia. Nina hakika majibu yapo. Anafuata Mheshimwa Hafidh Ali Tahir.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Kabla ya kusema lolote na mimi niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi kwa mpenzi wetu Prof. Haroub kule Zanzibar na Sheikh Suleiman Gorogosi pale Lindi, Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema nitajitahidi leo, nataka nijitahidi sana niwe na *tone* ambayo itakuwa ni laini inayofahamika sana na iliyokuwa haina jazba.

SPIKA: Sio rahisi. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nitajitahidi na nilitaka kusema katika maelezo yangu, wala mimi sitaki kugusia suala la kuchanganya udongo aah, sigusi mimi huko. Kwa sababu ninachojuwa udongo ule nusu umetoka Bara na nusu umetoka Zanzibar na wale waliokamata pale chini mmoja ni kijana kutoka Zanzibar na mmoja kutoka Bara. Sasa sitaki kujua aliyechanganya ni nani kwa sababu najua watu hawa wawili walikaa, wakazungumza wakakubaliana tufanye Muungano, wewe utakuwa Rais. Sasa Rais ndiyo anachanganyisha, sasa mimi sitaki kwenda huko.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, tuliungana mwaka 1964 tunayo mambo ambayo tumezungumza tangu mwaka 1964. Wapo watu ambayo wameyazungumza hayo mambo ya Muungano, tunayazungumza. Kwa hiyo, tuna Muungano mwaka 1964, tuna mambo yaliyotokea katika Muungano, tuna kero za Muungano na tunaelekeea mbele bila ya Muungano huu kuvunjika, maana ninachotaka kusema asitokee mtu hapa akafikiria kwamba Muungano huu utavunjika, haiwezekani. Anayekuwa na fikra za kuvunja Muungano huu maana yake anataka kuondoa udugu wa dhati uliokuwepo baina ya wananchi wa Tanzania Bara na wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kingine ninachotaka kusema, asije mwenzetu mmoja akasema huu Uzanzibar ambao tumeungana na Tanzania Bara, basi kuna mtu anamiliki pale Zanzibar peke yake, hakuna. Zanzibar *is a cosmopolitan country*, hakuna mtu aliyefufuka pale chini ya ardhi hata mmoja, hakuna. Sote tulio baki tumekikuta kile kisiwa. Iwe Mwarabu, Mhindi na kadhalika maana yake asije mtu kama mie ni

Mzanzibar hapana. Kuna taratibu zinazotufanya kuweza kuwa Mzanzibar. Sasa nilichotaka kusema, sitaki kuelekea kule ambako kwa kusema, basi tunaonewa sana, hapana. Nilichotaka kusema leo tufanye nini ili tuondoe haya yaliyokuwepo sasa hivi kuelekea katika ufanisi wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, mengi tumeshazungumza hapa, mengi sana, kero ziko kweli kero za Muungano hakuna anayekataa. Tuna miaka 45, zipo kero, lakini kero zinazungumzwa. Lakini sasa tutazame na hizi kero nazo zinapelekwa pelekwa vipi? Tusizipe ushabiki sana. Mimi nakubali kero, tena mimi peke yake zinanikera, lakini mimi nataka kuzungumza huko tunakokwenda mbele. Kwanza nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpungeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu leo. Juzi nilisema katika maelezo yangu kwamba nina miaka kama minne nazungumzia suala la Zanzibar na Michezo. Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi kama alikuwa ameona siku ambayo alinikosha mimi na Wazanzibar, basi juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alinikosha kwa sabuni ya *lux*, ile sabuni inayonukia.

Lakini hilo halitoshi, ninachotaka kumwambia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya juzi, kule Zanzibar akija akisikia kuna maandamano ya kumuunga mkono kwa hotuba hiyo asishangae. Wanamuunga mkono vijana kule Zanzibar. Sasa kama sikuchukua nafasi ya kumpongeza nitakuwa mwizi wa fadhila. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchukua hatua yake ya kuutia nondo zaidi Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta hii ya mazungumzo. Ni jambo la faraja sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimesema leo sitaki kuzungumza yale ambayo yamezungumzwa, lakini nataka kuzungumza mengine ya kutia nguvu zaidi katika Muungano. Rais wa Jamhuri ya Muungano hivi sasa ni Jakaya Mrisho Kikwete kwa bahati nzuri. Nasema, bahati nzuri anaendelea katika kipindi chake cha pili mwaka 2010 na nasema anaendelea kwa sababu sina wasiwasi. Hayo magazeti yanayozungumza sijui kuna nani anataka kuja kuna mambo na taratibu zake, lakini atamaliza miaka yake mitano.

Lakini wakati atakapokuwa anamaliza miaka yake mitano Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, atakuwa na macho na darubini nzuri kuangalia upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kuna nini, ndiyo kazi yake kubwa atakayokuwa nayo mwaka 2010 na natarajia atakuwa haweki kiti chake akazunguka tu, hapana. Ataangalia kwa sababu Zanzibar kule kuna uchaguzi wa Rais, kuna uchaguzi wa Wabunge na Wawakilishi. Lakini pakubwa tunapokamata ni hapa kwenye Uchaguzi wa Rais. Kwa sababu bila ya kuwa na Rais wa Mapinduzi Zanzibar maana yake ndio kuna dosari hapo na yeye ndio Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo macho yake nayo yawe yanatazama upande wa pili ili ile hadhi yake ya Rais wa Jamhuri ya Tanzania iweko pale.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ambacho nataka kusema katika hili, Urais wa Zanzibar si jambo la masihara. Urais wa Zanzibar ndio utakaoleta hadhi na heshima ya Muungano huu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa Rais huyu akiwa ametoka katika Chama cha Mapinduzi. Lakini nataka kuwaambia wenzangu ambao juzi hapa

walikuwa wanamzungumza zungumza sana Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini nilichotaka kusema kwa sisi Wazanzibar na mimi niliposimama hapa, najua Mzanzibar ni wa aina gani katika siasa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwa Zanzibar na hapa nilipoomba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aangalie macho yake, basi mmoja katika kada ambao tutawahitaji katika uchaguzi huu ni Benjamin William Mkapa, kwetu sisi hana dosari. (*Makofi*)

Tunazungumza ujisadi na mambo mengine, lakini sasa nataka niseme jambo moja ambalo hivi sasa ndani ya Jamhuri ya Muungano linazungumzwa sana, ujisadi. Lakini sasa njoo kule Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu majuzi aliwataka Mawaziri wake waje kule watembee na mimi ningekuomba ungekuja siku moja ukakaa kiasi cha wiki hivi au siku tano, ukaja ukasikia Wazanzibar wanasema nini, ukajifunza Wazanzibar wakoje, usije ukakutana na sisi humu Bungeni tu. Maana yake hili neno ujisadi kwa kule kwetu Zanzibar ni mchochezi, mnafiki, mvurugaji mambo, sawa sawa na mtu pale ulipooa mkeo akaja akaingia katikati akatia maneno, huyu ni fisadi. Sasa kwa kule kwetu pia tunamwita huyu mzushi, ndio ujisadi huo kwa kule Zanzibar.

Lakini tuache watu watohoe hili neno na liende hivyo hivyo. Ndio maana ukaona sisi Wabunge kutoka Zanzibar linapozungumzwa suala la ujisadi ndani ya Bunge hajanyanya hata mmoja kuzungumzia ujisadi kwa sababu tumeliacha liende kama linavyokwenda ujisadi. Kwa sababu sisi ujisadi tunajua maana yake nini, sasa tuacheni hivi hivi tulivyo, lakini ukija kule Zanzibar na hili ndilo nataka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete baadaye aje atulie kidogo aliangalie, sisi kule kwetu tunaita mtu mlafi.

Mheshimiwa Spika, mtu mlafi na fisadi vitu viwili tofauti. Mlafi ni mtu asiyetosheka, huyu ndio mlafi, mlimbikizaji mali, chake anataka kiwe chake na chako wewe kiwe chake, huyu ndio mlafi. Sasa naikamata hii makusudi nikakwambieni bakieni na neno lenu ujisadi na sisi kule Zanzibar tuachieni na letu mlafi. Lakini ninachotaka kusema, mwaka 2010 na nimemgusa Mheshimiwa Jakaya Kikwete hapa, unapokuja uchaguzi ule Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano ambaye ndio Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi awe na macho arobaini katika kutafuta huyu mtu atakayemsaidia katika kuleta uhimili mzuri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndio nilikokuwa naelekea.

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar tuna embe zinaitwa bolibo. Bolibo zote sio tamu. Kuna bolibo nyingine kali, japoquwa rangi yake nzuri, halafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete awe anapokea salamu kama zile za Mpoto japoquwa mimi sitaki kutafuta nauli, lakini nikipata nafasi nitakwenda. Nataka awe anafahamu kwamba asije akakumbana na watu wenye asili ya kuruwiji. Kuruwiji ni ndege mmoja mzuri sana, kuruwiji alikitesa sana kichaka. Alipokwenda kwenye kichaka akakisifu sana kichaka kile kizuri kinanukia udi na hadithi nyingine kwa sababu alitaka kulala, amelala mpaka asubuhi alipoamka akakutukana vibaya mno kile kichaka. Sasa namtahadharisha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete hapa bolibo zote sio tamu na asije akawemo kwenye hadithi ya kuruwiji na kichaka. Lakini tupate mtu madhubuti ambaye atatuondoa hapa tulipokwama katika Jamhuri ya Muungano, atakayetuelekeza huko tunakokwenda sisi Wazanzibar ili kero hizi ziondolewe.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba wapo ambao wanaweza kutoondoaa hapa tunapopiga kelele sasa hivi. Maana yake nataka nikuhakikishie tena kwamba wapo ambao wanaweza kuunganisha Chama cha Mapinduzi na *CUF* wanaopiga kelele, wapo. Usije ukashangaa haya aliyojasema Mheshimiwa Mnyaa hapa yaliyotokea kule Baraza la Wawakilishi kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na *CUF* na CCM walifika mahali wakashikamana. Tunakoelekea mwaka 2010 yupo mtu ambaye anaweza akatufanya tuwe hivyo, Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete apokee salamu zangu, awe macho asiende kwenye bolibo tamu zote na asimuige kuruwiji. Naondoka hapo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilimwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie sana suala la ajira ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na leo nataka nikumbushe jambo moja ambalo tumelisema humu. JKT imesharudishwa na tumetaka vijana wetu waende JKT lakini JKT iko chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kule Zanzibar kuna JKU, sasa kama JKT hapa Bara iko chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa nini kule Zanzibar JKU isiwe chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili vijana hawa wakajifunza kazi za mikono na nyingine zote za kilimo kama ilivyo kule Zanzibar. Hili lingefikiriwa ili kuondoa hizi bughudha zilizokuwako sasa hivi Jeshi la Wananchi wa Tanzania na JKT, Jeshi la Wananchi wa Tanzania JKU hawaijui, kumezuka nini?

Mheshimiwa Spika, sisi tunao vijana wetu tunataka tuwape kazi, si ndio hao hao tunataka darasa la saba waende! Basi waende! Waende kwa maana tuchukue vijana wa Zanzibar tuwalete Bara JKT wajifunze kama tulivyokuwa tunafanya zamani, wakirudi hawa watambulikane kwamba wako chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili wawewe kufanya kazi vizuri. Hili halijajibiwa na namwomba Mheshimiwa Waziri safari hii alijibu vizuri kwa sababu tayari tumeshakubali kwamba JKT iwe katika hali hiyo. Hii ni muhimu sana sawasawa na suala la vyombo vya Magereza, ninatoa mfano huo vile vile.

Lakini kwisho kabisa kabla ya kengele hajjalia, namwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa azunguzie suala la Wanajeshi Wastaifu. Kule Zanzibar tuna wanajeshi wastaifu wako katika hali dhalili, dhiki, wanatisha, wanaogopesha!

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilisema hapa kwamba Askari ana cheo cha *Major* anauza dagaa kwa baiskeli. Sio sahihi! Watu kama hawa tuangalie na tuwawekee utaratibu maalum ili wasije wakatia aibu katika nchi yetu. Ni aibu kumkuta *Major General* anatoka kwenye Jeshi baada ya miezi sita mtu huyu unamkuta anauza nyanya. Haiwezekani! Hili sio jeshi la wananchi wa Tanzania. Jeshi la wananchi wa Tanzania liwe na utaratibu wa kuwaenzi wanajeshi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Tahir. Nakupongeza umejitahidi sana kutokupanda jazba. Lakini nakushukuru kwa mchango wako. (*Kicheko*)

Sasa mchangiaji wangu wa mwisho ni Mheshimiwa Luka Jela Siyame.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nishiriki katika kujadili Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais mambo ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira. Awali ya yote naomba nami nishirikiane na wenzangu kutoa rambirambi kwa vifo vilivyotokea vya Prof. Haroub Othuman. Sheikh Gorogosi na kwa leo kule mjini Tunduma kwa kifo cha kijana mmoja ambaye inasemakena ameuwa wakati wa vurugu ambazo zimetokea kati ya wananchi na vyombo vya dola. Naomba wananchi wawe wavumilivu waachie sheria ichukue mkondo wake maana vurugu hizi hazitawafikisha popote, sana sana umwagaji damu utaendelea. Naomba vyombo vya dola viweze kuwavumilia wananchi kwa kukaa na kujadili kwa pamoja maana kwa bahati mbaya sana leo hii mwenge wa uhuru umeingia Jimboni kwangu na ndiko huko Tunduma na inatokea vurugu wakati mwenge ni ishara ya amani kitu ambacho nisingetegemea kitokee kwa leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais kwa hotuba yake nzuri na naomba pia niwapongeze watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na nitakuwa ni mchache wa shukrani nisipomshukuru Makamu wa Rais kwa kuiongoza Ofisi yake na kuendesha mambo yote kwa busara na kwa hakika yale ambayo yamesomwa kwenye hotuba hii leo yanaonyesha ni kwa kiasi gani amekuwa mahiri katika utekelezaji wa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sitaongea sana juu ya mambo ya muungano, lakini naona ni vyema niseme kidogo kwamba yale yote yaliyozungumzwa tumeyasikia na naamini kama walivyotangulia wenzangu wakasema malalamiko yaliyopo yanaweza yakazungumzwa na yakatekelezeka ili mradi pande zote ziwe na utulivu. Niliingia wasiwasi kwa kiasi kikubwa pale msemaji mmoja aliposema inaonekana katika nchi hii kiumbe yupo juu ya muumbaji wake. Kauli ile nafikiri sio njema sana kwa yejote ambaye anaitakia amani nchi hii. Kwa sababu kama tulivyokwisha kusema, kero zinazungumzika na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kwa kule Zanzibar inayafanya kazi hayo mambo. Yako mambo ambayo ni ya kisheria baada ya hapo kunakuwa na Kanuni zake ambazo baada ya hapo zinahitaji kutekelezwa na utekelezwaji ni mambo ambayo yanaweza yakajadiliwa pia. Kwa hiyo, nadhani tuwape nafasi wafanye yale wanayoweza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba sasa niingie kwenye mambo ya mazingira. Napenda nianze kusema mimi ni Mtanzania nilikuwa nikiona nchi hii kwa upande wa Mlima Kilimanjaro ule Mlima ukiwa na theluji kwenye vilele vyake, nilikuwa nikiuona Mji wa Mbeya ukiwa na maji yanayotiririka kwa mwaka mzima na ndege wanaozunguka kwenye miti na mandhari yake nzuri, nilikuwa nikiona misitu ya Mgororo pale Mafinga ikipandwa na kukua kwa uzuri kabisa lakini jinsi muda ulivyokwenda hivi sasa Mbeya ukienda unapokewa na yumbi ambalo linaonekana kama wingu lililotanda mji hauonekani, ukienda Mlima Kilimanjaro theluji haipo na Morogoro ukija ni moto unachomwa karibu kila mwaka na kwenye miti ile ambayo ilikuwa inapendeza sasa hivi ni mashamba ya mahindi. Hii yote ni uharibifu wa mazingira ambao kwa kiasi kikubwa umeletwa na shughuli za binadamu. Naomba nielekeze uharibifu huo huo kwa Wilaya yangu ya Mbozi hususani Jimbo langu la Mbozi Magharibi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nilikua nikiona Jimbo hili likiwa na miti mizuri ya mininga, miyombo na mbuga nzuri za wanyama pamoja na misitu ya hifadhi. Kwa uchache Mbuga ya Isalalo na Uwanda wa Hifadhi ya Mbuga za wanyama ambao ulikuwa unajulikana kama Mbuga ya Hifadhi ya Uwanda, hivi sasa hiyo miti inakatwa, inapukutishwa inatumbukia kwenye ile mito yetu inaharibu mazingira yetu kwa kupeleka magogo hadi kwenye miradi yetu ya umwagiliaji hadi inabomoka. Ule uwanda wa Ziwa Rukwa kulikokuwa na Mbuga ya Uwanda kulikuwa na wanyama aina ya pekee kwa Kiingereza wanaithwa *pook* kwa Kiswahili kwa kweli sijui. Lakini nafikiri ilikuwa ni sehemu pekee katika nchi hii ambao walikuwa wanapatikana wale wanyama baadaye walipoona hali ni hatari wakahamishiwa Ulanga na ukipita utawaona kule Ulanga badala ya kule Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Rukwa sasa hivi linakauka kutokana na *overgrazing*, malisho yake yamekuwa ni mbuga na sasa hivi ni jangwa linakaribia kulikausha lile Ziwa. Tumeona uchomaji wa moto wa mwaka mzima. Hivi sasa ukipitia kuanzia ile Rukwa yenye mpakani mwa Sumbawanga hadi unapita Mbeya ni moto ambao utafikiri usiku ukija ni mchana jinsi ambavyo mbuga zinaungua. Napenda niishukuru Serikali kwamba imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha inaweka utaratibu kuanzia Wilayani, kwenye Kata hadi vijijini ambapo wananchi wamepewa mamlaka ya kusimamia hayo maeneo. Lakini nafikiri kuna vitu viwili vinavyohitajika. Cha kwanza ni kuhakikisha hawa wananchi wanapata ile elimu ya Hifadhi ya Mazingira waone kwamba yale mazingira ndiyo uhai wao.

Cha pili, ni hawa wananchi kuona kwamba wao ndiyo wanawajibika kwa mazingira yao kwa sababu upotevu wa mazingira yao kama ambavyo tumeshuhudia katika miaka michache iliyopita utaleta uharibifu mkubwa na upotevu wa mvua. Zama zile sisi tulikuwa na mvua kuanzia Mwezi Oktoba hadi mwezi Juni. Lakini sasa hivi hadi mwezi Januari kunakuwa hakuna mvua na baada ya hapo ikishaanza kunyesha kufika mwezi Aprili inaisha. Hii yote ni dalili ya uharibifu wa mazingira, hivyo nawaomba tena wananchi wajaribu kuona mazingira yao kwamba ndiyo uhai kwa sababu wao ndiyo wanategemea kilimo kwa kiasi kikubwa. Sasa bila kuhifadhi hayo mazingira kutakuwa hakuna kilimo na umaskini utazidi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la pili nalo ni ule ukataji hovyo wa ile miti. Hii inachangiwa kwa upande mwengine na kwamba hawana uchaguzi. Hiyo ndiyo nishati ya kupikia na kufanya shughuli zote muhimu kutokana na kwamba kule hakuna umeme kama nilivyosema kwenye hizo hotuba nilizopita kwamba katika lile Jimbo umeme upo Tunduma tu na pale Mpemba hata huko upo kwa sababu miji hiyo miwili ipo kwenye njia kuu ya *national grid* ya umeme vinginevyo na kwenyewe kungekuwa na matatizo hayo hayo.

Napenda nizidi kusema kwamba tunahitaji elimu kubwa kwa hawa wananchi wetu. Kuna suala lingine ambalo lipo kwenye vyanzo vya maji katika ile Wilaya ya Mbozi nikianza na pale pale Makao Mkuu ya Wilaya Vwawa ambapo kuna chanzo cha mto mmoja unaitwa Nkhana. Pale kwenye chemichemi za chanzo cha mto huu ambao ni

mkubwa ambao unakwenda karibu kilometra 200 kufikia Ziwa Rukwa, kuna nyumba zimejengwa, kuna miti ya mianzi ipendwa na kuna migomba imepandwa na watu wanachimba vyoo ndani ya mita kumi kutoka pale kwenye hiyo chemichemi na hivi sasa huo mto unakauka kiangazi. Hii yote ni uharibifu wa mazingira na pengine kutojari wale watu ambao wako *down stream* wataishije hapo baadaye. Hivyo ningeomba Serikali hususani Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ichukue hatua za kuhakikisha inaokoa wananchi zaidi ya 150,000 ambao wanategemea maji ya mto huo.

Mheshimiwa Spika, pale Tunduma iko habari ambayo sio njema, nayo ni ya ujenzi holela mpaka kwenye vilima vya ule mji kiasi cha kwamba haisababishi tu uharibifu wa mazingira bali hata uwezo wa kuwashudumia wananchi kwa sababu matatizo kama ya maji kuyavusha na kuyapandisha hadi kwenye milima walikojenga nyumba inakuwa sio rahisi kwa Serikali yoyote. Hivyo, wale waliopewa mamlaka ya kusimamia ugawaji wa ardhi wanapaswa kuchukua tahadhari kabla hawajaanza kuwagawia wananchi viwanja hivi. Kwa sababu inaonekana, hivyo viwanja vimepimwa kihalali, hivyo basi, wale wananchi imbele ya safari tutakapoamua kuchukua hatua watatugharimu maana watahitaji fidia ambayo hatutakuwanayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwaomba hawa wananchi kwamba ingekuwa ni vyema wafuate taratibu za mamlaka za Wilaya za kupata hivyo viwanja badala ya kuvivamia. Pia naomba niseme tena kwamba tunahitaji hawa wananchi wasichome moto kama wanavyofanya hivi sasa ili kuweza kurudisha yale mazingira yalivyokuwa ya kupendeza badala ya hivi sasa tunaona ni jangwa linatujia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inamlinda kila raia wa Tanzania aishi kwa amani lakini yanayojitokeza hivi sasa, inaonekana wazi kuwa Katiba hiyo imezidiwa kutokana na uvunjifu wa sheria hii mama kwa uovu unaofanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa idadi ya watu imeongezeka na uvunjadi wa amani umeongezeka kupita kiasi. Kwa mfano, idadi ya watu katika Mkoa wa Mwanza na Shinyanga imeongezeka sana matokeo yake ni kuharibu mazingira. Katika maeneo haya, uzazi wa mpango haukuzingatiwa na elimu nayo ilichelewa kuwfikia. Matokeo yake, uharibifu wa mazingara kwa kukata miti na ufugaji wa mifugo usio na tija, ukaachiwa uendelee bila kudhibitiwa na kwa bahati mbaya hakuna elimu bora ya ufugaji ndio maana idadi ya ng'ombe ni wengi wasio na kipimo na ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira na chanzo cha migogoro katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, wafugaji hao sasa wamepewa kibali na Serikali hii hii, kwenda kuharibu mazingira ya Mikoa yote Tanzania ili igeuke jangwa. Inasikitisha, ofisi hii ya Mazingira inavyonyanyasika kwa kutopewa bajeti ili kusimamia mazingira ya Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Morogoro, Iringa, Lindi, Mtwara na Pwani. Tunaenda wapi?

Kama wafugaji wamejiundia Tume ya Haki za N'gombe, yenyе haki na nguvu zaidi kuliko haki ya binadamu, aitwaye mkulima, je, Wizara hii mpo?

Mheshimiwa Spika, wakulima 63 wameuawa Kilosa wakilinda mazingira yao lakini mifugo inayoharibu mazingira imetetewa kwa nguvu ya fedha kiasi Serikali imetetereka na kutetemeka na kufuta mpango wa kuhamisha wafugaji, ‘ole wao wakulima wasio na sauti na mtetezi’ na Ofisi ya Makamu wa Rais wamewekwa kando na kuachiwa Wizara ya Mifugo ishughuliki tatizo hili. Je, kesi ya Ngedere ukaipeleka kwa Nyani haki itapatikana? Jamani, mmeitelekeza nchi inateketea!

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza, ni mzaha ambao hautafanikiwa kama suala la mifugo halitashughulikiwa. Bado muda kidogo Tanzania itateketea. Yanayotokea Tarime, ni sababu ya ng’ombe. Mauaji ya Kilosa ni sababu ya ng’ombe. Upungufu wa mvua na njaa kushamiri, ni sababu ya ng’ombe hivi bado hamjazinduka?

Tanzania hii ikifa, wote tutakufa njaa kuu inayotabiriwa miaka ijayo ambayo inatokana na ufugaji holela. Tutajuta kwa sababu juhudzi za Wizara hii hupuuzwa na Wizara nyingine na hata maagizo yao yanapinduliwa na viongozi wa hata wa chini. Tafuteni jibu la ongezeko la ng’ombe nchini la sivyo janga linakuja kwa kasi ya radi na tutateketea wote kwani wakulima hawana uwezo wa kupinga wenye mifugo na Serikali inawatetea kwa woga.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Nchi, Muungano, Waziri wa Nchi, Mazingira na Watendaji wao, kwa hotuba na mikakati mizuri katika bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri na kupata maelezo katika maeneo yafutayo, kwanza, tabia ya uchomaji ovyo misitu imeendelea kukua sehemu nyingi nchini. Ili kuokoa nchi kuelekea kwenye majanga ya ukame na uharibifu wa viumbi asili, ipo haja ya kuimarisha Sheria zinazohusu Mazingira, ili kutoa elimu, adhabu kali, kwa lengo la kupunguza tabia mbaya za makusudi na hata bahati mbaya za uchomaji moto misitu nchini. Ni lini marekebisho ya sheria yatafanyika na sio kuziachia mzigoto Halmashauri za Wilaya majukumu na lawama zote!

Mheshimiwa Spika, pili, ukataji wa miti ya asili na uvunaji misitu ya Serikali. Ukataji miti ya asili unaongezeka kwa kasi na magogo kusafirishwa nje ya nchi. Hali hii inaharibu sana mazingira hasa katika maeneo ya Mikoa ya Pwani, Tanga, Morogoro na Lindi.

Mheshimiwa Spika, ukataji huu unahitaji kusimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, je, kuna uhusiano na mikakati gani ya pamoja kati ya Wizara hizi mbili za Maliasili na Utalii na Mazingira, ili kuepusha uharibifu wa mazingira. Je, haipo haja ya Wizara ya Mazingira kisheria kuwa sehemu ya mamlaka ya juu ya ukataji wa miti ya asili kwa lengo la kuhifadhi Mazingira? Kwa nini Wizara hizo mbili zisikae pamoja na

kutengeneza kanuni bora zaidi ili kwa pamoja zisimamie hifadhi ya mazingira ya eneo la misitu ya asili?

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa miti katika mashamba ya Serikali kwa mfano Mashamba ya Mitiki ya Lunguza Muheza na Kilosa, unafanyika kwa kasi kubwa kiasi cha kuhatarisha maeneo ya miti kama vile Ziggi, Wilaya ya Muheza, kitendo ambacho ni hatari kwa hifadhi ya mazingira. Je, Wizara ya Mazingira inasaidia kutoa ushauri gani kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, juu ya kazi ya uvunaji wa miti na usafirishaji wa miti ya mbao nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, tatu, usafirishaji mkaa nje ya nchi. Kutokana na usimamizi usio bora wa misitu na miti ya asili, kumepelekea Tanzania kuwa nchi inayosafirisha mkaa kwenda nje ya nchi kama vile Mombasa, Comoro (inawezekana pia Zambia na Malawi, Rwanda na Burundi). Kitendo hicho kinaashiria uharibifu wa mazingira kwa kiwango cha juu! Hata kama Wizara ya Maliasili na Utalii inawajibika kwa usimamizi, nini jukumu la Wizara ya Mazingira? Tatizo kama hili linapojitokeza waziwazi bila kificho, je, hatuoni bado ipo haja ya kuboresha ushirikiano kati ya Wizara hizo mbili ili kuboresha mazingira katika maeneo ya asili?

Mheshimiwa Spika, nne, upandaji miti Kimkoa. Wilaya ya Muheza, inaongoza kwa upandaji miti katika Kampeni ya Kitaifa ya mwaka 2007 – 2008. Hata hivyo, Wilaya ya Muheza haipo mionganoni mwa Wilaya zilizopata Hati za TAM, wala kuwemo katika Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwekezaji (*PADEP*).

Mheshimiwa Spika, hii inawezekana kwa watendaji wa Idara husika katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuhitaji elimu ya ufahamu katika maeneo hayo. Je, Wizara ya Mazingira itachukua hatua gani kuisaidia Wilaya hiyo hasa ikizingatiwa kwamba imechelewa sana kuajiri Afisa Mazingira!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, baada ya hotuba iliyosomwa mbele yetu, napenda kusema kuwa ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye Halmashauri zetu, Idara za Maliasili haziwezesewi kwa maana ya kupewa hela ili kutekeleza majukumu yake. Ni dhahiri kwamba Idara hiyo watumishi wake wanajikuta hawana kitu cha kufanya. Hata pale wanapopewa maelekezo ya kupanda miche kama 10,000, wanajikuta hawana fedha. Ni vema Idara hiyo ingewezeshwa kwa kutengewa fedha katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, hali ya mazingira katika miji mikubwa na midogo, siyo nzuri. Kwa mfano, unakuta usafi hakuna hususani mvua zinaponyesha. Katika miji, utakuta hakuna usafi wa vyoo, ma-*dampo*, mahoteli na nyumba za kulala wageni.

Mheshimiwa Spika, upo mfumko wa *NGO*'s nyingi ambazo zinafadhiliwa fedha na wafadhili/Wizara, kwa kigezo cha kuendeleza masula yahusuyo mazingira. Kwa hakika, ni vema *NGO*'s hizo zikadhibitiwa kwa sababu inaonekana fedha zinazotolewa hazifanyi kazi zinazoombewa. Nashauri uwepo udhibiti mkubwa wa *NGO*'s hizo.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mawaziri wa Nchi na watendaji wote kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/2010. Aidha, nawapongeza kwa usimamizi mzuri wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia matumizi makubwa ya nishati ya kuni na mkaa unaotokana na miti, ninashauri Wizara ya Mazingira kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Nishati na Madini, kwa madhumuni ya kuharakisha matumizi ya nishati ya gesi asilia kwa kupikia na kuendeshea mitambo mbalimbali pamoja na magari. Kwa kufanya hivyo, nchi itaokoa miti mingi ambayo inakatwa kwa ajili ya kuchoma mikaa na kuni.

Aidha, moshi mwingi mzito utokanao na matumizi ya petroli na deseli kwa ajili ya kuendeshea magari na mitambo mingi, itapungua pia na hivyo kupunguza madhara ya moshi kwenye mazingira yetu na tabia ya nchi. Tunaweza pia kufaidika kwa kupata *Carbon Credits*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Magadi – *Lake Natron*. Pamoja na hoja nzuri ya kulinda mazingira kwenye eneo la *Lake Natron*, bado napenda kuendelea kuishauri Serikali iandae mipango ya kuanza kutekeleza miradi ya “*Soda Ash*” (magadi) katika ziwa *Natron* kwa faida za kiuchumi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tuliambiwa Serikali inafanya tathmini ya kiuchumi na ki-Mazingira kabla ya kufanya uamuza kuhusu utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa uchumi wetu. Je, tathmini hiyo imefika wapi? Nasisitiza Serikali ifanye haraka kukamilisha tathmini hiyo kwa manufaa ya uchumi wetu. Mimi bado ninaamini sana kwamba nchi hii inauhitaji mradi huu bila kuathiri mazingira yetu.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo, nauelekeza zaidi juu ya uchafuzi wa hewa kutokana na hewa mkaa izalishwayo na magari hasa yale yasiyofanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ione umuhimu wa kutunga sheria (kama haipo) ya kusimamia mazingira hasa hewa ya mkaa itokanayo na magari chakavu na yasiyofanyiwa matengenezo. Magari mengi yanatoa moshi mwingi sana yakiwa barabarani kiasi kinachohatarisha mustakabali wa mazingira ya nchi na kuhatarisha pia afya za watoto na wananchi wengine wanapolazimishwa kuvuta hewa hiyo bila ridhaa

yao. Hali iliyofikiwa kwa sasa haiwezi kuvumilika na ni wajibu wa Serikali kulivalia njuga suala hili ili liweze kupungua.

Mheshimiwa Spika, nashauri magari yote yanayotoa moshi kupita kiwango kinachoruhusiwa kitaalam, yakamatwe na wahusika wafkishwe mbele ya vyombo vyasheria. Tusipokuwa wakali leo, athari ya hewa ya mkaa yatakuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, nitumie fursa ya kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, za kimaendeleo kwa nchi yetu kama hatua ya kuwaondolea umaskini wananchi.

Nitumie fursa hii, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib (Mb), Waziri wa nchi mwenye dhamana na majukumu ya Muungano, pia Mheshimiwa Hajat Dr. Batilida Salha Burian (Mb), Waziri mwenye dhamana ya Mazingira, Makatibu Wakuu na Watendaji wao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu nyeti ambayo yana changamoto katika nchi yetu, ni suala la Muungano. Katika siku za hivi karibuni, kwa makusudi ama kwa nia mbaya ya kutoutakia mema Muungano wetu, baadhi ya maneno yamenza kuzushwa kana kwamba Waasisi wa Muungano wetu, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mzee Abeid Amani Karume, walikosea katika kuunda misingi wakati wa uanzishaji wa Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, maneno yanayotumika hivi sasa sio maneno bora sana katika kuimarisha Muungano wetu. Je, Serikali kuitia ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa Waziri wa Muungano, ni mikakati ipi ambayo imeandaliwa katika kutoa elimu kwa kizazi cha sasa ili kutoa uelewa wa misingi imara ya Muungano wetu?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, kwa idadi kubwa ya wananchi wa nchi zetu hizi mbili, Tanzania Bara na Zanzibar, umri wao ni wale waliozaliwa ndani ya Muungano, waliozaliwa nje ya Muungano, umri wao sasa umekuwa mkubwa kwa maana hiyo upo umuhimu mkubwa wa kutoa elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, vipengele vya Katiba ambavyo ni kero, vinapatiwa ufumbuzi gani? Mfano kama vile mgawanyo wa rasilimali, Ibara ya 133, 134 (a), (b) na (c), vinafanya kazi kwa kiwango gani? Ni vema vipengele hivi vikaelezwa bayana na kujua utekelezaji wake, kwa kufanya hivyo kutaondoa manung'unico.

Mheshimiwa Spika, masuala ya mafuta, gesi, michezo na kadhalika, ni muhimu kupata ufanuzi wa kina ili kuondoa hali ya kutokuelewana kama kauli za hivi karibuni zilizotolewa ndani ya Bunge hili Tukufu na Baraza la Wakilishi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuongoza Muungano hasa katika nafasi nyeti kama Rais wa Jamhuri na Makamu wa Rais, ni hadhi kubwa sana pamoja na kinga na maslahi mengine baada ya viongozi hawa kukoma madaraka, ninapendekeza hadhi yao iendelee kutambuliwa na kupewa hadhi ya juu kabisa, kiheshima ikiwemo kutunukiwa Nishani Maalum ya Heshima ya Muungano kama ishara ya kuwaenzi na kukumbuka mchango wao kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mazingira, pamoja na uwepo wa Wizara hii, ni dhahiri mtandao wa Wizara hii, naweza kusema ni kama umeshia ngazi ya Taifa. Mtandao wa Wizara hii, ni muhimu sana kwa ngazi zote; Mkoa, Wilaya hadi kwenye Kata. Kuwa na *Environmental Officer* peke yake kwa ngazi ya Mkoa ama Wilaya, haitoshi. Maisha yetu kwa kila siku, yanahitaji na yanaendana na utunzaji wa mazingira, hivyo kutokuwa na waratibu wa kutoa elimu juu ya masuala ya mazingira, ni kutoitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *NEMC*, pamoja na kuwa katika Kanda za Mwanza, Mbeya na Arusha, ni muhimu pia kuwa na kituo cha kazi Kanda ya Kati kwa maana ya Mkoa wa Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma. Uwepo wa kituo cha *NEMC* Kanda ya Kati kutasaidia sana katika kutoa ungalizi na elimu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia hotuba hii, Wizara ione umuhimu wa kuja kutoa ushauri nasaha kwa wananchi wa Ziwa Kitangi, wa vijiji vya Tulya, Mesi, Doromoni, Shauritanga, Migilango, Geta na vyote vinavyozunguka Ziwa hili ili kuliokoa na uharibifu ambao kwa kiwango kikubwa imesababishwa na uharibifu wa mazingira. Kupotea kwa kina kutafanyaZ hili kupotea na mazao ya samaki nayo kupotea.

Mheshimiwa Spika, naomba pia ushauri uje utolewe namna ya kutunza hekta 35,600 za msitu wa Mlima Sekenke uliozinduliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kadhalika msitu wa Kinampanda, msingi wa kutunza na kuhifahi maeneo haya kitaalam, kutasaidia kutunza vyanzo vya maji na kuvuta mvua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, natoa pongeza sana kwa hotuba nzuri, yenye kuonyesha matumaini mema. Ninayo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, elimu ya mazingira kwa umma. Wilayani Chunya hasa kwenye Jimbo la Songwe, wapo wachimbaji wadogo wa dhahabu, wafugaji, wavuvi, wakulima wachoma mkaa na wapasua mbao. Matokeo ya shughuli za vikundi hivi, ni uchafuzi na uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Hali hiyo inatokana na vikundi hivyo kutokuwa na elimu ya uhifadhi wa mazingira. Nashauri elimu hiyo itolewe kwa vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Dunia wa Mazingira – *GEF*. Vikundi vyote nilivyovitaja hapo juu hasa vile vya wachimbaji wadogo, wavuvi na wapasua

mbao, hutumia vitendea kazi duni sana. Nashauri utaratibu ufanyike kuviwezesha vikundi hivyo ili kazi waifanyayo iwe na tija kupitia mfuko wa *GEF*.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira Rukwa. Hali ya uharibifu wa mazingira na athari zinazotokea Ziwa Rukwa hasa upande wa Kusini mwa Ziwa Rukwa, Wilayani Chunya, Jimboni Songwe, baadhi ya athari ni kama zifuatazo:-

- (a) Kupungua kina cha maji kutoka mita 14 (1990) hadi mita 4 (2008); na
- (b) Ziwa kuendelea kupungua ujazo – kukauka yaani ukingo wa maji (*lake shore*) kuzidi kunyauka (*shrinking*) kutoka umbali wa kilomita $1\frac{1}{2}$ (2005) hadi kilomita 7 (2009).

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zilizoleta athari hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- Kulundikana kwa mifugo kwenye bonde la Rukwa;
- Kilimo holela (*unorganized farming agriculture*); na
- Kuongezeka/kulundikana kwa mchanga na udongo, *sedimentation or siltation*

Mheshimiwa Spika, nashauri jitihada zifanyike na Wizara kama zile zinazofanyika katika maziwa mengine kama vile *Lake Natron*, Lake Victoria na Lake Tanganyika katika kuhifadhi mazingira kwenye Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, hawajafanya ziara Chunya kwenye Majimbo yote mawili ya Songwe na Lupa, wananchi wanaomba muwatemelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, nchi yoyote inayoendelea, inakabiliawa na matatizo makubwa ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Sababu za msingi, ni shughuli mbalimbali zinazofanywa na binadamu.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kuzuia uharibifu wa mazingira bado hazitoshi kwani ukienda maeneo ya wachimbaji madini kuna matumizi ya aina mbalimbali za kemikali ikiwemo zebaki, ambayo imekuwa ikiharibu vyanzo mbalimbali vya maji. Hivi karibuni Mkoa wa Mara, yametokea maafa na wananchi kuathirika ngozi na kemikali inayotiririka katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya viwanda pia bado kuna matatizo ya utunzaji wa mazingara kwani muundombinu ya utupaji taka na maji taka yenye kemikali sio mzuri. Hivyo, wananchi wamekuwa wakilalamikia hali hiyo mfano Kiwanda cha Ngozi mjini Moshi. Vile vile, Kiwanda cha Khanga na Vitenge Mbagala.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni viwanda vingi viko karibu na makazi ya wanadamu. Nashauri watu wa Mipango Miji wahakikishe maeneo ya viwanda yasiwe karibu na makazi ya wananchi ili kuwanusuru na athari mbalimbali zinazotokana na shughuli za viwandani.

Mheshimiwa Spika, uchafu uliokithiri katika miji yetu, ikiongozwa na jiji la Dar es Salaam inatia aibu, usafi haufanyiki ipasavyo. Nashauri kuwe na utaratibu wa mashindano ya usafi kuanzia ngazi za vitongoji na mitaa na vile vile mashindano hayo yawe kati ya Mkoa na ikiwezekana Mkoa, itakayoshinda itangazwe na ile miji inayoongoza kwa uchafu itangazwe ili iwe rahisi kwa Halmashauri husika na wakazi wa Mikoa hiyo kuchukua hatua. Pia hatua zichukuliwe kwa wananchi wanaochafua mazingira, mbona nchi jirani ya Rwanda wameweza, kwa nini tushindwe?

Mheshimiwa Spika, vilevile mafunzo ya umuhimu wa usafi itolewe kwani moja ya faida ya usafi ni kuepuka magonjwa ya milipuko, yakiwemo kipindupindu na magonjwa mengi ya tumbo. Vile vile mazalio ya mbu yatapungua hivyo malaria nayo itapungua. Mabwana Afya katika Halmashauri zetu wafanye kazi na kama hawatoshi waongezwe.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya vyoo yasisitizwe kwani baadhi ya wananchi wanaoishi maeneo yenye mito na maziwa, hujisaidia kwenye maeneo hayo badala ya kuchimba vyoo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifuko ya plastiki, bado juhudzi za kuzuia matumizi ya mifuko hiyo hazitoshi. Kampeni ya kuzuia matumizi hayo, ikiwezekana viwanda vya mifuko ya plastiki vifungwe au vibadilishe teknolojia ya utengenezaji mifuko hiyo au uwepo utaratibu mzuri wa *ku-recycle* baada ya matumizi ya mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Utunzaji wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika, napongeza hatua zilipofikia ingawa imechukua muda mrefu kuanza. Nashauri elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi wanaoishi maeneo ya Ziwa hili ili wafaidike na mradi huo na ili waweze kutoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa mradi huo.

Vile vile nashauri, pesa nyingi zisiishie kwenye matumizi ya kuendesha ofisi, semina na makongamano badala yake ziende kwenye mradi husika ili wananchi wafaidike, lengo la mradi lipatikane na lionekanae kutokana na faida watakayoipata wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mkaa na kuni, bado matumizi hayo yanaendelea kwani wananchi hawana njia mbadala za kutumia katika shughuli mbalimbali za nyumbani. Bajeti ya mwaka jana ilisisitiza matumizi ya moto poa lakini pamoja na kwamba kodi ilifutwa kwenye mafuta na majiko yake lakini ufanisi wake ni mdogo sana kwani yanapatikana maeneo ya mjini tu.

Vile vile, matumizi ya majiko haya hayaendani na hali halisi ya ukubwa wa familia zetu, mfano mapishi kwa mfano maharage inachukua mafuta mengi sana hivyo

wananchi wengi hawawezi gharama yake. Nashauri juhudi ziongezwe ili nishati mbadala ipatikane ili kunusuru nchi yetu isiwe jangwa. Isisitizwe matumizi ya majiko yanayotumia kuni na mkaa kidogo wakati juhudi zingine zikifanyika katika kukomesha matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kutokana na kukosekana kwa juhudi za kukomesha matumizi ya magogo, kiwanda cha chumvi Uvinza bado kinatumia kuni au magogo katika shughuli zake za kila siku. Mazingra yanaharibika sana na eneo la Uvinza linaendelea kuwa jangwa. Mwekezaji yule alipochukua kile kiwanda aliahidi kubadili teknolojia ya matumizi ya kuni au magogo lakini mpaka sasa kiwanda kinazalisha chumvi kwa nishati inayotokana na magogo.

Naomba hatua zichukuliwe ili Uvinza – Kigoma isiendolee kuwa jangwa kwani miti ikiisha Uvinza, atahamia maeneo mengine ya Mkoani Kigoma matokeo yake Mkoa wote utageuka jangwa na ile mvua ya uhakika itapotea na lile wazo la Kilimo Kwanza, Kigoma, litapotea kwani si maeneo mengi yanayotumia kilimo cha umwagiliaji. Kwa taarifa tu, Kigoma imo katika Mikoa sita ya kilimo Tanzania, tuinusuru isiharibiwe!

Mheshimiwa Spika, tuitunze Tanzania ili itutunze, mazingira yakiharibiwa, waathirika ni Watanzania wenyewe.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Batilda Salha Burian (MB), Waziri wa Nchi Mazingira, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib (Mb), Waziri wa Nchi, Muungano pamoja na watendaji wote wa ofisi hii kwa maandalizi mazuri ya bajeti ya mwaka wa fedha 2009/10.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 32 katika kitabu cha hotuba ya bajeti, aya ya 49, inahusu Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari Ukanda wa Pwani; Maziwa, Mito na Mabwawa, warsha mbili tu ndizo zilizofanyika na mkakati umetafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza.

Maoni ni kwamba warsha mbili tu kwa mwaka ni dogo sana ukilinganisha na hali mbaya ya uharibifu unaoendelea katika maeneo tajwa. Nashauri mkakati tajwa utafsiriwe kwa lugha inayolewaka kwa wananchi walio wengi ili utekelezaji wake uwe rahisi na mwelesi.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuondoa magugu katika mto Mara, unaomwaga maji yake Ziwa Victoria uelezwe kwani mto huo uko katika hatari ya kutoweka kutokana na magugu maji.

Mheshimiwa Spika, bunge lako Tukufu lielezwe mafanikio yanayopatikana baada ya Serikali kutoa ushuru kwa majiko ya motopoa ili kuepuka ukataji wa mti kwa ajili ya kupikia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na ukataji miti unaendelea maeneo mengi nchini kutokana na ukosefu wa nishati mbadala. Pamoja na Serikali kuweka Siku Maalum ya Upandaji Miti, bado hakuna taarifa sahihi ya utunzaji wa miti hiyo inayopandwa kila mwaka nchini kote. Serikali iwe na utaratibu wa kutoa taarifa ya utunzaji wa miti hiyo kila mwaka ili wananchi wawe na mwamko zaidi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi katika maeneo yenye uchimbaji wa madini, wamekuwa wakilalamika kuhusu uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na wawekezaji.

Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba tamko la Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mazingira kuhusu athari walizopata wananchi wanaoishi karibu na mradi wa North Mara na zitakazochukuliwa kwa mwekezaji iwapo itagundulika kuwa maji yalikuwa na sumu iliyosababisha athari kubwa kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu kuundwa kwa Tume kuchunguza uharibifu wa mazingira katika mradi wa mwekezaji huyo, North Mara Gold mine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye kueleweka.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri aende Wilaya ya Kilombero na Ulanga, ili akaone mwenyewe hali ya uharibifu wa mazingira katika Bonde la Mto Kilombero ambalo Serikali ilikubali kuwa *Ramsar Site* kutokana na ardhi yake oevu na chepechepe.

Mheshimiwa Spika, naomba tusichanganye mambo ya kilimo na uharibifu wa mazingira kwa sababu Mheshimiwa Rais amesema Mkoa wa Morogoro uwe Ghala la Chakula la Taifa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mheshimiwa Muhammed S. Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Makatibu Wakuu wa Wizara zote chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuimarisha Muungano pamoja na mambo yote yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, niitumie fursa hii pia kumpongeza kipekee Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa jinsi alivyowasilisha hotuba ya bajeti kwa ufasaha wa juu suala ambalo limetufanya kuielewa bajeti vema.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhili, kama sitatambua jitihada za Mheshimiwa Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo amekuwa msaada kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhimiza maendeleo ya nchi yetu na masuala ya Muungano na mazingira. Ninamponeza sana na Mungu aendelee kumpa nguvu, afya na maisha marefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuzuia matumizi ya mkaa kwa matumizi ya nyumbani. Ninapenda kutamka wazi kuwa, nami nipo pamoja na Serikali katika kuwatahadharisha Watanzania kuacha kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, hii inatokana na athari ya kumaliza miti na kusabaisha ukame, jangwa na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, azma hii ya Serikali bado ina utata kwani bado nishati mbadala na ya kudumu, tena yenye gharama nafuu, haijapatikana. Zoezi hili litafaulu tu endapo Serikali itatoa nishati mbadala pamoja na kupeleka umeme vijiji kwa njia mbalimbali ukiwemo umeme wa upepo ambaao unawezekana Singida. Hivyo basi, Wizara ya Nishati na Madini inayo mchango mkubwa katika kuwapelekea wananchi nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Siku ya Upandaji Miti, ninaipongeza Serikali kwani imekuwa na siku maalum ya kuhimiza upandaji miti kwa nchi nzima. Kupitia siku hiyo moja, Watanzania wamekuwa wakipanda miti mingi sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kudumu wa kuhimiza wananchi kukata miti na kupanda miti kila siku ili pasipatikane upungufu wa miti ambapo athari yake ni kubwa sana. Ninaimani Serikali itatoa maelezo wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kero ya mifuko ya rambo, natambua juhudhi za Serikali dhidi ya kupambana na uchafu kupitia mifuko ya rambo kwa kutumia tahaadhari mbalimbali.

Napenda kuishauri Serikali kuwa kwa watumiaji wa mifuko hii ya rambo ni wengi na kila moja ana uelewa tofauti, izuie kabisa kutumia mifuko hii na badala yake tutumie vikapu vinavyosukwa na akina mama wa Mikoa mbalimbali jambo ambalo litawapa vipato wanawake na Watanzania kwa ujumla. Nitasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa miti ya Mikaratusi. Kwa kuwa Serikali imetambua na kujiridhisha kuwa miti hii inanyonya maji ardhini kwa kiwango cha juu, pamoja na wito wa Serikali wa kukata miti hii, mpaka sasa zoezi hili linakwenda polepole sana na inazidi kukausha vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kauli ya Serikali katika zoezi hili ili miti hii kwa vile yote ni mikubwa, ivunwe na kutengeneza mbao ili ipandwe miti isiyio na madhara kwa ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuhifadhi maeneo yenyeye uoto wa asili kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji. Ninaamini Serikali inatambua na inaona maeneo yenyeye uoto wa asili ambavyo yanavamiwa na kulazimisha kujenga nyumba za makazi suala ambalo linaharibu kabisa matumizi ya maeneo hayo. Ninaomba kujua mkakati wa Serikali katika kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo maalum ya kumwaga taka. Pamoja na Serikali kutoa maelekezo kwenye Halmashauri za Wilaya zote kuwa na maeneo maalum ya kutupa takataka, bado kuna uzembe wa baadhi ya maeneo kutupa takataka ovyo ovyo na kuharibu mazingira na kusababisha maambukizo ya magonjwa hasa watoto ambao bado hawana uelewa wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nategemea mchango wangu utatolewa majibu na waheshimiwa Mawaziri wakati wa majumuisho na nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ninawatakitia utekelezaji mwema, pia Serikali ijaribu kuwaongezea bajeti kipindi kijacho ili waweze kutekeleza majukumu yao barabara.

MHE. MKIWA A. KIMWAGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ndiyo ulizaa Tanzania, kama hivyo ndivyo basi lazima kulikuwa na makubaliano. Sasa basi, kama makubaliano hayo yalikuwepo, nini kero ya Muungano na inatoka wapi? Bila shaka makubaliano yamekiukwa na ni kwa nini yakiukwe bila kushirikisha wananchi? Maoni yangu, ni bora kuwa na Serikali tatu kwa sababu kila nchi kabla ya Muungano ilikuwa na Serikali yake, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ndipo tupate Serikali ya Muungano wa Tanzania. Nadhani kwa kufanya hivyo, kero za Muungano zitapungua.

Mheshimiwa Spika, pia kuongezwa vifungu, kwani makubaliano ya Muungano yalikuwa ni mambo kumi na moja (11) lakini sasa yamefikia 22 au zaidi hapo, hiyo ndilo kosa kubwa na ndio chanzo cha chokochoko hii ya Muungano. Hivi hata hili hawalionti na kuliweka vizuri?

Mheshimiwa Spika, napenda kusema pindapinda hii mwisho wake kuongeza kero za Muungano. Hivi Serikali ya Tanganyika iko wapi mbona wenzetu wa Zanzibar wanayo Serikali yao? Je, kama Serikali ya Mapinduzi wanatumia Mfuko wa Serikali yao ya Zanzibar, je, Serikali ya Tanganyika wanatumia Mfuko gani? Kama tunatumia Mfuko wa Muungano, hamuoni hii si haki kwani Mfuko wa Muungano ni wa Serikali mbili (2)? Kwa nini hasa hatutaki kukuza ufahari wetu Tanganyika? Kwa kigezo hicho ndiyo sababu nami naona Serikali tatu, ni muhimu, kinyume cha hapo, kero hazitaisha, zitaongezeka siku hadi siku. Kwa kuwa Serikali hii ni tulivu na sikivu, tunaiomba iwe na macho na masikio na isikie na kuona, Tanzania ni yetu sote na tunapaswa kutoa mawazo na maoni ili kupunguza kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mawazo yangu kuhusu mazingira. Tanzania ni nchi yenyeye rutuba na mazingira ya kupendeza sana na yenyeye madini ya kutosha lakini kuna uharibifu wa mazingira wa kawaida ambao unaendelea. Naomba ofisi ya Mazingira, Kanda ya Ziwa, kufuatilia baadhi ya viwanda ambavyo humwaga maji yenyeye

dawa zenye *Cemico* ambayo ni hatari kwa walimao mboga kando mwa viwanda hivyo. Kama Kiwanda cha Soda kilichopo Igoma, Mjini Mwanza, humwaga maji hayo nje ya kiwanda, kwenye mashamba ya wananchi, hebu fuatilieni.

Mheshimiwa Spika, watu wengine ambao ni waharibifu wakubwa wa mazingira, ni wachimbaji wa madini. Wachimbaji wakubwa hutumia madawa makali na baadaye hufanya kama bwawa nje ya kempu yao na maji haya huwa yana sumu, pia huchimba mashimo marefu na hata kuuondoa mchanga ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ya Mazingira, kulegeza sheria kidogo kwa wachoma mkaa, kwani zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hutumia mkaa kwa sababu nishati mbadala kama umeme na gesi, kwanza ni ghali na pili maeneo mengi hasa vijijini haupo. Ninyi wenyewe ni mashahidi, jinsi Wabunge wanavyodai umeme Majimboni kwao. Watendaji wenu huko chini wamekuwa kero hata kama utakutwa na gunia moja tu la mkaa au kuni, utasumbuliwa sana. Pamoja na kuhifadhi mazingira ambapo ni kitu cha muhimu lakini na maisha ya watu wetu nayo ni muhimu.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa mambo machache yanayonisibu sana. Kwanza uchafuzi wa mazingira hasa Mji wa Dar es Salaam umekua sugu kwa uchafu. Mitaro ya kupeleka maji machafu yanayopita kwenye makazi ya wananchi, yanayotoka kwenye viwanda, wananchi wa Mabibo pamoja na Mbagala wanapata shida sana. Ukiangalia pale Mbagala na Mabibo, kuna wafanyabiashara, je, Wizara hii ina mkakati gani wa kushughulikia suala hili ikiwa ni pamoja na utupaji taka hovyo, mfano plastiki na pampasi? Je, Wizara ina mpango gani wa kupata magari ya kusomba taka, yakapangiwa sehemu muhimu panapojulika kuliko kutupa taka hovyo na kusababisha mlipoko ya magonjwa? Hata hivyo, kwa taratibu hizi bila kutengeneza mikakati ya dhati suala hili la uchafu halitaisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza ni kwa nini lile bomba la maji machafu liko Ikulu, kule baharini na ni kwa nini lisihamishwe pale? Ni aibu kubwa sana maana tuna wageni wa kila aina wanaokwenda Ikulu pamoja na wavuvi wanaofikishia samaki zao pale feri.

Mheshimiwa Spika, uchafu Ziwa Victoria, imekuwa kero watu wanamwaga uchafu Ziwanu na lina magugu maji. Tuna visiwa vingi lakini kwa uchafuzi uliopo, kuna mlipuko wa magonjwa. Serikali ina mikakati gani?

Mheshimiwa Spika, uchomaji moto msitu wetu wa Buligi, Biharamulo mpaka wanyama wote walikimbia. Je, uchomaji mkaa pamoja na kukata kuni hovyo, wananchi wetu tunawasaidiaje kuacha uharibifu wanaoufanya? Ni elimu gani wanapatiwa ili waache uchomaji moto huu?

Mheshimiwa Spika, uchafuzi kwenye vyombo vya kusafiria hasa treni, inachafua mazingira kwa kutupatupa kinyesi hovyo. Naomba Wizara ifuatilie suala hilo. Mfano wa mji au mkoa wa kuigwa kwa kuwa na usafi wa hali ya juu, sijawahi kuona sehemu nyingine safi kama Kilimanjaro, Moshi, kule kupata mlipuko, itakuwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tena sana Rais wetu amalize suala la Zanzibar isiwe wimbo hapa ikaja kusababisha nchi yetu kuwa na vurugu kama majirani zetu, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi, sisi tunaomba tusifike huko. Rais wetu ni muungwana wa mambo mengi, hili tunaona ni jambo dogo. Naomba mambo haya ya ishe kabla ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni msikivu mzuri tu, amshauri Rais amalize mambo haya maana ni kero na itaonekana ni siasa lakini inawatesa wananchi wengi wazawa walioko kule na inawakera lakini hawana pa kusemea, naomba mfanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mungu ibariki Tanzania na nawatakia bajeti njema.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waasisi wa Muungano wetu, Mwalimu Nyerere na Mheshimiwa Abeid Amani Karume, kwa uamuzi wao wa kuunganisha nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar. Muungano wetu ni mzuri na ni wa kidugu na hatuna budi kuuenzi na kuimarisha zaidi Muungano huu. Katika kuuenzi na kuimarisha Muungano huu, ni pamoja na kutatua yale yanayoonekana ni kero, yangezungumzwa na kutolewa uamuzi kwa haraka maana kukaa kimya ndiyo inaonekana kuna mpasuko fulani na kulegalega kwa Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, vikao vinavyoendelea kwa ajili ya kujadili mambo haya, vinavyoongozwa na Makamu wa Rais na Waziri Kiongozi, viko kimya, wananchi hawaelewi nini kinazungumzw na mambo gani yamepatiwa ufumbuzi. Suala hili ndilo linalosababisha kuonekana kana kwamba hakuna chochote kinachofanyika. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri aeleze mambo yaliyopatiwa ufumbuzi, hayo manung'uniko yataisaha.

Mheshimiwa Spika, Mungu ubariki Muungano wetu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. USSI AME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na wataalam wake wote kwa kuleta bajeti ambayo ni nzuri na yenye kutia moyo kwa pande zote mbili za Muungano lakini pia ni bajeti ambayo ina lengo la kudumisha Muungano wetu ambao sasa una miaka 45 na ni mfano katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kuunda na kutangaza Tume mpya ya Pamoja ya Fedha, naiomba sana Serikali iweze kulitolea maamuzi suala hili ili kumaliza tatizo ambalo limechukua muda mrefu na kuwa kama ni kero za Muungano. Hata hivyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii atapofanya majumuisho anieleze kupitia Bunge, ni tatizo gani ambalo linakwamisha kutolewa maamuzi katika Tume hii ya Pamoja ya Fedha?

Mheshimiwa Spika, baada ya Zanzibar kushindwa kujiunga na *OIC* kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar ilikubali na kuamua kwamba Tanzania kama Jamhuri ijiunge na taasisi hiyo ya Kiislam kwa maslahi yetu wote. Naomba Waziri wakati wa kufanya majumuisho anipe maelezo ni kwa nini mpaka leo hii Tanzania kama nchi, haijajiunga na taasisi hii?

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. OMAR SHEHA MUSSA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, anayehusika na Muungano kwa hotuba yake iliyogusa mambo mbalimbali yanayohusu Muungano pamoja na mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia juu ya jambo moja ambalo ni jukumu la Wizara ya Nchi, Muungano. Jambo hilo ni lile la kero kubwa kabisa ya siku nyingi ya mambo ya Muungano na ambalo halijapatiwa ufumbuzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili ni lile linalohusu mgawanyo wa mapato na matumizi ya Muungano kwa pande mbili zinazohusika, Tanzania Bara na Zanzibar, kama Sura ya Saba ya Katiba ya Jamhuri inavyoeleza kuhusu mambo ya fedha hasa kazi za Tume ya Pamoja ya Fedha (*JFC*).

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nchi, Muungano, ina dhamana na jambo hili na hivi sasa inaongozwa na Waziri aliyeuwepo Serikalini kwa muda usiopungua miaka thelathini na tano au zaidi. Kwa uzoefu wake huo, hakuna sababu kwa nini kipindi hiki sasa (2009/2010) suala hili lisipatiwe ufumbuzi wa kudumu na kudumisha Muungano wetu amba hivi sasa umedumu kwa zaidi ya miaka 45. Ni kweli kabisa kuwa nimeona kwenye hotuba ya Serikali iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Uchumi, kuwa Serikali hizi mbili ziko katika hatua ya kutoa mapendekezo yao juu ya jambo hili, baada ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuwasilisha ushauri wao juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa Sheria ya kuanzishwa Tume ya Pamoja ya Fedha, ilianzishwa tokea mwaka 1996 na ilichukua miaka saba (hadi 2003) ndio Tume hiyo ikaundwa na kuteuliwa kwa muda wa miaka mitano ya awali (2003 – 2008). Miaka mitano ya awali, ilikwisha Machi, 2008 na Tume ya Pamoja ya Fedha ya pili, iliteuliwa tena baada ya miezi tisa kupita (Disemba, 2008).

Ucheleweshaji huu na wenyewe unachelewesha ufumbuzi wa kero hii ya Muungano, kero ambayo ni kubwa na inadhoofisha Muungano wetu. Kama miaka saba na mitano mingine imepita (12 years) jumla, bado ufumbuzi wa jambo hilo haujapatikana, ukiachilia mbali miaka ya nyuma iliyopita, je, ni lini jambo hili litapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kuwa jambo hili limalizike ndani ya mwaka huu wa fedha 2009/2010. Vinginevyo mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Chumbuni, tutashindwa kuvumilia na kuikosoa Serikali ya Jamhuri ya Muungano hadharani (Bungeni) na nitaomba Waziri aachie ngazi (ajiuzulu) kwani atakuwa

ameshindwa kazi zake, hasa kwa kuzingatia kuwa yeye ni Waziri wa zamani, anayejua suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo, namuomba Mheshimiwa Makamu wa Rais (ingawa yeye si Mbunge mwenzetu, akazane sana kuhusu kero hii ya Muungano na alisimamie mwenyewe jambo hili ili limalizike ndani ya muda wake akiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na makadirio ya Wizara husika, sina pingamizi, nayakubali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu huo wa maandishi na nasema ahsante.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR, Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza hotuba ya Waziri, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian na Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib, napenda kupongeza pia uongozi mzima wa ofisi hii pamoja na wafanyakazi wake wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Shein, kwa kazi nzuri na ushirikiano mzuri kwa ajili ya kuimarisha Muungano wa Tanzania. Napenda pia kuipongeza ofisi ya Zanzibar kwa kazi nzuri inayofanya na kwa ushirikiano inaotupa

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni kitu muhimu sana kwa maslahi ya wananchi wote. Naiomba Serikali iendelee kutoa elimu inayohusu Muungano wetu maana wananchi wengi hawauelewi vilivyo na ndio maana baadhi ya wananchi hawaupi *support* Muungano hasa Vyama vya Upinzani wa Zanziba. Bila Muungano, nchi yetu hasa Zanzibar hatuwezi kuimarika kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiulinzi.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana uanzishwaji wa Mfuko wa *TASAF* hapa Tanzania. *TASAF* imechangia sana maendeleo ya wananchi hasa katika kisiwa cha Pemba. Miradi kama ya barabara, afya, elimu, kilimo na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuanzisha miradi mbalimbali inayosaidia waathirika wa UKIMWI, mazingira na kadhalika. Nashauri *TASAF* iendelee na kuzipatia ofisi za *TASAF* zana za kufanyia kazi kama gari, pikipiki na vifaa vya ofisini hasa katika ofisi za Pemba.

Mheshimiwa Spika, nashauri pamoja na wananchi wa Zanzibar kuajiriwa katika ofisi ya Muungano lakini bado haikidhi haja. Nashauri Serikali iwapatie ajira wananchi wa Zanzibar katika ofisi za Muungano zilizoko Tanzania Bara; maana wananchi wa Zanzibar na wao wanao uwezo mzuri wa kielimu na utendaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kila mwaka huwa tunaelezwa kwamba vikao vinakaa ili kutatua suala la kero za Muungano, ukweli tatizo hili linachangiwa na watendaji na hasa *TRA*. Wafanya biashara wakubwa hupendelea kuteremsha mizigo yao Zanzibar kutoana na kuweza kutoa mizigo yao kwa haraka na wakati. *TRA* wanajuwa na makusanyo ya fedha hizo yanaingia Mfuko wa Hazina ya Serikali ya Zanzibar. *TRA* wakaanza vikwazo na kwa kuwatoza wafanyabiashara malipo ya mara mbili. *TRA* wakasababisha wafanyabiashara wasiteremshe tena bidhaa zao bandari ya Zanzibar. Tuelewa wazi uchumi wa Zanzibar, sehemu ya kupata mapato ni bandari.

Mheshimiwa Spika, kero hizi kila kukicha zinazidi kuimarika kwa upande mmoja wa Muungano kuelemea upande mwingine. Hivi sasa Wenzetu wa upande mmoja wa Muungano yaani Bara wameanzisha kero kubwa ya suala la magari. Tumepata kuongea na viongozi wa *TRA* kuhusu tatizo la kutoza toza mara mbili magari kwamba ni uonevu na walikiri kwenye Kamati ya Bunge ya *PAC* na wakasema watarekebisha lakini hadi leo wanawanyanyasa wanaoleta magari kutoka Zanzibar. Mimi nina mashaka kuwa wanafanya makusudi na ushahidi ninao. Nahisi Bara wanataka waipangie Zanzibar makadirio yao ya fedha lakini ieleteke kwamba Zanzibar ina Serikali kamili. Cha ajabu Mzanzibar akija na *TV* moja, hutakiwa alipie, haya yote ni kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, suala la Wapinzani kuhusu vitambulisho, hili si la kujadiliwa humu ndani, iachiwe Serikali ya Mapinduzi. Wapinzani hawana hoja kwa hili.

Mheshimiwa Spika, kusimamishwa wafanyakazi wa *TRA* Zanzibar, lengo la *TRA* Makao Makuu, wafanyakazi wale wa Zanzibar, ni kuwaondosha kwa sababu bei za magari Zanzibar, ni kubwa kuliko Bara. Lengo la *TRA*, Zanzibar magari yasiteremshwe na haya yanafanya makusudi. Mfanyakazi wa *TRA*, Zanzibar akitoa bei pungufu kidogo tu anasimamishwa kazi. Hii ni kati kero za Muungano na kila siku vikao lakini wananchi wa Zanzibar wanaendelea kupata matatizo yasiyopata jawabu.

Mheshimiwa Spika, mgao wa 4.5%, watendaji wa Zanzibar wameshatoa maelezo juu ya mgao huo lakini sehemu moja ya Muungano hawatoi, kwa nini wanapata kigugumizi? Zanzibar ni nchi sio Mkoa nadhani baadhi ya watendaji wanahisi Zanzibar kama Mkoa, hiyo ni dhana potofu. Naomba tukae ili kuondosha kero hizo ili vizazi vyetu tuvirisishe mambo mazuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QAMSSY: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha nikawa mzima na nikaanza kuchangia hoja hizi zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika na wenyeviti wote kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa *speed and standard*.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sikuwatendea haki, Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Batilda, wa Mazingira na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, wa Muungano pamoja na watendaji wao wote kwa jinsi walivyoandaa hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, naanza na hotuba ya Muungano, naiomba Serikali iuangalie sana Muungano kwani kama mlivyogundua kama una kero basi una kero kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama ungekuwa wewe si muadilifu basi Wabunge wa Zanzibar wasingekuwa na cha kuzungumza kwani unapozungumza unaambiwa jambo hilo si la Muungano. Sasa Mbunge yuko ndani ya Bunge asizungumze jambo lolote la Zanzibar? Katika Bunge hili, unaweza ukataka kusema jambo, wenzetu wanasesma, Zanzibar Majimbo yao ni madogo tofauti na yetu, sasa je, hatuoni kama hatuwartendei haki wenzetu wa Zanzibar? Kungekuwa na Serikali tatu, kungekuwa hakuna malalamiko, ingekuwa Serikali ya Tanganyika, Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano.

Kwa hiyo, hapa tungekutana katika mambo ya Muungano tu. Naiomba Serikali iache mambo ya kutosikiliza maoni ya wananchi yao kwani nchi nyingi zimeingia katika machafuko kwa sababu kama hizi za wananchi kutokusikilizwa katika mambo yenye maslahi ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuchangia kuhusu mazingira, ni masikitiko makubwa kuona kuwa Serikali imechelewa kuchukua hatua kwenye Mgodi wa North Mara mpaka wananchi wameathirika na hali yao ni mbaya sana. Naiomba Serikali iwachukulie hatua kali wahusika wa sakata hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kumka hali nikiwa mzima. Pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, kwa imani yako kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hotuba iliyo mbele yetu, ni wazi tunafahamu umuhimu wa muungano pamoja na kasoro ndogo ndogo zilizozomo na pia mazingira, kuna ongezeko la upandaji miti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano. Kuna kila sababu Watanzania kudumisha Muungano wetu ila tuwe tayari kutatua yake yanayoleta kero katika Muungano huo. Kwa kuzingatia miradi minne ya kitaifa, uwanja wa ndege huko Pemba uko kwenye ukarabati na kwa lugha iliyotumika, uko katika hatua za matayarisho. Napata wasiwasi kama ukarabati hautakwenda haraka maana eneo hili ni muhimu kwa usalama wa maisha ya watu.

Uwanja wa ndege wa Pemba hali yake ni mbaya sana, uwanja huu hauna sifa ya kutua ndege, kinachofanyika ni kuchezza shilingi chooni yaani uhakika wa uokozi haupo. Licha ya sifa ya uwanja kukosekana, uwanja huo una gari moja la kuzimia moto. Ndege zinazotua Pemba ni ndogo sana, hii inatokana na kukosa sifa za kuziwezesha ndege

kubwa kutua. Kuhusu ofisi, wale wanaokuja kuwasindikiza wenzao hukosa eneo mahsusini la kukaa. Naiomba Serikali itoe kipaumbele juu ya ukarabati wa uwanja huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero za Muungano, kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kipindi cha miaka miwili (2) nyuma, ilitoa orodha ya mambo yanayopaswa kuondolewa katika Muungano ikiwa ni pamoja na posta, elimu ya juu, mafuta na gesi asilia, biashara ya nje, simu na kadhalika. Je, kero hizi zimefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, ukipima katika Serikali zetu mbili, yaani SMZ na Serikali ya Muungano, mara nyingi SMZ na watu wake ndio wanazitoa kero hizi za Muungano, kwa nini? Naiomba Serikali ituelezee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuvunjika kwa muafaka kati ya *CUF* na CCM, msimamizi mkuu ni Muungano. Baada ya kuvunjika kwa muafaka, Muungano kama baba umeshindwa kuwatuliza watoto wake yaani *CUF* na CCM na kuendeleza malumbano ya kisiasa jambo ambalo linaweza kupelekea kuvunjika kwa amani. Au tumesahau yalotokea Unguja na Pemba watu kufa kwa mtutu wa bunduki?

Mheshimiwa Spika, eneo la mazingira, napenda kuzungumzia juu ya upandaji miti, naipongeza Serikali kwa hatua zake kwa kupanda miti ngazi hadi ngazi katika nchi yetu pia kuikata miti siku hadi siku. Kutokana na hali ya umaskini katika nchi yetu, Serikali imeshindwa kuzuia ukataji miti kwa ajili ya mkaa. Napata wasiwasi mkubwa kwamba miti inayopandwa ni kidogo ukilinganisha na miti inayokatwa. Ni vizuri katika hili, Serikali iweke bei nafuu kama mafuta ya taa, majiko ya kisasa ili tunusuru nchi yetu kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mazingira, maeneo muhimu yametandwa na moshi mkali ambao huhatarisha maisha ya watu, kuna magereji na viwanda mijini. Kwa kuzingatia moshi ni hatari kwa maisha ya wanaadamu, hivyo basi Serikali ilazimike kutenga maeneo mahsusini kwa kazi hizi za gereji na viwanda.

Mheshimiwa Spika, suala lingine baya ni kuona minara ya simu kuwemo mijini, minara mingi na pia hutoa sauti. Ni vema suala hili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMMeD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kila siku au kila mwaka kuwa nachangia kuhusu kero zinazowapata wafanyabiashara wa Zanzibar, kutozwa Ushuru wa Forodha na VAT mara mbili kwa bidhaa ambazo wanataka kuzileta Tanzania Bara, jambo ambalo ni kero kubwa ya Muungano wetu, bado Serikali ya Muungano haijachukua hatua yoyote kila siku inatoa ahadi tu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni tatizo ambalo linawakera sana Wazanzibar na hata wa Tanzania wote kwa ujumla ambao hupata usumbufu mkubwa wanapopita katika bandari za Tanzania Bara wakitoka Zanzibar. Ili kuondoa tatizo hili, ni lazima hatua za haraka tena za kudumu zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kama hakuna uwezekano wa kulitatua jambo hilo kubwa Tanzania Bara basi ni bora itangazwe rasmi kuwa Zanzibar ni bandari huru (*Freeport*) ili iagize bidhaa za biashara huko Zanzibar bila kulipa VAT na '*Import Duty*' na bidhaa hizo zikiletwe Tanzania Bara ndio zitozwe ushuru unaostahili kwa mujibu wa sheria za kodi za *TRA*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, Muungano wetu bado una matatizo mengi ingawa kumekuwa na juhudzi za kutatua matatizo mengi ambayo yapo kwa mfano tatizo la kuchangia gharama na kugawana mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, gesi asilia tayari inaendelea kuchimbwa sehemu mbalimbali na matumizi yake yanaeleweka lakini hatujaelezwa ni kiasi gani cha mapato kilichopatikana na kwa upande wa Zanzibar ni asilimia ngapi imekwenda huko? Ndio sababu pamoja na Mshauri Mwelekezi kutoa semina kwa Baraza la Wawakilishi lakini Baraza hilo likikataa ushauri huo. Je, taarifa itakayotolewa ni vipi itasaidia kutatua tatizo la gesi asilia na mafuta?

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi ilioingizwa ya Serikali ya Mapinduzi na ambayo inafanyiwa kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuombewa ufadhili ikishindikana itakuwaje na Zanzibar ni sehemu ya Muungano Kikatiba?

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi wanaofanya kazi katika taasisi za Muungano wametoka upande mmoja. Je, ni lini sasa kutakuwa na usawa wa watumishi hao ili kuondoa kero hizo?

Mheshimiwa Spika, tatizo la gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalotokana na mchango wa wahisani kwa misaada isiyokuwa na masharti kwa Tanzania, hili bado halijapatiwa ufumbuzi na wala hakuna nia sahihi, kwa nini tatizo hili limechukua muda mrefu? Je, ni lini sasa litatatuliwa ili kusaidia Zanzibar katika kipindi hichi ambacho kuna tatizo la kuperomoka uchumi wa dunia?

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano ya awali, kulikuwa na vifungu au mambo kumi na moja tu ya Muungano lakini hivi sasa vimeongezeka hadi kufikia 22. Nyongeza hii haisaidii Zanzibar bali inaidhoofisha Zanzibar. Kwa mfano, hapo awali Rais wa

Zanzibar alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar lakini hivi sasa ni Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum, hii ni kuidhoofisha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo si ya Muungano lakini yanasimamiwa na Serikali ya Muungano. Hii inatokana na Mfumo wa Muungano wa Serikali mbili. Mfumo wa Serikali tatu ungeondoa tatizo hili pamoja na matatizo mengine. Serikali ya Muungano pia kuwakilisha Tanzania Bara kunatia wasiwasi mkubwa kwa mustakabali wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vikao baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, haviwezi kufikia hatima ya matatizo ya Muungano kwa sababu havina uhalali kwani vikao hivi ni baina ya *creator* (Zanzibar) na *creature* (Muungano), kilipaswa kiwe baina ya *creator* na *creature* yaani Zanzibar na Tanganyika na sio Zanzibar na Muungano.

Mheshimiwa Spika, Akaunti ya Pamoja ya Fedha, Ibara ya 133 ya Katiba inasema kwamba wachangiaji wa Mfuko wa Pamoja, ni Serikali ya Zanzibar na ya Muungano na sio Serikali ya Zanzibar na ile ya Tanganyika. Hii ni kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, pia Zanzibar ina mfuko wake amba si wa Muungano. Je, Tanzania Bara inatumia mfuko gani kwa yale mambo ambayo si ya Muungano?

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira utaendelea kukua kwa vile Serikali haijawa na njia mbadala ya kuzuia utumiaji wa kuni na mkaa. Pia usambazaji wa umeme bado haujatosheleza mahitaji ya wananchi hasa walioko vijiji na hata huko ambako umeme tayari umekwashafika gharama ni kubwa kiasi kwamba wananchi walio wengi wanashindwa kuutumia kwa kutomudu gharama. Pamoja na kuhamasisha upandaji miti lakini pia Serikali inapaswa kutafuta njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Muungano na Mheshimiwa Dkt. Batilda Salha Burian, Waziri wa Nchi, Mazingira pamoja na watendaji wao wote amba wametoa mchango mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kutoa mchango wangu katika hotuba hii kuhusiano na mazingira. Kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika hotuba yake kwamba Serikali inaendelea kupiga marufuku uingizwaji wa mifuko laini ya *plastic* ambayo haijafikia kiwango kinachotakiwa ama kilichowekwa na Shirika la Viwango (*TBS*).

Mheshimiwa Spika, bado ipo haja ya lazima kwa Serikali kuongeza mikakati ya kuzuia uingizwaji wa mifuko hiyo kwa kuwa bado ipo nchini na inaingizwa kwa wingi kutoka nchi jirani kuititia njia za panya katika mipaka ya nchi zetu. Tuseme kule mipakani mwa nchi zetu mifuko hii inavuka vipi kuingia nchini mwetu? Je, Serikali haikuweka wafanyakazi wetu kule mipakani au tuseme kuna kitu gani kinachosababisha

uingiaji wa mifuko hii? Naiomba Serikali kuwatupia macho hawa watendaji wetu wa mipakani kuona ni kiasi gani na wao wanatekeleza wajibu wao kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia pia kuhusu hali ya baadhi ya miji yetu hasa jiji la Dar es Salaam. Maeneo ya Kariakoo ni machafu sana kiasi ambacho yanatoa harufu mbaya inayotokea katika mitaro ya maji machafu na wakati mwengine maji yenye vinyesi yanayotoka katika baadhi ya makaro ya majumba na kutiririka kwenye barabara kuu hasa ya Msimbazi na kuharibu mazingira.

Bayu zaidi, barabara hiyo hutumiwa na wafanyabiashara kupanga bidhaa mbalimbali kama vile nyanya, vitunguu, mbatata, mihogo na kadhalika ambavyo vitu hivi vinatumwa na wananchi wetu huku maji hayo machafu yakiwa yanapita, jambo hili linachafua mazingira na kuhtarisha maisha ya walaji au watumiaji wa bidhaa hizo. Naiomba Serikali kama ilivyofanya ukaguzi wa kushtukiza katika biashara ya mifuko laini basi ni vyema idhibiti uchafu huo ili kunusuru uchafuzi wa mazingira na kunusuru afya za wananchi wetu pia.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie katika mambo ya Muungano. Mimi binafsi naamini kwamba Muungano ni jambo moja lililo zuri sana katika nchi zetu hizi mbili (Tanzania Bara na Zanzibar) na natoa pongezi zangu kwa Muungano wetu kutimiza miaka 45. Wananchi wengi wanaupenda Muungano na wanapenda udumu lakini tatizo la wananchi walio wengi wanadolilalamikia katika Muungano wetu huu, ni kwa zile zinazoitwa kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika hotuba yake, ukurasa wa 80, nanukuu: “*Hata hivyo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano vinatafutiwa ufumbuzi kwa kufanya vikao vya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.*”

Mheshimiwa Spika, pia katika ukurasa wa 12, Waziri ameeleza kwamba, nanukuu:-

“*Ofisi imeendelea kuratibu gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalotokana na mchango wa wahisani kwa misaada isiyokuwa na masharti kwa Tanzania... .*”

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumzia hapa ni kwamba wananchi wanaendelea kuhoji huku kuhakikiwa vikwazo katika utekelezaji wa Muungano na kuratibiwa gawio la asilimia 4.5 hadi leo hii vimefikia wapi na mambo haya ya kuhakiki na kuratibu yatamalizika lini?

Ili sasa wananchi wapate kusikia hatua kamili zilizofikiwa na kwa nini vikao hivi vya pamoja havitoi taarifa za wazi juu ya hatua wanazofikia badala yake yanaelezwa baadhi ya mambo machache sana kama vile utatuzi wa haki za binadamu, Tume ya Uchaguzi na uvuvi wa bahari kuu, kila inapotolewa maelezo ya hatua ya kero za

Muungano basi maelezo ni mambo hayo hayo. Inawapa wasiwasni wananchi na kuona kama kwamba hakuna kitu kingine kinachojadiliwa zaidi ya hayo yanayoelezwa mara zote. Hivyo, naiomba Serikali izisimamie Kamati hizi za Pamoja katik kutoa taarifa kwa kila hatua wanayofikia badala ya kukaa kimya tu na kuwapa wananchi jambo la kuhoji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

MHE. ZAYNAB MATITU VULU: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mkamu wa Rais Dr. Mohammed Ali Shein kwa juhudzi zake za kusimamia na kuhimiza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote kwa utendaji kazi ulio bora na hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni jambo la msingi kwa maisha ya viumbe wote, mimea, ardhi, maji na hali ya hewa. Kutokana na umuhimu huo, Wizara hii inabidi ijiimarishe na kuweka usimamizi wa kuona kwamba inashirikiana na Wizara nyingi kama, mifugo, kilimo, maji, mawasiliano na uchukuzi ili kusiwe na uharibifu wa mazingira kwa maana kuacha mifugo kuhamahama toka Mkoa kwenda Mkoa, ukataji ovyo wa misitu ambayo huleta mmomonyoko wa ardhi na hata ukame. Ni vema Wizara ishirikiane na kusaidia kuishauri Serikali kabla haijachukua uamuzi wowote wa kutoa kibali kwa ajili ya shughuli zozote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la hali ya hewa duniani inabidi nchi yetu izidi kusimamia na kulinda maeneo yake yote ili kuhakikisha tunalinda maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe inaongeza nguvu zaidi katika Halmashauri zetu ambazo ndio wasimamizi wakuu wa maendeleo ya nchi yetu, kwani huko ndiko kwenye misitu, mbuga, mashamba na misitu. Waongeze mafungu ya fedha na kutoa Elimu zaidi ili kuweza kuwa wasimamizi Wakuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inabidi iwe na eneo maalum la dampo badala ya kuhamahama na lisiwe karibu na makazi ya watu. Dampo hilo liwe la kisasa katika uteketezaji wa taka hizo na kuwe na Sheria ambayo itazuia watu kujenga karibu na dampo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza sana kwa namna ulivyo makini katika kuliongoza Bunge letu kwa kuzingatia ipasavyo *checks and Balances* za mihimili mikuu mitatu ya nchi yetu, yaani Serikali, Bunge na Mahakama na panapostahili vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib - Waziri wa Nchi, (Muungano) na Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian - Waziri wa Nchi (Mazingira) kwa hotuba nzuri waliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, Mheshimiwa Dr. Burian aliahidi wakati wa bajeti ya 2008/2009 kwamba Wizara yake ingewatuma Wataalam kwenda Kilosa kukagua uharibifu wa mazingira unaoendelea kusababishwa na mafuriko ya Mto korofi Mkondoa katika Mji wa Kilosa pamoja na vijiji vya Tindiga, Mahi, Malangali na vingine vya jirani. Namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu wakati anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Wataalam wanapendekeza hatua gani kuhusu *river training* ya mto Mkondoa?

Mheshimiwa Spika, tatizo la mafuriko yanayoletwa ni makubwa mno kuliko maelezo yaliyomo katika mchanga huu. Toka mwezi Machi hadi Mei mwaka huu 2009, Shule ya Msingi Mkondoa ilifungwa na kuwashamisha zaidi ya wanafunzi 500 kwenda kufuata masomo kwenye Shule ya Msingi Mazinyungu yenye zaidi ya wanafunzi 600. Sababu ya kufungwa ilikuwa kuepuka hatari kubwa ya majengo na wanafunzi kusombwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, katika miezi tajwa hapo juu nyumba nyingi za wananchi na mashamba yao, katika Vijiji vya Kata za Mabwerebwere na Kilangali wamelalamika kuyahama makazi yao ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali, ilipe suala hili umuhimu wa pekee ikiwa ni kumwomba Mheshimiwa Waziri akubali mwaliko wa kuja kutembelea maeneo angalau mawili ya Wilaya ya Kilosa, yaani Kata za Mabwerebwere, Kilangali na Kidodi ili ajionee mwenyewe hali halisi ya mazingira husika.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni la ufanuzi kuhusu sera ya ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha na kuyahama makazi na mashamba yao milimani ili kuitikia wito wa kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vya Tundu, Ruaha na Kifinga, wasiopungua 300 waliokuwa na makazi (baadhi ya kudumu na baadhi ya muda ingawa wanayamiliki – kimila), walielimishwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa pamoja na Shirika la WWF. Katika mlolongo wa maandalizi ya kuhamishwa, mtathmini wa ardhi na mali kutoka Halmashauri ya Kilosa, alitumwa kutathmini mali za wananchi hao. Pia, kwa msaada wa WWF mwaka 2008 walipewa maeneo mbadala ya kulima, lakini mpango huo haukufanikiwa. Hivyo hawakulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini walitegemea fidia, kwa kuwa ndivyo Afisa wa Serikali alivyowaarifu. Wananchi hao walishafika hadi Ofisi ya Wizara ya Ardhi kwa ajili ya ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kujua Mheshimiwa Waziri afafanue kwa kuwa wananchi hawa wameyahama maeneo yao kuyanusuru mazingira, kuna namna yoyote na fungu lolote la Serikali na mfuko wowote wa wafadhili unaoweza kuwapa kifuta jasho wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) - Mheshimiwa Batilda S. Burian kwa hotuba yake nzuri pamoja na wasaidizi wake. Naishukuru Serikali na wananchi kwa namna wanavyolismamia suala la upandaji wa miti katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Naishauri Serikali kuwa kila Wilaya, Mkoa au Kata ziwe na siku zake za kupanda miti kiwilaya, kimko pengine hata kikata katika maeneo yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, nzungumzie kuhusu viwanda, magereji yaliyojengwa katika makazi ya wananchi. Viwanda vidogo vidogo vimejengwa katikati ya miji, katika Halmashauri zetu kiasi kwamba kelele huwa ni nyingi sana na moshi mwingi unaotokana na viwanda vidogo katikati ya mji. Naishauri Serikali iwe na mpango madhubuti wa kutenga maeneo ya viwanda, gereji. Vile vile kuna wanaoshughulika na biashara za mama lishe wawe na sehemu rasmi za kufanya biashara zao kwa faida ya walaji kulinda Afya za wananchi, hali za wananchi hasa wanaishi kijijini ambao wengine wao ni maskini wanashindwa kumudu kununua mafuta ya faa, wanakimbilia kutumia kuni na mkaa, kwa kiasi kikubwa huchangia kuharibu mazingira ya nchi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya mkaa imeshamiri sana, naishukuru Serikali kuangalia bei ya mafuta ya taa kwa kupunguza kodi ya mwananchi wa kawaida aweze kumudu kununua na pawe na mpango mkakati wa kutengeneza majiko ya kutumia mkaa na kuni kidogo kulinda mazingira. Watumishi wa Halmashauri kwenye Idara za misitu zisimamiwe na kulinda misitu, watendaji wa Halmashauri ndio wapewe sehemu kubwa kwa wananchi ambapo misitu ni mingi. Jukumu la Halmashauri ya Wilaya ni kuwa na maana ya kuheshimu Madiwani na watumishi wote kwa kushirikiana na wananchi kilinda misitu yetu. Wavune tu wakati unapokuwa umefika na pawepo na utaratibu wa kupanda miti mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la mazingira lipo kwenye migodi ambayo yana wawekezaji. Mazingira yameharibiwa hasa kemikali zinazoingia kutoka mgodini na kuelekea kwenye mito. Mfano katika mgodi wa *North Mara* ambao upo Nyamongo, wananchi wengi wameathirika na kemikali kutoka mgodini inayoingia Mto Tigite baada Mto Mara na kuelekea Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu wananchi wamelalamikia mgodi kuwa maji machafu yenyе kemikali yanaingia Mto Tigite, pamoja na Baraza la Madiwani, lakini Serikali iliwapuuza, viongozi wa madhehebu mbalimbali, Mashirika mbalimbali yamelipigia kelele sana, wakati wote Serikali imekuwa na msimamo wake, kuwa hakuna sumu (Kemikali) inayotoka mgodini kwenda Mto Tigite. Matokeo yake sasa wananchi wengi wa maeneo ya Nyamongo hasa Kata za Kemambo, Matongo na Kata ya Kibasaka. Wananchi wengi wamekufa pamoja na mifugo, mingi imekauka kutokana na kinachosadikiwa kuwa sumu (kemikali inayoka Mgodini). Kwa taarifa ya vyombo vyaya habari, zaidi ya wananchi 21 na ng'ombe na nbuzi zaidi ya 300 wamekufa pamoja ya

mamia kwa maelfu ya wananchi na mifugo ikiwa imeathirika sana kwa matokeo haya kila siku kutakuwa kunatoka vifo vya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifunge mgodi wa *North Mara* na kurekebisha dosari ambazo zipo ili wananchi na mali zao zisiteketee. Iundwe Kamati Teule ya Bunge ili itoe matokeo ya haraka kunusuru maisha ya wananchi hao wa Kata za Nyamwaga, Nyarokoba, Matongo, Kamambo, Kibasuku pamoja na Watanzania kwa jumla maana kemikali hii huingia Ziwa Victoria ambapo watumiaji wa samaki wanaathirika kwa kula samaki wa sumu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa juhudi kubwa zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, pia niseme kuwa ninashangazwa sana na uwezo mkubwa wa Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dr. Shein jinsi anavyofanya kazi kubwa, bila kupumzika na kila wakati kwa maneno yenye kufariji na hekima kubwa. Mheshimiwa Dr. Shein ni mashine! Mwenyezi Mungu azidi kumtia nguvu ili azidi kumsaidia Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kufanya kazi za taka kama mkandarasi na sasa naendelea na usafi. Waheshimiwa Wabunge walichangia juu ya suala la taka Dar es Salaam hasa wakati wa mvua na kusababisha kuziba mifereji, pia juu ya ubovu wa magari ya taka.

Mheshimiwa Spika, hivi Waziri mmeshawahi kukaa na makandarasi hao na kujuu mazingira yao ya kazi yakoje? Ni kwa nini makandarasi wote wa taka wawe na magari ya kufanana, mabovu, yenye sura mbaya? Tatizo kubwa ni nini? Mimi majibu ninayo, lakini niseme tu, suala la taka hasa kwa mji mkubwa kama Dar es Salaam ni vyema likaongezewa ushirikiano wa karibu kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ni vema Manispaa ziwezeshe kkusanya kodi moja kwa moja, aidha kuitia mfumo fulani kama walivyo *EWURA*. Aidha, kuitia kodi za majengo na viwanja, au utaratibu mzuri zaidi, ama sivyo kuna siku hali itakuwa mbaya zaidi. Halmashauri zinaonekana kuwa na uwezo mdogo. Natambua kuna juhudi mbalimbali zimefanywa na Serikali, lakini suala la dampo la kudumu ni sawa na donda ndugu.

Mheshimiwa Spika, hivi wakihamishwa leo wakandarasi wasitupe taka Kigogo, kwa hali hii iliyopo, wataweza kupeleka taka Pugu Kajiungeni? Mfumo unatarajia nini? Japo nimemwona Mheshimiwa Waziri akikemea juu ya uchafuzi, suala la upandaji wa miti lipo safi, taka bado hatujapata ufumbuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Awali kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Mazingira kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara yake ambayo ina ubunifu mwangi wa jinsi ya kupambana na uharibifu wa mazingira katika nchi yetu. Pia Mheshimiwa Waziri ameikamilisha nchi yetu katika masuala ya Kimatifa ambapo ameiwezesha nchi yetu kupata mafungu ya kuborehsa mazingira zikiwemo fedha za ‘carbon trade’.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wote Ofisi ya makamu wa Rais kwa kazi zao nzuri za kila siku pamoja na maandalizi mazuri ya hotuba iliyosomwa leo. Mchango wangu wa leo utagusia maeneo maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunao mkakati wa kuhifadhi ardhi vyanzo vya maji, bahari, maziwa na mito, ni vyema Wizara hii ikashirikiana kwa karibu zaidi na wadau ambao wako katika harakati kabla ya mkakati huu kutangazwa. Kwa mfano tunayo *Marine Park* ambayo inashughulikia hifadhi ya bahari. Maafisa wa *Marine Park* wamekuwa wakifanya doria katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Mtwara na kukamata wavuvi na nyenzo za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wavuvi wa maeneo ya Nalingu, Msanga Mkuu na Chuno wanalamika kuwa *Marine Park* iliwaahidi kuwa itawapatia nyenzo za kisasa kwa ajili ya uvuvi endelevu lakini hajafanya hivyo. Masikitiko yao ni kwamba bahari ndilo shamba lao lakini hadi sasa hawana shughuli mbadala kwa ajili ya ustawi wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu ni kwamba, jamii hizi zikizuiliwa kuvua samaki bila kupatiwa njia mbadala, wanaweza kuanza shughuli za uchomaji mkaa ambazo zina uharibifu mkubwa zaidi wa mazingira. Hivyo, naishauri Wizara iliangular hili kwa kuziagiza Halmashauri zitenge mafungu kutoka *ASDP*, *TASAF*, mkopo ya JK na mengineyo kwa ajili ya kuwapatia wavuvi njia mbadala za kuendesha maisha yao, pia kupatiwa nyenzo bora za uvuvi. Akina mama wawezeshwe kuanzisha vitalu vya miche ya miti kama ajira na njia ya kuhimiza hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, wachomaji chokaa wa Mtwara wanaomba wawezeshwe kupata nishati mbadala kama makaa ya mawe ili kuepuka utumiaji wa magogo ambaou unapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa sasa wanatumia minazi iliyozeekaa, lakini hofu yao ni kwamba baada ya muda minazi hii itakwisha. Wao wako tayari kununua makaa ya mawe ili wanachokiomba ni kufikishwa kwa makaa ya mawe Mkoani Mtwara ili waweze kununua.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Chongokani kilikwishapata elimu ya mazingira. Kwa sasa wanaomba boti kwa ajili ya wao wenyewe kufanya doria kwani hawana imani na doria za Serikali kutokana na kuvuja kwa tarehe za doria jambo ambalo linaathiri

mafanikio ya jitihada zao za hifadhi ya bahari katika eneo lao. Pia wananchi hawa wana wasiwasi na uaminifu wa Watumishi wa Halmashauri yao wa Idara ya Mazingira kutokana na kwamba milipuko baharini inazidi kuongezeka. Hivyo wanaomba Watumishi hawa wahamishwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara ishirikiane kwa karibu na Halmashauri zetu pamoja na *NGO* za ngazi zote. Pia naomba Halmashauri ziwezeshwe kupata mbegu za miti.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Muhammed S. Khatib - Waziri wa Nchi (Muungano) Mheshimiwa Dr. Batlda S. Burian - Waziri wa Nchi (Mazingira) Makatibu wote na Watendaji wa Wizara hizo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuleta kilele cha mazingira Mkoani Tabora. Kwa kuwa Mkoa wa Tabora una sehemu kubwa ya misitu na wananchi wengi wanaamua kufanya (Giti) kazi ya kuhifadhi misitu kwa kushirikisha vikundi:

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuvunga mkono vikundi hivyo ili waendeleze jitihada hizo kwenye maeneo ambayo hayajavamiwa na wafugaji kwa kushirikisha wananchi kwa kila kijiji? Kwa mfano Wilaya ya Sikunge na Urambo zinaongoza kama kuhifadhi Mazingira hasa kwa kupitia vikundi vyta wanawake, ambavyo pia hupanda miti, ni vyema wakapata, Semina/Mafunzo, misaada ili wapate uelewa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Waziri wa Mazingira, atembelee Mkoa wa Tabora kwa makini ili wapate nafasi ya kuangalia uvamizi wa mifugo kwenye Kata za Wilaya ya Uyui, Urambo, Sikunge (Tura, Kizengi, Pandemlowoke) na kuandaa taratibu za upandaji miti wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, naomba ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Prof. Mwandsoya katika Wilaya ya Sikunge kwa vikundi vyta wanawake vitolewe maelezo ambayo ni Sh. 500,000/= kwani hajaondoka na Ofisi. Wananchi wana vikundi wanadhani nimekula fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba mazingira ya maji taka ya viwandani ambayo yanatiririka kwenye mifereji ya Jiji la Dar es Salaam – Ilala, Temeke na kadhalika viangaliwe na kusimamiwa kwa Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya *plastic* imerudi upya mijini kwa viwanda vyote kutengeneza chini ya viwango, viloba vyta maji na maziwa navyo ni tatizo na Halmashauri nyingi hazina magari ya kusombea taka hasa kwa miji mikubwa. Ni vyema sasa Wizara hii ikashirikiana na TAMISEMI kuweka mikakati ya kuweka miji taka.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ipange jinsi ya kutumia Ofisi hizo kwa kupanga baadhi ya Kamati za kudumu za Bunge kwa nyakati tofauti zifanye vikao huko

kwa wiki mbili kwani itakuwa haina maana ya kujenga Ofisi huko, tena ya heshima. Vikao vya uongozi vya Bunge vifanyike huko mara kwa mara, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Askari wanadai madai yao mara kwa mara, yafuatiliwe kwani ni madai ambayo hata Bara yapo hasa kwa wastaafuli.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Nyumba za Polisi ziboreshwwe na pia kukarabati Ofisi zao za Wilaya na Mkoa. Kwani madai kama hayo ni kero pia kwa Zanzibar. Naomba pia Askari hao wapatiwe vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzaia wote tunataka Muungano udumishwe, hivyo haki stahili zitolewe mapema kama vile Bara.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa *TASAF* waangalie jinsi ya kukamilisha miradi Visiwani ambayo haikukamilika katika kipindi cha mwaka 2008/2009, kwani kwa kutokamilisha miradi hiyo itarudisha nyuma maendeleo yao na pia kuwavunja moyo wananchi kwa maeneo waliyositolea (nguvu za wananchi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa Dr. Batilda Salh Burian kwa kuwasilisha kwa pamoja hotuba zao.

Mheshimiwa Spika, nchi masikini duniani zinashughulikia zaidi upatikanaji wa chakula na kuyapa mgongo masuala ya mazingira ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja ya maisha ya binadamu. Ili Tanzania isifanye makosa kama ilivyo kwa nchi nyingine, mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna Sheria ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ili kulinda mazingira. Kuna tetesi kuwa ndugu zetu wa Kenya wanatengeneza na baadaye kutuletea mifuko (midogo, myeusi) ya plastiki ambayo kule Kenya imepigwa marufuku na haitumiki. Naomba Mheshimiwa Waziri alichunguze suala hili na alitolee ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda mazingira Serikali huhamasisha upandaji wa miti kwa maelfu, lakini kazi hii sio endelevu maana miti baada ya kupandwa hufa maama haishughulikiwi. Kama zipo takwimu za miti ili yopandwa na ambayo hadi leo ipo hai kwa kila Wilaya naomba tutajiwe.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya bahari pia yanachafuliwa kwa uvuvi haramu. Tunazona juhudi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi za kuchoma makorokoro ili kunusuru uhai wa samaki, ni budi Wizara ya nchi mazingira ikatoa ushirikiano wa karibu na Wizara ya mifugo na uvuvi ili kukomesha uvuvi kwa kutumia mabomu, kemikali, utupa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Muungano wa Tanzania una matatizo mengi. Lakini wingi wa matatizo sio hoja. Hoja ni kwa kiasi gani Watanzania tuko tayari kuziondoa zile zinazoitwa kero za Muungano kwa sababu Kamati nyingi zimeundwa na ushauri mwingi umetolewa, lakini kasi ya utendaji ni ndogo sana kiasi kwamba wengi wetu tunadhani mambo yalivyo sasa hayatakiwi kubadilika. Inawezekana huu ni mkakati maalum. Kama hivyo ndivyo, basi ni kwanini tuendelee kupoteza pesa za walipa kodi kwa kukutana kwa kunywa chai tu?

Mheshimiwa Spika, ili kujuua kiini cha migogoro ya Muungano wetu, nashauri Waasisi wa Muungano wetu kutokea Tanzania Bara na Zanzibar wakutane maana bado wapo ili waulizane haya yaliopo sasa au yanayofanywa sasa: Je, ndio waliyokubaliana walipotaka kuungana na kama yameongezeka ni nani aliyeaongeza? Nashawishika kuamini kuwa ingawa Ofisi ya Waziri kiongozi Zanzibar na Ofisi ya Waziri Mkuu ndio waliokabidhiwa jukumu hili lakini hawatoshi kwa sababu wenyewe wapo.

Mheshimiwa Spika, lazima kurudi kwa *article of union* ili tuone tulipojikwaa na kutoka hapo tusonge mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lililo wazi hapa ni kuwa Muungano wetu umekosa uwazi (*Transparency*) hauainishi mambo ya Tanzania Bara ambayo sio ya Muungano ambayo hivi sasa yamo ndani ya Muungano kwa mfano Wizara ya maji, Miundombinu na kadhalika. Mfano mzuri ni bajeti ya muungano ambayo ni moja ya mambo yote ya Tanzania Bara na ya Muungano. Hiki ni kizungumkuti, lazima kiwekwe wazi ili haki na wajibu wa kila mdai uonekane.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, hongera sana Mheshimwa Waziri kwa hotuba kubwa, nzuri yenye mpangilio mzuri na zaidi ya yote ulimaliza kusoma na kuwasilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi zaidi kuhusu rasimu ya mwongozo wa ujenzi wa minara ya mawasiliano hususani katika eneo la hifadhi kama Ngorongoro. Miradi mingi ya Wananchi wa Ngorongoro kama ujenzi wa shule, Zahanati, Mabwawa nakadhalika zinacheleweshwa sana au kutojengwa kabisa kwa sababu ya tathimini ya mazingira (*EIA*). Wananchi wa ngorongoro wanahitaji mawasiliano kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba upigwaji marufuku mifuko ya plasitki uharakishwe kwa sababu imetuulia mifugo mingi na Wanyamapori, kuokoa ng'ombe aliye kula/aliyemeza plasiki ni kumfanyia oparesheni na madaktari wa mifugo wenye ujuzi huo ni wachache vijijini.

MHE. DR. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Kitabu hiki kimehodhi kwa kina hoja za mazingira na kutoa nafasi ndogo ya hoja za Muungano. Napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na ukanda wa pwani ya Tanzania. Kuhusu *MACEMP*, natoa shukrani kwa Wizara hii kwa kubuni mradi

huu wa kuwasaidia wananchi Zanzibar na Miradi ya kuwasaidia wananchi wanaoishi pwani kwa kuwapatia boti, yaani ni ukombozi safi. Nashauri sasa tufuatilie boti hizo zilizotolewa *free* na tuhakikishe kama zimewafikia walengwa zote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *PADEP*, Ujenzi wa barabara za Pemba, Mzambarani Takao hadi Finya kilometra 8.3, Kwale – Kojan kilometra mbili, Mzambarani Karim hadi Mapofu kilometra 8.3, Kipagani – Kangagani kilometra tatu na barabara Daya mpaka Mtanwa kilometra 13.1 Je, kweli barabara hizio zimejengwa au ziko katika *process* za kujengwa? Tupewe ufanuzi kwani barabara hizo bado ni za tope. Kama bado kujengwa: Je, ujenzi utaanza lini hasa?

Mheshimiwa Spika, kuchangia gharama na kugawana mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Yameanza malumbano katika Baraza la Uwakilishi juu ya uchimbaji wa mafuta, je, hili halizungumziki? Si pande zote zikubaliane tu? Kama Zanzibar wanaona mafuta yatoke katika mambo ya Muungano, kuna ugumu gani kutokubaliana? Kwa nini hili liachwe litugawe? Nashauri mbali na *consultant* kufanya *study*, viongozi wa juu wa pande zote mbili basi wakae na wakubaliane tu. Hili lisije likatugawa, sote ni ndugu.

Mheshimiwa Spika, gawiwo la 4.5%. Muda mrefu suala hili limekuwa linajadiliwa. Wazo la kuboresha mgao kutokana na hali ngumu ya mapato Zanzibar, ni suala linalohitaji kufikiriwa. Tunaelewa mapato yatokanayo na makusanyo ya shughuli za kiuchumi za Muungano ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya kiuchumi Zanzibar, ni vichache na mapato yake yanazidi kudidimia hasa kutokana na kushuka kwa bei ya karafuu na kudorora kwa shughuli za utalii, baada ya kipigo cha kuporomoka kwa uchumi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, suala hili wataalamu wa pande zote mbili wasilione haya na lisitiwe ubinagsi. Baba lazima amsaidie mwana atake asitake. (Tanzania iisaidie Zanzibar – kiuchumi). Si hiyo tu, Tanzania bara ifanye kwa makusudi kuiombea Zanzibar misaada. Shukrani nyingi kwa juhudhi kubwa inayochukua SMT kwa kuona hali ya SMZ kiuchumi; ila juhudhi za pamoja za pande zote zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, SMZ nayo ifikiriwe kupata *relief* ya fedha zilizotolewa kutokana na *financial crisis*. Hii itasaidia wakulima wa karafuu kuboresha mashamba yao na kwa Serikali kufikiria kuanzisha mazao mengine ya biashara. Aidha, uvuvi wa bahari kuu sasa upewe kipaumbele ili rasilimali zitokanazo na bahari sasa zitumiwe ipasavyo na kuchangia Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. SMZ ifanye kwa makusudi kusaidia wataalamu wachumi, wenye fani za kibiashara, kilimo wakae na wenzao na SMZ kupeana changamoto ya namna ya kuijendesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Makamu wa Rais. Ni vema Makamu akitembelea vijijini Bara awachukue wataalamu, viongozi, Wabunge toka SMZ ili hao wakaone na

wajifunze mambo mbalimbali ya kuchochea ukuaji wa uchumi nchini kwetu ili warudipo Zanzibar wawe Walimu kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa ukarabati wa Ikulu Wete, bado Ikulu ndogo Chake isiachwe. Pia majengo ya *head offices* za Polisi Chake, karakara na Polisi Wete zipewe uzito kuwekwa katika hali inayofaa.

Mheshimiwa Spika, *value for money*, majengo yanayojengwa yaendane na kima cha fedha kinachotolewa. Nampongeza Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mgodi wa North Mara, ufungwe na *analysis* ifanywe na hatua za *prevention* zifanywe, walioathirika wawe *compensated*.

Mheshimiwa Spika, usafi wa mazingira. Uongozi wa nchi wa ngazi za utendaji, waende na kujifunza Moshi.

Mheshimiwa Spika, *effect* za kumega SUMATRA tunazona sasa, *search and rescue*, Kamati ziboreshw na ziwezeshwe. Fedha iliyokuwa inakusanya SUMATRA zilisaidia sana ufuutiliaji wa mambo ya *safety* katika *maritime industry*.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nipongeze sana utendaji kazi wa Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa kweli anafanya kazi inayotukuka na anatakiwa awe mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana wewe, Mawaziri wenizio, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri mnazofanya.

Mheshimiwa Spika, upande wa utunzaji wa mazingira kwa kweli inabidi nguvu na pesa iongezwe zaidi kuokoa mazingira yetu ambayo yanazidi kuharibiwa kwa kufyeka miti na kuharibu vyanzo vya maziwa, Waswahili husema ‘kinga ni bora kuliko tiba’. Sasa hivi ukataji wa miti umeongezeka kwa asilimia kubwa sana, mkaa magunia na magunia yanaingia mijini, cha kushangaza zaidi hawa watu wengi wanakuwa hawana vibali na wala hakuna mtu wa kuwakamata.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi umefika muda wa kukuza Kitengo cha Mazingira kifike hadi Wilayani na kwenye Kata. Sasa hivi Mabwana Miti hawatoshi, kwa hiyo, ulinzi wa misitu yetu hautoshi kabisa.

Kuna haja ya kuwaajili Mabwana Miti na pia umefika wakati sasa wa kuimarisha upandaji miti vijijini na kwenye kata. Upandaji miti unaofanyika kila mwaka kitaifa hakuna kitu kinachofanyika kwani miti hupandwa siku moja na hakuna anayerudi tena kuiangalia na kuitunza.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Halmashauri za Wilaya nyingi hazitili uzito Wizara ya Maliasili upande wa misitu na wanyamapori. Kitu kinachotakiwa ni lazima Serikali itafute mbadala wa mkaa wa miti, mbadala huo ni mkaa wa mawe kwa vijiji na gesi mjini. Hakuna njia ya mkato tukitaka kuokoa misitu yetu ni lazima kuchagua njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni lazima Serikali kupanga matumizi bora ya ardhi ili wananchi wetu waachane na kilimo cha kuhama hama.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana kazi kubwa tunayoifanya ya kulinda Muungano wetu, kwa kweli ni Muungano wa kipekee hapa duniani. Ninachoomba, tujitahidi sana kutatua matatizo madogo madogo yanayozua manung'uniko toka pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana jitihada inayofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwenye kuwaondolea umaskini wananchi wetu kuititia mifuko mbalimbali. Ninachoomba ni jitihada hizi zifike mpaka kwenye ngazi za vijiji ambako ndipo Watanzania wengi ambao wako kwenye dimbwi la umaskini wanaishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi za dhati kwa Makamu wa Rais, pamoja na Mawaziri wake bila kuwasahau Watendaji wote wa Ofisi hii kwa kuchapa kazi kwa bidii pamoja na changamoto nzito wanazozikabili.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni mfano wa kuigwa katika Bara letu la Afrika pamoja na kuwa wapo baadhi ya watu wachache wenyewe tamaa ya madaraka wanaubeza Muungano huu, lakini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu hawataweza kuuvunja. Penye mafanikio pia yapo matatizo. pamoja na mafanikio mengi mazuri yaliyotokana na Muungano wetu na mengine mengi yanaendelea kuonekana, hata hivyo yapo matatizo yanayolalamikiwa hasa na upande wa Zanzibar kwa mfano; suala la mafuta na gesi asili kwa SMZ kuitisha sheria ya kuwa suala hilo si la Muungano, je, SMT inasemaje kuhusu mafuta na gesi asilia baada ya uamuzi wa SMZ wa hivi karibuni?

Mheshimiwa Spika, suala la gawio la asilimia 4.5 kwa SMZ linalotokana na mchango wa wahisani kwa misaada isiyokuwa na masharti Tanzania. Kuna kigugumizi gani katika jambo hili ambalo ni la siku nyingi sasa? Kwa nini hatuambiwi matokeo ya Mshauri aliyeteuliwa na pande zote mbili za Muungano kushughulikia suala hili. SMT haioni kuwa wanawapunja SMZ katika mgao huo kutokana na ushahidi wa mgao wa mwaka 2008/2009 ambapo SMZ ilitengewa mgawo wa shilingi 23 bilioni lakini hadi mei shillingi bilioni 23.5 zimetolewa, je, shilinhi 0.5 milioni zilitoka wapi? Hii imedhihirisha kuwa bado kuna fedha zaidi ambazo SMZ inatakiwa ipate ifikapo Julai, 2009 na hii ni dhahiri kuwa SMT inatakiwa iliangalie suala hili kwa uangalifu ili kuondoa manung'uniko kwa SMZ.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa *IMO* (*International Marine Organisation*), Serikali haioni kuwa SMT kuwa na chombo chake cha usimamizi wa chombo hiki (*IMO*) na SMZ kuwa na chake, ni kukiuka

Katiba ya nchi na kwamba vyombo/wakala zilizoundwa na Serikali hizi mbili zitashindwa kufanya kazi vizuri kwa maana ya kupingana juu ya maamuzi yao hasa usajili wa meli ambao upande mmoja wa nchi utaruhusu meli hiyo kusajiliwa baada ya kukataliwa upande wa pili na meli hiyo kuleta maafa baadaye? Mfano ni wa hivi karibuni ambapo imesemekana meli iliyozama kwenye bandari ya Malindi Zanzibar ilikataliwa kusajiliwa Tanzania Bara lakini ikasajiliwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kero ya wafanyabiashara kutozwa ushuru mara mbili, ni ya miaka mingi, ni lini hasa kero hii itamalizika? Sambamba na suala la mizigo kutoka Zanzibar hasa magari kutozwa *storage charges* kubwa ukilinganisha na magari mengine yanayotoka nje ya Tanzania ambapo wenyе magari hayo hupewa siku saba (*7days*) bila kulipia *storage charges* wakati gari linatoka Zanzibar hupewa muda wa saa 24 au na ziada ya muda hulipishwa *storage charge*. Serikali haioni kuwa jambo hilo ni kero linalofanywa kwa makusudi? Naomba maelezo?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliwataka wenyе mabasi hasa yaendayo Mikoani kuweka *dust bin* kwenye mabasi yao, jambo ambalo hadi sasa hakuna basi hata moja lililotekeleza agizo hilo, Serikali inasema nini baada ya kupuuzwa kwa agizo lake kwa kuwa abiria wamekuwa wakitupa taka ovyo na kwenda kinyume na matakwa ya kuboresha usafi wa mazingira sambamba na utupaji ovyo wa chupa za maji mijini? Serikali haioni kuwa wakati umefika kwa Kampuni zinazotengeneza na kusambaza maji kwenye chupa za plastiki viajiri wakala watakaokusanya chupa zote zinazozagaa mitaani na hasa kwenye mitaro ya maji machafu ambapo watu wanaokusanya chupa hizo huwa wanaona kinyaa kuziokota na hivyo kuziba mitaro wakati wa mvua na kusababisha mafuriko?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na udumu Muungano wetu. Mungu ubariki Muungano wetu na Tanzania kwa jumla, Amina.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Siyame amehitimisha orodha ya wale Waheshimiwa Wabunge waliopata kushiriki katika mjadala huu wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Kabla sijawaita Waheshimiwa Mawaziri wawili kwa mpangilio naomba tutambue uwepo wa watendaji wakuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais kama ifuatavyo:-

Nadhani watakuwa kule katika eneo la watumishi. Kwanza ni Bi. Ruth Mollel - Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, yupo Bw. Mubarak Abdul Wakil - Naibu Katibu Mkuu yule pale, Bw. Raymond Moshi - Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Bw. Eric Mugurusu - Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira, Bw. Elisha Suleiman - Katibu wa Makamu wa Rais, Bi. Fakharia Shomari - Naibu Katibu wa Makamu wa Rais, Bw. Boniface Kasongwa - Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Sera, Bw. Francis Molayi - Kaimu Mkurugenzi Idara ya Muungano na Bw. Bonaventure Baya - Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Wale pale, karibuni sana.

Sasa mpangilio ni kwamba atatangulia Waziri wa Nchi. Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa dakika 20 na atahitimisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais

Masuala ya Mazingira kwa dakika 25, jumla wanazo dakika 45. Sasa namwita Waziri wa Nchi, Masuala ya Muungano - Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Waheshimiwa mbalimbali ambao toka asubuhi walikuwa wakichangia. Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais ninayehusika na Muungano. Waswahili wanasema: "Nguvu za mamba ni kwenye maji" na mimi naona kama nimo kwenye maji sasa hivi, nina nguvu kweli kweli kwenye Wizara hii ya Mambo ya Muungano. Lakini pia Waswahili wanasema kwamba: "Kila kitu kina mwendawazimu wake". Kwa hiyo, mimi ni mwendawazimu wa kulinda muungano huu na naona fahari kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Yeye mara kwa mara hunisaidia mambo mbalimbali na baadhi ya wakati humsaidia yeye kukaa kwenye kiti chake pale. Mara nyingi na yeye hakai muda mrefu, mara anarejea mwenyewe, kwa hiyo ndiyo hivyo nitafanya nini! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Uzini kwa kunivumilia kwa muda mrefu sana nisipokuwepo lakini nafikiri kwamba wanaridhika na mimi sana kwa jinsi ninavyofanya kazi kwa jitihada kubwa sana. Kwa kifupi, wakati tunaingia katika Jimbo la Uzini kulikuwa hakuna barabara hata futi moja ya lami. Sasa hivi tuna barabara ya Kidimni – Kitope, Dunga – Kinyasini, Njia Nne – Bamba. Ni kazi ya Waziri wa Muungano huyo. Pia tulikuwa hatua Zahanati za kutosha. Sasa hivi kuna Zahanati Bambi, Mchangani, Miwani, Uzini, Ghana na Mpapa.

Pia tulikuwa hatuna shule za chekechea lakini sasa hivi tunazo zipo Mpapa, Mchangani Kiboje na Umbuji. Yako mengi sana, kwa hiyo naomba wananchi wangu wa Jimbo la Uzini waamini kwamba tupo pamoja tuendelee kuwasaidia zaidi. Tulikuwa hatuna maji ya bomba lakini sasa hivi yapo matangi Ghana, Mgenihaji, Bambi, Umbuji na Manzese. Tulikuwa hatuna umeme, sasa umeme upo Jimbo zima. Baada ya kusema hayo machache sasa niende kwenye hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nina muda mfupi sana, sijui kama nitamaliza lakini ningependa uniongezee dakika zako ili nimalize. Kwanza, tunapokea ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge yote mambo mazuri yaliyoshauriwa na tunaahidi tutayatekeleza. Lakini pia pamekuwa na maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge kwa mfano Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Omar Chombo, Issa Kassim Issa, Masolwa Cosmas Masolwa, wote hawa walizungumza juu ya wafanyabiashara wa Zanzibar wanaolipa kodi mara mbili. Hili jambo tunalijua, lipo kwenye agenda yetu na tunajitahidi jambo hili limalizike kwa sababu limekuwa ni kero kubwa. Tunaamini litamalizika tu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Issa na Masolwa ni usajili wa magari. Hili pia limo kwenye agenda yetu na tunalifanyia kazi.

Lingine limezungumzwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Omar Ali Mzee ni kwamba jinsi gani Wazanzibar wapata ajira katika Serikali ya Muungano. Hili pia lina agenda yake, kuna watu wamepewa kazi watushauri na baadaye tutalifanya kazi.

Hili sio tatizo hata kidogo kwa sababu tunalijua wenyewe. Lingine ni kuhusu elimu ya Muungano ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Faida Bakar kwamba kuna haja ya kuendeleza na kuimarisha elimu ya muungano ili watu wajue muungano wetu. Mheshimiwa Juma Killimbah pia amezungumza juu ya kinga ya viongozi wetu wakubwa Makamu wa Rais na Rais wanapostaafu. Lazima tuwape heshima zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niende kwenye hoja nyingine. Limezungumzwa suala la mafuta na nashukuru Mheshimiwa Mnyaa amezungumza suala la mafuta na amenekuu *Hansard* ya mwaka 1968 juu ya mafuta. Nastaajabu kama anakubali kwamba mafuta haya yameingia mwaka 1968 lakini mwanzo waliniparamia wakasema limeingizwa kinyemela la mafuta haya, kumbe anajua kwamba yameingizwa tangu mwaka 1968.

Lakini kwenye *Hansard* Mheshimiwa Rashid Kawawa alikuwa Waziri Mkuu anasema kwamba: “*Kulikuwa na makubaliano kati ya SMT na SMZ namna ya kuliingiza jambo ndani ya Muungano. Hansard inasema hivyo. Baba wa Taifa alikwenda kuzungumza na Baraza la Mapinduzi (Makofi) kwamba sasa umefika wakati wa kutilia mkazo jambo la mafuta kwa sababu mabepari na wakoloni siku zote walikuwa wakisema kuwa Tanzania hakuna mafuta na sisi tuna waamini kabisa. Jambo hili ni kubwa na lazima tulitolee macho zaidi. Waheshimiwa Wamezungumza, Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais Karume, alipofika hapa siku zile alimwambia Rais Baba wa Taifa kwamba kule wamekwisha kubaliana safi kabisa jambo hili liwe la Muungano kwa kuwa ni jambo kubwa kabisa na jambo hili lilifikishwa mbele ya cabinet*”

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili jambo limeingizwa rasmi katika Bunge hili kwa ridhaa ya pande mbili za Muungano bara na visiwani na *Hansard* hii hapa ipo. Isitoshe kuna Sheria ya Mafuta ninayo-copy, amesaini Mwalimu Nyerere tarehe 25 Julai, 1968. Kwa hiyo, wale walionishambulia kwamba mimi naingiza mambo kinyemela sasa nawaambia sio kweli na jambo hili likuwa halali kabisa. Tuliache hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nini hatma ya mafuta haya? Tumezungumza kwamba sasa hivi kuna mshauri mwelekezi ametuelekeza Serikali mbili namna ya kugawana mapato ya mafuta na gharama zake. Tunasubiri maelekezo hayo baadaye Serikali itaamua.

Wapo wameuliza hapa kwamba: Je, ile gesi ambayo inachimbwa huku Tanzania Bara mbona Zanzibar haipati haki yake? Jibu lake ni kwamba tunasubiri *formula* itakayotolewa na Serikali ya Muungano na Zanzibar wakishakubaliana, basi gesi hii pia SMZ watapa haki yao hata kama miaka mia moja iliyopita.

Kwa hiyo, huo ndiyo ukweli ulivyo, subirini tuamue jambo hili. Pia limezungumzwa suala la Tume ya Pamoja ya Fedha kwamba mpaka leo tunachelewa. Ni

kweli lakini Kamati ile ya Tume ya Shellukindo imeshamaliza kazi yake, taarifa ipo kwa Serikali ya Muungano na Zanzibar na sasa hivi inashughulikiwa ili waweze kufika hatima yake.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maoni machache ya Mheshimiwa Hafidh kuhusu embe bolibo na *kuruwiji*. Lakini mambo haya mambo ya JKU ya Zanzibar ifundishwe na JKT nafikiri ni jambo jema sana itabidi lazima Serikali zikubaliane kama kuna uwezekano. Lakini mimi sina uamuhi hapa, kama inawezekana lakini naamini inawezakana kabisa na mimi naafiki kwamba iwezekane na ikiwezekana, basi vijana wetu wapate mafunzo ya jeshi ili wawe wakakamavu zaidi. Hili ni jambo jema sana.

Kuhusu mambo ya Mheshimiwa Mnyaa nitaunganisha na maoni ya dada yangu Mheshimiwa Riziki kwa sababu yanafanana sana. Kwanza wanazungumza kwamba kuna haja ya kuwa na Mahakama ya Katiba kutatua matatizo. Mimi sijaona popote pale kwamba Mahakama ya Katiba inaundwa kutatua matatizo bali inaundwa kuondoa migogoro au kutokuelewana. Kwa hiyo, Mahakama ya Katiba itaitwa pale endapo Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano hawaelewani. Kwa hiyo, haiwezi ikaundwa Mahakama ya Katiba kwa ajili ya matatizo haya ambayo sisi wenyewe tunayamudu.

Mheshimiwa Spika, amezungumza pia kwamba kuna barua ya tarehe 3 Mei ya SMZ ambayo inaelezea mambo 12 yaliyomo kwenye Muungano yaondolewe. Sisi Serikali ya Muungano hatujayapata, kama yapo njiani kwa *DHL* hatujui toka mwaka 2003 lakini hatujayapata na utaratibu ya kuyaondoa haya sio kinyemela, lazima yaandaliwe na Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano yazungumzwe katika *cabinet* yaje hapa na tuamue na tukiamua 2/3 ya kila upande.

Kwa hiyo, barua yako hiyo ya maelezo hayo ya Mei 23 sisi Serikali ya Muungano hatujayapata ambayo yanapendekeza kwamba Usalama wa Taifa, Polisi kadhalika itolewe, hatuna habari nayo na ukiwa na *copy* tuletee hiyo ili tuone kama tunaweza kusaidia ikafika mbele. Lakini mpaka sasa hatuna habari nayo kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kauli ya Mheshimiwa Rais ambayo amesema ya kunywa chai na kahawa. Mimi nafikiri Mheshimiwa Rais alikuwa na busara sana! Anatuambia nini? Kwamba zungumzeni kama ndugu, kama marafiki, kunywa kahawa na chai huku mnacheka. Ndiyo maana yake. Sio mnakaa pale mnazungumza kila mtu na jambia chini pale, utanitambua leo, hapana.

Kwa hiyo, Rais ametoa busara kwamba ninyi ni ndugu bara na visiwani endeleeni kuzungumza, jadilianeni ili baadaye mfikie muafaka. Hii inarejea hoja ya Mheshimiwa Mnyaa. Ametaja hapa orodha ya Tume nyingi sana, mimi nafikiri ni jambo jema hilo kwa sababu binadamu tunakwenda kwa majadiliano sio kwa vita. Tume hizi zote, hata Mfumo wa Vyama vingi umekuja kwa Tume pia. Kwa hiyo, kuna kitabu cha muafaka kati ya Serikali ya Muungano na Zanzibar cha mwaka 1994.

Kwa hiyo, nasema suala la kuwa na Tume nyingi kuzungumza masuala ya Muungano ni jambo jema kwa sababu linaonesha kiasi gani watu wanaolewa na kukubaliana. Mimi simlaumu kabisa Mheshimiwa Rais au kuwepo na Tume, ziwepo Tume, tutakaa kitako tutaelewana tu, la muhimu tufikie malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine amezungumza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Aboud Jumbe hakusikilizwa, Azimio la Tanganyika halikusikilizwa, Nyalali hakusikilizwa. Lakini hasemi ukweli kuhusu Aboud Jumbe na Seif Shariff, angesema kwamba aliyemfitini Aboud Jumbe ni Seif Shariff. Ndiyo aliyoiba nyaraka kwenye droo yake akampa Nyerere. Kwa hiyo, haya yote hayasemi hasa chimbuko la Aboud Jumbe kufukuzwa ni fitina ya Seif Shariff Hamad. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili la Azimio la Tanganyika, Tanganyika wakati ule ilikuwa na Chama kimoja cha CCM, Azimio la Tanganyika ndani ya Muungano. Tatizo ilikuwa ni kwamba hoja ile ilikwenda Bungeni bila kupata kibali cha Chama Tawala. Mnakwenda kubadilisha mfumo wa Serikali nani kakutumeni? Ndiyo hoja ilikuwa, tukaelewana yakamalizika. Hoja ya Nyalali aliwahoji watu kuhusu mambo ya Muungano na hoja kuhusu Serikali ngapi.

Zanzibar watu 3,000 walijitokeza, watu wanne walitaka Serikali tatu sawa na asilimia 0.13; watu 32,275 kutoka Bara watu 45 walitaka Serikali tatu sawasawa na asilimia 0.13. Kwa hiyo, kwa vipi utawasikiliza watu wenye asilimia ndogo kama hii? Hawa hawana *majority* na ndiyo maana wakaachwa. Kwa hiyo, hoja ya Nyalali naijibu na hoja ya Aboud Jumbe ninajibu na Azimuo la Tanganyika ninajibu. Lete hoja nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine wamezungumza juu ya Mfumo wa Kamati hii ya Muungano ambayo inaongozwa na Makamu wa Rais. Wanasema kwamba Kamati hii sio halali. Lakini kwenye kitabu chao pale bahati mbaya hawamtaji Makamu wa Rais, wanamtaja Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi na nafikiri wamekimbia ili nisiwabane. Lakini Kamati hii inaongozwa na Makamu wa Rais mwenye dhamana ya Muungano.

Kwa hiyo, amehalalishwa na kwa Katiba na *instruments* zake. Isitoshe hili ni agizo la Rais wa nchi hii, kasema nataka iundwe Kamati na wewe ndiyo utakuwa Mwenyekiti wake. Kwa hiyo, uhalali wa Kamati hii mimi siliioni kama siyo halali na ameomba Wabunge nyie eti mkubali ifutwe, kataeni. Kwa sababu ukifanya hivyo unakwenda kinyume na Katiba yako, Katiba ambayo Rais ana mamlaka ya kumchagua mtu kushughulikia na pili ni kinyume na kauli ya Rais wetu ambaye amefanya hivyo.

Wakati mwingine Wapinzani wana shida kweli! Jambo wakilipenda wanashangilia, wakilichukia hawalipendi. Waliomba sana Mheshimiwa Rais ingilia kati muafaka na Rais huyu huyu sasa kwa hili hawalitaki ila la muafaka Rais aingilie kati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aendelee kuhudhuria vikao hivyo halali na mimi nitahudhuria. Tunaishi hivyo na ndio mkate wetu wa kila siku hatuwezi kuacha.

Suala lingine ni kuingizwa mambo katika Muungano kwa kinyemela; mara wanazungumza hili, mimi ambalo linanikera sana kwa sababu ukienda kwenye *Hansard* yapo mengi haya toka 1964 kila jambo linaingia, mpaka mtu akikohoa wanaandika kakohoa, kacheka au kafukuzwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni la Mikataba ya Muungano. Tunaambiwa kwamba, Muungano huu si halali na kwa hiyo Mkataba ndio uwe wa kuongoza nchi yetu; yanatoka wapi hayo; hawa wataalamu wa Sheria au hawajui? Hata mimi mtu wa kawaida najua haiwezekani hivyo. Mkataba unakuwa chimbuko la jambo tu, baadae Katiba ndio inakuwa juu yake na sheria inafuta hivyo. Kwa hiyo, hakuna makosa Mkataba ni kama historia sasa hivi na *archives* tulianza hivi, tulifanya hivi lakini sasa hivi Mkataba huu hauna umuhimu kwa sababu ulikuwa kama chimbuko la Muungano wetu na ndio tabia ya Mikataba yote Duniani

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, wanazungumza juu ya Tanganyika, mimi naona hapo ndugu zetu hawa wanaizungumzia sana Tanganyika. Hawajui mwanzo wala mwisho, wenyewe Tanganyika yao wenye hawasemi, wakati tunapata uhuru kulikuwa na watu milioni kumi na moja wa Bara, sasa hivi wapo milioni 40, wengi wameshakufa amebakia Mzee Ngombale sijui na wenzake basi. Wengi Tanganyika yao haipo imepotea na wengine wengi wamekuja wala hawajui Tanganyika imekaaje, wote ni watoto wa Muungano huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naona ajabu, ndugu zangu ninyi mnalilia Tanganyika wee, maiti si yako, mnagalagala chini mnalia machozi na kupaka mafua faaa!; maiti wala si wako! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani ndugu zetu wa Upinzani wanafanya mambo ambayo hayana msingi wowote. Serikali ya Tanganyika haipo, nchi ya Tanganyika haipo, Zanzibar pia haipo sasa kuna Taifa moja na Taifa lenyewe ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi sasa kuna mamlaka moja tu, kwa hiyo, msirejee kule nyuma tulikotoka, tupo tayari kurekebisaha mambo yetu, matatizo yetu, lakini nasema suala la Tanganyika halina nafasi; wenyewe Tanganyika yao waliogombea wengi wao walishakufa, wamebakia wachache hata habari hawana. Sasa hivi walio wengi ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Masuala ya Muungano,nadhani hakika hapo ulipoketi ndio penyewe hasa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa muda wa dakika ishirini na tano. Mheshimiwa Waziri (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kama kawaida, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama hapa tena kujibu hoja za Waheshimiwa

Wabunge. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa jinsi unavyosimamia na kuendesha Bunge, hasa kwa wakati huu wa majadiliano ya Hoja ya Serikali niliyoiwasilisha asubuhi ya leo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwashukuru Akina Mama wa Mkoa wa Arusha, ambao ndio wameniwezesha mimi kusimama hapa. Napenda kusema tu kwamba, nitaendelea kuwatumikia na nitaendelea kuunga mkono jitihada zao za kuweza kuwafanya Akina Mama wa Tanzania, waweze kupunguza mzigo wa kazi kama nilivyoahidi, pale nitakapojaliwa nitaendelea kutoa matrektta ya *power tillers* kwenda na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakati wa mawasilisho ya Hotuba yangu, nilitoa shukrani mbalimbali, naomba nimalizie kwa kumshukuru mume wangu, watoto na wazazi wangu, kwa upendo na ushirikiano wao mkubwa. (*Makofi*)

Sasa niruhusu niende kwenye hoja mbalimbali ambazo zimejadiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ikiongozwa na Mheshimiwa Job Ndungai, kwa michango na ushauri wao ambao tumeupokea. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango na ushauri wao, ambao tumeupokea na tumejibia hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika masuala ya mazingira, kwa mchango wake mkubwa, ambao ameutoa hapa na hoja ambayo ameilezea kwa msisitizo mkubwa, hasa masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Tunamponeza na tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Riziki Omar Juma, ambaye ni mkwe wangu na ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri ya masuala ya Muungano. Wote hawa tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wabunge wote, waliochangia hoja hizi hapa. Hoja hii imechangiwa kwa kuongea hapa Bungeni na imechangiwa kwa maandishi na Wabunge 36. Hoja nyingi zimetolewa wakati wa kuchangia hapa, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutazijibu hoja hizi kadiri muda utakavyoruhusu na nyingine tutazijibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, niruhusu niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia humu Bungeni kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John Paul Lwanji, Msemaji wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Masuala ya Muungano, Mheshimiwa Job Ndungai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na

Mazingira, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Yahya Khamis Issa, Mheshimiwa Charlse Mwera, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na Mheshimiwa Muhammed Seif Hatib - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)

Mheshimiwa Spika, wachangiaji waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Omari Ali Mzee.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mhoga Said Ruhwaya, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ahmed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Hadija Salum Al-Qassym, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis na Mheshimiwa Fatma Mikidadi.

Mheshimiwa Spika, nianze na michango mbalimbali ambayo imechangiwa na Kamati ya Bunge ya Masuala ya Mazingira. Napokea ushauri wa Kamati kwamba; ni muhimu Ofisi yetu ikamalizia utaratibu wa kutafsiri Ripoti ya Hali ya Mazingira. Tunasema tunaikamilisha Ripoti hii na tayari tuna muhtasari wa Kiswahili na Ripoti kamili itatoka ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunapokea ushauri wa kukamilisha kanuni mbalimbali. Tayari kanuni ya papo kwa papo imekwishakamilika na tuna kanuni za tozo za ada mbalimbali za usimamizi wa mazingira (*Environmental Fees and Charges*), ambayo pia imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilituelekeza kwamba, ni vizuri tufanye maamuzi sahihi kuhusu masuala ya mifuko ya *plastic* na sisi tunesema kama tulivyoweza katika bajeti yetu, tunafanya tafiti. Kama Kamati ilivyoelekeza, tuone hasara tutakayoipata kama tukipiga marufuku mifuko ya *plastic* na baada ya pale tutafanya uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana kabisa na Kamati kwamba, ongezeko la idadi ya watu nchini ni budi likazingatiwa. Tunashukuru kwamba, Tume ya Mipango, chini ya

Ofisi ya Rais, tayari imeliona hili na sasa hivi inalifanyia mikakati ili kuona jinsi gani Tanzania tutaweza kujihimili na kuweza kuwa na Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielekeza tuongeze zaidi elimu ya mazingira kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali. Tunasema kwamba, tutazidi kuongeza elimu, tutazidi kuongeza masuala mazima ya ubunifu, tayari tuna Mradi wa Kusafisha Jiji la Dar es Salaam, andiko ambalo tumeliwasilisha katika Shirika la Maendeleo la Mazingira na tunategemea kupata ufadhili ili Jiji letu la Dar es Salaam liweze kuwa safi na tuwe na mkakati amba ni mzuri kwa kuhusisha Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilizungumzia suala la North Mara, lakini nimesema kwa sababu suala hili limezungumziwa na wengi, naomba liwe suala la mwisho kulitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa jinsi alivyoliezea suala la mabadiliko ya tabia ya nchi kwa uzito wake na kwa jinsi alivyoitaka Serikali sasa kuchukua hatua. Napenda kumhakikishia kwamba, Serikali imekwishachukua hatua, tayari tuna Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi. Sasa hivi Serikali inachofanya ni kupata gharama halisi ya fedha itakayohitajika kutekeleza Mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, Mkakati huo unahu masula ya mifugo katika maeneo ya ukame, unahu masula ya kuridhisha miundombinu katika maeneo ambayo ardhi imeharibika kwa maana ya barabara na madaraja, lakini pia kuangalia maeneo ya Ukanda wa Pwani, ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi, wameelezea maeneo ambayo yameathirika sana.

Mheshimiwa Spika, nimweleze Mheshimiwa Mnyaa kwamba, katika kutekeleza mambo haya, tunafanya pia kwa kuzingatia masuala mazima ya Zanzibar na Pemba. Kwa hiyo, masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi, hayajaathiri tu upande wa Tanzania Bara, lakini pia Zanzibar na tunashirikisha japokuwa hili siyo suala la Muungano, lakini tunafanya kazi kwa pamoja na fedha zitakapopatikana Zanzibar pia itaingizwa. Niseme tu kwamba, kuititia Mradi wetu wa REG, Zanzibar imeingizwa na tunategemea kuwa na Miradi ya pamoja kuititia fedha za Norway.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi ambayo yameelezewa hapa ni suala zima la chanzo cha maji kwamba, kuna tafsiri tofauti kati ya Sheria ya Mazingira na Sheria ya Maji. Niseme tu Sheria ya Mazingira ndio itakuwa juu ya zile sheria nyingine kama kutakuwa na mgongano katika masuala ya mazingira. Tayari Wizara ya Maji inafanya mapitio ya Sheria yake ili kurekebisha na kuwa na uwiano wa maeneo na mita zinazohitajika kutegemeana na umbali wa mito na vijito.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitueleza kwamba, sasa ni budi Serikali kufanya miradi ya kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Miradi iwe tayari; tumeshaiandalia na tumeshaanza kufanya na tunaanza kutekeleza zaidi. Niseme kwamba, tayari tumeshatayarisha kanuni na utaratibu mzima wa kushiriki katika *gas* ya ukaa

ambayo tutatoa maelezo kwa wananchi na itapitia katika ngazi zote za Serikali ili sasa iweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ametuelezea mambo ya msingi sana. Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Mwalyosi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati yetu na ni Mtaalamu wa masuala ya *Environmental Impact Assessment*, kwa hiyo, mengi aliyoyazungumza ni masuala ya ushauri na sisi tunasema tunazingatia, tutaendelea kuzingatia na tutaendelea kushirikiana naye.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwa wabunifu na pale tutakapohitaji ushirikiano wake kutohana na utalaamu wake wa muda mrefu katika masuala ya mazingira, basi tutaomba tushirikiane pamoja. Kuhusu suala la ongezeko la watu nchini, kama tulivyoleza ni suala ambalo limeonekana haliwezi likawekwa pembedi kama tunataka kuwa na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwalyosi, alituelezea pia juu ya tatizo zima la umaskini na jinsi gani tunaweza kuhakikisha kwamba, masuala ya mazingira yanaendana na masuala mazima ya kuondoa umaskini. Niseme tu kuwa, mikakati mbalimbali inafanyika kupitia bajeti yetu; kama utakavyoona masuala ya Ukanda wa Pwani, tumeelekeza miradi mbalimbali kusaidia wakazi wa maeneo ya Pwani kwa maana ya ufagaji na uvuvi. Katika maeneo mengine kuimarisha masuala ya ufugaji nyuki na kilimo cha paprika. Zote hizo ni jitihada za kuhakikisha kwamba, mazingira yanaweza kukidhi matakwa ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kujiimarisha zaidi kwa kuwasaidia wananchi kupata mbegu na kuanzisha bustani ya miti, ambayo inaweza kuwa miti ya matunda na aina mbalimbali ili waweze kupata kipato.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Charles Mwera, alinitumia *ki-note* kidogo mapema kama siku tatu zilizopita, kuhusu suala zima la North Mara. Tulizungumza lakini baadae nitatoa maelezo. Niseme tu kwa yale aliyoniandikia; alizungumzia masuala ya upandaji miti na sisi tunasema tayari mkakati upo, kila Mkoa na kila Wilaya wanakuwa na utaratibu wao wa kupanda miti. Sisi tutakachofanya ni kufuatilia, kuhakikisha kuwa zoezi hili linafanyika na tutaendelea kuratibu.

Mheshimiwa Spika, vile vile alizungumzia masuala ya kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda na shughuli za *garage*. Masuala hayo pia yalizungumziwa na Wabunge wengi na niseme kwamba, tayari tunashirikiana na Serikali za Mitaa ili yale maeneo yaliyotengwa, yasiwe karibu na makazi na sisi tutaendelea kukagua kuona kwamba vigezo vinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Hassan Mshangama naye alizungumzia masuala mengi ya jinsi ya kuokoa maeneo ya Lushoto, ambayo ni *rain catchment*, ambapo sasa hivi inaweza ikageuka kuwa jangwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mshangama kwamba, eneo hili litaguswa na Mradi wa REG na tutahakikisha kwamba, maeneo ya misitu ya asili yanarudi katika uasili wake na uoto wa asili haupotei.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine ya kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, tunasema kwamba, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo. Suala hili limezungumzwa pia na Mheshimiwa Ligallama, ambapo alisema kwamba, kaulimbiu hii ya Kilimo Kwanza, isitafsiriwe kwamba, kila eneo sasa hivi linatakiwa lilimwe. Mheshimiwa Ligallama, alituambia kwamba, ni vizuri basi tukabainisha maeneo kwa mfano eneo la Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, tunataka Mkoa wa Morogoro uwe Ghala la Chakula la Taifa, lakini siyo kwamba kila eneo sasa litalimwa hata katika maeneo ya ardhi owevu na maeneo mengine. Kwa hiyo, ni vizuri tukashirikiana na Wenzetu wa Wizara ya Kilimo na Mkoa, kuhakikisha kwamba, kaulimbiu hii haitafsiriwi vibaya kwamba, kila eneo sasa liingie kwenye shughuli ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, naye amezungumzia masuala mazuri ya jinsi ya kuimarisha mitandao katika maeneo ya ngazi ya chini ya Mkoa. Ni kweli mitandao hiyo ilikuwa dhaifu, kwa sababu hakukuwa na Maafisa Mazingira. Kada hii ya Maafisa Mazingira ndio kwanza inaanza, tayari tuna Wilaya zaidi ya 42 zimeshaajiri na sasa hivi kupitia msisitizo ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliuelekeza, baada ya ziara yake Mkoa wa Dar es Salaam, tuna uhakika kwa mwaka huu wa fedha, Halmashauri zote zitakuwa zimeajiri Maafisa Mazingira katika Halmashauri zao. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Killimbah.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Killimbah pia aliomba NEMC ifungue ofisi katika Kanda ya Kati. Tunasema tuimarishe uwezo, tumeanzisha Kanda tatu, nia ni kufika na Kanda ya Kati; kwa hiyo, tutafikia huko na tunafuata ushauri wako.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgana Msindai, alizungumzia juu ya suala zima la kuongeza nguvu ili kuokoa mazingira na amesema tushirikiane na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Misitu ili kuongeza Maafisa Misitu kuweza kuhakikisha kwamba, misitu hii haikatwi na watu hawavamii maeneo yale na kukata miti ya asili kwa ajili ya kutengeneza mkaa. Sisi tunasema kwamba, hilo tumeliona; sasa hivi tunatengeneza kanuni ambayo itazuia ukataji wa miti hata ile ambayo itakuwa ni ya mtu binafsi, bila kuwa na kibali kutoka kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msindai, pia alizungumzia masuala ya mipango bora ya ardhi. Sisi tunasema kwamba, tumeliona hili na hasa baada ya mgogoro wa Wafugaji na Wakulima na ni jambo ambalo linafanyiwa kazi na tayari kuna andiko la kuweza kuangalia suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, alizungumzia suala zima la Ofisi yetu kufanya kazi karibu na Wizara ya Nishati na Madini katika kuhakikisha kuwa, matumizi ya nishati ya *gas* ya kupikia na nishati mbadala inapatikana. Niseme kuwa, tunawashukuru kwa ushauri huu na hivi sasa Waziri wetu anayeshughulika na masuala ya Madini, yuko Nchini Misri kwa ajili ya kuiwakilisha nchi katika Mkutano Mkubwa wa Taasisi inayoshughulikia Masuala ya

Nishati Mbadala (*International Renewable Energy Agency*) na tunategemea kupata miradi mingi ya masuala ya nishati mbadala kuitia Agency hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, dada yangu, amezungumzia pia masuala ya nishati mbadala. Hili suala ni changamoto kubwa, maeneo mengi bado matumizi ya mkaa ni makubwa. Sisi tunasema, tunajielekeza katika Ilani iliyotutaka tuongeze matumizi mbadala ili kuokoa ukataji mkubwa wa miti. Tutaendelea na suala hili, kwa kushirikisha taasisi mbalimbali na kuitia miradi mbalimbali, kuongeza kasi katika kueneza nishati hii mbadala vijijini kama ilivyotuelekeza.

Kuhusu mifuko ya plastiiki, tunakubaliana na wazo lake kwamba, hii mifuko ipigwe marufuku. Tunachotaka ni kuvuta muda, tupate wajasiliamali waweze kuleta bidhaa mbadala tuweze kuhusisha watu wengi zaidi. Hivi sasa ni viwanda kumi na mbili tu vinashughulika na biashara ya mifuko ya *plastic* na vinaajiri watu elfu mbili. Kwa hiyo, bado idadi ni ndogo na tunaweza kupata watu wengi zaidi, ambao watashiriki katika biashara hii kama tutaweza kutumia vikapu na mifuko mingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi, alituelezea pia suala zima la *River Training* ya Mto Mkondoa. Suala hili hata mwaka jana alilielezea ya kwamba ni Mto ambao unahamahama, sisi tuliwasilana na wenzetu wa UNIP ili kupata mtaalamu ambaye atawea kuja kushirikiana nasi katika suala hili. Tumepata ahadi kwamba, tutaweza kumpata mtaalamu, tukishampata tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili kazi hii iweze ikafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala mengine ambayo ametueleza kama umuhimu wa kutembelea maeneo hayo na kuweza kuongea na wananchi; tunesema tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe, alituelezea umuhimu wa elimu ya hifadhi ya mazingira na sisi tunesema, tutashirikiana na yeze mwenyewe kwa utaalamu wake na kuweza kuwapa elimu wachimbaji wa madini, ambao wanachafua mto katika maeneo ya kule Chunya. Kupitia Ofisi yetu na yeze mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, tutasaidiana kuandaa mradi ambao utaweza kufadhiliwa na GEF.

Mheshimiwa Dr. Sigonda pia alizungumzia juu ya suala la Ziwa Rukwa na hili limezungumzwa pia na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. Mimi sikulisema hili katika bajeti yangu, lakini nia ya ofisi yetu ni Maziwa yote sasa hivi kupata miradi. Tumeshazungumza, mimi binafsi nimezungumza na Balozi wa Finland na ameonesha dalili ya kutaka kusaidia. Kwa hiyo, naweza nikasema, ndani ya mwaka huu tunaweza kupata kitu.

Mheshimiwa Spika, sikutaka kuliweka kwa sababu sikupata kauli na sikujuu ni kiasi gani tunaweza kupata, lakini niseme tu kuitia Mradi wa REG, tutafanya shughuli nyingine ambazo zinaweza kuhifadhi maeneo yale ili kuhakikisha kwamba, uoto ule wa asili na athari hiyo ya maji ya Ziwa hilo kupungua inapungua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, amezungumzia suala la dampo la taka kuwa mbali; hili tuliliona lakini ni dampo la kisasa ambalo linaweza kusaidiwa. Sisi kupitia Mradi wa Jiji tuliotengeneza na wenzetu wa UNEP, tutashirikiana ili kuhakikisha matatizo ya uchafu na usimamizi wa mazingira kwa Mkoa wa Dar es Salaam unazingatiwa, kwa kushirikisha makandarasi na wale watu wanaoshughulika na zoezi zima hili la usimamizi wa taka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Kijiko, alizungumzia masuala mazima ya umuhimu wa kusaidia wananchi kupata mbegu za kupanda miti, vile vile kushirikisha NGOs mbalimbali ziweze kushiriki katika kupata miradi mbalimbali. Mimi nasema, hilo tutashirikiana na amesema kuna NGOs nyingine ambazo zinatumia fedha za wafadhili kwa kisingizio cha hifadhi ya mazingira, lakini hazifanyi hivyo; tutazifuatilia na kama zitakuwa zinakiuka basi tunaweza tukawashughulikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, alituelezea masuala mazima ya kuhakikisha kwamba, sheria inatungwa na inasimamiwa kuhusu uchafuzi wa hewa na magari yanayokiuka viwango yanashughulikiwa. Sasa kupitia sheria yetu ya tozo, magari kama hayo yataanza kutozwa na tutakapokamilisha basi tutatoa taarifa ili wananchi wajue na waweze kuona mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na wenzetu wa miundombinu na wa kupitia SUMATRA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Telele, Mbunge wa Ngorongoro, alizungumzia masuala mazima ya ujenzi wa minara. Suala hili pia lilizungumzwa na Mheshimiwa Balozi Mshangama, Mbunge wa Lushoto. Tuseme tu umuhimu wa tathmini ya athari kwa mazingira ni muhimu sana katika minara hii inayojengwa hata katika eneo ambalo ni la milima. Sisi tumeshakamilisha mwongozo, ambao unarahisisha sana utoaji wa hii minara bila ya kuwafanya wasubiri kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wakiweza kuteleza viwango vile na tukakagua, basi hakuna mlolongo utakaowafanya wasubiri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, alielezea masuala mazima ya uharibifu wa viumbe asilia na kwamba sheria itungwe. Tunazingatia ushauri huu, ambao lengo ni kuhakikisha kuwa, bianuwai ya viumbe mbalimbali haipotei.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, alitueleza kwamba, tutafute jibu la ongezeko la ng'ombe. Kwa kweli jibu hili inabidi tutafute wenzetu wa maeneo ya Kaskazini, kufuatia ukame wamepoteza mifugo wengi sana na tunaona kwamba, tusipoliangalia hili tunaweza kuboresha mifugo yetu na kusaidia kuwa na maeneo ya mifugo ambayo yanatambulika na kuhemishika, basi tutakuwa tunapata matatizo makubwa sana. Tutashirikiana na wenzetu wa sekta nyingine kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, alielezea masuala mazima ya kuhifadhi mazingira na kuangalia maeneo yetu ya mazingira hasa ya Ukanda wa Pwani yanazingatiwa; na hili nimesema kama nilivyoeleza kwingine kwamba tunafuatilia.

Mheshimiwa Spika, pia Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, aliulizia agizo letu la kutoza tozo ya papo kwa papo limefikia wapi na watu wanazidi kutupa chupa za maji ovyo kupitia kwenye basi na vyombo vingine vya usafiri. Sisi tumekwishakubaliana na Jeshi la Polisi na sasa hivi tuneshaandaa mwongozo ambao utatekelezwa katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha na kuweza ku-*charge* watu kupitia kwa wenzetu trafiki ambao watakuwa wanasmama katika maeneo hayo ya barabarani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, alizungumzia masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi na kueleza kwamba, ni vizuri elimu ikaboreshwa na sisi tukasema itaboreshwa. Ametueleza pia masuala ya ufukwe na ukataji wa mikoko; hili tunalizingatia sana, kwa sababu ni maeneo ambayo yameathirika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, ametuelezea masuala mazima ya uharibifu katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa na hili tumelizingatia.

Mheshimiwa Anastazia Bura, ametuelezea kwa kirefu sana, masuala mazima ya kushirikisha asasi zisizo za kiserikali. Ametuelezea masuala mazima ya kusaidia wavuvi na masuala mazima ya kushirikisha wanawake. Tunakubaliana na ushauri wake na kupitia miradi mbalimbali ya mazingira, tutaendelea kutekeleza hayo na kushirikisha wenzetu wa uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Tabora, ametuelezea uharibifu mkubwa wa misitu na mifugo mingi katika maeneo ya Wilaya na Mkoa, hasa katika Wilaya ya Uyui, ambapo idadi ya mifugo ni kubwa kushinda hata wananchi wa eneo lile. Tumesema suala hilo ni tatizo na tutaendelea kulifuatilia na tutawashirikisha wenzetu wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum Kigoma, amezungumzia suala la Uvinza. Sisi tunasema, viwanda ambavyo vinatumia magogo kwa ajili ya shughuli za uendeshaji, vianze kutafakari upya, kwa sababu tulishatoa taarifa na sheria inaagiza viwanda hivyo lazima viwe na mashamba ya miti; vinginevyo ni lazima waoneshe hiyo miti wanaitoa wapi. Vile vile matumizi ya nishati imeelezewa na nimelielezea hapo mwanzoni, lakini pia masuala mazima ya kushirikisha wananchi kupitia elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba niruhusu nitoe maelezo kuhusu suala zima la Mradi wa North Mara, nadhani ni eneo ambalo limechangwa kwa hisia kubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na sisi tumeliona hilo na tunakubaliana na Wabunge kwamba, jambo kama hili likitokea na likiwa linaoneshwa katika kiwango kile ni budi likapata maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa North Mara uliana kabla ya Sheria ya Mazingira, kwa hiyo ni Mgodi ambao haukuwa umefanya *Environmental Impact Assessment*, lakini

tunao mfumo wa ufuutiliaji wa *monitoring assessment* kama inavyotaka sheria, kwa miradi ambayo imeanza baada ya sheria.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 12 Mei, 2009, Baraza la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*), lilipokea taarifa ya uvujaji wa kemikali kutoka Mgodi wa North Mara kama sheria inavyotaka, kwa miradi kama hiyo ikitokea tatizo kama hilo. Taarifa hiyo ya mgodi, ilieleza kuwa uvujaji ultokana na wizi wa maturubai yanayozuia uvujaji wa kemikali.

Mheshimiwa Spika, kama utaona katika picha, eneo lile la kati ambalo ni jeusi, ndiyo lenye maturubai ambayo huwa yanazungushwa ili kuzuia upenyaji wa kemikali isiende kwenye ardhi. Kufuatia taarifa hizo, Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, lilifanya ukaguzi katika eneo la tukio tarehe 14 Mei, 2009; utaona ni siku mbili tu baada ya kupata taarifa kutoka kwa mwenye mgodi.

Mheshimiwa Spika, tulivyofika kule, Baraza liliona kwamba ni kweli kulikuwa na wizi wa maturubai na baadhi yalionekana katika nyumba na mabanda ya biashara za baadhi ya watu wa maeneo yale yakitumika kama paa na nyingine zikitumika pembedi ili kuzuia juu na mvua.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo ulibaini mambo yafuatayo: Kwanza, ni kweli maturubai yaliibiwa na zilichukuliwa mita za mraba elfu kumi na tano kutoka mabwawa mawili. Kwa kawaida, mabwawa yanatunza maji yenye kemikali zinazobaki kwenye miamba, kwa hiyo ni lazima kuwekwa maturubai ili kuzuia kemikali kupenya na kuingia ardhini.

Mheshimiwa Spika, pili, maji yenye kemikali kutoka kwenye mabwawa hayo, yalikuwa yakivuja na kusambaa hadi kufikia Mto Tigethi, ingawa vipimo vya maji vilivyofanywa na Afisa wa Bonde vilionesha kuwa na viwango vya kawaida, maana *upstream* ilikuwa PH6, ambayo ni *acidic* kwa lugha ya wataalam. Eneo la tukio ambalo ni lile la mgodi, ni PH 4 *acidic*, kwa kawaida PH ya maji inakuwa *recommended* ni PH 7.0. Kwa hiyo, kwa kiwango kile cha 6 na 4, bado ilikuwa ni kiwango ambacho kinaweza kikakubalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tarehe 23 Juni, 2009, katika maeneo hayo hayo, *upstream* ilikuwa PH 8, ambayo sasa hii ilikuwa ni alkaline. Eneo la tukio ilikuwa ni PH 5.7 ambayo ni *slightly acidic*. Vile vile ilionekana kuwa, nyasi katika eneo hilo zilikuwa zimekauka. Kufuatia ukaguzi huo, Baraza lilitoa maelekezo kwa mgodi kutekeleza mambo yafuatayo:-

- (i) kukarabati mabwawa hayo kwa haraka iwezekanavyo kwa kurudisha maturubai yaliyoibiwa;
- (ii) Baraza lilielekeza Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Ofisi yake ya Bonde, kuchukua sampuli za maji kutoka Mto Tigeti na kupima ubora wake;

- (iii) Baraza liliagiza Viongozi wa Wilaya na Vijiji kuchukua hatua za makusudi kuzuia wizi na uharibifu kupertia utaratibu uliokuwepo wa ulinzi shirikishi; na
- (iv) Baraza liliagiza mgodi kutoa elimu kwa jamii inayozunguka Mgodi kuhusu umuhimu wa yale maturubai katika mabwawa hayo ili wananchi wajue.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo, Baraza limebaini upungufu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, maturubai yaliibiwa, Mgodi ulihitajika kurejesha maturubai mapema, ukizingatia umuhimu wake katika mabwawa hayo. Hata hivyo, maeleo yaliyotolewa hayakuzingatiwa na yalikuwa hayajatekelezwa hadi tarehe 24 wakati Tume yetu ilipokwenda kufanya ukaguzi. Alipoulizwa mwenye mgodi alisema kwamba, kutokana na *supplier* kushindwa kutekeleza matakwa ya mgodi haraka, walitegemea wangeweza kupata maturubai yale kutoka Arusha katika kipindi cha wiki mbili walizopewa, lakini ilivyofika wiki mbili hawakuweza kupata na waliweza kupata hivi majuzi na timu ilivyokwenda imeeleza kwamba kesho wanaanza kusambaza maturubai.

Mheshimiwa Spika, pili, Mgodi haukufanya jitihada za kutosha kwa kutumia njia mbadala ili kuепуша uchafuzi huo, hatua ambayo wangeweza kuchukua ni pamoja na kusafisha maji hayo yaliyokuwa yakichirizika. Tatu, njia nyingine ambayo ingeweza kutumika ni kuchimba mashimo na kuzuia usambaaji wa kemikali, yaani unachimba shimo lingine pembeni ya hilo shimo ili *linkage* ikitokea, iingie kwenye shimo lingine badala ya kusambaa, lakini haikufanyika na walipoulizwa walisema hawakuwa na ardhi ya kutosha na ni kweli eneo lile la Mgodi ni finyu. Walisema kwamba, kipindi kile walikuwa wanajadili na mwenye eneo la pembeni, kuweza kukubaliana gharama za fidia ili waweze kupata eneo hilo katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, lakini pia elimu ya jamii haikutolewa na Mgodi kama walivyoelekezwa, kwa hiyo, hatua zilizoelekezwa na *NEMC* kuchukuliwa na nyingine ambazo zitachukuliwa kufuatia matatizo ya mazingira katika Mgodi wa North Mara ni kama ifuatavyo:-

- (i) Hatua za dharura, kwanza, ulielekezwa kufanya ukarabati wa mabwawa kwa kurudisha yale maturubai, hatua hii imekwishaanza kufanyiwa kazi na kuanzia kipindi kile cha uchunguzi walikuwa wameshaanza kuchimba na injinia alikuwepo pale na wamewaeleza wakaguzi wetu kwamba, maturubai yameshafika na tarehe 30, yaani kesho wanaanza kutandaza katika mabwawa.
- (ii) Baraza lilielekeza kwamba, Wizara ya Maji na Umwagiliaji isitishe kibali cha Mgodi kumwaga maji katika shimo la gotana na maji yanayotoka katika maeneo mengine kuingia kwenye Mto Githeke.

Mto huu tumeelekeza kwamba, usitumiwe kwa shughuli za migodi hata kama kipimo cha ubora wa maji kinasemekana kukidhi viwango ili kurudisha imani ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upungufu uliojitokeza, Baraza litachukua hatua zifuatazo:-

- (i) kuagiza na kusimamia mradi kurejesha mazingira yake ya asili.
- (ii) kuagiza Mradi kugharimia tathmini ya ubora wa maji katika visima vyote vinavyotumika na wananchi kuzunguka eneo la Mgodi na kama itagundulika kwamba, kuna visima ambavyo maji yake havikidhi ubora unaotakiwa, basi Mgodi utatakiwa uchimbe visima vipya.
- (iii) Mgodi utawajibika kulipa fidia endapo uchunguzi unaofanyika sasa hivi kuitia wenzetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, utathibitisha kuwa kuna athari ya afya kwa watu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine za Serikali; mimi binafsi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mazingira na Wawakilishi kutoka Maji na Umwagiliaji, Afya na Ustawi wa Jamii, Mambo ya Ndani, pamoja na baadhi ya Wabunge, kama walivyoelekeza na kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge, tunakubaliana na ushauri wao mzuri na ushauri Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira kwamba, tarehe 3 sisi kikosi hiki tuondoke tukiwa na Mbunge wa eneo lile, pamoja na wale Mawaziri wa Sekta ambazo zinahusika na suala hili na baadhi ya Wajumbe kutoka Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini na ile ya Ardhi na Maliasili ili tuweze kukutana na Uongozi wa Mgodi na kuongea na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ni muhimu, pamoja na matatizo yote linaonesha kwamba, kuna mahusiano mabaya kati ya wawekezaji na wananchi wa eneo hilo. Nadhani katika ngazi yetu ya siasa, tunaweza tukaona ni kitu gani kitaweza kufanyika baada ya yale ya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza litafuatilia utekelezaji wa mambo haya na kama haitaridhishwa na utekelezaji wake, haitasita kusitisha shughuli za Mgodi kwa mujibu wa sheria kama vile Baraza lilivyopata nguvu yake katika sheria. Serikali ya CCM, inalinda maslahi na ustawi wa wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, pamoja na msisitizo wetu kwenye uwekezaji, lakini hatuwezi kamwe kumbeba mwekezaji ambaye shughuli zake zitaonesha kwamba, zinaathiri mazingira na afya ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na hususan kwa ufanuzi wa hali ilivyo huko Tarime kwenye Mgodi wa North Mara na maeneo ya jirani.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni kukubali kuyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka 2009/2010, hoja hiyo imetolewa na Waziri na imeungwa mkono, lakini kwa utaratibu wetu itabidi kwanza ipitie hatua ambayo Katibu ataitangaza.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 26 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 *Administration and General Sh. 4,492,974,000*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 *Administration and General Sh. 3,018,079,600*

Kif. 1002 *Finance and Accounts Sh. 363,316,000*

Kif. 1003 *Policy and Planning Unit Sh. 732,452,200*

Kif. 1004 *Inf. Edu. And Communication Sh. 567,642,500*

Kif. 1005 *Internal Audit Unit Sh. 184,529,600*

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 *Procurement Management Unit Sh. 5,024,129,900*

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. *Subvote 1006*, kifungu cha *Basic Salary*, nilikuwa naomba maelezo ...

MWENYEKITI: *Procurement Management Unit* haina mishahara!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitengo ni kipyaa na kama unavyoona, kimeanza kupata fedha mwaka huu. Fedha zake za mwanzo zipo kwenye *administration*. Kwa hiyo, kwa mwaka huu ndiyo wamepata katika vifungu hivi, mwaka kesho watapata kama walivyofanyiwa *Internal Auditing Unit*, kifungu namba 105, ambapo sasa ni mwaka wa pili tangu hicho kitengo kimeanzishwa na kuingizwa katika bajeti za Hazina.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila madaliko yoyote)*

Kif. 2001 *Union Secretariat* Sh. 51,443,421,100

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani akiwasilisha hotuba yake, alisema kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilipendekeza au iliajinisha mambo kadhaa, ambayo iliona hayo ni kero na ikapendekeza hatua ya kuyachukulia ili kwayo upatikane muafaka. Kwa masikitiko, wakati akijibu masuala haya, Waziri alisema mapendekezo hayo hajayaona kwake na hayajafika; kama hilo ni kweli na kama hali ndiyo hiyo, haionekani hapa kwamba kuna tatizo la msingi kuwa hata mapendekezo ya SMZ hayafiki panapohitajika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme kwamba, kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mapendekezo yake; ni haki yake sisi hatuingilii. Wana haki kabisa ya kuamua walitakalo, lakini kimsingi, mimi nahusika na mambo ya Muungano, hayo hatujayaona, kama anayo anilettee.

MWENYEKITI: Kwa mujibu wa Kanuni na kwa sababu tulikwishatengua Kanuni, huwezi kusimama mara ya pili. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Mohammed Mnyaa. Hivi ninyi haya mnayoyasema mmeyapata wapi, ninyi hamko Serikalini ni ya kweli haya? Basi mimi naagiza tuletewe ili Spika aweze kuyaangalia uhalali wake halafu tutaona. (*Makofit/Kicheko*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa tisa wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, kuna haya mambo ambayo tunashukuru Mungu, yameshapatiwa ufumbuzi na bahati nzuri hata kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu pia yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufanuzi; atuambie Waziri wa Nchi (Muungano), haya mambo yote yenye matatizo jumla ni mangapi? Kama hana orodha hapa atupatie baadaye, kwa sababu wasiwasi wangu ikiwa katika kipindi cha miaka 45 tumetatua mambo matatu tu, kwa hesabu rahisi tu ikiwa mambo haya yapo kumi, ina maana tutahitaji miaka 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, siku hizi mimi nimeshakuwa na ngozi ngumu kidogo.

MWENYEKITI: Unafafanua la kwanza, kwa sababu hayaruhusiwi mawili ni moja?

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi hili la kwanza.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):
Mohamed acha jazba, zungumza kwa upole bwana! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matatu ni yale ambayo yametokana na kuunda Kamati hii, haina maana kwamba, toka nchi hii kuanza ni matatu haiwezekani. Hii ni kutokana na kuundwa kwa Kamati. Niseme tu kwamba, hatuwezi kuwa na orodha iliyomalizika haiwezekani, huu ni Muungano wa binadamu, kuna mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kitabia na watu na kadhalika; matatizo yatakuwepo tu tuvute subira.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka Waziri alirekebishe jina langu, mimi naitwa Yahya Kassim Issa, siyo Yahaya Hamis Issa ni Yahya Kassim Issa.

MWENYEKITI: Ulimi ulitereza tu, anakufahamu sana huyu.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hansard yameshaingia mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi niko katika item 271100, kipindi kilichopita kulikuwa na shilingi bilioni 23, sasa kimezidi mara mbili zaidi mpaka shilingi bilioni 50; je, anaweza kutueleza ni kwa ajili gani na mgao wake ndiyo baina Bara na Visiwani au namna gani?

MWENYEKITI: Hii ni neema.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ni za wafadhili kwa ajili ya SMZ, zinapitia Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, wakiongeza zinakuwa nyingi, neema hii inategemea na wale wafadhili wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahya huwezi kuzungumza mara ya pili, nilidhani ufurahie tu neema hii maana hata kuongozeka mnatia mashaka, ninyi wenzetu vipi tena, ingepungua ni tabu lakini kuongezeka nako ni tabu tena? Hili si deni hii ni neema

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 Environment Sh. 6,929,954,000

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, kabla sijamuuliza Mheshimiwa Waziri, nilikuwa nataka kutumia nafasi hii, kumshukuru sana Waziri Mkuu, kwa ile hotuba yake juu ya watu wa pamba. Nimefurahi sana na mimi nakuomba sasa utekelezaji uwe mara moja, kwa sababu tutaingia matatizo ya watu

kuweza kuleta madai ambayo siyo ya lazima. Nakushukuru sana kwa mwitikio huo wa Serikali na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hili jambo la North Mara, ambalo nimejaribu ku-check hapa katika *program*, nimeona niweke kwenye *Environment Protection* maana nilikuwa nafikiri ingeenda kwenye *Section* ya NEMC lakini hakuna. Kwa hiyo, basi ni-*apply* mazungumzo yangu kwenye *Communication and Information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia ukurasa wa 94 wa Hotuba ya Waziri, sijaona *item* imetolewa kwa North Mara ambayo inaonekana haikufanyiwa *Environmental Impact Assessment*. Halafu pia nimeona kwamba, tangu imeanza ni mwaka jana tu ndiyo imepewa. Sasa kwa yale ambayo yameonekana yametokea na yanagusa watu wengi na siyo jambo la dharura kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba ni kwa sababu ya yale maturubai yaliyoibwa, maana yalioneckana kwenye *television* na athari ya yule mama ambaye mdomo umekauka na mabaka kila mahali, haliwezi kuwa ni jambo ambalo limetokea jana au juzi au mwezi mmoja. Sasa mimi najiuliza; hivi kwa nini Serikali inawaachia watu kama hawa kufanya shughuli bila kuweka watu wetu kwanza kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri?

MWENYEKITU: Hebu uliza tena sijui kama Waziri ameelewa, mimi sijakuelewa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida kama nilivyosema, kunakuwa na *Environmental Impact Assessment*. Ukiona katika *list* hii, karibu migodi yetu yote isipokuwa sasa hivi Bulyanhulu, ndiyo wamepewa hati kwamba imetathminiwa na ni sawa sawa. Madhara ambayo yametokea North Mara, siyo kwa sababu tu ya yale aliyotueleza kwenye picha pale, maana yake ni wazi tuliyona kwenye runinga; ni madhara ya muda mrefu mpaka mtu kukauka mdomo.

MWENYEKITU: Sayansi ya wapi hiyo; wewe hujui kemikali inaunguza mara moja?

MHE. JOHN M. CHEYO: *If you want to argue as a Chemist, I am a Textile Chemist; kwa hiyo, I understand chemistry.*

MWENYEKITU: *Then It seems you have lost your knowledge!*

MHE. JOHN M. CHEYO: *No, no! I am arguing now;* namuuliza Waziri kwamba, inakuwaje Serikali inakubali *operations* zenyé madhara kama hayo kwa watu wetu kutokea na bila kuchukua hatua zinazostahili? Mojawapo ya hatua ni kwamba, *no operation* zingepaswa ku-take place mpaka watu wamefanya *Environmental Impact Assessment*, ndio maana kuna hilo jambo.

MWENYEKITU: Nadhani ulikuwa umepumzika wakati Waziri anaeleza, kwa sababu Waziri ameeleza kabla; huu ni mmoja wa migodi iliyoanza kabla hatujabadili

sheria kuweka *condition* kwamba, ni muhimu hiyo *Environmental Impact Assessment* ifanyika kabla. Hilo ndiyo tatizo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Umeshalijibu Mheshimiwa Mwenyekiti?

MWENYEKITI: Tumekwishapita hapo Mheshimiwa Mbunge.

MHE. JOHN M. CHEYO: Kama ni elekezo la Spika nitakubali, lakini sijaridhika na jibu lako.

MWENYEKITI: Mimi sijibu natoa maelekezo.

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe; maana ya Kamati ya Matumizi ni kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri mhusika. Ufanuzi huo unaweza usikidhi kile unachotaka wewe, siyo lazima uupende, yaani ni kwamba umepata tu ufanuzi ndiyo maana ya Kanuni. Jambo hili siku moja nitalieleza vizuri zaidi, kuna baadhi ya wenzetu hasa wa Kambi ya Upinzani wana hulka ya udikteta kabisa, yaani anataka lile analolitaka yeye lazima wote tukubali kwa nini hii? Tutaendesha vyama vyetu namna hii?

Mtu wa namna hii hebu mfikirie akikaa kwenye kiti sasa anaendesha, kuna mtu kweli anasema humo UDP? Matatizo makubwa kabisa. Anasema kemikali haiunguzi mara moja; amesomea chemistry kweli?

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, hujanielewa.

MWENYEKITI: Aah! *Sit down Sergeant-at-Arms* mtoe nje kwa mujibu wa Kanuni. *Get him out.* (*Makofi*)

(*Hapa Mheshimiwa John M. Cheyo Alitolewa Nje ya Ukumbi*)

MHE. JUMA S. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niombe ufanuzi chini ya *program* hii ya *Environmental Protection*. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kuelewa Serikali imefikia wapi katika kufanya *Environmental Impact Assessment* kuhusiana na Mradi wa Lake Natron? Mradi huu ni muhimu sana kwa uchumi wetu na katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, sikusikia maelezo yoyote kuhusu hilo. Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimwombe radhi shemeji yangu, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa; unajua ulimi wa Kimasai bado ni mgumu kidogo, kwa hiyo, unisamehe sana ndiyo najifunza hivyo Kipemba na Kizanzibari. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Kaboyonga, alizungumzia suala la Lake Natron, lakini kwa sababu nilijaribu kujibu hoja za kila Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza, nikaona niende kwa haraka. Kama tulivyokubaliana sisi Serikali, tulivyotamka hapa katika Bunge hili wakati wa kipindi cha Bajeti kwamba, tutamuweka

mtaalam mwelekezi, ambaye atafanya tathmini na utafiti wa kina kwa sababu anayefanya tathmini ya athari ya mazingira kwa maana ya uwekezaji ni yule ambaye anawekeza. Sasa sisi kwa maana ya Baraza, tunafanya uchambuzi na kuweza kuona kama itakuwa na athari au haitakuwa na athari.

Uchambuzi wa kwanza tuliona kwamba, itakuwa na athari na yule mwekezaji alisema watakwenda kufanya tathmini nyingine, kwa maana ya kuhamisha eneo na kufanya shughuli nyingine.

Kama hiyo haikutosha, tuliona bora tujiridhishe kwa kumuweka mtaalam ambaye atafanya utafiti wa kina na mtaalam yule amekwenda kule na ameshaanza kazi. Sasa hivi yupo katika kutuandikia taarifa, ambayo atatuelekeza namna ya kufanya maamuzi kama tathmini itakuja kutoka kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, nilipata ujumbe kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Mwanne Mcemba anisamehe, alizungumzia mambo mengi ya majitaka viwandani na masuala ya mazingira na vikundi vya akina mama.

Naomba niseme, amezungumzia mchango mkubwa na mimi nimekubali kwamba, tutatembelea Tabora kuona maeneo yale na athari zake. Ahsante sana. (*Makofit*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote
)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh. 6,830,000,100

MHE. ZUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *Subvote* 6309 na ile nyingine ya 6389. Ukiangalia kwa mwaka huu, *Subvote* 6309 imepewa zaidi ya mara mbili ya zile za mwaka jana na zote ni za ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; lakini za Ofisi ya Dar es Salaam zimepunguzwa kwa takriban kama asilimia 70 hivi. Nilikuwa naomba maelezo; kwa nini imepungua au Ofisi ya Dar es Salaam inakaribia kukamilika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lyimo kama ifuatavyo: Ni kweli kama alivyosema mwenyewe kwamba, Dar es Salaam kulikuwa na ofisi ambayo imekwishakamilika na tumeshahamia. Kwa majengo ya Zanzibar, bado yanaendelea kujengwa. Sababu ndiyo hiyo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia *Subvote* hiyo hiyo na *item* hiyo hiyo. Nilikuwa nimejumlisha ujenzi,

construction VIP office and residence in Zanzibar. Nimepata kama shilingi 9,250,636,300 kwa makadirio kuanzia 2007/2008.

MWENYEKITI: Kwenye kifungu gani hicho sasa hicho hicho?

MHE. SALIMU HEMED KHAMIS: Kwenye hiyo *sub vote* 6309, nilijumlisha *construction of V/P office and residence in Zanzibar* kutoka mwaka 2007/2008 mpaka hii 2009/2010, kwa hesabu zangu nikapata shilingi 9,250,636,300. Baada ya kupata hesabu hiyo, nikawa na wasiwasi kidogo nikasema hii nyumba iko wapi Zanzibar, jimbo langu liko Pemba lakini Zanzibar vile vile ni mwenyeji?

Hii nyumba inagharimu shilingi bilioni tisa. Labda Mheshimiwa Waziri atueleze, kutokana na fedha ambazo zimekuwa zikitolewa kila mwaka mpaka imefikia idadi hiyo; hiyo nyumba iko wapi na kweli inalingana na *value for money* isije ikawa hii ni kama mfano wa *Twin Towers* ya Benki Kuu? Naomba ufanuzi. Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyejekiti, bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hajui liko wapi, lakini jengo hili liko Tunguu pale jirani na Uhamiaji. Yapo majengo mawili; moja Ikulu ya Makamu wa Rais na la pili ni Ofisi ya Makamu wa Rais. Karibu utaona. Nakukaribisha. (*Makofi/Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit* Sh. 147,000,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 5001 – *Environment* Sh. 8,893,887,900

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyejekiti, niko kwenye *Subvote 5001, item 6509 - Tanzania Costal Management Project*. Inaonekana dhahiri, inakwenda sambamba na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri; Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Inaonekana inakwenda sambamba na hapa inaonekana kuna USD 801,843,000, msaada wa Marekani; zote ni fedha za kigeni hakuna *local*.

Sasa nilitaka kujua na zimeombwa kwa jina la Tanzania; je, hizi fukwe za Visiwa vyta Unguja na Pemba zitatoka katika fungu hili hili au hizi ziko Bara tu na sisi tutaweza kuzipata nyingine maana naona kila kitu kinasogezwa huku? Sasa naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, huu Mradi ni Mradi ambao ulikuwepo na unaendelea sasa katika awamu ya pili. Kwa hiyo, itakuwa ni vigumu kuanza kuingiza *component* ya eneo

lingine. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mnyaa kwamba, sasa hivi kuna mikakati na sisi Tanzania tumejumuishwa katika Kamati ya Afrika, inayoshughulikia masuala ya mmomonyoko wa fukwe na Ukanda wa Pwani.

Kwa hiyo, katika moja ya mikakati hasa inayotokana na athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi ni kuona jinsi gani ya kunusuru maeneo yetu ya Ukanda wa Pwani na fukwe zetu. Kwa hiyo, kupitia miradi itakayoanzishwa na miradi ambayo sasa tunatafutia ufadhili, uko chini ya *program* ile ya NAPA itahusisha pia na Zanzibar. Hii ni miradi ya kipaumbele na kutokana na dokezo la kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya Mkutano wa Senegal, ametueleza sasa hivi tubainishe maeneo yote ya Tanzania yaliyoathirika na mmomonyoko katika maeneo ya Ukanda wa Pwani, yaweze kufanyiwa mchakato wa kuwa na miradi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa Fedha 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu, liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Nafurahi kuwatangazia kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano, limeyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Nawatakieni nyote Mawaziri na Watendaji, mkafanye kazi nzuri itakayosogeza mbele maendeleo ya nchi yetu. Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nilitaka kidogo hasa kwa faida ya wenzangu wanaokalia Kiti hiki; Kiti hiki kama kikiwa kinadharauliwa, itashindikana kabisa kufanya kazi humu.

Kanuni ya 73 iko wazi kabisa katika hili. Mbunge au Waziri atakayezungumzia jambo/mambo ambayo hayaruhusiwi ni pamoja na kwamba, Spika amekwishamkanya. Anaweza kuamriwa na Spika au Naibu Spika au Mwenyekiti, akatishe hotuba yake na

kukaa mahali pake. Hilo nililifanya, nilimwambia Mheshimiwa John Cheyo akae chini, kwa sababu hakukuwa na faida yoyote ya kuendelea. Endapo Mbunge au Waziri akitakiwa na Spika ajirekebishe na akakataa kufanya hivyo, Spika anaweza kumwamuru Mbunge huyo atoke mara moja nje ya Ukumbi wa Bunge na abaki huko nje kwa muda wote uliosalia wa kikao cha siku hiyo. Kwa hiyo, zinaendelea tena na adhabu nyingine ambazo ni kumtoa kwa siku tatu na kadhalika. Sasa huko hatukufika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba wenzangu wanaokalia Kiti hiki, tuzingattie hilo. Tusipofanya hivyo, ikiruhusiwa Mbunge abishane na Mwenyekiti, Naibu Spika na Spika, tutakuwa kichekesho kwa dunia nzima kabisa.

Mheshimiwa John Cheyo, anafahamu kanuni zetu, unaruhusiwa kusema mara moja wakati wa Kamati. Kabla hatujatengua tuliruhusu mara mbili. Unatolea ufanuzi anachokiona yeye ndiyo kikubaliwe na Kiti. Haiwezekani, kwa sababu kiti hapa kimekaa kama refa, kuitendea haki Serikali na kumtendea haki Mbunge. Huwezi kumwondoa anayesimamia shughuli hizi hapo. Ukijaribu kumwondoa hapo ni kwamba, unaleta fujo tu. Kwa hiyo, naomba wenzangu tufanye kama ilivyofanyika leo Spika anavyosimamia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.10 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 30 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)

